**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**SHULE YA FANI NA SAYANSI YA JAMII**

# MUUNDO NA MTINDO KATIKA DIWANI HURU ZA *MSIMU WA TISA* NA *RANGI YA ANGA*

**(STRUCTURE AND STYLE IN THE ANTHOLOGIES OF *MSIMU WA TISA* AND *RANGI YA ANGA*)**

**NA**

**EUNICE WAVINYA NZIOKI**

**C50/CE/25920/2013**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**MACHI, 2020**

# UNGAMO

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi wala haijapata kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi ____________ Tarehe 23/06/2020

**EUNICE WAVINYA NZIOKI**

**C50/CE/25920/2013**

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu.

Sahihi ____________ Tarehe 7/7/2020

**PROF. GEOFFREY. KITULA. KING'EI**

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

Sahihi ____________ Tarehe 23/06/2020

**DKT. RICHARD. MAKHANU. WAFULA**

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

## SHUKRANI

Namshukuru Rabana kwa kunipa fursa na afya njema ili kufanikisha kazi hii. Vilevile kwa kunipa hekima na satua ya kuchanganua masuala ya kiakademia. Jina lako lihimidiwe duniani kote. Shukrani zangu za dhati pia ziwaendee wasimamizi wangu Profesa Geoffrey King'ei na Dkt. Richard Wafula, waliojifunga kibwebwe kunielekeza ipasavyo bila kuchoka. Hekima, ukarimu na maarifa yenu yalinipa ilhamu ya kuifanya kazi hii kwa umakini hadi tamati. Mungu awabariki na azidi kuwapa hekima kwa ajili ya kizazi kilichopo na kijacho. Nawashukuru wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili kwa maelekezi mliyonipa wakati wa utetezi wa pendekezo langu la utafiti. Maarifa na ushauri wenu ulinifaa zaidi.

Shukrani za dhati zimwendee mume wangu kwa kunifadhili na kunitia moyo masomoni. Isitoshe, kuwatunza watoto wetu wakati nilipokuwa chuoni. Nawashukuru pia watoto wangu kwa kustahimili kutokuwepo kwangu wakati mliponihitaji zaidi. Mungu awabariki nyote na kuwapa ufanisi maishani.

Nawashukuru pia wazazi, ndugu na mashemeji kwa kujitolea kuwatunza watoto wakati nilipokuwa masomoni. Mungu awapanulie mipaka. Aidha, shukrani ziwaendee walimu na marafiki wangu wa karibu, Dorcas Ngina, Catherine Nyika na Bwana Edward Omae kwa kunichochea kujiunga na masomo ya uzamili. Ushauri wenu ulinifaa sana. Mungu abariki kazi ya mikono yenu.

Nawashukuru wanalugha wenzangu kwa kunitia moyo wakati mambo yalikuwa magumu. Naomba neema ya Mungu iwatoshe mnapozidi kufanya utafiti wenu. Mtafikia ufanisi.

Inshallah! Kwa wakutubi wa idara, Christabel na Lucy, pokeeni shukrani zangu kwa maelekezi na ukarimu wenu. Neema ya Mungu iwe nanyi.

Namshukuru Mary Gitata kwa kujitolea kwa udi na uvumba kuhariri kazi yangu na kuipiga chapa ipasavyo.

Ninatambua mchango wa kila mmoja aliyechangia katika kuifanikisha kazi hii. Nawatakia kila la heri maishani mwenu. Inshallah!

## TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapendwa marehemu Alice Meli Nzioki na John Nzioki Musau kwa kujikaza kisabuni kuniwekea msingi bora wa masomo.

Kwa mume wangu, Timothy Mwinzi Muthini kwa kunifadhili na kunitia moyo wakati nilipopitia changamoto katika safari hii ya ufanisi. Mungu akubariki na akuepushe na shari maishani.

Kwa watoto wangu, Victor Muuo Mwinzi na Joy Mutanu Mwinzi, mlistahimili mengi nilipokuwa masomoni. Nawaenzi na kuwapa mkono wa tahania kwa kunihimiza kumaliza safari hii.

Kwa ndugu zangu na familia ya Bwana na Bibi Joseph Makau na Bwana na Bibi Mathews Mwongela, Mungu awabariki kwa kujitolea kwa hali na mali kuwatunza watoto wangu nilipokuwa masomoni.

# IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchambua na kutathmini muundo na mtindo katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Ni dhahiri kwamba vipengee hivi ni muhimu katika kumdhibiti msomaji wa mashairi teule na kumwelekeza katika kuuelewa ushairi huu. Utafiti huu uliongozwa na malengo haya: kutathmini sifa mbalimbali za muundo, kuchunguza dhima ya sifa za kigrafolojia, kuchambua sifa za kitamathali na zinazotegemea muktadha katika diwani teule. Data ya uchanganuzi ilitolewa katika diwani mbili za Kithaka wa Mberia: *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014). Diwani hizi ziliteuliwa kimaksudi miongoni mwa diwani zinginezo kutokana na matumizi yake ya miundo tengemano na ukwasi wa matumizi ya lugha. Aidha, mtunzi amekulia katika mazingira ya humu nchini; jambo ambalo lilirahisisha uhakiki wa mashairi yake. Isitoshe, wepesi wa mawazo yake, upekee wa mtazamo wake na umakinifu, ni mambo ambayo yanavuta hisia za msomaji na kumshurutisha kuwa na tajriba mpya.. Uhakiki wa muundo na mtindo wa ushairi huru ulizingatia sampuli ya mashairi teule katika diwani zote mbili, tasnifu, majarida na tahakiki mbalimbali. Data ya pili ni ya nyanjani na ilijumuisha mahojiano na mtunzi teule wa diwani zote mbili. Utafiti huu ulitumia nadharia changamano: nadharia ya uhakiki ya umuundo na nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Nadharia ya uhakiki ya umuundo iliasisiwa na Ferdinand De Saussure mnamo karne ya ishirini. Mawazo yake yaliendelezwa na Culler (1975) aliyeangazia umuundo katika ushairi. Alisisitiza kwamba ushairi ni ishara zinazojisimamia bila kudhibitiwa na mtunzi na ufasiri wa maana unatokana na namna vipengee vya kimuundo huchagizana kimaana. Kutokana na nadharia hii kutokuwa na urejelezi wa nje, nadharia ya uhakiki wa kimtindo ilitumika kufidia udhaifu huu. Nadharia hii iliasisiwa na Coombes (1953) na kuendelezwa na Leech (1969). Coombes alisema kuwa ili kuchanganua mtindo katika kazi fulani lazima vipengee vinavyofanya kazi fulani ya fasihi vivutie, pia mtunzi hana budi kuonyesha umaarufu wake katika matumizi ya lugha. Tasnifu hii imegawanyika katika sura sita. Matokeo ya data iliyokusanywa yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Muundo na mtindo katika mashairi teule ni vipengele vya kimsingi katika utunzi na usomaji. Ilibainika kwamba mtunzi wa mashairi teule hatungi mashairi yake kutokana na ombwe tupu wala kiholela bali huteua lugha na maumbo kimaksudi ili kuwasilisha ujumbe kwa njia inayoeleweka kwa hadhira na kwa namna ya kuvutia. Isitoshe, ridhimu katika ushairi haidhibitiwi tu na kuwepo kwa vina na mizani kama wanavyodai wanamapokeo bali hudhibitiwa na mtiririko wa mawazo katika akili ya mtunzi; mawazo ambayo huathiri muundo na mtindo wa ushairi. Utafiti huu utawafaa wahakiki, watunzi, wahadhiri na wasomi katika kuuelewa ushairi huru. Aidha, mashairi teule sio kazi iliyoandikwa kwa lugha nathari bali yana sifa za kishairi ambazo zinaonyesha ubunifu na umilisi wa lugha wa mshairi.

# ABSTRACT

The main objective of this research was to analyze and evaluate the use of structure and style in the two anthologies of *Msimu wa Tisa* and *Rangi ya Anga* and their effectiveness in enabling the reader to understand the message. The study aimed at analyzing the features of structure in the two anthologies, analysis of graphological features of style as well as the use of symbolism (metaphor, simile, imagery, metonymy and allegory) and register in the two anthologies by Kithaka wa Mberia. The primary source of data was sampled from collection of poems written by Kithaka wa Mberia namely: *Msimu wa Tisa* (2007) and *Rangi ya Anga* (2014). The two anthologies were purposefully selected due to their diversity in structure and style. The poet, being a Kenyan native, made it easy to identify with his work. His swiftness of thoughts, uniqueness of his perspective and progressivity of his poise is extremely compelling forcing the reader to experience something new. Data was analyzed through close reading of the poems, theses, citations, magazines and reference books. Interview with the author was also used to get the secondary data. This research used two theories of literary criticism namely: structuralism and stylistics. The initiator of structuralism was Ferdinand De Saussure in the $20^{th}$ Century. Culler (1975) specifically applied structuralism to the analysis of poetry. In this case, a poem was seen as an object freed from the control and intention of the author and that any interpretation should be based on the relations of statements and words in the text. Since this theory doesn't lay emphasis on the context, the researcher used the second theory to cater for the contextual problems raised in the poems. The second theory, Stylistics was initiated by Coombes (1953) and expounded by Leech (1969). This theory stresses the use of style as a strategy of portraying beauty in literature. The project was divided into six chapters and presented descriptively. Features of structure and style in the two anthologies were found to be fundamental in writing, analysis and appreciation of poetry. In this case, the findings of the study indicated that the author of the two anthologies doesn't write out of a vacuum or without knowledge but with a perceived intention to use language in a way that attracts and enables the reader to understand his/her message. In these anthologies, rhythm isn't determined by rhyme and the use of meter in a stanza as it is in prosodic verse but it is determined by the flow of thoughts in the mind of the poet which as well determines the structure and style of the poem. This research was targeted to benefit researchers, poets, lecturers and scholars in understanding and analyzing the features of structure and style in the two anthologies. The anthologies are not a collection of words but have poetic features that portray creativity and innovation in the use of language.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

**Arudhi** : Ni kanuni za kimapokezi za utunzi wa ushairi kwa kuzingatia sifa za kimuundo kama vile, mishororo, vina, mizani na beti.

**Kisinkronia** : Haya ni mahusiano ya vipengee vya lugha vilivyo mkabala.

**Maumbo ya kimaksudi** : Haya ni maumbo yanayodhamiriwa na mtunzi wa ushairi; hayatokei kisadfa.

**Maumbo ya picha** : Haya ni maumbo ya kiajabu; yasiyokuwa ya kawaida na yanayokiuka kanuni za muundo wa mashairi ya kimapokeo.

**Mazingira** : Ni mandhari ya mtunzi yanayohusisha muktadha wa kimaumbile, mahali, wahusika na wakati.

**Mtindo** : Ni umbo la ndani la ushairi linalojumlisha matumizi ya fani na tamathali za usemi kama vile takriri, tashbihi, jazanda, sitiari na mbinu nyinginezo.

**Muundo** : Ni uhusiano uliopo baina ya vijisehemu vinavyojenga ushairi, hususan, mpangilio wa sauti, silabi, maneno na mistari.

**Shairi** : Utungo wenye mpangilio mahususi wa maneno, unaotumia lugha ya mkato ili kugusia suala maalumu.

**Umbo** : Ni mkao au sura ya nje ya ushairi.

**Ushairi huru** : Huu ni ushairi ambao unakiuka sheria za kale za utunzi wa mashairi ambazo zilishadidia muwala wa beti, vipande vya

mishororo, mishororo, urari wa vina na mizani na utoshelezi wa maana katika mishororo.

| | | |
|---|---|---|
| **Wanamapokeo** | **:** | Ni watunzi wanaotunga mashairi kwa kuzingatia kanuni za kiarudhi. Mathalan, urari wa vina, mizani, beti, mishororo na vipande vya mishororo. Watunzi hawa ni kama vile Muyaka Bin Haji, Shaaban Robert, Amri Abedi, Mathias Mnyampala, Mwalimu Hassan Mbega na wengineo. |
| **Wanausasa** | **:** | Ni watunzi wa ushairi ambao wamekiuka matumizi ya kanuni za kiarudhi na badala yake kuzingatia matumizi ya lugha, jazanda na taswira kudhihirisha kiwango cha juu cha utunzi. Watunzi hawa ni kama vile Ebrahim Hussein, Mugyabuso Mulokozi, Kulikoyela Kahigi, Euphrase Kezilahabi, Kithaka wa Mberia na wengineo. |
| **Wizani** | **:** | Ni kasi ya usomaji wa shairi. |

## AKRONIMU

| | |
|---|---|
| **CIA** | : Central Intelligence Agency |
| **FRELIMO** | : Mozambique Liberation Front |
| **RENAMO** | : The Mozambican National Resistance |

## YALIYOMO

**UNGAMO ... ii**
**SHUKRANI ... iii**
**TABARUKU ... v**
**IKISIRI ... vi**
**ABSTRACT ... vii**
**UFAFANUZI WA ISTILAHI ... viii**
**AKRONIMU ... x**
**YALIYOMO ... xi**

**SURA YA KWANZA ... 1**
1.0 Utangulizi ... 1
1.1 Suala la Utafiti ... 6
1.2 Maswali ya Utafiti ... 9
1.3 Malengo ya Utafiti ... 9
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ... 10
1.5 Upeo na Mipaka ... 12
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ... 14
1.7 Msingi wa Nadharia ... 19
1.7.1 Nadharia ya Uhakiki ya Umuundo ... 20
1.7.2 Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo ... 26
1.8 Mbinu za Utafiti ... 33
1.8.1 Muundo wa Utafiti ... 33
1.8.2 Vigeu vya Utafiti ... 34
1.8.3 Mahali pa Utafiti ... 34
1.8.4 Sampuli na Njia za Kuteua Sampuli ... 34
1.8.5 Ukusanyaji wa Data na Vifaa vya Utafiti ... 35
1.8.6 Uchanganuzi wa Data ... 36
1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti ... 36
1.8.8 Maadili ... 37
1.9 Hitimisho ... 38

**SURA YA PILI: SIFA ZA KIMUUNDO KATIKA MSIMU WA TISA NA RANGI YA ANGA.....39**
2.0 Utangulizi.....39
2.1 Matumizi ya Idhini nyingi za Kishairi.....40
2.1.1 Matumizi ya Mafungu ya Maneno..... 41
2.1.2 Matumizi ya Mishata..... 44
2.1.3 Mipangilio mbalimbali ya Mistari..... 46
2.1.4 Mpangilio wa Maneno au Sauti Kimaksudi..... 49
2.1.5 Matumizi ya Lugha ya Mkato na yenye Mnato..... 50
2.2 Matumizi ya Lugha ya Kimuziki.....54
2.3 Muundo wa Ushairi unaathiri Upokezi wa Ujumbe......57
2.4 Muundo wa Ushairi huathiriwa na Vipengele mbalimbali......61
2.5 Utumiaji  Michoro kuwasilisha Ujumbe maalum.....70
2.6 Matumizi ya Mistari yenye urefu tofauti.....73
2.7 Hitimisho.....79

**SURA YA TATU: SIFA ZA KIGRAFOLOJIA KATIKA MSIMU WA TISA NA RANGI YA ANGA.....81**
3.0 Utangulizi.....81
3.1 Ukiukaji wa Njia za Kawaida za Kuakifisha.....82
3.1.1 Dhima ya Alama ya Kihisishi [!]..... 82
3.1.2 Dhima ya Alama za Nukuu [“…”]..... 84
3.1.3 Dhima ya Nukta pacha [:]..... 87
3.1.4 Dhima ya Kiulizi [?]..... 88
3.1.5 Dhima ya Nukta mkato [;]..... 90
3.1.6 Dhima ya Mkato [,]..... 90
3.1.7 Dhima ya Kistari kifupi [-]..... 91
3.1.8 Dhima ya Herufi kubwa..... 93
3.2 Matumizi ya Marudio na Takriri.....94
3.2.1 Marudio kama Nyenzo ya Kimtindo..... 95
3.2.2 Takriri kama Nyenzo ya Kimtindo..... 99

3.3 Matumizi ya lugha ya kawaida yenye uwezo wa kuibua hisia, mguso na taathira....101
3.4 Matumizi ya Toni katika Kuwasilisha Ujumbe ........................................................106
3.5 Hitimisho.................................................................................................................110

**SURA YA NNE: SIFA ZA KITAMATHALI NA ZINAZOTEGEMEA MUKTADHA KATIKA DIWANI ZA MSIMU WA TISA NA RANGI YA ANGA112**
4.0 Utangulizi...............................................................................................................112
4.1 Matumizi ya Vipengele vya Kitamathali kuliko vya Kiarudhi katika Kuwasilisha Dhamira.................................................................................................................113
4.1.1 Jazanda.............................................................................................................. 114
4.1.2 Taswira.............................................................................................................. 119
4.1.3 Sitiari................................................................................................................. 128
4.1.4 Taashira............................................................................................................. 138
4.1.5 Tashbihi............................................................................................................. 144
4.2 Matumizi ya Lugha Kutegemea Muktadha.............................................................149
4.2.1 Sajili ya Siasa..................................................................................................... 151
4.2.2 Sajili ya Dini ...................................................................................................... 158
4.2.3 Sajili ya Zaraa ................................................................................................... 159
4.3 Hitimisho.................................................................................................................163

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO................164**
5.0 Utangulizi...............................................................................................................164
5.1 Muhtasari ...............................................................................................................164
5.2 Matokeo ya Utafiti ..................................................................................................167
5.3 Changamoto ...........................................................................................................171
5.4 Mafanikio...............................................................................................................172
5.5 Mapendekezo .........................................................................................................172

**MAREJELEO .........................................................................................................174**

**VIAMBATISHO ......................................................................................................180**

Kiambatisho 1: Mashairi ........................................................................................180
Kiambatisho 2: Wimbo ...........................................................................................228
Kiambatisho 3: Hojaji ............................................................................................229
Kiambatisho 4: Orodha Ya Wahojiwa ...................................................................231

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Ushairi ni kipera mojawapo katika fasihi ambacho kina mvuto zaidi. Haya ni kupitia muundo na mtindo wa uwasilishaji wake. Katika utangulizi wa swala la "Ushairi, Lugha na Mawazo", Heidegger (1971), anazua swala la tofauti iliyopo kati ya mfikiriaji mshairi na mshairi mfikiriaji; kwamba ili kuwa mshairi mkomavu kuna ufikiriaji ambao mshairi lazima akamilishe. Ufikiriaji ulio na usafi, uzito na umoja wa ushairi. Uwazaji wa kiwango hiki huongezea ubora na utaalamu wa lugha ya ushairi. Kutokana na maoni ya Heidegger, kuna tofauti kuu kati ya mtu anayewazia kuwa mshairi na yule ambaye tayari ni mshairi kabla awasilishe mawazo yake lazima awe amepevuka kiakili ili awasilishe kwa namna teule na ubingwa wa kupigiwa mfano.

Kulingana na Indede (2008), mwanadamu amekuwa akijaribu kuvumbua mambo mapya ambayo yataleta mvuto na kuchangamsha akili yake kiubunifu. Ndiposa washairi wengi wa kisasa wanashikilia kwamba ulimwengu unabadilika kwa hivyo utamaduni wa ushairi lazima ubadilike. Aidha, Mazrui (1988) anasema kwamba utamaduni hauna budi kubadilika maadamu uchumi na siasa za nchi zinaendelea kubadilika. Mwelekeo huo unasisitizwa katika mjadala wa Mwai (1988) anayeonyesha kuwa washairi wa kisasa wanaeleza kwamba fasihi hubadilika katika umbo na maudhui kwa hivyo ushairi wa Kiswahili sharti uruhusu mabadiliko yanayotokea katika ushairi huru. Kithaka wa Mberia, katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga* ameibuka na miundo mipya na ya kipekee ya kuwasilisha maudhui yake kwa lugha sahili na kwa namna ya

kuvutia msomaji kiasi ya kwamba mawazo yake yataganda katika akili na kudumu kwa muda mrefu.

Indede anazidi kusema kwamba mielekeo ya kifasihi ya kipindi baada ya uhuru ilivunja umbo la kitamaduni na kufanyia mjarabu maumbo mapya ya ushairi. Katika uchambuzi wake, ushairi wa awali uliotungwa na wanamapokeo uliangazia sifa zifuatazo: umbo la tarbia lenye mishororo minne, vipande viwili vya mishororo, mizani 8, 8 na urari wa vina na ulinganifu wa mizani. Baadaye mashairi yenye idadi tofauti ya mishororo na vipande zaidi ya viwili yalitungwa. Kufuatia ushairi wa Kezilahabi katika *Kichomi* (1974), washairi wa baadaye waliasi sheria za utunzi kama alivyonakili Abedi katika *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). Indede anasema lengo hasa lilikuwa kuleta mapinduzi katika umbo, miundo na mitindo katika ushairi kwa minajili ya kuepukana na uchovu uliotokana na mtindo ule ule wa urari wa vina na mizani. Isitoshe, wana-usasa walionelea kuwa ushairi wa awali haufikii umma wa kawaida kwa sababu ya matumizi ya lugha ngumu ya kimafumbo, methali na taswira ambazo si rahisi kufasirika. Ni kana kwamba waliutoa ushairi "chuoni hadi sokoni". Hii ina maana ya kwamba ushairi tu ulikuwa umetengewa wasomi ambao walimudu lugha wala sio mtu wa kawaida aliyepungukiwa na elimu.

Indede anakiri kwamba mifumo mbalimbali ya kielimu imechangia sana katika mabadiliko ya umbo la shairi; jambo ambalo limezua mtafaruku baina ya wanausasa na wanajadi wakidai kwamba mabadiliko haya yanatokana na athari za nje yakiwemo mataifa mbalimbali kama vile Marekani, Ujerumani, Uingereza na mengineyo. Kwa mujibu wa Kahigi na Mulokozi (1979: 2), fasihi ni sehemu ya utamaduni wa jamii.

Utamaduni huo umefungamana na muundo maalum wa uchumi, na hauna budi kubadilika wakati muundo huo wa kiuchumi unapobadilika. Kila kitu daima kipo katika hali ya mabadiliko. Kwa hivyo kubadilika kwa ushairi wa Kiswahili si kitu kigeni. Kulingana na Njogu na Chimera (1999), mabadiliko haya yalianza kutokea katika tungo za Euphrase Kezilahabi, Ebrahim Hussein, Mugyabuso Mulokozi na Kulikoyela Kahigi ambao waliandika tungo zisizofuata vina na mizani na kuziita mashairi ya kisasa; wengi wanayaita mashairi huru, masivina, mashairi ya kimapinduzi au mapingiti.

Kwa mujibu wa Kezilahabi (1977: 60), wanausasa wanasema kuwa hakuna sheria za kutunga mashairi. Wanadai kwamba kila mshairi ana njia yake ya kutunga mashairi, na njia yake ya kutoa mawazo ya kishairi. Anafafanua mawazo ya msimamo huu katika utangulizi wa *Kichomi* (1974). Anasema:

> Mtu yeyote akiniuliza
> Kwa nini vina na mizani
> Situmii na mistari na
> Beti sitoshelezi
> Nitamwambia: Rafiki
> Kuna njia nyingi za kwenda
> Bustanini.
> Lakini kama mtu yule yule
> Kunizoza akiendelea na kuniambia
> Nitamwambia;
> Rafiki, twende nyumbani kwangu
> Kwa mguu, na nyumbani kwangu
> Tukifika jaribu kunifunza
> Kutembea (uk.xiii)

Kwa hivyo, mshairi ana uhuru wa kutunga mashairi atakavyo mradi tu adhihirishe usanifu na akuze maudhui yake kwa uteuzi mzuri wa taswira na lugha. Hali kadhalika, Kahigi na Mulokozi (1979), wanasema kuwa ushairi huru umekiuka kanuni za arudhi (urari wa vina na mizani, mishororo, beti na muwala) na, badala yake kusisitiza hisia, ilhamu, taswira na maono. Kutokana na maoni yao inadhihirika kuwa kituo na kitivo cha

hisia za mtunzi chafaa kuwa katika kiwango cha juu ili kuacha wasomi wakiwa na hamu ya kutaka kuendelea kusoma. Vipengee vingine vya wanamapokeo vimehifadhiwa katika diwani teule lakini kwa mitindo tofauti hasa vina, mizani, mishororo na beti. Kwa mfano, ili kunukuu usemi halisi katika ushairi, ubeti unaandikwa kuegemea kulia ili kubainisha msemaji.

Kulingana na Abdilatif Abdalla ambaye ni mwanamapokeo, anampongeza Said Ahmed Mohamed katika utangulizi wa *Sikate Tamaa* (1980) kwa ujasiri alioufanya katika kubadilisha miundo ya ushairi uliozoeleka. Anaonyesha kwamba umbo la shairi lina nafasi kubwa sana ya kuweza kuvyaziwa miundo kadha wa kadha na ni matumaini yake kuwa watakaomfuata Said Ahmed Mohamed wataendelea kukuza sanaa hii.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), uhakiki wa ushairi wa Kiswahili unadhihirisha matumizi ya mbinu kadhaa za kimtindo hasa methali, nahau na misimu. Vipengele hivi ni muhimu katika kufahamu ubunifu na usanifu wa ushairi huru. Aidha, wanasema kwamba mwandishi Okot p'Bitek katika diwani yake ya *Wimbo wa Lawino* na, Alamin Mazrui katika *Chembe cha Moyo*, wametumia mtindo wa mashairi huru kuelezea maudhui yao kupitia uteuzi wa maneno kwa njia ya usanifu. Isitoshe, arudhi si vipengele vinavyojikita katika fonolojia ya sauti na silabi pekee bali pia katika sintaksia na muundo wa kisemantiki wa shairi.

Katika uchambuzi wa ushairi huru, Indede (2008), anasema ushairi huu umetawaliwa na hisia, ilhamu, taswira na maono. Anaeleza kuwa kituo na kitivo cha hisia za mtunzi lazima kiwe cha kiwango cha juu kiasi cha kumwacha msomi akiwa na hamu ya

kuendelea kusoma. Pia, wanamapinduzi si eti walikataa kutumia vipengee vya kimsingi katika utunzi wao ila wakati mwingine wanavihifadhi kwa mitindo mingineyo. Kwa mfano, wanabadili mpangilio wa mishororo. Tatu, wanamapinduzi wanakaidi kanuni hizo za kiarudhi kimaksudi. Nne, watunzi huzingatia matumizi ya lugha, jazanda na taswira kudhihirisha kiwango cha juu cha utunzi. Isitoshe, huzingatia matumizi ya ushairi picha kuonyesha uvumbuzi wa falsafa mpya ya kisanaa na uwazi wa ujumbe. Mwisho, wanamapinduzi wanasisitiza matumizi ya lugha sanifu na isiyo changamano.

Kutokana na uchambuzi huu, sifa hizi za ushairi wa wanamapinduzi zinadhihirika katika mashairi teule, hivyo kuupa uzito utafiti huu. Sifa za kimuundo ambazo zimeangaziwa katika utafiti huu ni: maumbo ya kimaksudi, mpangilio wa maneno katika uundaji wa mistari na matumizi ya mdundo usiobainika. Sifa za kimtindo zimehusisha matumizi ya viakifishi, mbinu ya marudio, takriri, jazanda, taashira, taswira, sitiari na tashbihi. Mwandishi Kithaka wa Mberia amewasilisha ushairi wake kwa upekee kuonyesha umbuji na ujumi wa kazi hiyo. Vilevile ameyawasilisha mawazo yake kwa urahisi, kwa njia huru na kudhihirisha kiwango cha juu cha usomi.

Aghalabu mshairi wa Kiswahili ana uhuru mkubwa katika matumizi na ubunifu wa msamiati, uumbaji wa miundo mbalimbali ya kisintaksia pamoja na tamathali za usemi (Zubkova-Bertoncini 2008). Kutokana na maelezo haya inadhihirika kwamba maudhui hueleweka vyema katika ushairi kupitia uwasilishaji wake kwa kutumia ishara maalum za lugha ambazo hujengeka katika matumizi ya tamathali za usemi.

Kupitia uchanganuzi wa diwani teule, msomaji atapata ufahamu zaidi kuhusu muundo na mtindo katika mashairi ya kisasa. Hali kadhalika, kuna haja ya wasomaji kutambua kwamba ushairi huru una hadhi katika jamii na utazidi kukua kila kuchao

**1.1 Suala la Utafiti**

Utafiti huu umechanganua matumizi ya muundo na mtindo katika diwani huru za *Msimu wa Tisa na Rangi ya Anga*. Ingawa utafiti umefanywa kuhusu mashairi huru ya Kiswahili hata hivyo, kunazo sifa nyingi za kimuundo na kimtindo ambazo hazijabainishwa wazi katika uchunguzi na ambazo ni za umuhimu katika kufahamu ubunifu na usanifu wa ushairi huru. Uchambuzi wa awali umeangazia muundo na mtindo katika mashairi ya kimapokeo kwa kina. Aidha, kuna wahakiki pia ambao wameshughulikia vipengee kadhaa vya kimuundo na kimtindo katika ushairi huru kama vile Masinde (1992, 2003) na Maitaria (2012). Utafiti wao haujafafanua moja kwa moja sifa za kimuundo na kimtindo katika ushairi huru lakini wameangazia vipengee mbalimbali kwa ujumla; jambo ambalo linatupatia ilhamu ya kuchanganua sifa hizi pamoja na dhima yake katika diwani huru za *Msimu wa Tisa na Rangi ya Anga*.

Historia ni upanga ulio na makali kuwili; hukata mbele na nyuma. Inatukumbusha vipindi mbalimbali katika maisha ya binadamu ambavyo vimetawaliwa na matukio tofauti. Njia moja ya kuwasilisha matukio haya ni kupitia fasihi. Misingi na mikondo ya historia ya jamii huipa fasihi umbo kimaudhui na kifani. Kipera mojawapo cha fasihi ambacho kinawasilisha ujumbe kwa njia ya mkato na yenye mvuto zaidi ni ushairi. Kulingana na Wamitila (2002), Momanyi (1998) na Mulokozi na Sengo (1995), Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu na huendelea kustawishwa kifani, kiumbuji na kimaudhui. Isitoshe,

King'ei na Kemoli (2001) na Njogu (1993) wanasema ya kwamba ushairi wa Kiswahili wa jadi ulikuwa katika masimulizi na kuwasilishwa kama nyimbo na kughanwa kisha baadaye ulianza kutungwa na kuhifadhiwa kimaandishi. Aidha, Mulokozi (1989) anathibitisha kwamba juhudi hizi zilifanyika mnamo karne ya kumi Kabla ya Kristo. Huku akimnukuu Kezilahabi (1983), anarejelea mihula minne ya ushairi wa Kiswahili. Mathalan:

Muhula wa Urasimu (hadi 1885): katika muhula huu mashairi yalikuwa yenye muundo wa utenzi na kusheheni maudhui ya dini na umwinyi. Baadhi ya tenzi zilizotungwa wakati huo ni kama vile, *Utenzi wa Hamziya* (1690), *Utenzi wa Tambuka* (1728), *Utenzi wa Inkishafi, Utenzi wa Mwanakupona, Utenzi wa Rasi-al-Ghuli, Utenzi wa Shufaka* na *Utenzi wa Muyaka bin Haji.*

Muhula wa Utasa (1885-1945): katika kipindi hiki, utunzi wa mashairi ulikumbwa na changamoto kutokana na athari za kikoloni. Kulikuwa na mabadiliko ya kiutawala na kielimu. Pia hati ya maandishi ilibadilika kutoka Kiarabu hadi Kirumi. Mashairi machache yaliyotungwa na washairi kama vile Hemed Abdalla hayakuzingatia sana kanuni za ushairi. Baadhi ya tenzi zilizopatikana ni Utenzi wa Vita vya Majimaji. Isitoshe, kanuni za uandishi wa mashairi zilianza kupotea.

Muhula wa Urasimu Mpya (1945-1960): katika muhula huu mashairi yaliyotungwa yalikuwa ya kiarudhi. Washairi walishadidia ya kwamba ili utungo uitwe ushairi haukuwa na budi kuzingatia urari wa vina na mizani. Watunzi wa mashairi walioshamiri wakati huu ni kama vile, Shaaban Robert, Amri Abedi, Said Karama na Ahmad Nassir.

Wakati huu, kitabu cha sheria za kutunga mashairi kiliandikwa. Walisisitiza matumizi ya mizani 16 katika kila mshororo, vipande viwili vyenye mizani 8,8 na mishororo minee katika kila ubeti. Waliamini kwamba shairi linafaa kuimbika. Mtindo uliotumika sana katika utunzi ni wa Muyaka bin Haji katika karne ya 18.

Muhula wa Usasa (1967 hadi leo): huu ni muhula wa mtazamo mpya wa kimawazo kisanaa. Washairi walikuwa wanatafuta uhuru wa kisanaa. Mgogoro baina ya wanamapokeo na wanamapinduzi unazuka kutokana na wanamapokeo kulalamika ya kwamba wanamapinduzi hawazingatii kanuni za kiarudhi katika utunzi wao. Kutokana na haya, wataalamu mbalimbali wana mitazamo anuwai kuhusu mabadiliko yaliyopo katika ushairi wa Kiswahili. Nchini Kenya kuliibuka washairi kama vile Alamin Mazrui, na swala hili limefikia kilele katika ushairi wa Kithaka wa Mberia ambao umeangaziwa kwa kina katika utafiti huu. Washairi hawa wakiongozwa na kazi ya Kezilahabi katika *Kichomi* (1974) na *Karibu Ndani* (1988) na Mashairi ya Kisasa yaliyoandikwa na Kahigi na Mulokozi (1973), walianzisha mwenendo mpya wa ushairi huru ambao uliasi kabisa mpangilio na utaratibu wa arudhi za kale. Hawa wameendeleza kampeni kali na madhubuti kwa kuwahimiza washairi wengine wafuate mtindo huo na kuendelea kufikiria juu ya mitindo mingine kama wanavyosema Mulokozi na Kahigi (1973) kwamba matumaini yao kwa watunzi wengi ni kuwa wataiga mfano wao wa kujaribu kuvumbua mitindo mingine; kwani wakishikilia tabia ya kutoibadili mitindo ya Kiswahili, watawafanya waandishi chipukizi hasa wale wa bara, waamini kuwa sanaa ya ushairi ni ngumu sana au inayohitaji kipawa cha pekee mno au kwamba sanaa hii ni ya watu wa pwani na wenye asili ya Kiarabu na uhusiano na dini ya Kiislamu.

Diwani huru za Kithaka wa Mberia: *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014) ni mashairi ambayo yamekiuka kanuni za utunzi wa wanamapokeo. Hali kadhalika, amezingatia maumbo ya picha yaliyo na upekee usioweza kulinganishwa na miundo mingine ya ushairi ulimwenguni. Inabainika wazi kwamba, mabadiliko mengi yametokea tangu kuanzishwa kwa ushairi huru na kutokana na haya, utafiti wetu umedhamiria kuchambua muundo na mtindo katika diwani huru za Kithaka wa Mberia: *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014).

**1.2 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i. Sifa mbalimbali za muundo zimedhihirikaje katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*?
ii. Sifa za kigrafolojia zina dhima gani katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*?
iii. Sifa za kitamathali na zinazotegemea muktadha zina dhima gani katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*?

**1.3 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu ulidhamiria kutimiza malengo yafuatayo:

i. Kuhakiki sifa mbalimbali za muundo katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga.*
ii. Kuchunguza dhima ya sifa za kigrafolojia katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

iii. Kuchambua sifa za kitamathali na zinazotegemea muktadha katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

**1.4 Sababu za Kuchagua Mada**

Tafiti nyingi juu ya ushairi huru zimeshughulikia maudhui, fani na dhima, mathalan, Masinde (1992), Mwania (2007), Wekesa (2008) na Maitaria (2012). Hata hivyo, kunazo sifa nyingi za kimuundo na kimtindo ambazo hazijabainishwa wazi katika uchunguzi na ambazo ni za umuhimu katika kufahamu ubunifu na usanifu wa ushairi huru. Jambo hili limeukweza ushairi huru na kuupa umaarufu zaidi.

Ushairi wa Kiswahili unazidi kupanuka kila uchao kutegemea mabadiliko katika hali ya maisha. Kulingana na Gromov (2006), kimsingi, ushairi wa Kiswahili kwa wakati wa sasa, umepanuka na umeweza kustawisha zaidi baadhi ya vipengele vya miundo teule vya lugha vinavyozoeleka miongoni mwa jamii au kuibua mitindo mipya ambayo hujengwa katika tamathali za usemi. Aidha, Mulokozi (2008), anaunga mkono maoni ya Gromov anaposema kwamba ushairi wa Kiswahili huweza kuathirika kifani na kimaudhui kutokana na mabadiliko ya kiwakati, kitamaduni na uhalisi wa maisha ya watu katika jamii. Aidha, ushairi huru sasa unafunzwa na kutahiniwa katika shule na vyuo nchini Kenya na kwingineko na kwa hivyo kuzidisha umaarufu wake. Ushairi huru unazidi kukubalika kama sehemu ya ushairi wa Kiswahili katika janibu nyingi.

Lugha ndiyo malighafi ya kimsingi katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kwa mujibu wa Indede (2008) na Msokile (1992), lugha ambayo hutumiwa katika utungo huo huwa yenye kuzingatia mpangilio maalumu wa maneno ambao huteuliwa

kwa makini na kwa ufasaha zaidi ili kuweza kuwasilisha ujumbe uliotarajiwa. Kwa mujibu wa Nzuki (2002), dhima ya ushairi wa Kiswahili hutokana na uhusiano uliopo kati ya umbuji wa fani zilizotumiwa na maudhui ambayo huwasilishwa katika muktadha wa utamaduni wa jamii. Kutokana na matumizi ya sifa za kimuundo na kimtindo katika ushairi huru, utamaduni wa jamii husika hubainika wazi. Kwa hivyo kulikuwa na haja ya kutafiti vipengee vya ubunifu vilivyotumika katika kubuni muundo na mtindo wa aina hii ya ushairi.

Data iliyochanganuliwa imetolewa katika diwani huru za Kithaka wa Mberia: *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014). Kusudi kuu ni kupata data kamilifu kwa ajili ya utafiti. Kazi hizi zimeteuliwa kimakusudi kwa sababu mtunzi ni mmoja wa wanausasa waliokiuka sheria za utunzi za wanamapokeo. Isitoshe, ni mwandishi mkongwe katika uandishi wa kazi mbalimbali za ushairi huru. Kwa mfano, *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine* 2001), *Redio na Mwezi* (2005) na *Doa* (2018).

Kithaka wa Mberia ametumia lugha kuonyesha hali ya mazingira ya binadamu hasa mimea, udongo hata wanyama. Haya yanadhihirika katika ushairi wa “Wanda”, “Mwea”, “Nyanda za Minga” na mengineyo. Isitoshe, amehakiki hali halisi ya jamii ya Afrika kisiasa, kiuchumi na kitamaduni tangu Kenya ilipojipatia uhuru hadi mwaka wa 2008. Katika mashairi yake ya hivi karibuni ya *Doa* (2018) amedhihirisha ukiukaji wa haki za binadamu kwa kuzingatia sampuli thelathini hasa katika nchi zanazoendelea. Ametumia lugha kwa usahili, miundo tengemano na mitindo tofauti kusawiri hali tofauti tofauti katika maisha ya binadamu. Utunzi huu umeonyesha ukwasi na umbuji wa lugha alionao mtunzi.

Mashairi mengi ambayo ni huru yameandikwa na waandishi kutoka Tanzania mfano wa Euphrase Kezilahabi katika mashairi yake ya na *Kichomi*, *Karibu Ndani* na *Dhifa;* jambo ambalo linayalazimu mashairi yaegemee mazingira ya mwandishi kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, utafiti wa Nasimiyu (2016), unaangazia jinsi mazingira ya kijamii na kihistoria katika nchi ya Tanzania yanavyoathiri uwasilishaji wa maudhui katika diwani ya *Dhifa*. Tumechagua ushairi wa Kithaka wa Mberia kutokana na asili yake kama Mkenya ili kuwafaidi wasomaji nchini pia kuwafanya wajinasibishe nao kwa karibu kwa sababu anaangazia masuala halisi kama vile ya kijinsia, uongozi, njaa na kiangazi na ukoloni. Isitoshe, uchanganuzi wa ushairi huu utawafanya wasomaji kuelewa mazingira yao kwa kina.

Hali kadhalika, muundo na mtindo katika diwani hizi mbili ni muhimu katika kumdhibiti msomaji na kumwelekeza katika kuuelewa ushairi huu. Ushairi wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga* umetumia lugha inayaoeleweka na msomaji yeyote yule kupitia uteuzi wa lugha, maumbo halisi, mafumbo yanayofungamana na mazingira na mpangilio mahususi wa maneno bila kufungwa na kanuni za vina na mizani.

**1.5 Upeo na Mipaka**

Kutokana na tafiti zilizofanywa hapo awali kuhusu vipengee vya muundo na mtindo, tuliamua kuchagua mashairi teule thelathini na mawili kwa ajili ya utafiti huu. Mashairi haya yametolewa katika diwani huru za Kithaka wa Mberia, *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Mashairi haya yana matumizi anuwai ya miundo tengemano na ukwasi wa lugha. Vilevile, mtunzi amejikita katika mazingira ya humu nchini na nchi za Afrika kwa ujumla. Mashairi haya yaliangazia sifa mbalimbali za kimuundo kama vile: matumizi ya

idhini nyingi za ushairi, lugha ya muziki, mpangilio wa kazi katika mafungu, muundo wa shairi hubadilika kutegemea vipengele mbalimbali kama vile: dhamira, maudhui, matumizi ya lugha, wakati, wahusika na upekee wa mtunzi katika uwasilishaji wa ushairi, matumizi ya michoro na mistari yenye urefu tofauti. Sifa za kimtindo zilizoangaziwa ni kama vile: sifa za kigrafolojia zinazohusu ukiukaji wa sifa za kawaida za uakifishi, matumizi ya marudio na takriri, matumizi ya lugha ya kawaida yenye kuibua hisia, mguso na taathira na matumizi ya toni. Sifa zingine za kimtindo ni matumizi ya vipengele vya kitamathali na matumizi ya lugha kutegemea muktadha.

Data iliyochanganuliwa imetolewa katika diwani mbili za Kithaka wa Mberia: *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014). Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, mashairi yote matatu yalirejelewa: Rangi ya Anga (uk.1), Wanda (uk.27) na Zimwi la Theluji (uk.48). Aidha, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* mashairi yafuatayo yalirejelewa: Minyororo ya Njaa (uk.1), Usingizini (uk.3), Tope la Mizozo (uk.6), Werevu (uk.8), Msimu wa Tisa (uk.9), Msimu Mwingine wa Wasaliti (uk.12), Mkasa (uk.13), Kitini (uk.18), Wenda wazimu Kongo (uk.19), Mlima wa Dhahabu (uk.23), Darfur (uk.26), Mkataba Tena (uk.28), Waharifu Huru (uk. 30), Tume za Rais (uk. 31), Magenge matatu (uk.32), Johari Angani (uk.34), Mnara Mwangavu (uk.36), Mafuta yenye Damu (uk.48), Ni Kweli? (uk.55), Mdundo wa Dhiki (uk.56), Mkimbizi (uk. 57), Macho Mekundu (uk.59), Msumbiji (uk.71), Ntharene (uk. 74), Janga Jangwani (uk. 75), Ukarimu wa Ekweta (uk. 78), Maadui Wajanja (uk. 81), Kasisi (uk. 82), Asubuhi Hasiri (uk.84), Ndimi Zetu (uk. 87) na Muungano wa Afrika (uk. 90). Utafiti huu haukushughulikia kazi zote za mtunzi teule kwa sababu muda haukuruhusu.

## 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu ushairi huru wa Kiswahili kwa kuangazia maudhui, fani na dhima. Dhamira ya utafiti huu ni kuangazia kipengele cha fani hasa muundo na mtindo katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

Baadhi ya kazi zilizoshughulikia muundo na mtindo katika ushairi huru ni: Masinde (1992), Mwania (2006), Wekesa (2008), Gicuku (2011), Maitaria (2012), Ali (2016), Juma (2015), Kibaru (2016) na Onyancha (2016). Katika udurusu huu, mtafiti ameonyesha mchango wa kazi hizo na kubainisha tofauti iliyopo na utafiti huu. Baadhi ya watafiti wamefanya utafiti wao kwa kuegemea diwani teule. Miongoni mwao ni, Gicuku (2011), Juma (2015), Ali (2016) na Kibaru (2016). Kunao watafiti wengine ambao wameshughulikia vipengee hivi kwa kuegemea diwani nyinginezo. Miongoni mwao ni Mwania (2006), Wekesa (2008), Maitaria (2012), Njuguna (2015) na Onyancha (2016).

Utafiti wa Masinde (1992) ulishughulikia dhamira na mtindo katika mashairi huru. Alihakiki mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Kahigi na Mulokozi ili kubainisha kuwa ushairi huru una sifa muhimu za ushairi. Isitoshe, alieleza kwamba ushairi huru unapata uhai wake kutokana na uchambuzi wa mtindo unaohusu matumizi ya lugha yenye kuibusha maudhui na hisia za mtunzi. Alichambua mtindo kwa kuzingatia matumizi ya tamathali za usemi kama vile jazanda, takriri na taswira. Vilevile, alitumia nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Utafiti wake ni tofauti na huu kwa sababu utafiti wetu hauchunguzi tu dhima ya sifa za kimtindo pekee bali pia dhima ya sifa za kimuundo katika diwani za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*; sifa ambazo ni kuu katika utunzi wa ushairi huru. Hata hivyo, utafiti wake una mchango mkubwa zaidi katika utafiti wetu hasa kuhusu ufaafu wa

nadharia ya uhakiki wa kimtindo na uchanganuzi wa mbinu za kitamathali kama vile jazanda, takriri na zinginezo.

Naye, Mwania (2006), alichunguza matumizi ya usambamba katika mashairi huru. Aliangazia mashairi ya Euphrase Kezilahabi, Kithaka wa Mberia na Al Amin Mazrui. Alionyesha namna usambamba unawasilisha ujumbe kwa jamii lengwa akitumia nadharia ya semiotiki. Alibainisha usambamba huu kupitia nyenzo za ukiushi, uradidi, uchimuzi na utata. Utafiti huu ni tofauti na wetu ambao unaangazia vipengee zaidi mkiwemo uradidi. Utafiti huu unatupa mwanga zaidi kuhusu matumizi ya uradidi na ukiushi wa muundo katika ushairi huru.

Aidha, Wekesa (2008) amehakiki matumizi ya taswira katika ushairi huru wa Kiswahili. Alitumia nadharia ya semiotiki kuchambua mashairi ya Euphrase Kezilahabi, Kithaka wa Mberia, Mazrui na Kahigi na Mulokozi. Utafiti wake uliegemea katika kubainisha aina za taswira katika ushairi huru; jambo ambalo linatupatia mwongozo kuhusu mbinu ya kimtindo ya taswira katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Hali kadhalika, katika kutanguliza mada yake, ametoa ufafanuzi wa mbinu kadhaa za kimtindo ambao ni wa manufaa kwetu. Zaidi ya hayo, utafiti wetu ni tofauti na wa Wekesa kwa sababu haujajikita katika mtindo wa taswira pekee bali katika matumizi ya mbinu zingine za kimtindo kama vile uradidi, takriri, jazanda na taashira. Aidha umeegemea katika mashairi ya hivi karibuni ya Kithaka wa Mberia ambayo yanaakisi hali ilivyo katika jamii ya leo.

Utafiti wa Gicuku (2011) ulichunguza usawiri wa maudhui ya ndoa katika ushairi wa Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. Aliangazia mashairi ya *Kichomi* (1974) na Euphrase Kezilahabi, *Bara Jingine* (2001) na *Msimu wa Tisa* (2007) na Kithaka wa Mberia. Alitumia nadharia ya umuundo-utekelezi ambayo inaonyesha kuwa jamii ni mfumo unaochangiwa na vipengele vyake vyote ili kuwe na mshikamano. Tofauti iliyopo na utafiti wetu ni kwamba yeye alishughulikia maudhui ya ndoa na utafiti wetu unahusu muundo na mtindo katika ushairi wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga.* Hata hivyo utafiti wake ni wa manufaa kwetu katika kuelezea dhima ya vipengee vya muundo na mtindo.

Utafiti wa Maitaria (2012) umehakiki uainishaji wa ushairi wa Kiswahili-dhima ya methali. Alishughulikia kipengee cha kimtindo cha methali kama mbinu ambayo hutumika zaidi katika uwasilishaji wa ujumbe katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu ulitathmini kutumiwa na kutotumiwa kwa methali kama mbinu ya kubainishia maendeleo na mielekeo ambayo hudhihirika katika uwasilishaji wa ushairi huo. Aliangazia methali kama chombo cha kujengea taswira, sitiari, usambamba na taharuki miongoni mwa mbinu zingine. Vilevile, alishughulikia methali kama msingi wa ujenzi wa muundo na wizani. Tofauti iliyopo na utafiti wetu ni kwamba aliegemea uchanganuzi wa ushairi huru wa Euphrase Kezilahabi na wa kimapokeo wa Abdilatiff Abdalla kwa lengo la kutathmini matumizi ya methali. Pia alitumia nadharia mbili: fomula ya kisimulizi na nadharia ya semiotiki. Ijapokuwa utafiti wa Maitaria uliegemea suala la methali, una mchango mkubwa katika utafiti huu katika masuala ya kimtindo kama vile taswira, takriri, urudiaji na sitiari. Vilevile, umechangia sana katika kuhakiki vipengee vya kimtindo na kimuundo katika ushairi huru kama vile uakifishaji na mpangilio wa maneno mtawalia.

Utafiti wa Juma (2015) ulishughulikia ulinganishaji wa uwasilishaji wa mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. Katika utafiti wake, aliangazia mitindo ya taswira, jazanda na takriri katika diwani ya *Kichomi* (1974) na *Karibu Ndani* (1988) vilivyoandikwa na Euphrase Kezilahabi. Aidha aliangazia mashairi ya Kithaka wa Mberia hasa *Bara Jingine* (2001) na *Msimu wa Tisa* (2007). Alitumia nadharia ya uhakiki wa kimtindo kama ilivyo katika utafiti wetu. Alilinganisha matumizi ya mbinu hizi katika diwani zote mbili kwa kuangazia mashairi mawili mawili chini ya kila mojawapo ya mbinu. Katika uchambuzi wa taswira, aliegemea picha iliyowasilishwa na taswira hiyo, kwa mfano, uoni, harufu, joto, mwendo, mguso na usikivu, tofauti na utafiti wetu ambao umeangazia kwa undani aina tatu kuu za taswira: maono, hisi na fikra. Utafiti wake unahusu ulinganishaji wa uwasilishaji wa mashairi wa waandishi wawili wenye asili tofauti na katika vipindi tofauti vya kihistoria ilhali utafiti wetu umeangazia uchambuzi wa mashairi ya mwandishi mmoja katika vipindi vilivyokaribiana vya kihistoria.

Naye, Njuguna (2015) alishughulikia ukiushi katika ushairi wa Amri Abedi na Kithaka wa Mberia kwa kutumia nadharia ya kimtindo na kihemenitiki. Anaunga mkono maoni ya Chatman (1971) kwamba ukiushi ni ukiukaji wa arudhi. Aidha, anaegemea maoni ya Cluysenaar (1976) ya kwamba ukiushi ni upotoshi wa matarajio yanayohusu viwango mbalimbali vya lugha: semantiki, leksia, sarufi, fonolojia ya sentensi au virai. Tofauti iliyopo na utafiti wetu ni kwamba utafiti wake ulijikita katika ukiushi pekee bali utafiti wetu ulijikita katika kuchambua kwa ujumla dhima ya sifa za kimuundo na kimtindo katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Utafiti wake ni wa manufaa kwetu katika uchambuzi wa baadhi ya vipengee vya kimuundo na kimtindo.

Isitoshe, Ali (2016) alihakiki matumizi ya kinaya katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Mashairi yaliyochambuliwa ni: *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine* (2001), *Redio na Mwezi* (2005) na *Msimu wa Tisa* (2007). Utafiti huu ulilenga kubainisha jinsi kinaya kimetumika kukejeli vitendo visivyofaa vya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika diwani teule. Nadharia ya uhakiki wa kimtindo ilitumika. Utafiti wake umekuwa wa manufaa kwetu hasa kuhusu matumizi ya mbinu ya kejeli kushutumu vitendo viovu vya wanajamii. Mbinu hii imedhihirika katika utafiti wetu hasa katika uchambuzi wa sifa za kimtindo kuhusu matumizi ya lugha kutegemea muktadha. Tofauti iliyopo kati ya utafiti wa Ali na wetu ni kwamba alishughulikia mbinu ya kinaya ambayo hatujashughulikia katika utafiti wetu badala yake tumeshughulikia mbinu zingine za kimtindo kama vile, takriri, urudiaji, taswira, taashira, jazanda, sitiari na tashbihi katika mashairi teule katika *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*, mojawapo yakiwa ni mashairi aliyoyaangazia katika kuchambua mbinu ya kinaya.

Utafiti wa Kibaru (2016) umeshughulikia taashira ya mazingira katika ushairi wa Kiswahili: Mfano wa *Diwani ya Sauti ya Dhiki* na *Msimu wa Tisa*. Utafiti huu ulilenga kuchunguza namna watunzi wa *Sauti ya Dhiki* na *Msimu wa Tisa* wametumia taashira ya mazingira katika diwani zao kama mbinu ya sanaa. Utafiti huu ulibainisha namna watunzi wa diwani teule walitumia taashira ya mazingira kutoa fasiri mbalimbali za ujumbe kulingana na muktadha wa jamii kuwasilisha maudhui ya kazi zao. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya semiotiki inayoonyesha namna mshairi anavyotumia ishara ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwa walengwa, tofauti na utafiti wetu ambao ulitumia nadharia ya uhakiki ya umuundo na kimtindo. Katika *Msimu wa Tisa*, mtafiti aliegemea katika mashairi matatu pekee: Bunge la Tisa, Tope la Mizozo na Ukombozi ili

kudhihirisha taashira ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Katika utafiti wetu, taashira imeangaziwa katika mashairi anuwai sio tu katika *Msimu wa Tisa* pia katika *Rangi ya Anga*. Hata hivyo utafiti wa Kibaru ulitupatia mwanga katika uchambuzi wetu.

Hali kadhalika, Onyancha (2016) alihakiki changamoto za mikondo mipya ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili kwa kutumia nadharia ya kimtindo. Utafiti wake uliangazia mikondo mipya ya kutunga mashairi tofauti na maumbo yaliyozoeleka kwa kurejelea mashairi katika *Tunu ya Ushairi* (2013). Aliangazia mabadiliko ya maneno, kibwagizo na mistari katika ushairi wa kiarudhi pamoja na ushairi huru, picha na arudhi. Alionyesha kuwa mikondo ya kutunga mashairi ya awali inaweza kuendelezwa kwa namna nyingine katika harakati za kujirekebisha na kujiunda upya katika mpito wa wakati. Tofauti na utafiti wetu ambao umejikita tu katika ushairi huru hasa katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*; ushairi ambao umekiuka sheria za utunzi za wanamapokeo bali si kuziendeleza. Kwa sababu mshairi huru ana uhuru wa kuwasilisha mawazo yake bila kufungwa na sheria za kiarudhi. Hata hivyo, utafiti wake ni wa manufaa kwetu hasa katika kuangazia sifa za kimuundo za ushairi katika diwani teule.

Kutokana na tafiti na tahakiki ambazo zimepitiwa, ni wazi kuwa bado kuna vipengee vingi vya muundo na mtindo katika ushairi huru ambavyo havijafanyiwa uchunguzi kwa mapana na marefu, kwa hivyo kulikuwa na haja ya kuvitafitia.

### 1.7 Msingi wa Nadharia

Nadharia ambazo ziliupa msingi utafiti huu ni nadharia ya uhakiki ya umuundo na nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Kutokana na nadharia ya uhakiki ya umuundo

kusisitiza mahusiano baina ya vipengele vya kazi ya kisanaa bila kuwa na urejelezi wa nje, nadharia ya uhakiki wa kimtindo imetumika kufidia udhaifu huo. Nadharia hii inarejelea muktadha wa matumizi ya lugha ili kuleta maana halisi na kamili katika fasihi. Kwa kuzingatia mihimili ya nadharia hizi, ufafanuzi, uhakiki na tathmini ya matumizi ya sifa za kimuundo na za kimtindo yameshughulikiwa.

### 1.7.1 Nadharia ya Uhakiki ya Umuundo

Nadharia ya uhakiki ya umuundo ni pana na wahakiki mbalimbali wameitumia kwa malengo tofauti tofauti. Kimsingi, hii ni nadharia inayochunguza mahusiano yaliyopo baina ya vipengele vya kimsingi katika lugha, fasihi na nyanja zingine ambapo mifumo mbalimbali ya kimuundo inajengeka. Nadharia hii iliibuka kutokana na udhaifu wa kufafanua dhana ya lugha ulioanzishwa na wanamapokeo akina Plato, Aristotle na Socrates. Mtazamo wa wanamapokeo haukuwa wa kisayansi na ulipuuza lugha ambazo hazikuwa zimeandikwa pia ambazo hazikufuata kanuni za kisarufi za lugha bia ya Kilatini.

Waasisi wa nadharia ya umuundo ni Ferdinand De Saussure na Leonard Bloomfield mnamo mapema karne ya 20. Hali kadhalika, Mulokozi (1989), anasema kuwa mwasisi anayetajwa sana katika nadharia hii ni Saussure (1966), aliyependekeza mtazamo wa kiisimu kuhusu lugha kinyume na wataalamu wengine walioshughulikia historia na sura maalum za lugha fulani. De Saussure alivutiwa na miundo inayohimili lugha zote, huku akijaribu kuonyesha kwamba lugha zote za ulimwengu zinaweza kutathminiwa kwa kaida maalum za umuundo. Alizua istilahi, ‘Langue’ na ‘Parole’ kuelezea dhana ya lugha. De Saussure aliegemea sana dhana ya ‘langue’.

Nadharia ya uhakiki ya umuundo husisitiza vipengele vya kazi ya sanaa na jinsi vinavyohusiana hadi kuikamilisha kazi hiyo. Huangalia namna sehemu mbalimbali za kazi za sanaa zilivyofungamana. Hii ina maana kwamba neno halihitaji urejelezi wa nje ili lipate maana na kazi yenyewe ilivyoundwa ndivyo hutoa maana. Jinsi maana imeumbwa ina dhima kubwa kuliko maana yenyewe. Kulingana na Wafula na Njogu (2007), wahakiki wanaoegemea mkondo wa Saussure huzingatia kwamba matini husika ni mfumo unaojisimamia na hivyo basi huwa hamna haja ya kutumia mambo ya nje ili kuhakiki kazi ya fasihi. Wahakiki huzingatia matini kama kiungo kamili kinachoweza kuhakikiwa kivyake. Hivyo basi mhakiki wa umuundo hujaribu kuweka wazi sarufi ya matini pamoja na sheria za jinsi matini hiyo hufanya kazi.

Kutokana na mtazamo wa De Saussure wa kiisimu kuhusu lugha, mhakiki Leech (1969), anahakiki ushairi kwa kuzingatia nadharia ya umuundo. Anasema kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vyema bila kuwepo na ufahamu wa lugha ambayo ni kipengee muhimu katika kuwasilisha mawazo na hisia za mtunzi.

Leech anasisitiza kwamba lugha ya kishairi hujikita katika vitengo vitatu: fonolojia na grafolojia, umbo na semantiki na viwango hivi huingiliana ili kujenga muundo. Kutokana na mtazamo wake, inabainika kwamba kuna mtagusano baina ya sauti, silabi, viambishi, mofimu, maneno na sentensi. Sauti maalum zinaweza kutumika kuunda maneno ambayo yanaweza kurudiwa kujenga muundo fulani. Leech anaangazia vilevile matumizi ya viakifishi na mpangilio wa sentensi ili kujenga aya. Mtunzi anaweza kuamua kutumia viakifishi ama akose kuvitumia kutegemea maneno aliyoyatumia. Haya yote yanajenga

muundo wa shairi. Kwa mujibu wa Leech & Short (1981), ujumi au urembo wa muundo wa matini ndio huvutia msomaji.

Naye, Scholes (1974), anapohakiki kazi za washairi wa awali, nyakati za urasimi, waliozingatia sifa za kiarudhi kama vile Shklovsky, Shelley na Coleridge, anasema kwamba waliazimia kuwasilisha masuala halisi kwa jamii kwa njia tata bali si ya kawaida ili kuufanya ushairi uwe wa kipekee. Anazidi kusema kwamba mtunzi Wordsworth aliyeegemea mashairi ya kiarudhi pia alichoshwa na mtindo huu wa mashairi ya kiarudhi na kuanza kuandika tumbuizo; mashairi yaliyoegemea ubunifu na hisia na ambayo yalisawiriwa kuwa ya hadhi ya chini.

Katika uandishi wake, Wordsworth (1797), anasema ya kwamba mshairi ana uhuru wa kutumia lugha namna ambavyo inatumika katika jamii; iwe nyepesi na inayozingatia mazingira ya wanajamii; jambo ambalo Coleridge analipinga. Kulingana na Pricket (1975), anapohakiki ushairi wa Wordsworth na Coleridge anatambua ya kwamba Coleridge ameegemea uhakiki zaidi kuliko kuwa mshairi naye Wordsworth ni mshairi. Kulingana na Wordsworth, hisia za mtunzi ni muhimu katika kuwasilisha ujumbe kupitia ushairi. Isitoshe, ushairi unafaa kusawiri hisia na matukio ya binadamu, kwa hivyo matumizi ya lugha inayotumiwa katika jamii ndicho chombo muhimu katika kuwasilisha hisia hizo. Aidha, ushairi unaangazia matukio halisi katika jamii. Zaidi ya hayo, anasema ya kwamba kutokana na ishara zilizomo katika jamii, maneno huundwa, ambayo hatimaye hujenga lugha; kauli inayopuuza vipengee muhimu vya lugha.

Scholes anasisitiza kwamba uamilifu wa ushairi hudhihirika kupitia matumizi ya vipengee vya sauti, wizani na taswira. Vilevile kupitia maana inayochanuzwa kupitia mahusiano ya vipengee vya kimuundo kwa mtazamo wa kisinkronia. Aidha, sifa za kiisimu za ushairi zinabainisha ushairi kutokana na usemi wa kinathari. Hali kadhalika, anasema kuwa matini na namna lugha itumikavyo ni vipengee muhimu katika kufasiri ujumbe.

Mgogoro uliozuka baina ya Coleridge na Wordsworth uliibusha umuundo katika ushairi. Wafuasi wa Ferdinand De Saussure walikuwa katika mstari wa mbele kuangazia mashairi kwa mtazamo wa kimuundo. Mfuasi anayetambulikana zaidi ni Jonathan Culler. Culler (1975) alitilia mkazo vipengee vifuatavyo vya umuundo katika ushairi:

i. Ushairi ni ishara zinazojisimamia bila kudhibitiwa na mtunzi.
ii. Ushairi ni maarifa ambayo hayahitaji ufasiri wa kibinafsi kutoka kwa msomaji.
iii. Ufasiri wa ujumbe katika ushairi unafaa kuegemea matini wala sio urejelezi wa nje. Ufasiri huu unafaa kuwa halisi.
iv. Msomaji wa ushairi ni mpokeaji tu si mhusika mtendaji katika utunzi wala ufasiri wa maana apendavyo.
v. Ushairi unahusu upangaji wa maneno kwa utaratibu; maneno ambayo huchagizana kimaana. Kwa hivyo mfasiri wa ujumbe anafaa kuangazia mahusiano yaliyopo baina ya maneno/mafungu ya maneno.
vi. Ufasiri wa maana utategemea tajriba ya msomaji katika usomaji wa mashairi. Kwa hivyo atatoa maana ya kisemantiki.

Kwa hivyo mfuasi Jonathan Culler alisisitiza mihimili hiyo ya umuundo na ambayo ilifaa katika utunzi wa mashairi nyakati hizo ili kuondoa suitofahamu iliyokuwepo baina ya wahakiki na watunzi wa mashairi. Vilevile, huu ni msingi bora wa uhakiki wa ushairi katika utafiti wetu.

Kulingana na Senkoro (1988), huko Ufaransa katika nusu ya karne ya 19, washairi kama vile Laforgue na Rimbaud "waliasi" sheria na kanuni za ushairi wa kimapokeo wa Kifaransa, sheria ambazo hadi wakati huo ndizo zilishikilia maana ya ushairi wa Kifaransa. Badala yake washairi hawa waliandika ushairi huria (*vers libre*). Huko Uingereza washairi kama William Henley na Mathew Arnold ni mifano ya wasanii waliotunga mashairi mazuri yasiyo na vina wala mizani, naye Walt Whitman aliishangaza Marekani hata kabla ya 1860 kwa kutunga ushairi uliowafanya wananadharia waanze kutoa maana mpya ya ushairi.

Senkoro anazidi kusema kwamba mgogoro katika ushairi wa Kiswahili umekuwepo kwa muda sasa hasa kuhusu maana ya ushairi kwa ujumla na maana ya ushairi wa Kiswahili. Sawa na mgogoro uliokuwepo Uingereza, Marekani na Ufaransa, mvutano huu pia uliathiri utunzi wa mashairi ya Kiswahili hasa katika Afrika Mashariki ambapo palitokea mgogoro baina ya wanamapokeo na wanausasa. Wanamapokeo wanasisitiza kuwa vina na urari wa mizani ni roho ya ushairi wa Kiswahili. Upande wa pili wako wanamabadiliko, washairi wa kisasa, ambao wanaeleza na kuthibitisha kuwa si lazima shairi liwe na vina na urari wa mizani ndipo liitwe la Kiswahili.

Kwa mujibu wa Perry (2004), ijapokuwa ushairi huru hauzingatii vina na kanuni za kimapokeo katika utunzi, malenga anaweza kuzingatia yafuatayo:

i. Kutumia vipengele vya muundo kuunda upya ushairi. Kwa mfano, mtunzi anaweza kurudia mistari kadhaa kuonyesha muundo mpya na wizani.
ii. Matumizi ya maneno maalum na teule kuleta ujumi wa ushairi
iii. Matumizi ya kihomolojia yaani maumbo ya picha na ya kipekee kuonyesha umilisi wa mtunzi katika kuelezea hisia zake.

Katika ushairi wa Kiswahili, wanamapokeo wanasisitiza vipengele vifuatavyo vya muundo: matumizi ya lugha ya mkato, vina, mishororo, mizani, vipande, urari na muwala wa beti. Wanamabadiliko nao si eti walitupilia mbali vipengele hivi lakini hawajafungwa na kanuni zao za utunzi. Kwa mfano, Kezilahabi anasisitiza mizani ya mapigo ambayo hudhibiti mwendo wa ushairi. Mapigo haya huitwa wizani. Wizani pia huainishwa na mambo kama vile urefu wa mstari au sentensi, uchaguzi wa maneno na jinsi hayo maneno yanavyohusiana yenyewe kwa yenyewe katika kujenga mstari, ubeti au hata shairi zima. Isitoshe, wizani pia huletwa na msisitizo wa marudio ya maneno.

Aidha, Mulokozi (1989) anasema kuwa muundo ni nadharia inayojibainisha kwa kuangalia ujumla wa uhusiano wa sehemu moja na nyingine katika kufanya kitu kizima. Isitoshe, Wamitila (2003), anasema kuwa muundo ni aina ya uhakiki ambayo inachunguza kaida zilizopo katika uundwaji wa kazi fulani. Hali kadhalika, anasema kuwa nadharia ya uhakiki ya umuundo inatilia mkazo kwenye muundo wa kazi; mwandishi hana nafasi.

Naye Ntarangwi (2003), anasisitiza kwamba lugha haiwezi kufanya kazi bila kuathiriwa na mambo mengine kama vile mazingira. Kwa hivyo, ili kufidia upungufu wa umuundo, nadharia ya uhakiki wa kimtindo imetumika pia. Nadharia hii imerejelea muktadha wa matumizi ya lugha ili kuleta maana halisi na kamili (jinsi vipashio hivyo vya lugha vinavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe) kupitia ushairi wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

### 1.7.2 Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo

Nadharia ya uhakiki wa kimtindo pia imetumika katika utafiti huu kwa madhumuni ya kuhakiki baadhi ya matini za lugha kama vile tashbihi, sitiari, jazanda, balagha, takriri na mbinu zingine za kimtindo. Nadharia hii inasisitiza kwamba kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Namna mtunzi wa ushairi anavyotumia lugha huathiri uelewekaji wake kwa hadhira.

Mwasisi wa nadharia ya uhakiki wa kimtindo ni Coombes (1963). Kulingana naye, mhakiki lazima azingatie mambo yanayofanya kazi fulani ivutie, mathalan, taswira, uteuzi wa maneno, urari wa vina na mahadhi ya ushairi. Mwandishi lazima aonyeshe umaarufu wake katika matumizi ya lugha wala si maudhui tu.

Kulingana na Crystal na Davy (1969), mtindo unaweza kufafanuliwa kwa njia nne kuu: kwanza, mtindo ni tabia ya mtu kuhusu matumizi yake ya lugha. Pili, mtindo ni jinsi jamii au kikundi fulani cha watu wanavyotumia lugha katika kipindi fulani. Tatu, mtindo ni tabia ya kueleza mambo katika mazingira fulani. Nne, kimsingi mtindo umekuwa ukihusishwa na fasihi kama maandishi “mazuri,” yenye sifa bora na yenye umaridadi.

Mhakiki mwingine wa nadharia hii ni Leech (1969). Alisisitiza kuwa huwezi ukachanganua fasihi kwa undani bila kuzingatia matumizi ya lugha kama vile methali, misemo, takriri, mdokezo na mengineyo. Nadharia hii ina misingi yake katika dhana kuwa lugha huchangia katika kufanikisha kazi ya sanaa, hasa katika ule uzuaji na ubunifu wa kifasihi. Hali kadhalika, kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha.

Nadharia ya uhakiki wa kimtindo ina viwango mbalimbali ambavyo humwezesha mchanganuzi wa matini ya kifasihi kuvizingatia ili kutekeleza uhakiki kwa njia ifaayo. Kulingana na Leech (1969), kuna aina mbalimbali za ukiushi wa kaida za matumizi ya lugha ambao hutokea katika mtindo wa ushairi. Viwango vya ukiushi ni kama ifuatavyo: ukiushi wa kimsamiati/kileksia, kisarufi, kilahaja, sajili, kifonolojia, kigrafolojia, kisemantiki na kimapisi/kihistoria. Aidha, kwa mujibu wa Ngara (1982), uhakiki wa kimtindo unafaa kutumia vipengele vya uchanganuzi vilivyotumiwa na mtunzi ili kuonyesha thamani ya matini na ujumi wa kisanaa. Isitoshe, anasisitiza sana uhakiki wa Kiafrika kuliko wa kigeni.

Isitoshe, Simpson (2004), anafafanua vipengee vya kimsingi ambavyo vinafaa kuchunguzwa katika kazi za kifasihi na mhakiki ambaye anatumia uhakiki wa kimtindo. Vipengee hivyo vya Simpson vinafafanuliwa na Wamitila (2008) ambaye pia anachangia pakubwa nadharia hii ya mtindo kwa kuegemea kiwango cha kisarufi, tamathali, usimulizi, uteuzi, uchimuzi, itikadi, mtazamo, muwala, mshikamano pamoja na mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo.

Vifuatavyo ni vigezo muhimu katika kuchunguza matini kutegemea nadharia ya uhakiki wa kimtindo kama wanavyoeleza Leech (1969), Simpson (2004) na Wamitila (2008).

**a. Kiwango cha Maandishi au Grafolojia/utendaji**

Katika kiwango hiki, vipengele vya kifonetiki, kifonolojia na kigrafolojia vinahusishwa. Kwa kawaida, kila kazi ya fasihi huwa katika maandishi fulani na mahususi tena huwa katika abjadi zinazoeleweka na kuzoeleka na walengwa. Hata hivyo, matini za kifasihi huweza kuwa na sifa za kimaandishi ambazo zinachimuzwa na hivyo kutilia uzito kiwango hiki cha ukiushi. Ukiushi huu unahusu mambo yafuatayo: kubadilisha matamshi ya maneno kama vile miujiza liwe "miuza"; na matumizi ya viakifishi kwa njia isiyo ya kawaida/kwa kusudi fulani; mpangilio wa aya au ukosefu wake (Leech 1969, Wamitila 2008).

**b. Kiwango cha Muundo**

Matumizi ya lugha kwa kawaida huhusisha uteuzi wa maneno au msamiati unaotumiwa. Kwa kuwa fasihi inatumia lugha kujieleza, vipengele ambavyo huhusishwa katika uteuzi huu ni vingi. Kuna kiwango cha kimsamiati (kileksia), matumizi ya lahaja, na kiwango cha rejesta/sajili. Ukiushi wa kimsamiati unahusu yafuatayo: kubuni maneno mapya kwa kutumia minyambuliko isiyo ya kawaida na ubunaji huu hutokea kwa kutofuata kanuni za kisarufi kama vile, fukara – fukarisha. Pia kuna matumizi ya maneno ya vikale kama vile, ng'andu (dhahabu); matumizi ya inkisari na mazda; kuchanganya ndimi/kuhamisha ndimi na matumizi ya maneno ya kigeni kama ya Kiingereza au Kilatini. Mwandishi pia anafanya uteuzi wa wahusika anaowatumia kwenye kazi yake; usimulizi anaoutumia na mtazamo wake na mada anayoishughulikia.

### c. Kiwango cha Kisarufi

Kulingana na Leech (1969) na Wamitila (2008), kiwango hiki ni mhimili mkuu wa matamshi ya kiisimu pia msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matumizi ya lugha yenyewe. Hujumlisha viwango vya kimofolojia na kisintaksia. Ukiushi huu huhusisha masuala kama kuboronga sarufi, matumizi ya anafora - neno moja kuanza kila mstari hasa katika nyimbo na mashairi na kurudiwarudiwa kwa sentensi au kifungu. Huwepo pia, ukiushi wa kilahaja na matumizi ya sajili. Kwa ujumla, huzingatia ukiushi katika muundo wa kawaida wa matumizi ya lugha, urefu wa sentensi na sentensi zenye dosari.

### d. Kiwango cha Kisemantiki

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), kiwango hiki kinahusu miundo ya lugha na lugha ya kitamathali. Huonyesha jinsi lugha inavyoathiri maana kwa njia fulani. Ukiushi wa aina hii unahusu matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo inavyofasiriwa katika hali za kawaida. Mara nyingi huhusisha matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Huwepo matumizi ya tamathali za usemi; mbinu ya kinaya, kweli-kinzani (paradoksi), oksimora (tanakuzi) kwa mfano, *Kiza katika Nuru* na S.A. Mohamed pamoja na mbinu ya sitiari, kwa mfano, ujana ni moshi. Isitoshe, huhusisha matumizi ya jazanda, yaani lugha ya picha za kimaelezo au taashira.

### e. Mazungumzo na Mbinu za Uwasilishaji Usemi na Mawazo

Katika kiwango hiki, mhakiki wa kimtindo anafaa kuchunguza mazungumzo au usemezano baina ya wahusika na mbinu nyingine ambazo zinatumiwa katika mazungumzo hayo kwa lengo la kuwasilisha usemi na mawazo ya wahusika (Wamitila 2008). Kulingana na Ngara (1982), wahusika wa riwaya wanawakilisha matumizi ya

lugha ya kawaida katika jamii kama binadamu wa kawaida. Aghalabu, binadamu hutumia lugha kwa njia ambazo zinatofautiana katika viwango vya misamiati, miundo ya sentensi, mkazo, na kadhalika. Tofauti hizi za kimatumizi zinapaswa kuonekana katika tungo za kifasihi hususan riwaya. Ni jukumu la mhakiki kuangazia tofauti zilizoko katika matumizi ya lugha miongoni mwa wahusika. Ikiwa wahusika ni wasomi au walioelimika huenda wakaongea Kiswahili sanifu kutokana na athari za elimu waliyopata. Wenye elimu ndogo huenda wakaathiriwa na lugha ya kwanza, na watumie lafudhi. Huwepo pia matumizi ya lugha za kigeni kama Kiingereza na Kilatini. Isitoshe, huku kutofautisha wahusika katika misingi ya matumizi ya lugha ni sifa nzuri ya uandishi na matumizi yao yanaakisi matumizi ya lugha katika jamii.

### f. Usimulizi au Muundo wa Masimulizi

Usimulizi hurejelea hali ya kuwepo hali au matukio katika hadithi yanayosimuliwa na kuleta mabadiliko. Uchunguzi wa muundo wa usimulizi unahusika kimsingi na uchunguzi wa ploti au msuko wa kazi husika. Matukio na visa katika matini ya kazi ya kifasihi lazima yafuate ruwaza fulani. Msuko unaweza kuwa wa moja kwa moja au changamano. Mpangilio wa matukio huambatana na wakati toka mwanzo hadi mwisho; au kuwepo kwa mbinu rejeshi. Vilevile kuna kuwepo kwa masimulizi. Mara nyingi, huwepo sauti inayotoa masimulizi ya mwandishi au ya mhusika mmojawapo. Masimulizi huweza kutolewa katika nafsi ya kwanza au ya tatu ambapo mhakiki atabainisha sifa hizi za kimtindo na athari inayoleta kwa wanaosimuliwa. Mara nyingine nafsi zote mbili (ya kwanza na ya tatu) hutumiwa ili kuleta athari fulani, kwa mfano, *Nguvu ya Sala* (1999).

Kulingana na Simpson (2004) na Wamitila (2008), kimsingi, matini za kifasihi huwa na muundo wenye sehemu tatu: mwanzo ambao ndio unaoelekeza kwenye mfuatano wa kiwakati. Jukumu la mwanzo ni mfichuo wa mhusika au dhamira. Kwa kawaida, mfichuo huweza kuwa mwanzoni, unaotokeza kwenye sura tofauti tofauti, mfichuo uliokawizwa na mfichuo ulioahirishwa; kisha sehemu ya kati (kiini), na mwisho ambao una utatuzi wa tatizo kuu ambalo ndilo kiini cha mgogoro.

**g. Itikadi, mtazamo na mtindo**

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), mwandishi huchukua mkabala fulani kuhusu anayoyazungumzia na mtazamo huu unaweza kuwa na mchango mkubwa kwenye upokezi wa maneno anayoyasema au jinsi mlengwa anavyoyaelewa au kukipokea kisa kinachosimuliwa. Vilevile, ni muhimu kuchanganua itikadi/mtazamo unaochukuliwa na msimulizi wa kazi inayohusika. Lugha huwa ni nyenzo muhimu ya kubainisha au hata kuchimuza mtazamo huo. Mchanganuzi wa kimtindo anastahili kuchunguza jinsi uteuzi wa maneno au uteuzi wa kiisimu unavyochangia katika kuuangazia mtazamo huo. Kwa ujumla, kulingana na Leech, Simpson na Wamitila, viwango hivi ni muhimu katika uchanganuzi wa mtindo katika kazi za fasihi.

Hali kadhalika, wahakiki mbalimbali wamefafanua dhana ya mtindo. Kwa mfano, Lodge (1981, 1988) anasema mtindo ni jinsi ya kujieleza kwa hadhira. Kwa hivyo, mwasilishaji huvyaza kwa usanii kauli zinazopatikana katika mawasiliano ya jamii ili yaibue maana fiche kupitia jazanda na sitiari. Isitoshe, Chapman (1982) anasema kuwa hakuna mtu anayeweza kujadili fasihi bila kuzingatia kuwa kuna matumizi maalum ya lugha. Aidha, Kimani Njogu na Chimerah (1999), wanasema kuwa mtindo ni ufundi wa kupanga na

kupangua. Ni ujuzi wa kujieleza na hutofautisha mtunzi mmoja na mwingine. Isitoshe, Wamitila (2010), anasema nadharia ya uhakiki wa kimtindo inajikita kwenye uchanganuzi wa lugha kwa kiasi kikubwa.

Kulingana na Senkoro (1982), mtindo ni muhimu sana katika uwasilishaji wa maudhui katika ushairi. Anasema kwamba ushairi ni utanzu wa fasihi unaotumia mpangilio wa lugha ya mkato, ya picha na yenye mapigo mahususi na kuendeleza maudhui yake kimuhtasari pamoja na huyaficha maudhui hayo ndani ya taswira na ishara.

Kutokana na ufafanuzi wa nadharia ya uhakiki ya umuundo na nadharia ya uhakiki wa kimtindo, vipengele vilivyosaidia katika utafiti wetu ni kama vifuatavyo:

i. Viwango vya kimofolojia na kisintaksia ni msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matumizi ya lugha yenyewe. Mhimili huu umetumika katika utafiti wetu kutathmini matumizi ya sifa za kigrafolojia kama vile, uakifishi, takriri na mbinu ya marudio. Vilevile, ukiushi wa urefu wa sentensi. Aidha, namna matumizi ya maneno maalum na teule huleta ujumi wa ushairi.
ii. Matumizi ya kihomolojia yaani maumbo ya picha na ya kipekee huonyesha umilisi wa mtunzi katika kuelezea hisia zake. Katika utafiti wetu, mhimili huu ulichangia pakubwa katika kuchunguza matumizi ya michoro katika diwani teule.
iii. Matini za kifasihi huweza kuwa na sifa za kimaandishi ambazo zinachimuzwa na kutiliwa uzito katika kiwango cha ukiushi. Mhimili huu ulichangia katika kuchunguza matumizi ya uakifishaji kwa njia isiyo ya kawaida au kwa kusudi fulani na mpangilio wa kazi kiaya au ukosefu wake.

iv. Vipashio mbalimbali vya muundo huingiliana na kujengana. Mhimili huu ulichangia katika kutambua vipashio vilivyojenga mashairi mbalimbali na mahusiano yake. Kwa mfano, mizani ya mapigo huweza kudhibiti wizani ambayo huainishwa kwa kuzingatia urefu wa mistari, uteuzi wa maneno na jinsi maneno yanavyohusiana yenyewe kujenga mistari, aya na shairi zima.

v. Miundo ya lugha na lugha ya kitamathali huonyesha jinsi lugha inavyoathiri maana kwa njia fulani. Mhimili huu ulisaidia kutambua athari ya lugha katika kuibusha maana hasa matumizi ya lugha ya kitamathali. Kwa mfano, taswira, taashira, jazanda, tashbihi na sitiari.

Kwa hivyo, katika utafiti huu, nadharia zote mbili zimeoanishwa ili kufafanua, kuhakiki na kuchanganua sifa za kimuundo pamoja na za kimtindo katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga.*

## 1.8 Mbinu za Utafiti

### 1.8.1 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti huu ni wa kimaelezo. Maelezo muhimu kuhusu sifa za kimuundo pamoja na za kimtindo zimeshughulikiwa. Sifa za kimuundo ni kama vile: matumizi ya kanuni nyingi za ushairi, lugha ya muziki, mpangilio wa kazi katika mafungu, muundo wa shairi unaobadilika kutegemea dhamira, maudhui, matumizi ya lugha, wakati, wahusika na upekee wa mtunzi katika uwasilishaji wa ushairi, matumizi ya michoro na mistari yenye urefu tofauti. Sifa za kimtindo zilizoangaziwa ni kama vile: sifa za kigrafolojia, matumizi ya vipengele vya kitamathali na matumizi ya lugha kutegemea muktadha katika diwani za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Ujumbe kuhusu wataalamu

mbalimbali ulitolewa maktabani ili kuweka misingi ya utafiti huu. Aidha maelezo kuhusu utafiti kwa ujumla yametolewa.

### 1.8.2 Vigeu vya Utafiti

Utafiti huu ulihusisha vigeu huru na vigeu tegemezi. Vigeu hivi ni muhimu katika utafiti wowote ule unaotarajiwa kuwa na matokeo bora. Vigeu tegemezi katika utafiti huu ni sifa za kimuundo, sifa za kigrafolojia na kitamathali pamoja na zinazotegemea muktadha katika diwani za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Utafiti huu ulichunguza dhima ya vigeu hivi kutegemea vigeu huru vifuatavyo: maudhui, wahusika, wakati wa utunzi, dhamira, mazingira na mtiririko wa mawazo katika akili ya mshairi.

### 1.8.3 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kupitia usomaji wa kina maktabani na mahojiano ya nyanjani. Data ya kimsingi ilitokana na uhakiki wa vipengele vilivyotajwa katika sampuli ya mashairi teule katika diwani za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Pia data ya upili ilitafutwa kutokana na tafiti juu ya mtindo na muundo wa ushairi wa Kiswahili kwa jumla katika tasnifu, vitabu, majarida na tahakiki mbalimbali. Sehemu ya pili ya utafiti ilijumuisha mahojiano na mtunzi teule wa mashairi yote mawili.

### 1.8.4 Sampuli na Njia za Kuteua Sampuli

Sampuli maksudi ilitumiwa kutoka mashairi teule katika diwani mbili za Kithaka wa Mberia, mathalan, *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Utafiti huu ulilenga mtunzi husika, Kithaka wa Mberia, ambaye aliteuliwa kimaksudi kutokana na utunzi wake wa mashairi huru kwa mikondo ambayo haijazoeleka katika utunzi na upekee wake katika matumizi

ya lugha kuibusha maudhui yanayofungamana na utamaduni wa Kiafrika. Kusudi kuu la kumteua ni kupata data ya kuaminika na ya asili kuhusu matumizi yake ya sifa za kimuundo na kimtindo katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

Sifa za kimuundo na kimtindo ziliteuliwa kimaksudi. Sifa za kimuundo ni kama vile: matumizi ya idhini nyingi za kishairi, lugha ya muziki, mpangilio wa kazi katika mafungu, muundo wa shairi unaobadilika kutegemea dhamira, maudhui, matumizi ya lugha, wakati, wahusika na upekee wa mtunzi katika uwasilishaji wa ushairi, matumizi ya michoro na mistari yenye urefu tofauti. Sifa za kimtindo zilizoangaziwa ni kama vile: sifa za kigrafolojia, matumizi ya vipengele vya kitamathali na matumizi ya lugha kutegemea muktadha katika diwani za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Baada ya kusoma mashairi yote kwa ujumla, ilibidi kufanya uteuzi wa kimaksudi ili kupata matini iliyofaa na toshelezi. Mashairi 18 yaliteuliwa katika kushughulikia sifa za kimuundo na 33 kushughulikia sifa za kimtindo. Data nyingine tuliyotumia ilitokana na vitabu vinavyofafanua nadharia ya uhakiki ya umuundo na uhakiki wa kimtindo, uhakiki wa kazi mbalimbali za Kithaka wa Mberia pamoja na wahakiki wa ushairi wa Kiswahili.

### 1.8.5 Ukusanyaji wa Data na Vifaa vya Utafiti

Data ya kimsingi ilitokana na kusoma kwa ufahamu na kwa kina, neno baada ya neno ili kuelewa kiundani vipengele vya muundo na mtindo vilivyomo katika diwani zote huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Baadaye uteuzi wa vipengele teule vya kuhakiki ulifanywa kimaksudi. Aidha, sampuli hii ya kusudio ilitumika kukusanya data zaidi kutoka kwenye majarida, tasnifu na tahakiki mbalimbali. Pia data ya upili ilitafutwa kutokana na tafiti juu ya mtindo na muundo wa ushairi wa Kiswahili kwa jumla kwa

kurejelea machapisho na vitabu vya nadharia. Sehemu ya pili ya utafiti ilijumuisha mahojiano na mshairi huru teule, mtafiti na mhadhiri wa fasihi. Matumizi ya hojaji wazi yalifanikisha mahojiano hayo. Hoja zilizojadiliwa zilinakiliwa katika kitabu kwa ajili ya kuhifadhi data hiyo. Data ya maktabani na nyanjani ilijumlishwa kwa ajili ya uchanganuzi. Data iliyokusanywa imebainisha kwamba sifa za kimuundo na kimtindo katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga* ni nyenzo muhimu katika utunzi na uwasilishaji wa maudhui.

### 1.8.6 Uchanganuzi wa Data

Hatua zifuatazo za uchanganuzi zilizingatiwa:

Katika hatua ya kwanza, utangulizi wa mada umeshughulikiwa. Hatua ya pili imeangazia sifa za kimuundo katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga.* Katika hatua ya tatu, sifa za kimtindo katika diwani zote mbili zimechanganuliwa, hasa, sifa za kigrafolojia katika diwani teule. Katika hatua ya nne, vipengele vingine vya kimtindo vimeangaziwa, hasa, vya kitamathali na vinavyotegemea muktadha ili kuwasilisha ujumbe. Katika hatua ya tano, matokeo ya utafiti, changamoto tulizokumbana nazo katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data, mafanikio na mapendekezo ya nyanja za kufanyia utafiti yaliangaziwa. Mihimili teule ya nadharia ya uhakiki ya umuundo na nadharia ya uhakiki wa kimtindo ilitumiwa kama mwongozo katika kutambulisha sifa za kimuundo na kimtindo katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

### 1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya uchanganuzi yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Maelezo hayo yalihusu matumizi ya muundo na mtindo katika diwani huru za

*Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Mpangilio wa sura ni kama ifuatavyo: Sura ya kwanza ilishughulikia utangulizi, hasa, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi ya nadharia, mbinu za utafiti na hitimisho. Sura ya pili iliangazia sifa za kimuundo katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga* kama vile: matumizi ya idhini nyingi za kishairi, lugha ya muziki, mpangilio wa kazi katika mafungu, muundo wa shairi unaobadilika kutegemea vipengele mbalimbali kama vile: dhamira, maudhui, matumizi ya lugha, wakati, wahusika na upekee wa mtunzi katika uwasilishaji wa ushairi, matumizi ya michoro na mistari yenye urefu tofauti. Sura ya tatu iliangazia sifa za kigrafolojia katika diwani zote mbili, hasa, ukiukaji wa sifa za kawaida za uakifishi, matumizi ya marudio na takriri, matumizi ya lugha ya kawaida yenye kuibua hisia, mguso na taathira na matumizi ya toni. Sura ya nne iliangazia vipengele vya kitamathali pamoja na vinavyoegemea muktadha ili kuwasilisha ujumbe. Sura ya tano iliangazia, matokeo ya utafiti, changamoto tulizokumbana nazo katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data vilevile, mapendekezo ya nyanja za kufanyia utafiti.

### 1.8.8 Maadili

Mtafiti alimtembelea mtunzi wa diwani teule, Kithaka wa Mberia ofisini mwake katika Idara ya Isimu, Chuo Kikuu cha Nairobi na kupokelewa vyema. Baada ya maamkizi, alijitambulisha kwake na kueleza azimio lake pamoja na umuhimu wa utafiti huu. Uzingativu huu ulijenga uaminifu na uwazi katika maelezo yaliyotolewa. Mtunzi alikuwa huru kujadili maarifa yake kuhusu diwani teule za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imejadili mambo ya kimsingi kuhusiana na utafiti wetu. Mambo haya ni pamoja usuli wa mada na suala la utafiti ambalo ni 'Muundo na Mtindo katika Diwani Huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*'. Mada hii ndiyo kiini cha utafiti wetu. Isitoshe, mtafiti pia ameonyesha maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, msingi wa nadharia, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada pamoja na mbinu za utafiti. Sura inayofuata inashughulikia sifa za kimuundo katika mashairi teule ya *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

# SURA YA PILI

## SIFA ZA KIMUUNDO KATIKA *MSIMU WA TISA* NA *RANGI YA ANGA*

### 2.0 Utangulizi

Sura hii imechunguza sifa za kimuundo katika diwani huru za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Muundo wa shairi huangazia vile shairi limepangwa na mahusiano baina ya elementi zinazojenga shairi hilo. Mihimili ifuatayo ilitumika kama mwongozo katika kuchunguza sifa za kimuundo katika diwani teule:

i. Viwango vya kimofolojia na kisintaksia ni msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matumizi ya lugha yenyewe. Mhimili huu umetumika katika utafiti wetu kuangazia ukiushi wa urefu wa sentensi. Aidha, namna matumizi ya maneno maalum na teule huleta ujumi wa ushairi.

ii. Matumizi ya kihomolojia yaani maumbo ya picha na ya kipekee huonyesha umilisi wa mtunzi katika kuelezea hisia zake. Katika utafiti wetu, mhimili huu ulichangia pakubwa katika kuchunguza matumizi ya michoro katika diwani teule.

iii. Vipashio mbalimbali vya muundo huingiliana na kujengana. Mhimili huu ulichangia katika kutambua vipashio vilivyojenga mashairi mbalimbali na mahusiano yake. Kwa mfano, mizani ya mapigo huweza kudhibiti wizani ambayo huainishwa kwa kuzingatia urefu wa mistari, uteuzi wa maneno na jinsi maneno yanavyohusiana yenyewe kujenga mistari, aya na shairi zima.

Katika sura hii, sifa zifuatazo za kimuundo zimechanganuliwa:

i. Matumizi ya idhini nyingi za kishairi.

ii. Matumizi ya lugha ya kimuziki

iii. Muundo wa ushairi unaathiri upokezi wa ujumbe.

iv. Muundo wa ushairi huathiriwa na vipengele mbalimbali.

v. Utumiaji michoro kuwasilisha ujumbe maalum.

vi. Matumizi ya mistari yenye urefu tofauti.

**2.1 Matumizi ya Idhini nyingi za Kishairi**

Mashairi huru si kazi iliyoandikwa kinathari kama wasemavyo wanamapokeo. Kwa mfano, Abedi (1954) anayesema kwamba mengi kati ya mashairi ya kisasa yanaelekea kupunguza thamani ya mashairi ya Kiswahili mbele ya lugha nyingine. Aidha, wafuasi wengine wa ushairi wa kimapokeo kwa mfano, Abdilatif Abdalla, Shihabuddin Chiraghdin, Hassan Mwalimu Mbega, Ahmad Sheikh Nabhany na wengineo wanaunga maoni haya mkono kwa kuonelea kwamba ushairi umekosa mwelekeo na kwamba kwa kuendeleza maumbo mapya, ladha ya ushairi inapotea na hatimaye utanzu wa ushairi utatoweka na kitakachotokea ni utanzu wa nathari unaotumia lugha kwa ufupi.

Washairi wa kisasa wana kibali cha kuwasilisha mawazo yao kwa namna huru bila kufungwa na mishororo na urari wa vina na mizani. Mtunzi yeyote yule hatungi kutokana na ombwe tupu bali kutokana na msukumo au ilhamu fulani; jambo ambalo linaathiri namna anavyowasilisha kazi yake. Kwa hivyo, mtunzi hawasilishi kazi kiholela tu. Ingekuwa hivyo, basi kila mtu angekuwa mtunzi wa ushairi huru. Mshairi ana uhuru wa kupanga mawazo yake jinsi atakavyo kusudi afanikishe uwasilishaji wa maudhui kwa namna atakavyo na kwa njia ya ubunifu. Utafiti huu unadhihirisha ya kwamba, mtunzi ana kibali cha kuzingatia yafuatayo:

i. Matumizi ya mafungu ya maneno

ii. Matumizi ya mishata
iii. Mipangilio mbalimbali ya mistari
iv. Mpangilio wa maneno au sauti kimaksudi
v. Matumizi ya lugha ya mkato na yenye mnato

### 2.1.1 Matumizi ya Mafungu ya Maneno

Katika mahojiano yangu na Kithaka wa Mberia, kuhusu matumizi yake ya muundo na mtindo katika diwani za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*, yaliyoandaliwa ofisini mwake, Chuo Kikuu cha Nairobi, alisisitiza kuwa diwani teule zimezingatia muundo wa kimaksudi kutokana na mdundo wa muziki ulio katika fikra za mtunzi. Mashairi yaliyopo katika diwani za *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014) yamewasilishwa kwa namna ya mafungu. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* shairi la 'Ni Kweli?' *(uk. 55),* katika kifungu cha kwanza na cha pili. Mshairi anasema:

> Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
> Kwamba tunapokuwa na watoto
> Daima tumulike jamaa zetu wa kiume
> Kwa kurunzi kali ya uangalifu?
>
> Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
> Kwamba wapo wazazi wanatuma watoto
> Kwenda kutega mitego ya virinda hoteli
> Kusudi kuleta change na nguru nyumbani
> Kupigana na kikosi kikali cha njaa?...

Katika shairi hili, mtiririko wa mawazo unadhihirika kutoka fungu moja hadi lingine bila kuzua utata wowote. Idadi ya mistari katika kila fungu hutegemea mtiririko wa mawazo katika akili ya mtunzi. Vilevile, idadi hii ya mishororo hutegemea namna mtunzi anavyotaka kuwasilisha maudhui yake. Katika kifungu cha kwanza, kuna mistari minne huku vifungu vinavyofuatia vikiwa na mistari mitano. Katika uwasilishaji wa maudhui,

mtunzi anatanguliza wazo la dhuluma dhidi ya watoto inayotekelezwa na jinsia ya kiume. Katika kifungu cha pili, anaonyesha namna wazazi wanavyowashurutisha watoto kushiriki ukahaba ili kukabiliana na janga la njaa nyumbani. Katika kifungu cha tatu, mshairi anaangazia vile wazazi wa kiume wanavyowabaka wakembe wao wa kike. Hatimaye, katika kifungu cha mwisho, anaonyesha namna mabinti wanavyoshiriki uzinzi na wazazi wao wa kiume wakati wazazi wao wa kike wako katika shughuli mbalimbali nje ya boma.

Wakati mwingine, mtunzi huwasilisha kazi yake katika fungu moja tu. Kwa mfano, katika shairi la ‘Mdundo wa Dhiki’ (uk. 56). Anasema:

> Njoo! Pamoja tusikize mdundo wa dhiki
> Unaovuma bila kuamsha wanaolala fofofo
> Wakiota ndoto za nyongeza ya mishahara
> Kuendeleza vitambi vyao vya ujenzi wa taifa:
> Vumbi jeuri la migodi na machimbo
> Likichochewa na ndoto za utajiri
> Linavamia mapafu laini na dhaifu
> Na kulowea ndani bila nia ya kuhama
> Baridi yenye hasira nzito kama ukungu
> Rafiki wa mashamba ya majani-chai
> Inapiga mbinzi hadi uboho na wengu…

Katika shairi hili, mawazo ya mtunzi hayana mtuo mrefu ila mwishoni anapotamatisha mawazo yake. Katikati mwa kifungu ametumia mikato na nukta pacha kama vituo vifupi kwa ajili ya kudhibiti usomaji. Uwasilishaji wa kifungu hiki unatokana na mada anayogusia ya “Mdundo wa Dhiki’. Kwa hivyo, mawazo yake yanatoka kimuziki bila kukatizwa. Vilevile, anaonyesha mkururo wa dhiki zinazowapata wanyonge katika jamii; si mishahara duni, si mazingira mabaya kazini, si mateso ya uyaya, si athari za dawa za kulevya. Aidha, uwasilishaji huu unaonyesha kiwango cha juu cha ubunifu cha mtunzi na kuondoa uchovu wa kusoma mashairi yanayozingatia muwala wa beti.

Mpito wa wakati huathiri pia uwasilishaji wa ushairi. Mabadiliko yaliyopo katika jamii huathiri sanaa pia. Katika utunzi wa awali wa *Msimu wa Tisa* (2007), mada kuu katika kila shairi ni dhahiri ilhali katika diwani ya *Rangi ya Anga* (2014), aliyoiandika baada ya miaka saba, anampa msomaji nafasi ya kuchunguza, kutambua mada na kuchambua maudhui yanayojitokeza katika mashairi yake. Mtunzi ana uhuru wa kupanga kazi yake kiaya kutegemea mada kuu na vimada vyake ambavyo vinadhihirika kupitia maelezo. Ushairi wa diwani ya *Rangi ya Anga* ni kielelezo bora cha ushairi wa kisasa ambao unadhihirisha ubunifu huu wa mtunzi. Mtunzi amegawa ushairi huu katika mada tatu kuu: Rangi ya Anga, Wanda na Zimwi la Theluji. Kwa mfano, katika shairi la 1 (uk. 2), mshairi ametanguliza ushairi wake kwa kusema:

> Baina ya wawili maishani
> Uzito wa safari
> Ungelingana kama shilingi kwa ya pili,
> Utulivu kwenye kumbi za nyoyo
> Ungekuwa wa mizani sawa,
> Singejipa wadhifa wa mgambo
> Singepiga pembe ya swala pala
> Kuwakutanisha wanakijiji;
> Moyoni mwangu
> Hakungekuwa na ilihamu
> Ikiniwashawasha kwa utukutu
> Kama majani ya mpupu;
> Mwashomwasho usiokupwa
> Haungekuwa ukirusha mawimbi
> Yakibeba mvumo wa sauti
> Ukisema kwa uradidi:
> Himahima shika pembe
> Piga mbiu ya mgambo!

Katika kifungu hiki, mshairi ametanguliza kwa kuteka makini ya msomaji ya kwamba kuna jambo la dharura analolipasha kwa wanajamii. Katika mada ya kwanza, ameangazia dhuluma kwa jinsia ya kike. Kila aina ya dhuluma imeangaziwa kwa kuzingatia mada

ndogondogo zilizofafanuliwa katika mafungu. Mtunzi ametumia mbinu ya masimulizi kuwasilisha kazi yake ili msomaji aelewe ujumbe kwa urahisi. Kwa mfano, katika shairi la 2 (uk. 2). Mtunzi anasema:

> …Vilele vya milima
> Na mahindi ya bahari,
> Mmwesomweso wa nyota
> Na tumba la mbalamwezi,
> Bila kupigana mieleka
> Kwenye ukumbi wa ugambi
> Zinakubaliana kwa pamoja
> Kwamba kuwa navyo mkononi
> Ni upini wa upanga mkali
> Mkononi mwa mwanamume…

Kutokana na kifungu hiki, mtunzi anaangazia suala mojawapo la dharura ambalo ni taasubi ya kiume inayowapa wanaume nafasi ya kurithi rasilmali katika jamii (ardhi yenye rotuba, mimea iliyonawiri na mazao tele, mifugo na vitu vinginevyo) huku wanawake wakipuuzwa. Inadhihirika wazi kwamba, mafungu haya hayatokei kisadfa bali ni kimaksudi kutokana na mdundo au muziki ulio katika fikra za mtunzi.

### 2.1.2 Matumizi ya Mishata

Kulingana na Lutomia (2017: 6), mishata ni mistari ambayo haijitoshelezi kimaana; hutegemeana. Maana yake hukamilika katika mistari inayofuatia. Katika diwani teule, mistari hii imetokea kimaksudi sio kiholela. Inapotumika katika ushairi inaonyesha hali halisi ya mazungumzo japo kwa njia ya mkato na mnato. Mtunzi yu makini kupanga mistari yake kwa namna ambayo itakuwa rahisi kwa msomaji kuufasiri ujumbe unaokusudiwa. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Usingizini’ (uk. 3), matumizi ya mistari hii imejitokeza wazi. Mshairi anasema:

> Ardhi yenye siha na uchangamfu wa rutuba
> Imelala usingizi katika kitanda cha maumbile

Ikinong'onezana: "Anga linaonea nchi!"
Tambarare zenye uwezo wa kuhimili mamilioni
Zimeachiwa nguchiro, panya, mchwa na nyenze
Katika taifa linalotapatapa katika dimbwi la njaa…

Kutokana na kifungu hiki, kauli inayodokezwa katika mstari wa kwanza na wa pili imekamilika kimaana katika mstari wa tatu, kisha wa nne na wa tano maana imekamilika katika mstari wa mwisho wa kifungu. Mtunzi anaangazia ardhi yenye rutuba ambayo ni rasilmali muhimu kwa binadamu lakini haitumiki vilivyo ili kupigana vita na janga la njaa nchini. Aidha, ijapokuwa mistari hii ni mishata, imeanzia kwa herufi kubwa kwa kusudi la kusisitiza ujumbe.

Isitoshe, mistari mishata imetumika kuwasilisha masimulizi yaliyo katika akili ya mtunzi kishairi badala ya kutumia lugha nathari ambayo inatumika katika riwaya au hadithi. Haya yanadhihirika katika diwani ya *Rangi ya Anga* shairi la 'Rangi ya Anga' (uk. 13). Mshairi anasema:

Walikuwa wachanga
Katika kivuli cha shule
Hisia za ujana zilipovutana
Mithili ya sumaku na chuma;
Nyoyo zikalainika
Miili ikaitika mwito mkali-
Moto wa maumbile uliwaka
Na kisha kuzimika
Mithili mwako mbugani
Utupao ndimi angani
Na kisha kukata roho
Baada ya wingu la mvua
Kupasuka katika mbingu

Mmoja wa wawili washiriki
Aliendelea na mwendo shuleni
Akakusanya vyeti vya maana
Na kupata jina adimu nchini,

Leo, asubuhi anakula mayai
Na asali na siagi ya thamani,
Anavalia mavazi ya kuteua
Na kulalia godoro la gharama,
Anatumia fenicha ya mvuli
Na kulalia matakia ya veliveti…

Katika mifano hii, mtunzi anatumia mishata kutusimulia maisha ya wanagenzi wawili waliozini wangali shuleni. Anaangazia mwanzo wa mahusiano yao na tamati yao. Kwa kijana wa kiume yeye hakuathirika vibaya manake maisha yake yaliendelea na kunawiri ilhali ndoto nzuri za usoni za kijana wa kike zilikatizwa na ujauzito. Mpangilio huu unaondoa uchovu wa kusoma kazi iliyoandikwa kwa lugha nathari.

### 2.1.3 Mipangilio mbalimbali ya Mistari

Mtunzi ametumia mipangilio mbalimbali ya mistari katika diwani ya *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Kitini' (uk. 18). Anasema:

Tulipoguna kwa maumivu makali kwenye misuli
Juhudi za kizalendo zilipopamba moto yakini
Tulipotokwa na michirizi ya jasho tukisaka utu
Tulipopambana na dhiki ya giza la miongo miwili
Waziri aliyeridhika, alitushauri kwa ulimi wa kinaya
        Juhudi zenu zenye nia ya kung'oa chama
        Ni sawa na ubwege wa kutaka kukata mtini
        Kwa wembe ulionyolea tena na tena!...

Katika kifungu hiki, mtunzi ameegemeza mistari mitatu ndani kimaksudi kudhihirisha nukuu au usemi. Anaonyesha maneno ya kejeli anayoyatamka waziri kwa watetezi wa haki kwamba juhudi zao za kung'oa chama ziliambulia patupu, ni sawa na kujaribu kukata mtini kwa kutumia wembe.

Mshairi anaweza kupanga mistari kwa kurudia vitenzi maalum kwa kusudi la kusisitiza ujumbe fulani. Katika *Rangi ya Anga,* (uk. 14), mtunzi anasema:

…Banati alipotimuliwa, alitimuka
Alipotimuka, aliteguka
Alipoteguka…

Katika kifungu hiki, mtunzi anasisitiza ujumbe kwa kurudia vitenzi, 'timuka' na 'teguka' katika kauli tofauti ili kuonyesha namna banati alivyotimuliwa kutoka shuleni baada ya kuwa mja-mzito.

Hali kadhalika, mtunzi anaweza kupanga mistari kwa namna ya kuashiria kasi ya kitendo na hisia zinazoambatana na kitendo hicho. Kwa mfano, katika *Rangi ya Anga,* (uk. 14). Mtunzi anasema:

a
k
a
a
n
g
u
k
a
!

Kutokana na kifungu hiki, mtunzi ameonyesha namna banati alivyokumbana na majanga baada ya kuwa mja-mzito. Sentensi sahili, 'akaanguka' limegawika kisauti na kuandikwa kutoka juu hadi chini badala ya kutoka kushoto hadi kulia. Jambo hili linajenga taswira katika akili ya msomaji kuonyesha kuanguka kwa mwendo wa kasi na kishindo. Hisia za uchungu zinajengeka katika akili ya msomaji kuhusu matokeo ya mahusiano ya kimapenzi baina ya vijana yanayoathiri kwa pakubwa jinsia ya kike. Aidha, kule kugawa sauti kunaleta dhana ya msisitizo wa kitendo hicho.

Mistari vilevile imepangwa kuegemea kulia kwa kusudi la kutoa wazo na jibu. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 6, (uk. 10). Mtunzi anasema:

…Hiyo
Si taasubi
Ni desturi na mila!
Hizo
Si nyanyaso
Ni kanuni za jadi!
Hizo
Si dhuluma
Ni kaida za utamaduni!

Mpangilio huu unatupa taswira ya ukinzani uliopo baina ya utamaduni na haki za binadamu katika jamii hasa haki za jinsia ya kike. Mtunzi anaonyesha namna mwanamke, ambaye ana shahada ya uzamili anaunga mkono utamaduni unaomkandamiza mwanamke. Anashadidia ya kwamba taasubi ya kiume inapotawala katika jamii ni desturi na mila ambazo zinafaa kufuatwa wala si nyanyaso au dhuluma. Kauli hizi zinaleta hisia za chukizo kwa wanajamii, wakiwemo wanawake ambao bado wanaunga mkono tamaduni kandamizi. La kuchukiza zaidi ni kwamba hata wanawake wasomi hawajitokezi bayana kutetea wanawake wanaokandamizwa badala yake wanaunga mkono taasubi ya kiume. Isitoshe, vitenzi, ‘si’ na ‘ni’ vimetumika kuleta dhana ya msisitizo. Kwa hivyo, inabidi msomaji atilie mkazo maneno hayo katika usomaji wake. Mtunzi pia amepanga mistari yake kuonyesha ukinzani uliopo katika jamii kuhusu suala la taasubi kwa kubainisha sehemu ya kwanza na ya pili katika mstari mmoja. Kwa mfano, ‘Hiyo si taasubi’ (sehemu ya kwanza) ‘Ni desturi na mila’ (sehemu ya pili). Kwa hivyo, muundo huu unaambatana na mtindo kiumbuji kuwasilisha ujumbe kutokana na matumizi ya ‘si’ na ‘ni’ kuonyesha mbinu ya tanakuzi.

Mistari hii pia imepangwa kimaksudi kuunda ruwaza fulani. Kusudi kuu ni kuvuta makini ya msomaji. Mshairi ametumia mbinu ya tabaini katika uundaji wa mistari kuonyesha mtazamo wa wanajamii kuhusu masuala ya kijinsia.

### 2.1.4 Mpangilio wa Maneno au Sauti Kimaksudi

Jambo moja ambalo linadhihirisha ubunifu wa mtunzi katika mashairi teule ni mpangilio wa maneno na sauti. Mtunzi anazingatia mitindo mbalimbali ya kupanga maneno yake kutegemea ujumbe anaouwasilisha na mapigo au mahadhi anayotaka kuzua. Mpangilio huu pia hudhibitiwa na wizani ya ushairi wake. Kwa mfano, mtunzi anaweza kuamua kutumia mtindo wa kurudia neno fulani mwanzoni mwa mistari kadhaa ili kusisitiza ujumbe fulani. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* shairi la ‘Mafuta yenye Damu’ (uk. 48). Anasema:

> …Naona majeruhi, damu na maiti
> Maiti za wakulima mashambani
> Maiti za wachungaji malishoni
> Maiti za watoto shuleni
> Maiti za vikongwe vijijini…

Kutokana na kifungu hiki, mshairi ametumia fungu la maneno, ‘maiti za’. Aidha ametumia silabi ‘ni’ kusudi kudumisha mahadhi ya ushairi na kusisitiza ujumbe kwa msomaji. Mbinu hizi zimeangaziwa kwa undani katika uchambuzi wa mtindo. Katika ushairi huu pia kuna usambamba wa kategoria za maneno katika ushairi. Kwa mfano, katika kifungu hiki, mstari wa 2, 3, na 4 unazingatia mpangilio wa nomino, kivumishi, nomino na kielezi. Aidha, nomino zilizotumika ziko katika ngeli mbili pekee: U-ZI na A-WA mtawalia. Kusudi kuu ni kuonyesha vikundi mbalimbali vya walioathirika na vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi ya Sudan.

Mshairi pia anaweza kuandika maneno katika orodha ili kutenganisha orodha na maelezo. Kwa mfano, katika ushairi wa *Rangi ya Anga*, (uk.46). Anasema:

…Aulize waulizwa
Huku kuhamahama
Ili kuanzisha upya konde
Kunaleta shibe gani
Kuliko shamba aushi
La kabeji
Sukuma-wiki
Tamata
Mbiringanya
Pilipili-mboga
Mpunga
Mtama
Mahindi
Karoti
Kunde
Mbaazi
Wanga
Uto
Pamba
Machungwa
Maembe
Na mapera?...

Kutokana na kifungu hiki, mshairi ameorodhesha mimea (mbaazi, mtama, mahindi na mimea mingineyo) ambayo hupandwa na wakulima wanaoendeleza kilimo cha lima-hama-lima.

### 2.1.5 Matumizi ya Lugha ya Mkato na yenye Mnato

Ushairi katika diwani teule umetumia lugha ya mkato na inayovuta hisia za msomaji. Kulingana na Mulokozi (1989: 1), ushairi ni sanaa ya lugha inayoonyesha au kueleza jambo, wazo au tukio kwa namna inayovuta hisia kutokana na mpangilio maalumu wa maneno yaliyoteuliwa, kauli za mkato, picha na tamathali na inayowasilishwa kwa

hadhira kwa njia ya nyimbo au maandishi. Maoni haya yanaungwa mkono na Wamitila (2008: 226) anayesema kwamba ushairi ni sanaa ya lugha inayotambulishwa na mpangilio maalum wa mishororo au wa kisauti na kwa maneno mateule kwa kutumia mbinu za lugha zenye mnato na mbinu zinginezo za kibalagha na za kimtindo zinazomwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe kwa ufupi na kwa mkokotezo mkubwa unaoeleza kisa, hisia, tukio au hali kwa lugha ya mvuto.

Kauli za mkato ni kauli ambazo hutolewa kwa njia ya muhtasari na aghalabu hutumia tamathali za usemi kuelezea tukio au hali fulani. Kwa mfano, mtunzi wa diwani zote mbili ametumia lugha ya mkato katika anwani. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, anwani, 'Usingizini' (uk. 3) imefichama uvivu na mapuuza ya kilimo ambayo yamewafanya wananchi wafungwe katika minyororo ya njaa. Katika shairi la 'Tope la Mizozo' (uk. 6), mshairi anazungumzia mizozo ya kisiasa na namna viongozi wako mbioni kujinufaisha wenyewe wala si wananchi waliowachagua. Isitoshe, katika shairi la 'Msimu wa Tisa' (uk. 9), mshairi anaangazia msimu wa tisa wa uongozi, huenda ni msimu wa tisa baada ya Kenya kujipatia uhuru mwaka wa 1963. Shairi la 'Mkasa' (uk. 13) huenda linaangazia shambulio la kigaidi lililotekelezwa mjini Nairobi mwaka wa 2007; hii ni kutokana na jumba lililopulizwa la ubalozi wa mwewe. Nalo shairi la 'Kitini' (uk. 18) linaangazia uongozi ambapo viongozi walio mamlakani wanawasahau na kuwapuuza waja waliowapigia kura.

Katika shairi la 'Wenda-wazimu Kongo', watu waliokosa utu kutoka jamii ya Wahutu na Watutsi wanaangaziwa. Mshairi anazungumzia mauaji ya kinyama nchini Kongo yaliyotekelezwa na watu hawa. Anwani 'Mafuta yenye Damu' (uk. 48) inaangazia maafa

yaliyotokana na vita nchini Sudan vilivyozuka kutokana na mzozo wa umiliki wa rasilmali ya mafuta. Shairi la ‘Macho Mekundu’ (uk. 59) linaangazia dhiki inayowapata watoto katika dunia katili. Mshairi anaangazia namna watoto wanashiriki ubakaji, matumizi ya dawa za kulevya, ujambazi na vita wangali wakembe.

Lugha ya mkato haizingatiwi tu katika anwani, pia katika ushairi wenyewe. Kwa mfano, Katika shairi la ‘Magenge Matatu’ (uk. 32). Mshairi anasema:

> Genge la kwanza la mazimwi
> Lilituahidi nchi bila minyororo ya kutojua, maradhi na umaskini
> Tukanengukanenguka viwanjani kwa shangwe na vigelegele;
> Mwongo na nusu wa upepo wa ulafi na ukungu wa ufisadi
> Ukazima mwenge wa utaifa na kuangusha uzalendo mtaroni
> Harufu ya ukabila ikachafua nchi kama uzushi wa kicheche
>
> Genge la pili la mazimwi
> Lilituahidi majira maangavu ya amani, upendo na umoja
> Tukajijeruhi koo kwa kuimba “Juu! Juu! Juu sana!”
> Baada ya miongo miwili viwavi na nzige wakitafuna nchi
> Jamhuri ilishuka katika jahanamu ya moto wa AK 47
> Zao la umaskini unaovuma kama bahari kwenye miamba
>
> Genge la tatu, nusu-mazimwi
> Lilituahidi katiba mpya na dawa kali dhidi ya ufisadi
> Tukaamini wimbo “Yote yawezekana bila Mfalme wa Nzige”
> Baada ya miaka minne ya hila, tamaa na uzingizi ulingoni
> Ahadi iliyomwesamwesa kama nyota ya taifa jipya
> Imemezwa na wingu la ujanja na harufu ya ufisadi

Katika vifungu hivi, mshairi anatupa muhtasari wa misimu mitatu ya uongozi nchini Kenya chini ya viongozi watatu. Huenda misimu hii ni chini ya viongozi wafuatao: Hayati Mzee Jomo Kenyatta, Rais Mstaafu Daniel Toroitich Arap Moi na Rais Mstaafu Emilio Mwai Kibaki, ambao wametawala Kenya tangu mwaka wa 1963 hadi 2007 wakati mtunzi aliandika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Badala ya kutumia lugha nathari kuelezea kila msimu wa uongozi na sifa zake; jambo ambalo litagharimu muda na nafasi, anatoa muhtasari kwa kutumia lugha ya kimafumbo.

Katika shairi hili, katika fungu la kwanza, mshairi anazungumzia msimu wa kwanza ambao ulijawa na ahadi za uongo. Kwa mfano, nchi bila minyororo ya ukoloni lakini baadaye mambo yakawa kinyume; nchi ikaanza kutawaliwa na ufisadi, ulafi na ukabila. Katika fungu la pili anazungumzia msimu wa pili uliotawaliwa na ahadi za kuleta amani, upendo na umoja. Baada ya miongo miwili, ufisadi na unyanyasaji vikachukua usukani. Katika fungu la tatu anazungumzia msimu wa tatu. Viongozi waliahidi katiba mpya na vita vikali dhidi ya ufisadi. Walikashifu uongozi wa awali lakini baada ya miaka minne wimbo ukawa ni uleule wa tamaa, ufisadi, hila na uzinzi.

Lugha hii ya mkato imetumika vilevile katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Kwa mfano, katika shairi la 'Rangi ya Anga' (uk. 10). Mshairi anasema:

> Sikiza sauti ya mzazi
> Ambayo inakuja juu
> Kama wimbi la sumu
> Ikimimina kemikali kali
> Katika akili asubuhi:
>> Usicheke kiholela
>> Kama wewe ni mwanamke!
>> Nyamaza! Futa machozi!
>> Ushindwaye na madogo
>> Kama mavazi yako
>> Ni kamisi na rinda!

Katika kifungu hiki, mshairi anawasilisha mawazo yake katika kifungu kimoja tu. Anazungumzia taasubi ya kiume inayotawala katika jamii huku akiibusha nafasi ya mwanamke katika jamii. Mwanamke anadharauliwa kwa kuonekana kushindwa na madogo huku kijana wa kiume akitarajiwa kuwa shujaa katika jamii. Mshairi ametumia lugha ya mkato katika kifungu hiki ili kunasa makini ya msomaji. Pia, kukuza fikra za msomaji anapowazia ujumbe ambao mtunzi anataka kuupitisha kupitia shairi hilo.

Aidha, kumpatia msomaji motisha ya kuusoma ushairi kwa sababu ya ufupisho wa ujumbe unaopitishwa kwa vifungu vifupi vifupi. Lugha hii pia inanata kutokana na matumizi ya tamathali za usemi kwa wingi. Kwa mfano, matumizi ya tashbihi kama vile: 'ushindwaye na madogo kama mavazi yako ni kamisi na rinda'. Kwa hivyo lugha ya mkato ni muhimu sana katika utunzi wa ushairi huru.

## 2.2 Matumizi ya Lugha ya Kimuziki

Katika mashairi teule, mdundo usiobainika umetumiwa kujenga wizani na kuathiri kasi ya msomaji. Mdundo huu unadhibitiwa na jinsi mawazo yanavyotiririka katika akili ya mtunzi. Kwa hivyo hauzingatii urari wa mizani katika kila mstari wa ushairi. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* shairi la 'Mafuta yenye Damu' (uk. 48). Mshairi anasema:

> Wasio na macho ya kuona ukunguni (silabi 14)
> Wanaona mafuta safi ya bei nafuu (silabi 15)
> Wanaona bidhaa nzuri za Khartoum… (silabi 12)

Katika kifungu hiki, idadi ya silabi inahitilafiana kutoka mstari hadi mwingine, kwa hivyo, muziki haudhibitiwi tu na urari wa mizani. Mapigo maalum yanabainika kutokana na namna amepanga maneno na sauti kwa namna teule ili kuzua mahadhi maalum; jambo ambalo linaathiri toni na wizani wakati wa usomaji. Katika shairi lili hili, kifungu cha pili, wizani na toni imetumika kuathiri hisia za msomaji pia. Kwa mfano, anatumia takriri silabi 'wa' na uradidi wa neno, 'wanaona' mwanzoni mwa kifungu hiki. Matumizi haya yanazua muziki wa aina fulani katika akili ya mtunzi na ya msomaji pia. Muziki huu unaendelezwa katika kifungu cha pili, mshairi anaposema:

> Naona majeruhi, damu na maiti
> Maiti za wakulima mashambani
> Maiti za wachungaji malishoni

Maiti za watoto shuleni
Maiti za vikongwe vijijini…

Kutokana na kifungu hiki, mshairi anatumia anafora na takriri silabi mwishoni mwa kifungu. Marudio ya kirai, ‘maiti za’ na takriri silabi, ‘ni’ yanajenga wizani na toni maalum.

Aidha, mtunzi wa diwani teule ametumia lugha ya kimuziki kupitia usambamba wa mistari. Haya yanadhihirika anapotumia idadi sawa ya mistari katika kila kifungu. Shairi la ‘Tume za Rais’ (uk. 31) ni mfano mwafaka. Mshairi anasema:

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tumnunulie kila mwanatume Hummer
Ichunguze kama njaa inaweza kuua
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Ihariri taarifa ya tume ya rais

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tumjengee kila mwanatume kasri
Ichunguze jina la rais wa Jamhuri
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Imtangazie Rais jina la Rais

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tuitengee nusu ya akiba ya Banki Kuu
Ichunguze kama rais ni rais bila tume za rais
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Imshauri rais kuhusu rais na tume za rais

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tuilipe kwa mkopo kutoka vitanzi vya Breton Woods
Baada ya miaka mitano ya kumandari na kunywa mvinyo
Wamshauri rais namna ya kuficha taarifa za tume za rais
Katika sefu za vyumba vya ndani vya mijengo ya rais

Katika shairi hili, mtunzi ametumia mistari mitano katika kila kifungu hivyo kudumisha wizani. Isitoshe, mstari wa kwanza katika kila kifungu umerudiwa. Aidha, mstari wa tatu katika kifungu cha 1-3 umerudiwa. Hali kadhalika, usambamba wa maneno unajitokeza

mwishoni mwa kila mstari wa nne na wa tano ambapo neno, ‘rais’ limetumika mwishoni. Matumizi haya yanadumisha mahadhi ya kimuziki mwanzoni mwa kila mstari, katika mstari wa tatu kutoka kifungu cha 1-3 na mwishoni mwa kila mstari wa nne na wa tano.

Isitoshe, kutokana na ufahamu ya kwamba Kiswahili ni lugha ya Kibantu, mdundo wa mashairi teule unalingana na mdundo wa nyimbo za Kibantu ambazo zipo chini ya utanzu wa ushairi simulizi, kwa hivyo ushairi huu unaweza imbika. Kwa mfano, kuna ulinganifu wa kimuundo katika wimbo wa Musa Sukuma (Equator Sound Band) kama ulivyonukuliwa na King’ei na Kisovi (2005: 132) na shairi la ‘Wanda’ katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 35).

**Musa Sukuma (Equator Sound Band)**

“Musa nimevumilia sana
Kupigwapigwa kama mimi punda
Na sura yangu imeharibika
Taabu…taabu…taabu…

Kweli Musa uliponioa
Sura yangu_________
Haikuwa na alama
Hata moja
Nilikuwa na afya nzuri
Nilinona kama ngoima
Ya Kirige

Musa kweli tafadhali ndugu
Tafuta bibi atakayeweza
Kuvumilia hizo tabia zako
Ukinywa pombe
Waninywea yeye
O kinywa munyeke
Wamnywea yeye
Taabu tabu…taabu…taabu”

**Rangi ya Anga (uk. 35)**

“Kama si makali ya panga
Kwa ujeuri na ukatili
Kuhujumu mashina ya miti,
Kingo za mito na vijito
Miinuko ya milima
Na miteremko ya mabonde
Bado yangekuwa na ng’ao
Za kulinda afya ya udongo
Na ile ya wakazi wake lukuki
Dhidi ya hasira inayotiririka
Ya mgeni mwekundu

Isingekuwa kazi ya kwato
Na ushirikiano wa ndimi na taya
Kugofua kinga za udongo
Hii damu ya ardhi adimu
Leo isingekuwa ikitiririka
Wala mwili wake azizi
Kuwa na majeraha mabichi”

Kutokana na mafungu haya, kama vile ridhimu ilivyo muhimu katika nyimbo za Kibantu, vilevile, imechukua nafasi kubwa katika diwani teule. Zaidi ya hayo, hubadilika kutoka

ushairi mmoja hadi mwingine kutegemea ujumbe unaowasilishwa na lugha itumikayo. Ridhimu katika shairi hili si taratibu yaani haipangwi kwa njia maalumu kama ilivyo katika ushairi wa kimapokeo. Aidha, haidhihirishwi kwa kuwepo kwa vina, viwe vya kati au vya mwisho badala yake mapigo yake yana mtiririko maalum wa mawazo ya mwandishi yanayojenga ridhimu hiyo. Katika wimbo, 'Musa Sukuma', silabi za mwisho hazilingani (na, nda, ka, bu…). Haya pia yanadhihirika katika shairi la 'Wanda' katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 35) ambapo silabi za mwisho hazilingani (nga, li, ti, to, ma, nde, o…) lakini kuna mapigo maalumu yanayotokea kimuziki na ambayo yanadhihirisha kiwango cha juu cha ubunifu wa mtunzi. Hali kadhalika, nyimbo za Kibantu hugawika katika mafungu. Katika wimbo tulioangazia, mafungu haya yana idadi tofauti ya mistari (4, 7 na 8); jambo ambalo linadhihirika pia katika shairi la 'Wanda' katika *Rangi ya Anga* (11 na 7). Kwa hivyo, lugha ya kimuziki inaweza jengeka bila kuzingatia urari wa mistari katika mafungu ya maneno. Isitoshe, lugha hii ya kimuziki huathiri hisia za msomaji kwa urahisi kuliko matumizi ya lugha katika hali ya kawaida.

Suala hili la lugha ya kimuziki katika mashairi linatiliwa mkazo na Kyalo Wamitila katika utangulizi wa Kezilahabi (2008: ii), anaposema kwamba msomaji anapoyasoma mashairi ya Euphrase Kezilahabi anahisi kama anausikiliza wimbo au muziki fulani. Aidha, muziki unaopigwa na ala ya jadi, 'zeze' unamweka msomaji katika muktadha wa Kiafrika anaoweza kujitambulisha nao; muziki anaoweza kuutambua na kuuimba.

**2.3 Muundo wa Ushairi unaathiri Upokezi wa Ujumbe.**

Katika sifa iliyotangulia ya muundo katika diwani teule, imebainika wazi ya kwamba lugha ya kimuziki humwathiri msomaji kwa kutumia wizani na sauti. Athari hizi

hutokana na kuwepo kwa mpangilio unaojitokeza kwa kadri mshairi anavyounda kazi yake. Mtunzi wa diwani teule ameuwasilisha ushairi kwa namna mbalimbali; jambo ambalo linaathiri hisia, kasi ya usomaji, toni, sauti na ufasiri wa ujumbe. Mpangilio huu husawiri fikra za mtunzi ambazo zinadhihirika kupitia uandishi. Mpangilio wa mafungu, mistari, maneno na sauti humwathiri msomaji kwa pakubwa. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Rangi ya Anga' (uk. 8). Mshairi anasema:

> Sikiza hiyo sauti
> Ulimi ukitoa kauli
> Kama upanga mkali
> Ukikata mmea mchanga:
>
> > Wewe sasa ni mtu mzima
> > Mshale wa mizani ya miaka
> > Unaonyesha miaka kumi na minne,
> > Mbona usiolewe na Mzee Malimali
> > Kusudi mahari ya ng'ombe na mbuzi
> > Ituzimie moto wa umaskini
> > Kama wingu kuu la masika
> > Likizima ukame nyikani?...

Katika kifungu hiki, mpangilio wa vifungu vyote unaathiri toni na sauti ya msomaji. Mshairi anatanguliza kwa kuonyesha kauli za msimulizi kisha anataja maneno yaliyosemwa na mnenaji ambaye tunakisia ni mzazi wa kiume akimshurutisha bintiye kuolewa na mzee kusudi wapate mahari waepuke umaskini. Mpangilio wa mistari katika sehemu ya kwanza na ya pili unamlazimu msomaji abadili sauti ili kuonyesha kwamba ni kauli za watu wawili tofauti. Msomaji atatumia toni ya makaripio katika sehemu ya pili, hivyo atakuwa ameufasiri ujumbe ipasavyo. Kwa mfano, katika shairi la 'Rangi ya Anga' (uk. 14). Mshairi anasema:

> …Banati alipotimuliwa, alitimuka
> Alipotimuka, aliteguka
> Alipoteguka
>
> a

k
a
a
n
g
u
k
a
!...

Katika kifungu hiki, mshairi anaonyesha mfululizo wa matukio katika maisha ya banati baada ya kufukuzwa shuleni kutokana na ujauzito. Kupitia mpangilio huu wa mistari na sauti, kasi ya usomaji inaathirika. Matumizi ya marudio ya vitenzi yanamfanya msomaji asome akitua huku akisisitiza ujumbe unaojitokeza. Isitoshe, msomaji atakatakata sauti anaposoma kitenzi' akaanguka'. Huku kuzipanga sauti kutoka juu hadi chini kunaleta hisia za huzuni kutokana na taswira inayojengeka katika akili ya msomaji.

Katika shairi la 'Wanda' (uk. 28), kifungu cha kwanza na cha pili, mshairi anasema:

Joto
Linapeperusha bendera
Linatawala kwa maringo
Na kiburi
Linanyanyasa tosi
Na macho
Harara inachokoza kwapa
Na kukereketa migongo

Tazama!
Tazama mayowe kimya
Yakiwayawaya angani
Na kwa ukaidi wa alasiri
Kutisha majani na maua
Na kubabaisha mijusi na nyuki…

Kutokana na vifungu hivi, mshairi anaangazia athari za joto kwa viumbe na mimea. Kila kifungu kinaanzia kwa neno moja ambalo athari zake zinadhihirika katika kifungu

kizima. Jambo hili linaathiri sauti na toni ya msomaji. Shairi hili linanasa makini ya msomaji kutokana na mpangilio wa maneno na mistari. Maneno, 'joto' na 'tazama' yanampa msomaji shauku ya kusoma shairi hili huku akidhihirisha machungu yanayotokana na uharibifu wa mazingira ambao unaleta kiwango cha juu cha joto. Kiwango hiki kimeleta hasara kubwa kwa viumbe wasio na hatia.

Katika shairi la 'Wanda' (uk. 33), mshairi anaonyesha hali ya kukata tamaa kutokana na uharibifu wa mazingira uliosababishwa na binadamu mwenyewe. Aanasema:

> …Ole wangu!
> Moyoni
> Napekechwa na uchungu:
> Wakulima
> Wameua miangati,
> Wagemaji
> Wamechinja mikoma,
> Wasonga-mizinga
> Wameangamiza mianjate;
> Vizazi vya mijunju
> Migunga
> Mibarao
> Na mitanda-mboo
> Vimetumbukizwa kaburini;
> Ngao ya maumbile
> Imeingia dosari
> Sasa dhoruba yenye kiburi
> Imepata fursa mwafaka
> Kuhasiri ardhi kwa hasira…

Katika kifungu hiki, mshairi anawataja waliohusika katika uharibifu huu kupitia mpangilio maalum wa maneno. Athari ya kimazingira haimwathiri tu mwandishi bali msomaji pia. Kuangamizwa kwa miti asili kama vile mitanda-mboo, mianjate, mikoma na mingineyo ni jambo ambalo linaibusha hisia za uchungu. Aidha, msomaji anapousoma ushairi huu atausoma kwa mwendo wa utaratibu na msisitizo kutokana na takriri sauti,

‘wa’ iliyotumika mwanzoni mwa mistari kadhaa. Isitoshe, mpangilio wa maneno unaoambatishwa na matumizi ya viakifishi, unadhibiti kasi ya msomaji. Sentensi fupi zinasomwa kwa mwendo wa kasi kisha mtuo.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, ushairi tulioangazia awali wa ‘Mafuta yenye Damu’, mtunzi ametumia anafora mwanzoni kwa kurudia kirai, ‘Maiti za’. Maneno haya yanazua hisia za hofu, uchungu na huzuni miongoni mwa wasomaji. Isitoshe, yanampa msomaji kutafakari zaidi kuhusu vitendo vya kikatili vilivyotekelezwa na wenyeji wa Sudan kutokana na mzozo wa mafuta. Marudio haya yanaufanya ujumbe ugande katika akili ya msomaji.

**2.4 Muundo wa Ushairi huathiriwa na Vipengele mbalimbali.**

Muundo wa ushairi teule si tengemano ila hubadilika badilika kutegemea dhamira, maudhui, matumizi ya lugha, wakati, wahusika na upekee wa mtunzi katika kuwasilisha kazi yake. Kulingana na Mazrui (1988: viii), ulimwengu hubadilika na hivyo utamaduni wa ushairi lazima ubadilike. Naye Mwai (1988: 5), anadhihirisha hayo anaposema kwamba fasihi hubadilika katika umbo na maudhui kwa hivyo ushairi wa Kiswahili sharti uruhusu mabadiliko yanayotokea katika ushairi huru. Maoni haya yana mashiko kwa sababu tangu kuanzishwa kwa ushairi huru, mabadiliko kadhaa ya kimuundo yamedhihirika. Mabadiliko haya hutokea katika utunzi wa mshairi binafsi au baina ya mshairi mmoja na mwingine. Mtunzi Kithaka wa Mberia ametumia miundo anuwai katika ushairi wake wa awali wa *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001); jambo ambalo limedhihirishwa pia katika diwani teule. Kusudi kuu ni kudumisha wizani maalum. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Tume za Rais’ (uk. 31), mtunzi

amezingatia mistari mitano katika kila kifungu. Katika shairi linalofuatia la ‘Magenge Matatu’ (uk. 32), mshairi ametumia mistari sita katika kila kifungu.

Idadi tofauti ya mistari inadhihirika katika ushairi mmoja. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mashairi mengi yana idadi tofauti ya mistari katika kila kifungu. Katika shairi la ‘Minyororo ya Njaa’ (uk. 1), kifungu cha kwanza kina mistari 4, kisha 5, 5, 6, 5, 5, 3, 4 na 4 mtawalia.

Mashairi mengine yana kifungu kimoja tu. Mawazo yote ya mwandishi yanaangaziwa tu katika kifungu kimoja. Kwa mfano, shairi la ‘Msimu Mwingine wa Wasaliti’ (uk. 12). Mshairi anasema:

> Vitimbakwira watarudi karibuni kutoka karamu haramu
> Utaziona barakoa za tabasamu kwenye nyuso zao
> Watakuja kutugawia peremende zenye sumu ya akili
> Watalewesha watu kwa pombe kutoka vibuyu vya maneno
> Wataahidi kesho yenye mapipa ya maziwa na mitungi ya asali
> Nasi, tukiongozwa na ramani ya tumbo na dira ya ubinafsi
> Tutapanga milolongo katika mvua na matope ya Disemba
> Kukaribisha labda msimu mwingine wa wasaliti.

Mtunzi anaendeleza na kuhitimisha mawazo katika shairi lililotangulia la ‘Msimu wa Tisa’ (uk. 9), kwa hivyo kupelekea kifungu chenyewe kuwa kifupi. Matumizi ya kifungu kimoja yanaonyesha mtiririko wa mawazo katika akili ya mshairi.

Vilevile, uruwazaji unajitokeza katika mpangilio wa mistari hasa wakati mtunzi anabainisha usemi wa mhusika mwingine. Kwa mfano, katika shairi la ‘Kitini’ (uk. 18) kifungu cha kwanza. Anasema:

Tulipoguna kwa maumivu makali kwenye misuli
Juhudi za kizalendo zilipopamba moto yakini
Tulipotokwa na michirizi ya jasho tukisaka utu
Tulipopambana na dhiki ya giza la miongo miwili
Waziri aliyeridhika, alitushauri kwa ulimi wa kinaya
    Juhudi zenu zenye nia ya kung'oa chama
    Ni sawa na ubwege wa kutaka kukata mtini
    Kwa wembe ulionyolea tena na tena!...

Katika kifungu hiki, mistari ambayo imeegemea kulia inaonyesha kauli ya waziri ambaye anawabeza wananchi ambao wananga'ng'ania kuuondoa uongozi dhalimu. Muundo huu umeshamiri katika diwani ya *Rangi ya Anga* hasa katika shairi la 'Rangi ya Anga' (uk. 7). Mshairi anasema:

Kwa macho dadisi
Tumeona mikwaruzo na kovu
Katika mikono na shingo
Na mashavu na vipaji
Kama kwamba chui aliyeudhika
Amepigana vita vya kulipiza kisasi
Dhidi ya binadamu kizimbani;
Tulipomulika kwa uchunguzi
Jawabu likatugonga masikioni
Kama kikawe cha manati:
    Mume amemwadhibu mkewe-
    Wanawake ni kama watoto
    Usipowarudi hupoteza njia!
Nyuso zetu zilipoingia kunyanzi
Kwa kutoridhika nyoyo
Sauti "ilifafanua"
    Mume ana haki thabiti
    Anaruhusiwa kumwadhibu mkewe-
    Si alilipa mahari!...

Katika vifungu hivi, ili kuwasilisha maudhui ya dhuluma ya kijinsia katika jamii, mtunzi ametumia usemi halisi wa msemaji hasa wa jinsia ya kiume. Hii ni njia moja ya kuvuta makini ya msomaji na kusaidia katika uelewekaji wa ujumbe. Mtunzi ameonyesha namna

mwanaume ana kibali cha kumpiga mkewe kwa sababu amelipa mahari na asipomwadhibu atapoteza njia.

Hali kadhalika, mshairi ametumia muundo wa masimulizi katika mashairi mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe wake kwa namna ya kuvutia. Masimulizi haya pia yanaangaziwa na Kyalo Wamitila katika utangulizi wa ushairi wa *Dhifa* (2008: ii), anaposema kwamba ushairi wake umehusisha mbinu za kifasihi simulizi kama utambaji na uganaji katika mashairi mengi na kuonyesha kuwa mashairi ya kisimulizi hayapatikani tu katika tendi na tenzi bali pia katika mashairi mafupi. Aidha, usimulizi pia unadhihirishwa katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 49). Mshairi anasema:

> Kwa kunyemelea
> Lilikuja zimwi jeupe
> Kwanza kwenye upwa
> Ambapo upepo
> Hupuliza manukato ya chumvi
> Kwenye pua za wakazi,
> Nyanda ambako
> Mipeketo na mikungu
> Na mianzi na mikoko
> Na mikanju na mivinje
> Huishi kwa Amani
> Pamoja na korongo
> Na kunguru na membe…

Katika kifungu hiki, kiambishi cha wakati uliopita (li) kimetumika katika masimulizi kuelezea mjo wa Waarabu, wamisheni na wakoloni katika nchi ya Kenya. Mshairi ametumia mbinu rejeshi kwa sababu anazungumzia matukio ambayo yalitendeka awali, hivyo kumkumbusha msomaji kuhusu historia ya Kenya.

Lakini wakati mshairi anatusimulia kuhusu athari za kimazingira katika shairi la 'Wanda' (uk. 28) anatumia wakati uliopo. Anasema:

> Joto
> Linapeperusha bendera
> Linatawala kwa maringo
> Na kiburi,
> Linanyanyasa tosi
> Na macho,
> Harara inachokoza kwapa
> Na kukereketa migongo…

Katika kifungu hiki, mshairi anatumia hasa wakati uliopo (na). Anataka kudhihirisha ya kwamba athari hizi bado zipo katika jamii. Hii ni njia mojawapo ya kumrejesha msomaji katika matukio halisi.

Matumizi ya wakati uliopo katika masimulizi pia yanadhihirika katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Mkasa' (uk. 13). Mshairi anasema:

> Kama kawaida, ndege wanaimba kwa uchangamfu
> Asubuhi inachanua, miali inapamba anga na ardhi
> Wanajiji wanamiminika jijini kutafuta riziki halali
> Pilkapilka zinahinikiza ndani nan je ya mijengo
> Mdundo wa maisha unaendelea kwa kasi ya dawamu…

Katika kifungu hiki, mshairi anasimulia utaratibu wa matukio wakati wa shambulizi la kigaidi nchini Kenya mnamo mwaka wa 2007.

Isitoshe, mtunzi anaunda sentensi zake kwa namna teule huku akilenga hadhira teule/lengwa. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk.28). Mshairi anasema:

> Jua!
> Ewe jua!
> Jua la adhuhuri,
> Mbona kwa ghadhabu
> Unaadhibu chembe za udongo

Kwa halijoto kama ya tanuri?

Jua!
Ewe jua!
Jua la wanda za mikwaju,
Mimea na samaki
Ndege na wadudu
Na wanyama na mito
Walikutenda ovu gani
Kukuchochea ulipishe kisasi
Kwa ghadhabu pujufu?...

Katika vifungu hivi, mshairi anazungumzia nafsi ya pili (ewe) ili kunasa fikra na hisia za msomaji. Anazungumza na anachokiashiria (jua) kama kipo katika mazingira yake. Vilevile, katika ukurasa unaofuatia, mshairi anasema yafuatayo:

…Ewe mkazi wa wanda
Wewe
Adui wa maumbile,
Wewe
Hasidi wa wewe mwenyewe,
Wewe
Ambaye umetia kitanzi
Kwenye shingo ya mazingira
Shingo yako mwenyewe
Shingo za wajukuu na vitukuu…

Kutokana na kifungu hiki, mshairi anaelekeza lawama ya uharibifu wa mazingira kwa nafsi ya pili. Anasisitiza ujumbe kwa kurudia nafsi huru, 'wewe'. Kwa mujibu wa Wordsworth (1797: 52), shairi linafaa kuwasilisha hisia na matukio halisi ya binadamu. Kutokana na ushairi huu, hisia za mtunzi zinadhihirika na ndizo zinazompelekea kupanga mawazo yake jinsi alivyoyapanga ili kuonyesha makali ya uharibifu wa mazingira katika jamii huku akiwakaripia waliohusika katika uharibifu huo.

Vilevile, mtunzi ana uhuru wa kujinasibisha na ulimwengu halisi katika kuwasilisha mawazo yake; jambo ambalo linaathiri miundo ya kisintaksia ya ushairi. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Mafuta yenye Damu' (uk. 48). Mshairi anasema:

…Naona titimko la wakazi wa Kusini
Wakimiminika Kenya na Ethiopia
Wakikwepa dhamira imara za risasi
Wakitoroka mauti kutoka Antonov
Huku vifaa vya kuchimba mafuta
Vikivamia maganjo yanayonuka damu

Usiniuzie petroli ya Kusini mwa Sudan
Sitaendesha gari kwa damu ya watu,
Picha za maiti za watoto wachanga
Zitanitumbukiza hospitali ya Mathare…

Katika vifungu hivi,mshairi anajiweka katika mazingira ya wahasiriwa wa vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi ya Sudan. Kwa mfano, anasema kuwa anaona titimko la wakazi wa Kusini, wakimiminika Kenya na Ethiopia.

Miundo ya kisintaksia pia huathiriwa na madhumuni ya mshairi katika kuwasilisha kazi yake. Mathalan, iwapo mshairi anataka kubashiri yatakayotendeka baadaye, itabidi atumie kiambishi cha wakati ujao. Kwa mfano, katika shairi la 'Msimu Mwingine wa Wasaliti', (uk. 12). Mshairi anasema:'vitimbakwira watarudi karibuni kutoka karamu haramu…Watakuja kutugawia peremende zenye sumu ya akili…'. Mshairi anabashiri yatakayotendeka baadaye iwapo viongozi wale wale wasaliti watashika usukani. Anawachora wakitoa ahadi za uongo kuwashawishi watawaliwa kuwapigia kura huku wakiukaribisha msimu mwingine wa wasaliti. Pia, iwapo mshairi anataka kusisitiza au kuweka kumbukumbu katika akili ya msomaji, atatumia marudio au takriri katika ushairi

wake. Kwa hivyo, anateua maneno katika sentensi kimaksudi. Haya yanadhihirika katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Asubuhi Hasiri’, kifungu cha mwisho (uk. 86). Mshairi anasema:

…Tusingekuwa na macho ya bundi au popo
Tungeona wabakaji na majambazi sugu
Tungeona Sankor na miwani yake ya giza
Tungeona mbegu ya machozi mekundu
Ambayo tumepanda kwa uchangamfu
Kwa siasa ya waropokwaji wa kulipwa
Na mfumo wa uchumi wa “kila mtu kivyake”

Uteuzi wa neno, ‘tungeona’ umetumika kimaksudi ili kusisitiza kwamba sisi kama wananchi tunafaa kulaumiwa kwa kutoshiriki kikamilifu katika mradi wa kuwaauni watoto wa mitaani ambao sasa wameishia kuwa wabakaji, majambazi sugu na watumizi wa dawa za kulevya. Mtunzi ametumia mpangilio huu katika kutamatisha ushairi wake ili msomaji aweke kumbukumbu ya anachozungumzia mshairi. Ni dhahiri ya kwamba uteuzi huu haujatumika katika vifungu vilivyotangulia lakini mshairi amehakikisha kwamba ameteua maneno yake kimaksudi kutegemea maudhui anayowasilisha. Maneno yaliyotumika kuunda sentensi na aya yanaangazia maudhui maalum. Mshairi anasema:

Macho yao ya miaka michache
Yamekamatwa na unyevunyevu,
Kwenye pua isiyojua manukato
Kumegandama makopo machafu,
Mvuke hatari wa gundi ya viatu
Unateka nyara mapafu na akili

Huku wamefanana na matambara
Hawa waliotupwa kwenye jalala,
Wanaomba kwa ishara ya mikono
Na kwa sauti inayodondoka ukiwa,
Wadogo wanamwandama mpitaji
Sawa na ‘ndamata’ au ‘nconge’ nguoni

Kwenye mapipa ya masalio ya vyakula
Wanateta na kutukanana na chungu,
Karibu na malundo na vitupwa vya jiji
Wakasirisha kunguru na kongoti,
Karibu na mijengo ya biashara za nyama
Wanashindana na mbwa, panya na nzi,
Wakiwania mabaki ya nyama-choma
Na mabaki ya ugali, viazi na bofulo…

Katika vifungu hivi, mtunzi anazungumzia dhiki wanayokumbana nayo watoto wa mitaani. Katika kifungu cha kwanza, mtunzi anaonyesha namna watoto wa mitaani wanashiriki vileo. Katika kifungu cha pili, watoto hawa wanakosa mahitaji ya kimsingi kama vile mavazi. Pia wanakuwa waombaji mitaani. Katika kifungu cha tatu, mtunzi anazungumzia vile watoto hawa wanakula makombo kutoka malundiko ya vitupwa vya jiji kutokana na ukosefu wa lishe.

Madhumuni ya mshairi huathiri namna anavyowasilisha kazi yake kimuundo. Kwa mfano, anaweza kuzua anwani ambayo inaathiri muundo wa ushairi wenyewe. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Magenge Matatu’ (uk. 32), mshairi anasema:

Genge la kwanza la mazimwi
Lilituahidi nchi bila minyororo ya kutojua, maradhi na umaskini
Tukanenguka nenguka viwanjani kwa shangwe na vigelegele;
Mwongo na nusu wa upepo wa ulafi na ukungu wa ufisadi
Ukazima mwenge wa utaifa na kuangusha uzalendo mtaroni
Harufu ya ukabila ikachafua nchi kama uzushi wa kicheche

Genge la pili la mazimwi
Lilituahidi majira maangavu ya Amani, upendo na umoja
Tukajijeruhi koo kwa kuimba “Juu! Juu! Juu sana!”
Baada ya miongo miwili viwavi na nzige wakitafuna nchi
Jamhuri ilishuka katika jahanamu ya moto wa AK47
Zao la umaskini unaovuma kama bahari kwenye miamba

Genge la tatu, nusu-mazimwi
Lilituahidi katiba mpya na dawa kali dhidi ya ufisadi
Tukaamini wimbo “Yote yawezekana bila Mfalme wa Nzige”

Baada ya miaka minne ya hila, tamaa na uzingizi ulingoni
Ahadi iliyomwesamwesa kama nyota ya taifa jipya
Imemezwa na wingu la ujanja na harufu ya ufisadi

Katika shairi hili, mshairi amegawanya mistari yake katika mafungu matatu. Katika kifungu cha kwanza, anazungumzia genge la kwanza la mazimwi. Katika kifungu cha pili, anazungumzia genge la pili la mazimwi na katika kifungu cha tatu anazungumzia genge la tatu la nusu-mazimwi. Mshairi amesawiri ujumbe ulio katika anwani katika mafungu matatu. Usambamba huu unampatia msomi nafasi ya kuuelewa ujumbe kwa urahisi. Vilevile, ishara hii ya 'Magenge Matatu' inaathiri hisia za msomaji na kumfanya atafakari zaidi kuhusu hali halisi katika jamii inayowakilishwa na ishara hiyo. Kwa hivyo, maneno hupangwa katika mistari kutegemea mtiririko wa mawazo katika akili ya msomaji.

**2.5 Utumiaji Michoro kuwasilisha Ujumbe maalum**

Mtunzi Kithaka wa Mberia anafahamika katika historia ya uandishi wa ushairi huru kwa matumizi yake ya michoro ya kimaksudi. Katika ushairi wake wa awali katika diwani za *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001), alitumia ishara ya michoro kuwasilisha maudhui maalum. Crystal na Davy (1969) wanasema kwamba matumizi ya sauti na michoro yenye maumbo maalum hudhihirisha ujumi, uhalisia na ufafanuzi zaidi kuhusu ujumbe unaopitishwa na mwandishi katika kazi ya fasihi.

Aidha, Pierce (1977: 228) alithibitisha matumizi ya ishara alipoangazia nadharia ya ishara katika kazi ya fasihi. Alisema kwamba ishara huonyesha uhusiano uliopo kati ya kiashiria na kiashiriwa. Alibainisha vitengo vitatu vya ishara, mathalan, ishara halisi ambazo zinaweza kuwa ni sifa, kanuni, desturi au tabia za kitu chenyewe. Pia, ishara

ambazo zinahusishwa na viashiriwa. Aidha, ni uhusiano uliopo kati ya kiashiria na kiashiriwa. Katika kitengo cha pili, alibainisha ishara katika vikundi vitatu: picha/mchoro, kielezo cha sifa au tabia na mfumo wa alama zinazowakilisha kundi fulani la mawazo. Maoni haya yanaungwa mkono na Hoopes (1991) anayesema kwamba ishara za picha, kielezo cha sifa na mfumo wa alama zinazowakilisha kundi fulani la mawazo huonyesha namna ishara zinazoonekana zinavyosheheni ujumbe wa kidhahania. Aidha, ishara hizi humsaidia mtafiti kutafakari zaidi kuhusu ujumbe unaowakilishwa na ishara hizo.

Katika sehemu hii tumeangazia ishara za picha katika diwani teule. Kithaka wa Mberia ana mazoea ya kutumia ishara za picha katika utunzi wake kuchora taswira ya jambo au kitu fulani. Kwa mfano, katika diwani ya *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001). Matumizi haya ya michoro ya kimaksudi yanadhihirishwa pia katika diwani ya *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Michoro hii imetumiwa kumpa msomaji taswira na ufahamu wa jambo au mada inayoangaziwa. Kwa mfano, katika *Msimu wa Tisa*, shairi la "Muungano wa Afrika", (uk. 90). Mshairi anasema:

"Tumezaa,
tukate kiunga mwana kwa makini
Tumlee,
tumtunze kwa mikono mikunjufu
Tumlishe,
tumpe chakula chenye lishe bora
Tumgange,
tumtibu akumbwapo na ndwele
Tumlinde,
tumkinge maadui wasimnyonge
Tumjenge,
tumwimarishe kano na misuli
Atuafu,

atufungua minyororo na unyonge
Atuinua,
atukweza hadi kilima cha shibe?"

Katika shairi hili, mshairi anaangazia 'Muungano wa Bara la Afrika' na kuandika shairi lake akitumia umbo la fumbato la viganja linaloonyesha umoja. Ishara hii inakaribiana kiumbo na ile ya 'Mwashi Mahiri' lakini inaashiria jambo tofauti. Ishara yenyewe inaakisi hisia za upendo, umoja na uzalendo wa Waafrika. Isitoshe, inaonyesha fikra za mtunzi kuhusu Muungano wa Afrika ambao unafaa kudumishwa ili kuvuna matunda bora.

Michoro ya kimaksudi pia imetumiwa kuonyesha kasi, hisia na msisitizo wa ujumbe. Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Rangi ya Anga' (uk. 14), mshairi anasema:

…Banati alipotimuliwa, alitimuka
Alipotimuka, aliteguka
Alipoteguka

a
k
a
a
n
g
u
k
a
!...

Katika kifungu hiki, mshairi ametuchorea taswira ya mkasa uliomfika kijana msichana aliyepachikwa mimba na mwenzake wa kiume wangali shuleni. Baada ya kufukuzwa shuleni, maisha yake yalikuwa ya dhiki; asiye na mbele wala nyuma; akatumbukia katika shimo la maangamizi. Mshairi anapanga sauti katika neno, 'akaanguka' kutoka juu hadi

chini ili kuashiria maangamizi. Isitoshe, anaonyesha kasi ya tukio hilo ambalo huathiriwa na mvuto wa ardhi. Msisitizo wa kitendo cha kuanguka unajitokeza katika kule kutenganisha sauti katika neno hilo. Mchoro huu unaibua hisia za uchungu na huzuni wakati msomaji anapotafakari yaliyomfika banati huyu. Vilevile, unaonyesha hisia za mshairi kuhusu dhuluma anayopitia mtoto wa kike katika jamii. Mchoro ufuatao unaakisi haya:

Michoro hii imetumiwa kuteka nadhari ya msomaji na kumpa nafasi ya kutafakari zaidi kuhusu ujumbe unaowasilishwa na mshairi. Ni njia moja ya kujiepusha na miundo iliyozoelewa ya beti, hivyo kuondoa uchovu wa usomaji. Isitoshe, michoro hii hujenga ruwaza ya ushairi kwa kuupa ushairi picha ya pekee na kuonyesha kiwango cha juu cha ubunifu wa mwandishi. Naunga mkono maoni ya Indede (2008: 12) anaposema kwamba ilhamu ya Kithaka wa Mberia ya kuwasilisha mawazo ya ndani kwa matumizi ya picha halisi ili kudhihirisha uwazi wa ayatamkayo, si tu maono mapya katika uvumbuzi wa usanii kisayansi bali pia uvumbuzi wa falsafa mpya ya kisanaa. Freeman (2007) anasema kwamba athari ya ishara za picha katika ushairi ni kuzua falsafa, hisia na picha au taswira katika lugha ambazo huwezesha akili ya mshairi au msomi kukabiliana nazo kama matukio halisi.

## 2.6 Matumizi ya Mistari yenye urefu tofauti

Sifa moja inayodhihirika katika diwani zote za ushairi wa Kithaka wa Mberia ni urefu usiolingana wa mistari. Mashairi mengi katika *Msimu wa Tisa* yamezingatia mistari mirefu ikilinganishwa na yale yaliyo katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Kwa nini mshairi akatumia muundo huu? Je, muundo huu wa mistari unazingatia kanuni zozote? Je, urefu

wa mistari unabainisha wizani? Kusudi kuu la mshairi ni kujenga ridhimu ambayo hutofautiana kutoka ushairi mmoja hadi mwingine. Ridhimu hii inatokana na namna mawazo ya mshairi yanavyotiririka katika akili yake na namna muziki unavyojengeka. Kwa hivyo, urefu sawa wa mistari si kigezo pekee cha kubainisha ridhimu.

Mawazo katika akili ya Kithaka wa Mberia yanadhibiti urefu wa mistari katika utunzi wake. Kwa mfano, katika ushairi wa diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Mwashi' (uk. 40). Mshairi anasema:

| | |
|---|---|
| Mwalimu, kuwemo ndani ya udongo | (silabi 12) |
| Hakutazuia kuinuka kutoka pumziko | (silabi 16) |
| Na kupanda jukwaa la maramar na mvuli | (silabi 14) |
| Kupokea hili koja la mawaridi adimu | (silabi 16) |
| Kutoka kitalu cha maua moyoni mwangu | (silabi 15) |
| | |
| Mwalimu, mikono azizi ya wazazi | (silabi 13) |
| Ilitumia vyema udongo wa malezi | (silabi 14) |
| Kufinyangia mwafrika mheshimika | (silabi 13) |
| Mzalendo mwenye ndoto angavu | (silabi 11) |
| Kiongozi mwongoza kwa vitendo… | (silabi 11) |

Katika vifungu hivi, urefu wa mistari unatofautiana kutoka kifungu hadi kingine. Haya yanadhihirika kupitia idadi ya silabi katika kila mstari katika kila kifungu. Idadi ya silabi inatofautiana kutoka mstari mmoja hadi mwingine katika kifungu kimoja. Jambo hili linaashiria mtiririko wa mawazo katika akili ya mtunzi. Kwa hivyo, mshairi  anawasilisha ujumbe kwa njia huru bila kufungwa na kanuni zozote zile.

Jambo lingine ambalo linadhihirika katika ushairi huu ni kwamba urefu huu unakaribiana sio tu katika vifungu hivi viwili bali pia katika vifungu vyote. Kwa hivyo, kuwa na umbo

maalum. Hii ni njia moja ya kudumisha wizani katika shairi zima, hivyo kuufanya ushairi uweze kuimbika.

Urefu tofauti wa mistari unaweza tokea kimaksudi kufuata utaratibu fulani. Kwa mfano, katika shairi la 'Tume za Rais' (uk. 31). Mshairi anasema:

| | |
|---|---|
| Napendekeza tuunde tume ya rais | (silabi 12) |
| Tumnunulie kila mwanatume 'Hummer' | (silabi 14) |
| Ichunguze kama njaa inaweza kuua | (silabi 15) |
| Kisha tuunde tume nyingine ya rais | (silabi 12) |
| Ihariri taarifa ya tume ya rais | (silabi 13) |
| | |
| Napendekeza tuunde tume ya rais | (silabi 12) |
| Tumjengee kila mwanatume kasri | (silabi 13) |
| Ichunguze jina la Rais wa Jamhuri | (silabi 12) |
| Kisha tuunde tume nyingine ya rais | (silabi 12) |
| Imtangazie Rais jina la Rais | (silabi 11) |
| | |
| Napendekeza tuunde tume ya rais | (silabi 12) |
| Tuitengee nusu ya akiba ya Banki Kuu | (silabi 16) |
| Ichunguze kama rais ni rais bila tume za rais | (silabi 15) |
| Kisha tuunde tume nyingine ya rais | (silabi 12) |
| Imshauri rais kuhusu rais na tume za rais | (silabi 15) |

Kutokana na vifungu hivi, urefu wa mstari wa kwanza na wa nne katika kila kifungu ni sawa. Usawa huu unatokana na uradidi unaojitokeza, hivyo kudumisha mahadhi mwanzoni mwa kila kifungu na katika mstari wa nne katika vifungu vyote vitatu. Usambamba huu wa mistari umetumika kimaksudi ili kuunda muundo mahususi wa ushairi huo.

Mshairi pia anaweza kutumia mistari mifupi na mirefu kwa zamu, kama ilivyo katika shairi la 'Muungano wa Mwafrika' (uk.90). Mshairi anasema:

Tumezaa, (silabi 4)
tukate kiunga mwana kwa makini (silabi 12)
Tumlee, (silabi 4)
tumtunze kwa mikono mikunjufu (silabi 12)
Tumlishe, (silabi 4)
tumpe chakula chenye lishe bora (silabi 12)
Tumgange, (silabi 4)
tumtibu akumbwapo na ndwele (silabi 11)
Tumlinde, (silabi 4)
tumkinge maadui wasimnyonge (silabi 13)
Tumjenge, (silabi 4)
tumwimarishe kano na misuli (silabi 11)
Atuafu, (silabi 4)
atufungua minyororo na unyonge (silabi 13)
Atuinua, (silabi 5)
atukweza hadi kilima cha shibe? (silabi 12)

Mpangilio huu ni wa kimaksudi ili kujenga picha la fumbato la viganja kuashiria umoja na ushirikiano. Vidole vyote vina urefu tofauti kulingana na majukumu yake katika kiganja. Mathalan, kidole cha gumba na cha kuashiria hutumika katika kuandika. Kidole cha kati hutumika katika kupiga chapa. Kidole cha pete na cha mwisho huimarisha fumbato. Vidole hivi vinaashiria nafasi tofauti za wanajamii lakini walio na lengo moja la kujenga bara la Afrika.

Mtunzi pia ana uhuru wa kuzingatia urefu autakao kwa kuanzia kwa idadi ndogo ya silabi kuelekea idadi kubwa. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la ‘Rangi ya Anga’ (uk. 10). Mshairi anasema:

…Hiyo (silabi 2)
Si taasubi (silabi 5)
Ni desturi na mila! (silabi 7)
Hizo (silabi 2)
Si nyanyaso (silabi 4)
Ni kanuni za jadi! (silabi 7)
Hizo (silabi 2)
Si dhuluma (silabi 4)
Ni kaida za utamaduni! (silabi 10)

Katika ushairi huu, mpangilio wa mishororo mifupi na mirefu unapunguza kasi ya usomaji na inabidi msomaji asome kwa utaratibu huku akitua baada ya kila fungu la maneno. Urefu wa mistari umedhibitiwa na fikra za mtunzi katika kuwasilisha ujumbe wake kwa njia ambayo itaeleweka na msomaji. Ametumia mbinu za tanakuzi kama vile, 'hiyo si taasubi, ni desturi na mila' kuonyesha kauli kinzani. Vilevile, ametumia tabaini kwa kutumia kisisitizi 'si'. Kwa mfano, 'Hizo si nyanyaso ni kanuni za jadi'. Mbinu hizi zinaonyesha mgogoro uliopo katika jamii kuhusu taasubi ya kiume. Isitoshe, kupitia mpangilio huu na idadi ya maneno katika kila mstari, ujumbe unaopitishwa unasisitizwa. Matumizi haya ya mistari mifupi na mirefu huondoa uchovu wa kusoma na kumpa msomaji hamu ya kusoma ushairi zaidi.

Mtunzi pia amegawa mistari yake katika vipande kutegemea dhamira yake. Alama ya mkato (,) imetumika katika kutenganisha vipande. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 14). Mshairi anasema:

> Banati alipotimuliwa, alitimuka
> Alipotimuka, aliteguka…

Katika kifungu hiki, mshairi amegawa mistari hii kimaksudi tu katika mistari teule wala si katika shairi zima. Ametumia mtindo huu kuonyesha matokeo ya vitendo. Kutua huku ni muhimu kwa msomaji katika kudhibiti usomaji wake. Isitoshe, kunaonyesha mtiririko wa mawazo ya mtunzi.

Mistari mingine imeundwa kwa kuzingatia neno moja hasa nomino au kiwakilishi. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Wanda' (uk. 33-34). Mshairi anasema:

Kutoka anga la kiangazi
Dhuluma
Zinanguruma kwa nguvu
Na kubabaisha mabonde
Na mawanda na vilima
Mithili mto ulioghafirika
Na kuasi kingo kwa hasira
Tazama jinsi kondoo
Kuku
Kurumbizi
Pimbi
Mikowe
Mbuzi
Mibono
Na sisimizi
Wanavyotapatapa
Katika dimbwi la joto-
Bwawa la huzuni!

Katika kifungu hiki, mshairi ametumia mstari unaoundwa kwa neno moja kuashiria orodha ya vitu. Kusudi kuu ni kutenganisha orodha na maelezo mengine. Ametoa orodha ya viumbe walioathiriwa na joto, mathalan, kuku, kurumbizi, pimbi, mikowe, mbuzi na mibono.

Viwakilishi navyo vimetumiwa hasa pale mtunzi anazungumzia kitu fulani moja kwa moja. Kwa mfano, katika shairi la 7 (uk. 37). Mshairi anasema:

Ewe kijani-kibichi, mrembo
Wewe nembo ya uhai,
Nakuotea daima,
Wewe
Ishara ya uzima
Wewe,
Kipenzi cha moyo
Mvua, ewe mvua, tamanio
Wewe
Mganga mahiri
Ungehitaji kulipwa kwa ghadhabu
Au kwa almasi, lulu au feruzi

Ili kukwangua hii shaka lowezi
Itokomee kutoka nyoyo za wakulima
Kwa kuinua bendera ya kijani kibichi
Na kuipeperusha kwa fahari
Kwenye mlingoti wa ua wa maisha…

Katika kifungu hiki, mshairi anazungumzia mimea iliyonawiri na mvua. Anatumia kiwakilishi' wewe' kusisitiza na kuashiria mazingira na mvua. Msisitizo huu unaonyesha hisia za mapenzi alizonazo mtunzi kwa mazingira na mvua.

## 2.7 Hitimisho

Sura hii imehakiki sifa za kimuundo katika diwani teule za *Rangi ya Anga* na *Msimu wa Tisa*. Imebainika kwamba ushairi si lugha nathari bali una idhini zake nyingi. Aidha, ni ushairi ambao unaweza kuimbika kutokana na sifa zake za kimuundo. Mtiririko wa mawazo katika akili ya mtunzi huathiri pakubwa uwasilishaji wake katika utunzi. Wizani inayojitokeza katika ushairi teule hutokana na mtiririko wa mawazo katika akili ya mtunzi. Hali kadhalika, wizani hii huathiri muundo wa kazi yake. Wizani hii hudhibitiwa na mpangilio wa mafungu, mistari, maneno na sauti. Aidha, muundo huu huathiri hisia, toni, kasi na sauti ya msomaji. Katika sura hii pia, imedhihirika wazi ya kwamba muundo wa ushairi teule si tengemano. Mtunzi hajazingatia muundo mmoja katika utunzi wake bali amebadili miundo kutegemea vipengele mbalimbali kama vile: dhamira, maudhui, matumizi ya lugha, wahusika na upekee wa mwandishi. Isitoshe, mtunzi hajafungwa na muundo maalum wa muwala wa beti na urari wa mizani katika kila mstari bali ana uhuru wa kuwasilisha ujumbe wake kishairi kwa kutumia michoro na mistari ambayo haina urefu maalum. Kwa hivyo, ushairi teule unaonyesha ubunifu wa kiwango cha juu cha mtunzi wala si maandishi ya kiholela holela yasiyokuwa na mantiki. Aidha, sifa za

kimuundo katika ushairi teule ni muhimu katika kuufasiri ujumbe wa mshairi. Sura inayofuatia inachunguza dhima ya vipengee vya kimtindo, hasa, sifa za kigrafolojia katika diwani za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

# SURA YA TATU

# SIFA ZA KIGRAFOLOJIA KATIKA *MSIMU WA TISA* NA *RANGI YA ANGA*

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia sifa za kigrafolojia katika diwani mbili teule, mathalan, ukiukaji wa njia za kawaida za kuakifisha, matumizi ya marudio na takriri, matumizi ya lugha ya kawaida yenye uwezo wa kuibua hisia, mguso na taathira na matumizi ya toni katika kuwasilisha ujumbe. Hizi ni sifa ambazo zina maana halisi bali si nasibishi. Matumizi haya ya lugha yameleta umantiki katika utunzi wa mashairi teule. Kwa mujibu wa Crystal na Davy (1969), dhima kuu ya mtindo ni kuchanganua matumizi ya lugha kutegemea muktadha. Naye Senkoro (1982: 8) anasema mtindo huonyesha kufaulu au kutofaulu kwa mtunzi katika kazi yake. Haya yanaendelezwa na Masinde (1992: 2) anayesema kuwa kinachotofautisha mashairi ya jadi na ya wanamabadiliko ni mtindo. Isitoshe, ushairi hupata maana na umuhimu wake sio tu kutokana na umbo la nje pekee bali pia matumizi ya lugha. Uchambuzi wa lugha ndio unaodhihirisha sifa za ndani za shairi na kuonyesha kwamba upekee wa shairi umo katika kunga za lugha zilizotumiwa. Uchanganuzi wa vipengele hivi vya kigrafolojia uliongozwa na mihimili ifuatayo:

1. Viwango vya kihomolojia na kisintaksia ni msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matumizi ya lugha yenyewe.
2. Matini ya kifasihi huweza kuwa na sifa za kimaandishi zinazochimuzwa na kutiliwa mkazo katika kiwango cha ukiushi.

Katika sura hii, sifa zifuatazo za kigrafolojia zimeangaziwa:

i. Ukiukaji wa njia za kawaida za kuakifisha.
ii. Matumizi ya mbinu ya marudio na takriri.

iii. Matumizi ya lugha ya kawaida yenye uwezo wa kuibua hisia, mguso na taathira.

iv. Matumizi ya toni katika kuwasilisha ujumbe.

### 3.1 Ukiukaji wa Njia za Kawaida za Kuakifisha

Viakifishi ni mojawapo ya kanuni muhimu katika utunzi wa mashairi teule. Kusudi kuu ni kuuwasilisha ujumbe kwa namna inayonasa hisi za msomaji pamoja na kudhibiti mwendo wa usomaji. Kulingana na Maitaria (2012: 398), viakifishi huutaka usomaji na upokezi wa ujumbe ubainike zaidi kwa kuzingatia uelekezi wa ishara hizo. Kwa hivyo, hadhira huweza kulisoma shairi kwa mwendo ulioafiki matarajio ya mshairi. Vilevile, viakifishi hutumika kuvunja mfululizo wa kauli au ujumbe unaowasilishwa.

Matumizi ya viakifishi katika mashairi teule ni mapana kutokana na lengo la kuwasilisha ujumbe kwa ukamilifu. Mtunzi wa diwani teule ametumia viakifishi mbalimbali kama vile nukta pacha [:], alama ya kihisishi [!], kiulizi [?], nukuu [“…”], mkato [,], nukta mkato [;], herufi kubwa na kistari kifupi [-].

#### 3.1.1 Dhima ya Alama ya Kihisishi [!]

Alama ya kihisishi imetumika kimaksudi katika mashairi teule. Kwa mujibu wa Wamitila (2008: 86), uakifishaji unaweza kutumiwa kuwasilisha hisia muhimu katika kazi ya fasihi. Aidha, ni nyenzo muhimu ya kujenga hisia ya kujitambulisha kwa msomaji na mhusika au wahusika wanaopatikana katika kazi fulani au hali inayowazunguka wahusika wenyewe. Katika utafiti huu, alama hii imetumika kuonyesha hisia mbalimbali za mtunzi ambazo zinastahili kupokelewa na msomaji pia. Katika diwani ya *Msimu wa*

*Tisa* shairi la ‘Mnara Mwangavu’ (uk. 38), kifungu cha 8, alama ya kihisishi imetumika kuonyesha toni ya dharau au kejeli. Mshairi anasema:

…Katika bara la giza la ikulu
Kwa miaka mitano miangavu
Kwa viganja bila hatia ya ujanja
Ulisuka utaifa kama wavu adimu
Ukachangamsha nyoyo za marafiki
Na kufunga vinywa vya maadui
Vilivyosubiri ndimi tayari
Kushusha hadharani:
Mwafrika hawezi!...

Katika kifungu hiki, mshairi anaonyesha mtazamo wa watu weupe kuwahusu Waafrika katika nchi ya Afrika Kusini ya kwamba Mwafrika hawezi tawala kwa vyovyote vile. Alama ya kihisishi iliyotumika inamwelekeza msomaji kutamka maneno hayo kwa dharau.

Alama ya kihisishi pia imetumika kuonyesha amri na kuvuta makini ya msomaji. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* shairi la ‘Mdundo wa Dhiki’ (uk.56). mshairi anasema: “ Njoo! Pamoja tusikize mdundo wa dhiki…”. Katika mstari huu, mshairi amevuta makini ya msomaji kusudi atambue dhiki wanazopitia wanyonge si kazini, si nyumbani si shuleni.

Vilevile, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* shairi la ‘Mkimbizi’ (uk. 57), kifungu cha 2, mshairi anasema:

…Mboni za kumbukumbu bado zinaona
Zinaona waja-wazito wakijizatiti mbioni
Wakijisukuma na kusukuma wanaosubiriwa,
Zinaona miili inayobubujikwa na damu
Ikijikokota kutafuta kivuli cha usalama’
Zinaona viwiliwili vya jamaa na marafiki
Vilikuwa na mafunza kandokando mwa njia!...

Katika kifungu hiki, mshairi anasawiri hisia za huruma zinazotokana na majanga wanayokumbana nayo wakimbizi. Matumizi haya ya alama ya hisi yanajenga taswira ya tanzia.

Matumizi ya alama ya kihisishi hayajadhihirika tu katika diwani ya *Msimu wa Tisa* pekee pia katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Katika diwani hii, alama ya hisi imetumika kusawiri toni ya chukizo. Kwa mfano, katika shairi la 'Rangi ya Anga' katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 4). Mmshairi anasema:

> …wasanii waliofungwa pingu za mila
> Wametungia nyimbo sumbufu kama mpupu
> Wakilalamika kwamba kijana wa kike
> Kukataa kukeketwa kunakokeketwa
> Ni kinyume na utamaduni wa kabila
> Ni kitendo kinachonuka vumba ya aibu!...

Katika kifungu hiki cha ushairi, mtunzi amesawiri toni ya chuki. Anaonyesha jinsi utamaduni unavyoshadidia ukeketaji wa mtoto wa kike na afanyapo kinyume ni kitendo kisichostahili. Aidha, mtunzi anadhihirisha dhuluma apitiayo mtoto wa kike. Katika usomaji, lazima msomaji adhihirishe toni ya chukizo; jambo ambalo vilevile linaathiri kiimbo. Matumizi haya ya toni ya chuki yamedhihirika katika shairi lili hili (uk. 7) na shairi la 'Wanda' (uk. 28). Kwa ujumla, alama ya kihisishi imetumika kuleta msisitizo ambao unatokana na mazingira ya mwendo usio wa kasi katika usomaji. Katika mazingira haya, mshairi huitaka hadhira iisome kauli iliyokusudiwa kwa usaili na kuwazia tukio linalowasilishwa.

### 3.1.2 Dhima ya Alama za Nukuu ["…"]

Alama za nukuu zimetumiwa kumwelekeza msomaji afahamu kuwa kauli hii ni ya mhusika mwingine wala si ya mtunzi mwenyewe. Pia, imetumiwa kumfahamisha

msomaji ya kwamba anafaa kubadili sauti yake iwe sawa na ya mhusika huyo mwingine. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* shairi la 'Usingizini' uk. 4, kifungu cha 7. Mshairi anasema:

> …Kwa nini tunajifanya nyumbu wa Maasai-Mara
> Ambao bila kuchukua hatua, miaka na mikaka
> Hupigwa dafirau na hasira nyekundu ya Mto Mara
> Na kuwa karamu kubwa kwa mamba na nderi
> Bila ya nyumbu asemaye: "Hayatakuwa tena!..."?

Katika kifungu hiki, kauli, "Hayatakuwa tena!" ni sauti inayokusudiwa kutoka kwa wananchi baada ya kuzinduka na kutambua kwamba wanafaa kujihami ili kupambana na baa la njaa. Msomaji anafaa kutamka kauli hiyo kwa ukali.

Alama hii ya nukuu pia imetumiwa kunukuu kauli zilizotolewa na watu wengine kwa njia ya methali, nyimbo au kauli za kawaida tu. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* shairi la 'Werevu' (uk. 8), kifungu cha 1. Mshairi anasema:

> …Angalizingatia kanuni za mkataba wa majemedari
> Silaha iliyokomboa taifa kutoka minyororo ya huzuni,
> Angalifahamu uaminifu ni akiba inayozaa matunda
> Na kukubali usemi: "Werevu mwingi huondoa maarifa…"

Katika kifungu hiki, mshairi ametumia methali,"Werevu mwingi huondoa maarifa". Inabidi msomaji atue kabla ya kutamka methali hii. Nukuu hili linaleta ufungamano wa usemi na suala ambalo limezungumziwa. Mshairi anaonyesha vile kiongozi alikaidi kuwajibikia taifa lake kwa kutumia ujanja kujilundikia mali. Nukuu hili linamfanya msomaji atafakari zaidi na adhibiti kasi ya usomaji.

Alama za nukuu pia zimetumika kwa kusudi la kukejeli. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* shairi la 'Waharifu Huru' (uk. 30), kifungu cha 2. Mshairi anasema:

…Vijana wa kike walifuata njia ya mchanga didimizi wa ukahaba
Wa kiume walikwama kwenye bonde la madawa ya kulevya
Na kisha kutumbukia katika dimbwi la wizi na unyang'anyi;
Bali katika wingu la unafiki wa "Amani, upendo na umoja"
Badala ya wahandisi wa jakamoyo kutetemeka mahakamani
Badala ya wenye damu viganjani kutupwa korokoroni
Wanaendesha mashagingi yenye bendera za mamlaka
Wanalipwa mishahara minono wakiitwa "viongozi wa taifa"!...

Katika mstari wa mwisho wa kifungu hiki, mtunzi anakejeli viongozi wanaoitwa "viongozi wa taifa" kwa kutowajibika katika kazi yao. Hawaenezi amani, upendo na umoja kama wanavyodai kwa sababu wanaowatendea wengine unyama bado wako huru. Haya yanadhihirika katika mstari wa 4 mshairi anaposema, : "Bali katika wingu la unafiki wa 'Amani, upendo na umoja". Msomaji anafaa kutamka kauli zilizonukuliwa kwa namna ya kuchukizwa.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Magenge Matatu', (uk. 32), katika kifungu cha 2 na 3, mshairi anasema:

…Genge la pili la mazimwi
Lilituahidi majira maangavu ya amani, upendo na umoja
Tukajijeruhi koo kwa kuimba "Juu! Juu! Juu sana!"

Genge la tatu, nusu-mazimwi
Lilituahidi katiba mpya na dawa kali dhidi ya ufisadi
Tukaamini wimbo "Yote yawezekana bila Mfalme wa Nzige"

Katika vifungu hivi, mshairi anamtaka msomaji aimbe kifungu hicho cha wimbo [Juu! Juu! Juu sana! na Yote yawezekana bila Mfalme wa Nzige]. Hii ni njia mojawapo ya kuongeza ujumi na ubunifu katika utunzi. Vilevile, ni njia ya kumshirikisha msomaji katika uwasilishaji.

Isitoshe, alama za nukuu zimetumika kuonyesha majina ya msimbo. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* shairi la 'Waharifu Huru' (uk. 30), kifungu cha 1 mstari wa 1.

Mshairi anasema: “Bila kutarajiwa, onyo za mashambulizi dhidi ya ‘wageni”. Ametumia jina hili ‘wageni’ kumaanisha watu wa kabila tofauti na la wenyeji. Mshairi ametumia jina hili la msimbo kimaksudi kumtaka msomaji atafakari zaidi kuhusu kauli hiyo na namna inavyooana na ujumbe wa shairi.

### 3.1.3 Dhima ya Nukta pacha [:]

Kulingana na Wamitila (2008: 87), uakifishaji huweza kutumiwa kuelekeza kwenye mantiki hasa kwa matumizi ya kiakifishi (:) ambacho huonyesha kuwa kinachofuata kinahusiana kimantiki, kisababishi na kilichotangulia. Hali kadhalika, matumizi ya nukta pacha ni muhimu sana katika kudhibiti mahadhi na wizani ya ushairi. Katika diwani mbili teule, nukta pacha ina matumizi anuwai. Mathalan, imetumika kunukuu maneno ya mhusika mwingine kando na mshairi. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 10), shairi la 7. Mshairi anasema:

Sikiza sauti ya mzazi
Ambayo inakuja juu
Kama wimbi la sumu
Ikimimina kemikali kali
Katika akili asubuhi:
    Usicheke kiholela
    Kama wewe ni mwanamke!
    Nyamaza! Futa machozi!
    Ushindwaye na madogo
    Kama mavazi yako
    Ni kamisi na rinda!

Katika kifungu hiki, mtunzi anamtarajia msomaji ageuze sauti yake ifanane na ya mhusika huyo ambaye ni mzazi wa kiume anapomkaripia mwanawe wa kiume.

Nukta pacha pia imetumika katika kutoa orodha na kuonyesha mabadiliko ya ridhimu kutoka kauli zilizotangulia. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la ‘Wanda’ (uk. 31). Mshairi anasema:

…Hizi kovu kirihi
Ambazo kwa kinaya
Zinaangalia mpita njia
Jana zilikuwa mashamba
Kulistawi:
Mawele
Kunde
Wimbi
Mtama
Mahindi
Na mbaazi…

Katika kifungu hiki, mshairi anaorodhesha aina ya nafaka: mawele, kunde, wimbi, mtama, mahindi na mbaazi. Matumizi haya ya orodha yanaathiri kasi ya usomaji.

Nukta pacha pia imetumika kutoa maelezo zaidi kuhusu jambo fulani. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la "Tope la Mizozo" kifungu cha 5, (uk. 6), mshairi anasema:

…Wendao kwa magari yakipeperusha bendera za jaha
Wameburura sheria za nchi kwenye mtaro mchafu:
Wakitumia ujanja kupigia debe mkataba wa umma
Wamehonga kwa mbuga za wanyama na vyeti vya ardhi…

Katika kifungu hiki, mshairi amefafanua zaidi kuhusu serikali ambayo imevunja sheria kwa kushiriki ujanja, ufisadi, dharau na ukiukaji wa haki. Mshairi anatarajia msomaji abadili hisia zake anaposoma kifungu hiki baada ya kutumia nukta pacha. Msomaji anafaa kuzingatia hisia za chuki. Hali kadhalika, matumizi ya nukta pacha katika kifungu hiki yamebainisha sehemu kuu na maelezo.

### 3.1.4 Dhima ya Kiulizi [?]

Mbinu ya kiulizi imetumika kwa wingi katika diwani mbili teule. Aghalabu maswali ya balagha yametumika ili kumfanya msomaji atafakari kuhusu ujumbe unaotolewa. Yametumiwa pia kuonyesha uzito wa ujumbe huo. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la "Darfur" kifungu cha 6, (uk. 27), mshairi anasema:

…Kwa nini waliojitwika jukumu la polisi wa dunia
Wamesimama kimya wakiangalia upande wa pili
Maisha ya watu milioni mbili yakiungua katika mwako?...

Katika kifungu hiki, mshairi anawashutumu polisi ambao hawakuwajibika kuzuia vifo vya watu walioteketezwa moto.

Alama ya kiulizi pia inadhihirika katika diwani ya *Msimu wa Tisa* shairi la 'Ni Kweli?' (uk. 55). Mshairi anasema:

…Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba wapo wazazi wanatuma Watoto
Kwenda kutega mitego ya virinda hoteli
Kusudi kuleta change nan guru nyumbani
Kupigana na kikosi kikali cha njaa?

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba baadhi ya wakembe wa kike
Hutiririkwa na machozi na damu
Baada ya wazazi wao halisi wa kiume
Kuwasagasaga kama nyama ya sambusa?

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba leo katika baadhi ya nyumba
Wake wanapokuwa katika shughuli za nje
Nyadhifa zao kuu za usiku wa manane
Hutekelezwa kikamilifu na mabinti?

Katika vifungu hivi, mshairi ametumia alama ya kiulizi kwa kusudi la kumtaka msomaji awazie kuhusu uozo wa kimaadili uliopo katika jamii: ukahaba, ubakaji na uzinzi. Aidha, anamtia mshawasha wa kutetea haki za mtoto wa kike katika jamii.

Hali kadhalika, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la "Wanda" (uk.47), mshairi anasema:

…Hii milolongo ya taya
Na pembe na nundu
Inafaidi vipi nyumbani
Zaidi ya viwele vichache
Vya ng'ombe wateule?

Katika kifungu hiki, mtunzi anamtia mshawasha mkulima ili azingatie njia mwafaka za kilimo.

### 3.1.5 Dhima ya Nukta mkato [;]

Nukta mkato imetumika kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu kauli inayotangulia hasa baada ya mafungu kadhaa ya maneno. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 2). Mshairi anasema:

> …Moyoni mwangu
> Hakungekuwa na ilhamu
> Ikiniwashawasha kwa utukutu
> Kama majani ya mpupu;
> Mwashomwasho usiokupwa
> Haungekuwa ukirusha mawimbi
> Yakibeba mfumo wa sauti
> Ukisema kwa uradidi:
> Himahima shika pembe
> Piga mbiu ya mgambo!...

Msomaji anatanguliza kwa kuonyesha ilhamu aliyonayo ya kusimulia yaliyo moyoni yanayomwasha kama majani ya mpupu. Baada ya matumizi ya nukta mkato, anafafanua zaidi jinsi ilhamu hii haiwezi kuondolewa na chochote; lazima asimulie. Katika kifungu hiki, msomaji anapofikia nukta mkato anafaa kutua kwa muda kisha aendelee na usomaji. Kituo hiki kitakuwa kirefu zaidi ya mkato.

### 3.1.6 Dhima ya Mkato [,]

Alama ya mkato imetumika kimaksudi katika diwani hizi mbili teule ijapokuwa si kwa wingi kama ilivyo katika ushairi wa kimapokeo. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Kasisi’, kifungu cha 1, (uk.82). Mshairi anasema:

> Ulishuhudia mito ya damu
> Ikitiririka katika Bonde la Ufa,
> Uliona mvua ya machozi

Ikilowesha kambi za wakimbizi,
Ulitazama ndoto za makabwela…

Katika kifungu hiki, mahadhi ya ushairi katika akili ya mtunzi yanamwelekeza katika matumizi ya mkato; hivyo unatokea kimaksudi tu. Mshairi ametumia mkato kuashiria kipumuo kifupi. Aidha, ametoa mawazo yake kwa mfululizo kisha anatua.

Katika diwani teule, matumizi haya ya mkato ni ya kimaksudi na hutokea katika mazingira yoyote yale ili kujenga ridhimu/wizani maalum. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* shairi la 2, (uk. 2). Mshairi anasema:

Vilele vya milima
Na malindi ya bahari,
Mmwesomweso wa nyota
Na tumba za mbalamwezi…

Katika kifungu hiki, alama ya mkato imetumiwa baada ya kila mistari miwili. Matumizi haya yanadhibiti kasi ya msomaji na kujenga wizani maalum. Aidha, matumizi ya alama hii ya mkato yanaonyesha mtiririko wa mawazo ya mtunzi. Isitoshe, yanampatia msomaji nafasi ya kutafakari zaidi kuhusu ujumbe unaowasilishwa na mtunzi. Kulingana na Wamitila (2008: 85), mtindo unaotumiwa wa kuakifisha unakuwa msingi wa kuakisi au kuonyesha jinsi mawazo ya mhusika kwa jumla yanavyotiririka. Katika shairi hili, baada ya mistari ya kwanza minne, mtunzi anawasilisha mawazo yake mfululizo hadi anatua katika mstari wa kumi kimaksudi.

### 3.1.7 Dhima ya Kistari kifupi [-]

Mshairi ametumia kistari kifupi kimaksudi kuonyesha usemi wa mtu mwingine. Kwa mfano, katika shairi la 6 (uk. 9) katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Mshairi anasema:

…Katika chuo kikuu
Nilisikia profesa
Vyeti nyumbani
Fedha mifukoni
Kipara utosini
Ndevu kidevuni
Tabasamu midomoni
Na T-bone viganjani
Akijigamba kwa wenza-
    Nilipoposa, nikachumbia
    Niliyemchumbia, nikamuoa
    Hakuzidi kumi na tatu
    Kwenye mizani ya miaka!...

Katika kifungu hiki, Profesa katika chuo kikuu ananukuliwa akijigamba vile alimchumbia msichana mdogo asiyezidi miaka kumi na mitatu.

Kistari kifupi pia kimetumika kudumisha mahadhi ya ushairi jinsi mtunzi ayapendavyo. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 30). Mshairi anatumia kistari kifupi katika kutambulisha aina ya kilimo cha lima -hama-lima badala ya kutumia neno moja tu.

Isitoshe, kistari kifupi kimetumika kuonyesha maelezo zaidi. Kwa mfano, katika shairi la ‘Hoteli Ukingoni mwa Mto’ katika diwani ya *Msimu wa Tisa* (uk. 92). Mshairi anasema:

…Wadudu wenye machachari
Wanawania vyumba na wateja-
Kuna wanaong’ong’a ukutani
Na wanaotambaa kiholela sakafuni…

Katika shairi hili, mshairi ameonyesha namna hawa wadudu wanaowavamia wateja na vyumba walivyo kwa wingi; si ukutani, si sakafuni. Mtunzi pia ametumia kistari kifupi kuturejesha katika matukio ya awali. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 9). Mshairi anasema:

…Wasemaji tuseme nini
Au tutulie yakini

Kama maji ya mtungi-
Aliyetunga mimba
Na kuibeba kwa miezi tisa
Na kwa uchungu na miguno
Kuleta mkazi ulimwenguni
Na kwa moyo mkunjufu…

Katika kifungu hiki, mshairi ameturejesha nyuma kutufahamisha yaliyompata kijana wa kike baada ya kutungwa mimba. Hatimaye anapojifungua kijana mwanamume, bado anambeza kwa kushindwa na madogo kama mwanamke. Kwa hivyo, mwanamke amekubali na kuridhika na hadhi yake ya chini katika jamii.

### 3.1.8 Dhima ya Herufi kubwa

Herufi kubwa imetumika aghalabu mwanzoni mwa kila mstari. Kwa mfano, katika shairi la 'Minyonyoro ya Njaa' (uk.1), kifungu cha 1, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Mshairi anasema:

Tumerudi kwenye dimbwi la huzuni
Kana kwamba kamba isiyoonekana…

Katika kifungu hiki, herufi kubwa imetumiwa kuonyesha mtiririko wa mawazo katika akili ya mshairi.

Herufi kubwa pia imetumika kwa ustadi kutajia majina ya pekee. Kwa mfano, katika shairi la 'Johari Angani' (uk. 35) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*,. Mshairi anasema:

…Kuruka juu ya Milima ya Nuba
Na kuvuka uchi wa Sahara,
Na kutazama bluu ya Mediteraneani,
Baada ya kupita nchi ya Da Vinci…

Katika kifungu hiki, kuna majina kama vile: Milima ya Nuba, jangwa la Sahara, bahari ya Mediteraneani na nchi ya Da Vinci. Mshairi anasifia teknolojia ya ndege ambayo imemwezesha kuvuka milima, nchi na bahari kuzuru nchi za mbali.

Hali kadhalika, herufi kubwa pia imetumiwa kunasa nadhari ya msomaji; jambo ambalo linamfanya atue na kutafakari zaidi. Kwa mfano, katika shairi la 'Msumbiji' (uk.72) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Mshairi anasema:

> …Ngoma ya machozi na mauti:
> Mbele uwanjani, RENAMO
> Nyuma, chini kwa chini, CIA
> Vijijini, macheo yanapowadia
> Ndlakama anawasha moto mkali
> Asubuhi, ghadhabu ya FRELIMO…

Katika kifungu hiki, matumizi haya ya herufi kubwa katika kuandika akronimu yamekusudiwa kuathiri jinsi ambavyo maana ya kifasihi itafasiriwa na msomaji na mhakiki. Kwa mfano, katika kifungu hiki, msomaji anapata fursa ya kutafakari zaidi kuhusu maafa yaliyosababishwa na hivi vyama vya kisiasa katika nchi ya Msumbiji barani Afrika. Isitoshe, matumizi haya ya akronimu, *RENAMO*, *CIA* na *FRELIMO* kudhihirisha vyama vya kisiasa ni muhimu katika kudumisha mahadhi ya ushairi badala ya kutumia maneno kwa ukamilifu.

### 3.2 Matumizi ya Marudio na Takriri

Kwa mujibu wa TUKI (2006: 740, 19), marudio ni mbinu ya kurudia neno au mafungu ya maneno. Nayo mbinu ya takriri ni marudio ya sauti au silabi. Kulingana na Wamitila (2008: 499), urudiaji hutumiwa kusisitiza, kama njia ya uelewekaji, kupiga mwangwi wa kazi nyingine, kuleta mtagusano wa kimazungumzo, kuzua wizani maalum, kuleta ujumi

wa uwasilishaji, kuweka kumbukumbu na kuleta uziada. Katika tasnifu hii, baadhi ya dhima hizi zimedhihirika wazi kupitia mashairi mbalimbali. Hali kadhalika, mbinu hizi mbili zimetumiwa na mshairi ili kutoa hisia zake kwa wasomaji, aidha kudumisha mahadhi ya ushairi. Katika mashairi teule, mtunzi ametumia mbinu ya marudio na takriri kimaksudi katika mazingira ya mwanzoni, kati na mwishoni mwa maneno au mistari. Hii ni njia mojawapo ya kuonyesha ubunifu alionao.

### 3.2.1 Marudio kama Nyenzo ya Kimtindo

Kuna matumizi anuwai ya mbinu ya marudio katika diwani teule. Mwanzo, kuna marudio ya wizani ambayo yanadhihirika kupitia mpangilio wa maneno katika mistari. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa* Tisa, shairi la ‘Tume za Rais’ (uk. 31), kila kifungu kina mistari mitano. Marudio haya ya mistari yamedhihirisha usambamba wa kimuundo katika ushairi huo. Isitoshe, kuna usambamba wa kitanakuzi ambao umetokea pale ambapo mbinu za ulinganuzi zimetumika. Kwa mfano, katika shairi la ‘Rangi ya Anga’ (uk.10). Mshairi anasema:

… Hiyo
Si taasubi
Ni desturi na mila!
Hizo
Si nyanyaso
Ni kanuni za jadi!
Hizo
Si dhuluma
Ni kaida za utamaduni!

Katika kifungu hiki, usambamba huu umedumisha mahadhi ya ushairi, kudhibiti kasi ya usomaji na kusisitiza ujumbe kwa msomaji. Urudiaji wa uelezaji wa kihisia umedhihirika kupitia usambamba huu wa kitanakuzi mshairi anapotumia, ‘ni’ na ‘si’. Anaonyesha

namna amekerwa na mila na kanuni za jadi ambazo zinaeneza dhuluma dhidi ya jinsia ya kike.

Mbinu ya marudio imejitokeza katika mazingira tofauti katika ushairi wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*, mathalan, mbinu ya marudio imetumiwa mwanzoni mwa mistari. Kuna marudio ya neno moja mwanzoni mwa mistari. Kulingana na Wamitila (2008: 486), huu ni urudiaji sahili wa msamiati. Kwa mfano, mtunzi ametumia marudio ya vihusishi katika *Msimu wa Tisa*. Kwa mfano, shairi la 'Mkasa' (uk.16). Mshairi anasema:

> **…Chini ya** jengo lililoporomoka la Chama cha Ushirika
> **Chini ya** mawe, vigae vya vioo na takataka
> Maiti arobaini za wasichana vipenzi vya taifa…

Katika kifungu hiki, kihusishi, 'chini ya' kimerudiwa kusisitiza maafa ya mporomoko wa jengo la Chama cha Ushirika. Isitoshe, kuna marudio ya nomino, 'jua' (uk. 28) katika kifungu cha 3 na 4. Mshairi anasema:

> …Jua!
> Ewe jua!
> Jua la adhuhuri…
>
> Jua!
> Ewe jua!
> Jua la wanda za mikwaju…

Katika kifungu hiki, mshairi ameghadhabishwa na jua ambalo limesababisha maafa ya mimea, wanyama, wadudu na uharibifu wa mazingira kwa ujumla. Vilevile, kuna marudio ya kiwakilishi'wewe' (uk. 37). Mshairi anasema:

> …Mvua, ewe mvua
> Wewe
> Daktarin mahiri wa mazingira…
> Nakuotea daima,
> Wewe
> Ishara ya uzima
> Wewe,
> Kipenzi cha moyo…

Katika kifungu hiki, mshairi ametumia kiwakilishi, 'wewe' kuashiria mvua ambayo inaleta tumaini kwa wanajamii. Hali kadhalika, mafungu ya maneno yamerudiwa mwanzoni mwa mistari inayofuatana. Kwa mfano, katika shairi la *Rangi ya Anga* (uk. 54). Mshairi anasema:

> …Kitanzi madhubuti
> **Sio cha** kamba ya mgoza
> **Sio cha** katani au mkonge
> **Sio cha** mbuyu au mfungate
> Bali cha chuma cha pua…

Kutokana na kifungu hiki, kifungu cha maneno, 'sio cha' kimetumiwa ili kusisitiza jinsi wakoloni walivyowadhibiti na kuwatawala Waafrika; ni saw ana kitanzi Madhubuti. Urudiaji huu umetumiwa pia kudumisha mahadhi maalum wakati wa usomaji. Vilevile, kuna marudio ya sentensi mwanzoni mwa kila kifungu cha ushairi. Huu ni urudiaji wa kimaumbo. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Tume za Rais' (uk.31), sentensi ifuatayo imerudiwa: "Napendekeza tuunde tume ya rais". Haya ni kinyume na ushairi wa kimapokeo ambapo kibwagizo aghalabu hutokea mwishoni mwa kila ubeti wala si mwanzoni. Jambo hili linadhihirisha upeo wa juu wa ubunifu. Vilevile, ni mbinu ya kunasa nadhari ya msomaji na kumsaidia kuweka kumbukumbu ya kile kinachozungumziwa.

Aidha, kuna marudio ya maneno katikati mwa mistari. Maneno haya yanaweza kuhusiana kimaana au yawe na maana tofauti. Kwa mfano, katika shairi la 'Tume za Rais', neno 'rais' limetumika kusudi kusisitiza zaidi 'tume za rais'. Kwa mfano, kifungu cha tatu, mstari wa mwisho: 'Imshauri *rais* kuhusu *rais* na tume za *rais*'. Ubunifu pia unadhihirika katika kuchezea chezea maneno, hivyo kutokea kama kitanza ndimi na kujenga mahadhi maalum ya kimuziki wakati wa usomaji.

Kuna marudio ya maneno mwishoni mwa mistari. Kwa mfano, katika shairi la ‘Tume za Rais’(uk. 31). Mshairi anasema:

…Napendekeza tuunde tume ya rais
Tuitenge nusu ya akiba ya Banki Kuu
Ichunguze kama rais ni rais bila tume za rais
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Imshauri rais kuhusu rais na tume za rais…

Katika kifungu hiki, neno ‘rais’ limerudiwa mwishoni mwa kila mstari isipokuwa mstari wa pili. Marudio haya yanaibua muziki wa aina fulani. Aidha, mshairi amekariri neno ‘rais’ ili kuhakikisha msomaji amefungwa na kauli hiyo asije akapata dhamira tofauti.

Katika diwani teule, mshairi pia amebadili nafasi ya kati ya neno na kulipatia nafasi ya mwanzoni. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 54). Mshairi anasema:

…Lilimfikia malishoni
Na kwa ujuzi na hila
Kumtia **kitanzi** pembeni
**Kitanzi** Madhubuti…

Katika kifungu hiki, neno ‘kitanzi’ limerudiwa kusudi kusisitiza vile Zimwi la Theluji (Mkoloni) lilivyochukua usukani na kumtawala Mwafrika.

Vilevile, neno la mwisho katika mstari limekuwa kianzio katika mstari unaofuatia. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 28). Mshairi anasema:

Jua!
Ewe jua!
Jua la wanda za mikwaju…

Katika kifungu hiki, neno, ‘jua’ limerudiwa. Urudiaji huu unaathiri hisia za msomaji anapowazia kuhusu athari ya jua katika mazingira halisi. Msomaji atachukizwa na

uharibifu wa mazingira unaosababishwa hasa na binadamu. Isitoshe, msisitizo huu utaweka kumbukumbu katika akili ya msomaji.

### 3.2.2 Takriri kama Nyenzo ya Kimtindo

Takriri ya sauti na silabi imetumika kwa wingi katika diwani teule kwa madhumuni yale yale tuliyoangazia awali. Kwa mujibu wa Leech (1969), kuna aina mbalimbali za takriri, mathalan, takriri irabu na konsonanti. Aina za takriri ambazo zimetumika katika diwani teule ni kama zifuatazo:

#### Takriri ya Konsonanti

Haya ni marudio ya sauti ya konsonanti katika fungu la maneno na hasa mwanzoni. Kulingana na Wamitila (2003: 215), istilahi hii hutumiwa kuelezea urudiaji wa sauti ya konsonanti. Kimsingi kurudia huku hutokea katika mazingira ya mwanzoni ijapokuwa kuna uwezekano wa kupatikana kwingineko. Muhimu ni kuwa kurudia huku kunajitokeza wazi. Katika ushairi wa Kiswahili, takriri irabu na takriri konsonanti hazijitokezi sana kama ilivyo katika Kiingereza kwa sababu Kiswahili hupendelea muundo wa konsonanti kufuatwa na irabu katika uundaji wa silabi. Kwa hivyo, takriri ya konsonanti katika utafiti wetu imeangaziwa kama silabi au sauti iliyoundwa na konsonanti na irabu; kwa hivyo kuwa takriri silabi inayoanzia kwa konsonanti. Takriri konsonanti/silabi imetumika mwanzoni katika diwani teule. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 13), shairi la 10. Mshairi anasema:

**…Na** asa**li** na siagi ya thamani,
A**na**va**li**a mavazi ya kuteua
**Na ku**la**li**a godoro la gharama,
A**na**tumia fenicha ya mvuli
**Na ku**ka**li**a matakia ya veliveti…

Katika kifungu hiki, silabi, ‘na’ ambayo imeanzia kwa konsonanti ‘n’ imerudiwa mwanzoni mwa kila baada ya mstari mmoja. Usambamba wa konsonanti unaodhihirika mwanzoni mwa mistari unaibua mahadhi maalum ambayo msomaji hana budi kuyafuata wakati wa usomaji.

Vilevile, takriri konsonanti/silabi imetumiwa katikati mwa mistari kama ilivyo katika ushairi tulioangazia katika (uk.13). Maneno, ‘**ku**kalia’ na ‘**ku**lalia’ yameanzia kwa ‘ku’. Haya yamedhihirika pia katika neno, ‘a**na**valia’ na ‘a**na**tumia’. Vilevile, silabi ‘li’ imerudiwa katika maneno yafuatayo: asa**li**, anava**li**a, kula**li**a na kuka**li**a. Takriri hii imetokea katikati mwa neno na kurudiwa katika mistari kadhaa. Aidha, mshairi anataka kusisitiza suala la wakati anapotumia kiambishi ‘na’ katika ‘anavalia’ na ‘anatumia’ kuonyesha ya kwamba hadi wa leo bado mwanamume anazidi kuimarika huku mwanamke akizidi kukandamizwa.

Isitoshe, takriri konsonanti imetumika mwishoni mwa mistari. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 13), shairi la 10. Mshairi anasema:

> Banati alipotimuliwa, alitimu**ka**
> Alipotimuka, alitegu**ka**,
> Alipotegu**ka**…

Katika kifungu hiki, mshairi ameonyesha mfululizo na ukamilifu wa vitendo katika kauli ya kutendeka hivyo kudumisha mahadhi maalum. Takriri hii pia imedhihirika katika diwani ya *Msimu wa Tisa* katika shairi, ‘Mafuta yenye Damu’ (uk. 48), kifungu cha 2. Mshairi anasema:

> Maiti za wakulima mashamba**ni**
> Maiti za wachungaji malisho**ni**
> Maiti za watoto shule**ni**
> Maiti za vikongwe vijiji**ni …**

Katika kifungu hiki, mtunzi amerudia silabi ‘ni’ mwishoni mwa mistari ili kudumisha mapigo maalum.

**Takriri ya Irabu**

Haya ni marudio ya sauti ya irabu katika fungu la maneno. Takriri hii ya irabu imetumika pia kama takriri silabi. Aidha, imetokea katika mazingira ya mwanzoni, kati au mwisho. Kwa mfano, katika ushairi tulioangazia hapo awali (tazama *Rangi ya Anga* (uk. 13), shairi la 10) irabu ‘a’ katika vitenzi: “**a**lipotimuliwa, **a**litimuka, **a**lipotimuka, **a**liteguka na **a**lipoteguka”, imetokea katika mazingira ya kati na mwanzoni mwa mistari ili kusisitiza nafsi ya tatu inayorejelewa. Mshairi pia ametumia takriri irabu katika mwishoni mwa mistari ijapokuwa si kwa wingi. Kwa mfano, katika shairi la ‘Mwashi’ katika diwani ya *Msimu wa Tisa* (uk 40). Mshairi anasema:

> …Ole wao wazungu weusi kama mak**aa**
> Na suti zao za milia na mikufu ya s**aa**…

Katika kifungu hiki, irabu ‘a’ imetumika katika neno ‘makaa’ na ‘saa’. Marudio haya ya irabu yanaibusha muziki wa aina fulani.

**3.3 Matumizi ya lugha ya kawaida yenye uwezo wa kuibua hisia, mguso na taathira**

Kulingana na Wamitila (2008: 228), tungo nyingi za kishairi huwa ndefu na ili kuweza kulifikia lengo lake la kimsingi la mawasiliano, hutegemea mbinu ambazo huziwezesha kuwasilisha ujumbe wake kwa athari kubwa. Haya yanafafanuliwa na Kyalo Wamitila katika utangulizi wa *Dhifa* (2008: i) anayesema kwamba lugha ya kawaida, ya mazungumzo, ya kila siku ndiyo lugha yenye uwezo wa kuibua hisia, mguso na taathira ambayo ni muhimu katika ushairi. Aidha, ushairi unaoacha athari si ule ambao

umejitenga na lugha hiyo bali ni ule unaoweza kumvuta na kumteka msomaji kwa kuitumia lugha hiyo. Usanii wenyewe upo kwenye kuuchukua huo ukawaida na kuufanya uweze kugusa hisia, kuyachokora yale mahasa ya ndani ya msomaji ambaye miaka mingi baadaye atakumbuka athari alizoachiwa na utungo huo. Kutokana na maelezo haya, hisia mbalimbali zimejitokeza katika mashairi mbalimbali katika diwani teule. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Mkasa' (uk. 15). Mshairi anasema:

> …Katika vitanda vinavyomtia mtazamaji ganzi
> Dondoko katika mipira inayoungana na chupa
> Zinapitia kwenye sindano zilizozama mikononi
> Kupambana na ukame katika mishipa ya damu
> Bendeji zenye mabaka yaliyoloa wekundu
> Zimefunika makuo kwenye nyuso zilizopondwa
> Na kubana miguu na mikono iliyovunjika
>
> Sakafuni, maiti zilizofunikwa kwa mablanketi
> Zimepangwa kwa safu kwa heshima ya huzuni
> Zikikumbusha kwamba maisha ni kibatari
> Kinawaka uwanjani anga likiwa tulivu
> Bali kuzimwa na upepo mwovu si kazi…

Katika vifungu hivi, mshairi anamwacha msomaji katika hali ya huzuni akiwazia kuhusu yaliyowapata waathiriwa wa mkasa wa bomu. Mkasa huu unasawiri mashambulizi yaliyotokea nchini Kenya mnamo mwaka wa 1998. Msomaji anapochorewa picha ya bendeji zilizoloa wekundu wa damu na maiti zilizofunikwa kwa mablanketi, ni taswira itakayobaki katika akili yake daima dawamu.

Hisia za uchungu zinadhihirika katika shairi la 'Wenda-wazimu Kongo' (uk. 19). Mshairi anasema:

> …Kichakani, mafichoni, bahati nasibu inampuuza:
> Bila kujali kite na nduru katika kimya cha usiku
> Bila kujali uja-uzito wake wa miezi tisa
> Genge la wahuni wenye nembo ya usalama
> Kwa zamu za chuki na dhuluma bila kifani
> Linashambulia, sio kwa ngumi au makkofi
> Bali kwa gruneti mwilini na mabomu akilini

Kwenye sehemu zinazowaka makaa ya uchungu
Inafuata dhiki kali ya vijiti na mitutu ya bunduki
Matundu yanayotiririka damu kwa fujo
Yanaunganisha njia jirani za mwili…

Katika kifungu hiki, hisia za uchungu zinadhihirishwa wakati mshairi anapozungumzia yaliyowapata raia kutokana na mashambulizi ya genge la wahuni wa Jeshi la Taifa. Wengi walikufa kutokana na mashambulizi ya gruneti, mabomu, bunduki na vijiti vilivyoshindiliwa kwenye njia ya uzazi.

Hisia za hasira zinadhihirishwa katika shairi la 'Mafuta yenye Damu' (uk. 48). Mshairi anasema:

…Usiniuzie petroli ya Kusini mwa Sudan
Sitaendesha gari kwa damu ya watu,
Picha za maiti za watoto wachanga
Zitanitumbukiza Hospitali ya Mathare

Katika kifungu hiki, mshairi amekasirishwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyosababishwa na mzozo wa umiliki wa mafuta nchini Sudan. Anakiri ya kwamba asiuziwe petroli kutoka Kusini mwa Sudan kutokana na mauaji ambayo yalitekelezwa wakati huo ambapo maiti za watu zilitapakaa kote nchini. Hisia hizi zinamwathiri msomaji pia.

Hali kadhalika, hisia za hasira zimedhihirishwa pia katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Wanda' (uk 29). Mshairi anasema:

Ewe mkazi wa wanda
Wewe
Adui wa maumbile,
Wewe
Hasidi wa wewe mwenyewe,
Wewe
Ambaye umetia kitanzi
Kwenye shingo ya mazingira

Shingo yako mwenyewe
Shingo za wajukuu na vitukuu…

Katika kifungu hiki, mshairi amekasirishwa na vitendo vya binadamu vinavyoathiri mazingira. Wanadamu wameshiriki mbinu zisizofaa za kilimo pamoja na kufyeka misitu huku wakiathiri udongo na makazi mema ya wanyama na wadudu. Hisia za kilio zinajitokeza katika shairi la 'Ni Kweli? (uk. 55). Mshairi anasema:

…Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba baadhi ya wakembe wa kike
Hutiririkwa na machozi na damu
Baada ya wazazi wao halisi wa kiume
Kuwasagasaga kama nyama ya sambusa?

Mshairi ametumia swali, 'Ni Kweli?' kugusa hisia za msomaji. Anaibusha suala la uozo wa kimaadili katika jamii. Mshairi analilia jinsia ya kike ambayo inadhulumiwa na jinsia ya kiume katika jamii. Wasichana wanalazimishwa kushiriki ukahaba angalau watafute kitoweo huku mabinti wakishurutishwa na wazazi wao wa kiume kushiriki ngono wakati wazazi wao wa kike wanapokuwa katika shughuli za nje.

Hisia za huruma zinadhihirishwa katika diwani ya *Rangi ya Anga*, ushairi wa 'Rangi ya Anga' (uk.26). Mshairi anasema:

Walimu wenye jukumu adimu la kuwalea
Watu wenye ukuruba wa ki-damu nao
Majirani waliowaona tangu wakiwa wakembe
Hao ndio hasidi wakuu maishani mwao
Hao ndio wawapigao kwa gruneti
Ndio wawatungao jinamizi tumboni…

Katika kifungu hiki, mshairi anazungumzia masaibu yaliyompata banati katika jamii kutokana na jamii kutawaliwa na taasubi ya kiume. Mshairi anamhurumia mwanafunzi wa kike ambaye anatiwa mimba na mwalimu ambaye anafaa kuwa kielelezo chema kwake, kisha hakuna hatua yoyote ya kisheria inayochukuliwa kumwadhibu mwalimu

huyu; yuko huru kama mbayuwayu tu. Hisia hizi za huruma hazina budi kumwathiri msomaji pia.

Hali kadhalika, mshairi anaibusha hisia za furaha katika shairi la ‘Ukarimu wa Ekweta’ (uk. 78). Anasema:

> Asanteni jua, mvua, udongo na hewa
> Ushirikiano wenu na mkono wa mkulima
> Umeifanya meza ya kiamsha-kinywa
> Kuwa mwandani wa kutamanika
> Katika urafiki wa kuaminika…

Mshairi amejawa na furaha kutokana na mazingira mazuri ya maeneo ya Ekweta. Anasifu jua, mvua, udongo, hewa na juhudi za mkulima katika uzalishaji mazao. Eneo hili la Ekweta ni chimbuko la matunda yaliyonawiri ya parachichi, chungwa, papai, ndizi, nanasi, embe, tufaa, pera na plamu. Msomaji anapolisoma shairi hili anafaa kufurahia kutokana na maneno ya shukrani yaliyotumika. Kwa mfano, ‘Asanteni’.

Hisia za woga zinadhihirika katika shairi la ‘Mkataba Tena’ (uk. 28) katika kifungu cha 5 na 6. Mshairi anasema:

> …Leo, wanawake na wasichana wa nyanda za mazoezi
> Wataishi kwa utulivu bila ukungu mzito wa wasiwasi
> Au jinamizi limerejea kuwafunika kwa wingu la dhiki?
>
> Serikali itawalinda kwa sheria zisizoogopa Bulkinum
> Au wanawake wanatarajiwa kujilinda wenyewe
> Labda kwa kuvaa sufi za chuma?

Katika vifungu hivi, hata baada ya serikali ya Sudani Kusini kutia sahihi mkataba wa amani na maridhiano, mshairi amefasiri kuwepo kwa woga kwa wananchi waliohasiriwa wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe. Jambo hili pia linaibusha hisia za woga kwa msomaji na kumwacha katika hali ya taharuki. Je, wanawake na wasichana wataishi

katika hali ya utulivu? Je, serikali itawalinda au watawachwa kujilinda wenyewe dhidi ya wahalifu na wahuni?

Kwa hivyo, inadhihirika kwamba ushairi katika diwani zote mbili umetawaliwa na hisia mbili: mbaya na nzuri; hisia mbaya zikidhihirika zaidi. Hii ni ishara ya kwamba hivyo ndivyo hali ilivyo katika jamii kwa sababu mshairi ni sauti ya wanajamii. Aidha, mtunzi wa diwani teule ameathiriwa na maisha ya wanajamii; jambo ambalo limeathiri utunzi wake. Mtindo wake wa matumizi ya lugha unaibua hisia ambazo zinamwathiri msomaji pia. Kwa hivyo, ni rahisi msomaji kujinasibisha nao.

### 3.4 Matumizi ya Toni katika Kuwasilisha Ujumbe

Kwa mujibu wa Wamitila (2008: 243), uchanganuzi wa mashairi hauwezi kuepukana na suala la sauti ya nafsi ya kishairi au ya mtu anayelisoma shairi hilo. Aidha, anasema toni inaweza kuangaliwa kwa njia mbili. Kwanza, kama dhana dhahania ya kisauti inayohusishwa na utungo na ambayo hufumbatwa na utungo huo na kuwa kama aina ya 'roho' yake. Aidha, kuna aina mbalimbali za toni: toni ya ucheshi, mzaha, dhati, kali, dhihaka, uchungu, huzuni na kadhalika. Pia, toni inaweza kuangaziwa kwa kurejelea 'usikikaji' wa sauti ya shairi. Usikikaji huu unaweza athiri maana ya ushairi au kwenda kinyume nao. Kutokana na maelezo haya, ni muhimu kwa msomaji kuchambua toni kwa kuangazia muktadha na uteuzi wa msamiati. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Tope la Mizozo' (uk. 6). Mshairi anasema:

> Serikali iliyoingia ikibeba vibuyu vya asali
> Ikivaa gwada pendezi lenye rangi za upinde-wa-mvua
> Ni kama binadamu aliyekula kiapo kisichovunjika:
> "Naapa, kamwe sitafuata barabara ya lami na usalama
> Daima nitapita kwenye njia ya tope zito la mizozo
> Ewe Mungu usiniondoe kutoka kwenye dimbwi la huzuni!...

Katika kifungu hiki cha kwanza, toni ya kejeli imedhihirishwa wakati ambapo mshairi anawasuta wanasiasa wa Chama cha 'Rainbow Coalition' nchini Kenya yaani 'Upinde wa Mvua', waliopigiwa debe na wananchi huku wakiwapa ahadi za asali lakini pindi tu walipoingia uongozini wakawasahau na badala yake kushiriki ufisadi ili kujilundikia mali.

Toni ya kejeli pia imedhihirishwa katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Kwa mfano, katika shairi la 'Zimwi la Theluji' (uk. 51-52). Mshairi anasema:

> …Kwa ukungu wa hila
> Zimwi la theluji
> Liliapa kwa mbingu
> Na ardhi na nyota
> Kwamba lilikuwa na dhima
> Ya wakala wa Mungu…

Katika kifungu hiki, mshairi anasimulia kuhusu 'Zimwi la Theluji'. Anakejeli vitendo vya 'Zimwi la Theluji' ambalo linaashiria wamishenari ambao walikuja kueneza injili kwa Wakenya, kumbe walijawa na hila ili kuweza kuwapisha wakoloni waingie nchini na kutamalaki huku wakinyakua rasilmali na malighafi ya nchi.

Toni ya chukizo pia imedhihirishwa katika mashairi kadhaa. Kwa mfano, katika shairi la 'Msimu Mwingine wa Wasaliti' (uk. 12). Mshairi anasema:

> Vitimbakwira watarudi karibuni kutoka karamu haramu
> Utaziona barakoa za tabasamu kwenye nyuso zao
> Watakuja kutugawia peremende zenye sumu ya akili
> Wataleweshा watu kwa pombe kutoka vibuyu vya maneno
> Wataahidi kesho yenye mapipa ya maziwa na mitungi ya asali
> Nasi, tukiongozwa na ramani ya tumbo na dira ya ubonafsi
> Tutapanga milolongo katika mvua na matope ya Disemba
> Kukaribisha, labda, msimu mwingine wa wasaliti

Mshairi anawaita wanasiasa vitimbakwiri kwa sababu wametawaliwa na ubinafsi. Kusudi lao kuu la kushiriki siasa si kuendeleza demokrasia bali kujinufaisha wao wenyewe. Nao wanajamii hawajabaki nyuma, ubinafsi na tamaa vinawaelekeza kuchagua viongozi wasiofaa.

Toni ya uchungu imedhihirishwa katika shairi la 'Magenge Matatu' (uk. 32). Mshairi anasema:

> …Genge la tatu, nusu-mazimwi
> Lilituahidi katiba mpya na dawa kali dhidi ya ufisadi
> Tukaamini wimbo, "Yote yawezekana bila Mfalme wa Nzige"
> Baada ya miaka minne ya hila, tamaa na uzingizi ulingoni
> Ahadi iliyomwesamwesa kama nyota ya taifa jipya
> Imemezwa na wingu la ujanja na harufu ya ufisadi

Mshairi ameghadhabishwa na uongozi nchini Kenya tangu kujipatia uhuru mnamo mwaka wa 1963. Kila msimu wa uongozi ulitawaliwa na ahadi ambazo hazikutimizwa; bado nchi inapigana vita na uzingizi, tamaa, hila na ufisadi. Uchungu huu unamwelekeza kutumia maneno, 'genge' na 'mazimwi' kurejelea vikundi vitatu vya viongozi wasaliti.

Toni ya ukali imedhihirishwa kwa wingi zaidi katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Kwa mfano, katika shairi la 'Rangi ya Anga' (uk. 8). Mshairi anasema:

> Sikiza hiyo sauti
> Ulimi ukitoa kauli
> Kama upanga mkali
> Ukikata mmea mchanga:
>
> > Wewe sasa ni mtu mzima
> > Mshale wa mizani ya miaka
> > Unaonyesha miaka kumi na minne,
> > Mbona usiolewe na Mzee Malimali
> > Kusudi mahari ya ng'ombe na mbuzi
> > Ituzimie moto wa umaskini
> > Kama wingu kuu la masika likizima ukame nyikani?...

Mshairi anaonyesha namna mzazi wa kiume anavyomshurutisha bintiye aliyehitimu miaka kumi na minne kushiriki ndoa ili kuzima moto wa umaskini katika familia.

Matumizi ya lugha kudhihirisha toni ya ukali yameendelezwa pia katika shairi la 'Wanda' (uk. 28). Mshairi anasema:

> …Jua!
> Ewe Jua!
> Jua la wanda za mikwaju,
> Mimea na samaki
> Ndege na wadudu
> Na wanyama na mito
> Walikutenda ovu gani
> Kukuchochea ulipishe kisasi
> Kwa ghadhabu pujufu?

Katika kifungu hiki, mshairiameghadhabishwa na makali ya jua kwa mimea, samaki, wadudu, wanyama na mazingira. Mtunzi ametumia lugha kuibusha toni ya dharau katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Rangi ya Anga' (uk. 10). Anasema:

> Sikiza sauti ya mzazi
> Ambayo inakuja juu
> Kama wimbi la sumu
> Ikimimina kemikali kali
> Katika akili asubuhi:
> Usicheke kiholela
> Kama wewe ni mwanamke!
> Nyamaza! Futa machozi!
> Ushindwaye na madogo
> Kama mavazi yako
> Ni kamisi na rinda!

Katika kifungu hiki, mzazi wa kiume anamshutumu mwanawe wa kiume kwa kumwambia kwamba hafai kucheka kiholela kama mwanamke wala hafai kulia na kushindwa na madogo kama mwanamke. Hii ni ishara ya kumdharau mwanamke.

Toni ya kusifu imejitokeza katika mashairi kadhaa katika *Msimu wa Tisa*. Kwa mfano, katika shairi la 'Ntharene' (uk. 74). Mshairi anasema:

…Ntharene, nembo ya ukarimu wa mashamba:
Kandokando mwa barabara ya mizingozingo
Wanakijiji wenye urafiki shakiki na udongo
Wamepanga wanga, mapapai, tamata na ndizi
Na parachichi, viazi vikuu na viazi vitamu…

Mshairi anasifu eneo hili kwa shughuli za kilimo zinazoendelezwa humo. Anatumia neno,'ukarimu' kuonyesha jinsi eneo la Ntharene lilivyo na rotuba. Pia ametumia neno, 'urafiki' kuashiria namna wakulima wa eneo hili wanavyofurahia kilimo cha kila aina ya mimea. Eneo hili linakuzwa kila aina ya vyakula ambavyo vinainua kiwango cha uchumi kwa wenyeji. Mazao yanayokuzwa ni kama vile, mapapai, tamata, ndizi, parachichi, viazi vikuu na vitamu.

Inadhihirika kwamba toni inaibuliwa na mshairi kutokana na matumizi yake ya lugha; jambo ambalo msomaji naye anafaa kutambua. Kwa hivyo, msomaji hana budi kuelewa toni ya ushairi ili kuufasili ujumbe ipasavyo.

### 3.5 Hitimisho

Sura hii imehakiki dhima ya vipengee vya kigrafolojia. Mathalan, viakifishi, marudio na takriri, matumizi ya lugha ya kawaida yenye kuibua hisia, mguso na taathira pamoja na toni katika kuwasilisha ujumbe. Mbinu hizi zinashabihiana kimatumizi na huibusha ujumbe moja kwa moja. Aidha, ni muhimu katika kujenga ujumi wa ushairi teule na kumpa msomaji motisha ya kusoma tena na tena. Kutokana na uchanganuzi huu, mbinu hizi ni muhimu katika kudhibiti usomaji wa ushairi teule pamoja na kujenga wizani. Kupitia vipengee hivi vya kimtindo, ubunifu wa mshairi umebainika. Hali kadhalika, vipengee vya kimtindo ni vingi sana visingeshughulikiwa katika sura moja tu; vingine

vitashughulikiwa katika sura ya tano. Sura ya tano inashughulikia dhima ya vipengee vya kimtindo vya kitamathali na vinavyotegemea muktadha.

# SURA YA NNE

# SIFA ZA KITAMATHALI NA ZINAZOTEGEMEA MUKTADHA KATIKA DIWANI ZA *MSIMU WA TISA* NA *RANGI YA ANGA*

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia vipengee zaidi vya kimtindo ambavyo vinajenga mashairi teule katika diwani mbili teule, mathalan, vipengee vya kitamathali na vile vinavyotegemea muktadha. Mtunzi amevitumia vipengee hivi kuonyesha umilisi wa lugha pamoja na upekee wake katika utunzi wa diwani teule. Kulingana na Mberia (1990: 81) mojawapo ya sifa muhimu za fasihi, ukiwemo ushairi, ni kuwasilisha fikra, hisi na tajriba kwa njia ya kupendeza. Aidha, kupendeza huko kunatokana na ufasiri wa lugha ilivyotumiwa kisanaa na kuwa vina na mizani si njia pekee ya kupambia shairi. Anasisitiza kwamba kuna sifa nyingine ambazo huchangia ufasiri wa shairi na laweza kuvutia kwa sababu ya matumizi bora ya jazanda, tashbihi, tashhisi, balagha, chuku na tamathali zinginezo. Maelezo haya yana baadhi ya mbinu za kitamathali ambazo tumetumia katika utafiti wetu.

Kwa mujibu wa Indede (2008: 80), wanamapinduzi wanasisitiza kwamba matumizi ya lugha, jazanda na taswira yanadhihirisha kiwango cha juu katika utunzi wa mashairi. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba diwani teule zimepanua uwanja wa hadhira kwa sababu ya lugha yake ya kawaida ambayo inawafikia hata watu ambao hawana talanta ya kubuni, kuimba wala kuhakiki ushairi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2008: 231), mtindo ni elementi muhimu sana katika kazi ya fasihi. Isitoshe, mchanganuzi wa matini ya fasihi anapaswa kuchunguza mambo mengi

yakiwemo uteuzi wa msamiati, matumizi ya tamathali za usemi na jazanda, dhamira, usimulizi na mbinu za usimulizi, wahusika, sifa za uakifishi zinazoelekea kukiuka njia za kawaida za kuakifisha na masuala mengineyo. Sura hii imechunguza baadhi ya elementi hizi. Vilevile, anasema kwamba mtindo ni dhana pana na huelezea zile sifa zinazoibainisha kazi fulani na kuitenga na kazi nyinginezo na labda hata kumtambulisha mtunzi anayehusika. Kutokana na maelezo ya Wamitila, mtindo alioutumia Kithaka wa Mberia unaonyesha upekee wake katika utunzi wa mashairi; jambo ambalo lilitupelekea kuchambua diwani zake mbili: *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Mihimili ifuatayo imetumiwa kuchunguza sifa za kitamathali na zinazotegemea muktadha katika Diwani teule:

1. Viwango vya kimofolojia na kisintaksia ni msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matumizi ya lugha yenyewe.
2. Miundo ya lugha na lugha ya kitamathali huonyesha jinsi lugha inavyoathiri maana kwa njia fulani.

Hali kadhalika, sura hii imechunguza dhima ya sifa zifuatazo za kimtindo:

i. Matumizi ya vipengele vya kitamathali kuliko vya kiarudhi katika kuwasilisha dhamira
ii. Matumizi ya lugha kutegemea muktadha

## 4.1 Matumizi ya Vipengele vya Kitamathali kuliko vya Kiarudhi katika Kuwasilisha Dhamira

Kulingana na Kuvuna, Mvati na Maliachi (1992: 21), tamathali za usemi ni mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika maandishi au mashairi kwa nia ya kuongeza maana kwenye lugha na fikra za mshairi au mwandishi. Naye, Wamitila (2003) anasema

kwamba tamathali za usemi hutumiwa kuelezea fungu la maneno au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi na kuwa na maana nyingine. Katika ushairi huu, vipengee mbalimbali vya kitamathali vimetumika ili kuufanikisha ujumbe. Baadhi ya vipengee hivi : jazanda, taswira, sitiari, taashira na tashbihi. Mtunzi ametumia mbinu hizi kuonyesha umilisi wa lugha pamoja na upekee wake katika utunzi wa mashairi teule.

### 4.1.1 Jazanda

Jazanda ni mojawapo wa tamathali za usemi ambazo washairi hupenda kutumia ili kuuficha ujumbe na kumpatia msomaji nafasi ya kutafakari zaidi. Kulingana na King'ei na Kemoli (2001: 55), jazanda ni ulinganishi wa moja kwa moja wa vitu viwili bila ya matumizi ya viunganishi. Aidha, ni matumizi ya lugha ambapo vitu, dhana na maneno hupewa maana isiyokuwa ya kawaida.

Katika utafiti wetu, ulinganisho wa kijazanda unadhihirika kupitia kauli/maelezo, taashira au taswira. Isitoshe, mshairi ametumia jazanda ambazo zinatokana na mazingira anayoyafahamu na yanayofahamika na hadhira lengwa. Kusudi la mshairi ni kurahisisha uelewekaji wa ushairi kwa hadhira yake. Hajatumia tu kauli bali ametumia michoro katika jalada iliyo na maana fiche.

Kithaka wa Mberia ametumia anwani za kijazanda katika *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga* kimaksudi. Amelenga kumpatia msomaji/mhakiki ufahamu zaidi. Pia, anakusudia mhakiki aweze kutafsiri na kufasiri ujumbe kwa njia bora zaidi. Aidha, kumfanya msomaji kufikiria kwa makini. Isitoshe,, kutia uzito zaidi katika ujumbe. Anwani 'Msimu wa Tisa' ni ishara ya Bunge Tisa katika nchi ya Kenya tangu 1963. Hivi ni vipindi vya

kisiasa nchini ambapo tamaa na ubinafsi unadhihirika kwa pakubwa. Haya yanaashiriwa kwenye jalada lake ambalo lina picha ya mwanamume mwenye kitambi ambacho uchi wake unadhihirika wazi, shati haliwezi kufungika kutokana na ukubwa wa tumbo lake. Hali hii inadhihirisha dunia iliyojaa uozo mwingi mkiwemo ubinafsi na ufisadi. Isitoshe, katika vipindi hivi tisa vya utawala nchini Kenya, mna uozo mwingi unaoendelezwa katika nchi zinginezo katika bara la Afrika kama vile Sudan na Msumbiji.

‘Rangi ya Anga’ vilevile ni anwani ya kijazanda kudhihirisha masuala mbalimbali yanayokumba jamii kama vile jinsia, mazingira, ukoloni na dini. Hii inamaanisha ya kwamba anga ya jamii ina rangi mbalimbali. Mchoro katika jalada unadhihirisha haya. Kwa mfano, kuna picha ya kiatu kinachokanyaga mwanamke kuonyesha namna wanawake wamedhalilishwa katika jamii hasa katika elimu, ndoa na vyeo. Isitoshe, mna mti uliokauka hadi mizizi kuonyesha namna mazingira yameathirika vibaya.

Jazanda haijadhihirika tu katika anwani na jalada pekee bali katika anwani za mashairi mengine. Kwa mfano, katika *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Usingizini’ (uk. 3), haimaanishi ya kwamba ni usingizi wa kawaida ila ni kuonyesha namna wananchi na hasa Wakenya wamebaki nyuma kimaendeleo badala ya kutumia rasilmali walizonazo kujipatia riziki. Kwa mfano, ardhi yenye rotuba imeachiwa nguchiro na panya badala ya wananchi kushiriki kilimo ili wajiepushe na janga la njaa. Mshairi anaonyesha namna viongozi pia hawajazinduka ili kuwaokoa wananchi kutokana na minyororo ya njaa.

Katika *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Tope la Mizozo’ (uk.6), mshairi ametumia jazanda katika anwani hii. ‘Tope’ ina ishara ya doa na ‘mizozo’ ni ugomvi au ghasia. Kwa hivyo,

hii ni serikali iliyojawa na uongozi mbaya usiozingatia demokrasia hata kidogo. Ni viongozi walio mbioni kupigania maslahi yao, kuendeleza siasa potovu na kutawaliwa na ufisadi, tamaa na ukoloni mamboleo. Wamevunja sheria za nchi kwa ujanja na kuwatumia wahuni wanaowadharau wenyeji na kuvamia haki zao hadi hamna usalama tena. Kwa mfano, katika kifungu cha tatu. Mshairi anasema:

> …Katika ukungu wa werevu bila maarifa
> Wenye tamaa kubwa ya kuwapiku wengine
> Walitumia ujanja kwenye sinia ya mamlaka
> Wakajitwalia minofu na kuwachia wenzao makano
> Gundi ya mkataba uliounga pamoja makundi
> Ikayeyushwa na moto wa hamaki ya haki…

Katika kifungu hiki, viongozi waliochaguliwa wako mbioni kujitwalia mali na kuwasahau wananchi waliowachagua. Mshairi ametumia maneno haya mawili, 'Tope' na 'Mizozo' katika anwani ya shairi hili kuupa uzito ujumbe wake na kunasa nadhari ya msomaji manake hamna mtu yeyote mwadilifu angependelea kupakwa tope au kushiriki mizozo.

Katika *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Msimu wa Tisa' (uk. 9), mshairi pia ametumia anwani hii kijazanda. Kwa mujibu wa TUKI (2004: 388), msimu ni kipindi kirefu cha wakati ambapo jambo au hali fulani hutokea; msimu wa maembe au upepo. Kwa kuzingatia takwimu zetu, anwani hii ina maana ya Bunge la Tisa katika nchi ya Kenya tangu kujipatia uhuru mwaka wa 1963. Anwani hii inamwacha msomaji katika hali ya taharuki ya kutaka kujua ni yepi mshairi anaangazia. Vilevile, inampa msomaji nafasi ya kutafakari zaidi kuhusu matukio ya kihistoria katika misimu minane iliyotangulia. Msomaji pia anapata nafasi ya kulinganisha na kulinganua matukio ya misimu iliyotangulia na msimu wa tisa.

Kando na anwani ya ‘Msimu wa Tisa’ kuna kauli za kijazanda zilizotumika. Kwa mfano, katika kifungu cha pili. Mshairi anasema:

> Ni nani atakayeimba wimbo wa uzalendo
> Katika huu ukumbi wa msimu laanifu wa tisa
> Ambamo nyoyo za waliotumwa kujenga taifa
> Zinadunda kwa mpigo wa ubinafsi uliokithiri-
> Ukumbi ambamo wingu la nzige wa jangwa
> Linakula karamu haramu kwenye mti wa jamhuri…

Katika kifungu hiki, ukumbi wa msimu laanifu wa tisa ni bunge la tisa ambalo limelaaniwa kutokana na ubinafsi wake. Badala ya kujenga taifa wanashiriki tamaa na ulafi na kufananishwa na wingu la nzige wanaoshiriki karamu haramu; wanafurahia matunda ya uhuru. Hawa viongozi katika kifungu cha tatu, walivamia ghala la taifa kwa tamaa inayovuma. ‘Ghala’ ina maana ya utajiri/ miliki ya taifa. Wako mbioni kujitwalia mali bila kujali wananchi.

Katika *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Kitini’ (uk. 18), anwani hii ina maana ya ‘katika uongozi au mamlaka’. Inadhihirika kwamba walio mamlakani wamestareheka na kuwasahau waliopigania uhuru. Mbinu hii ya jazanda imeendelezwa katika baadhi ya mashairi katika *Msimu wa Tisa*. Kwa mfano, shairi la ‘Wenda-wazimu Kongo’ (uk. 19), wenda-wazimu tu sio watu waliopungukiwa na akili na labda kuonekana wakienda uchi au kuzurura mitaani, ina maana ya genge la wahuni wa jeshi la taifa waliopungukiwa na akili kiasi ya kwamba hawana utu, wamefanya matendo ya kikatili kwa wananchi wenzao kama vile kuwapiga risasi hadi kifo, kuwaangamiza kwa kutumia gruneti na mabomu, kuwapiga kwa vijiti na kuwabaka kina mama. Dhana hii inanasa akili ya msomaji na kumpa hamu ya kutaka kujua ni yepi yaliyotokea Kongo kudhihirisha wendawazimu.

Katika shairi, ‘Mlima wa Dhahabu’ (uk.23), anwani hii ni ya kijazanda kumaanisha mabilioni ya fedha za kigeni nchini ambazo zimeathiri thamani ya shilingi. Vitimbakwiri wanatumia mamlaka yao kuagiza fedha hizo huku wakiifilisisha nchi. Jambo hili linaleta kupanda kwa gharama ya maisha na uhawinde kushika kasi. Wanaodhibiti hela katika Benki Kuu wanazidi kujinufaisha kutokana na hazina ya Benki Kuu huku uchumi wa nchi ukizorota. Mshairi anasema hii ni hazina nzuri ya kuhifadhi kupe mamlakani. Kupe hapa imetumiwa kijazanda kumaanisha vitimbakwiri.

Katika shairi, ‘Magenge Matatu’ (uk. 32), mshairi amezungumzia magenge matatu ya mazimwi. Neno, ‘genge’ lina maana ya kundi la watu nalo neno, ’mazimwi’ linaleta dhana ya viongozi waangamizi au wanaoleta madhara. Mshairi ametumia jazanda ili kutilia uzito ujumbe anaotaka kuupasha kwa wasomaji. Vilevile, anataka msomaji atafakari zaidi kuhusu makundi hayo matatu katika utawala wa nchi. Kundi la kwanza la mazimwi linaashiria viongozi chini ya utawala wa rais wa kwanza wa nchi ya Kenya ambao walitawaliwa na ulafi na ufisadi. Genge la pili ni kundi la viongozi chini ya utawala wa rais wa pili nchini ambalo japo liliahidi amani, upendo na umoja, walibadilika na kuwa waharibifu; wanafananishwa na viwavi na nzige. Genge la tatu ni nusu- mazimwi. Hawa ni viongozi chini ya rais wa tatu nchini. Ijapokuwa walishiriki uundaji wa katiba mpya na kuahidi kuuondoa ufisadi, bado ufisadi, tamaa na ujanja vilitawala.

Katika shairi, ‘Mafuta yenye Damu’ (uk. 48), mshairi ananasa nadhari na hisia za msomaji kwa kutumia anwani hii. ‘Mafuta yenye damu’ ni anwani inayoashiria namna watu wa Sudan walivyoshiriki vita na kumwaga damu katika harakati za kung’ang’ania

mabohari ya mafuta. Katika shairi, ‘Macho Mekundu’ (uk. 59), mshairi anaanza kwa kutupatia taswira ya macho mekundu. Je, haya macho mekundu yanatokana na athari gani? Mshairi anaonyesha athari za dawa za kulevya kwa watoto pamoja na maisha yao yaliyojaa dhiki. Mshairi anasema, ‘watoto hawa wanaishi katika mbuga katili’ kumaanisha wanaishi katika ulimwengu usiowajali wala usiokuwa na huruma.

Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la ‘Zimwi la Theluji’ (uk. 48) limebuniwa kwa kutumia jazanda. Jazanda hii inatuacha katika hali ya taharuki ya kutaka kujua hasa lililomo ndani ya shairi hili. ‘Zimwi la Theluji’ ni anwani ambayo inaashiria athari mbaya za weupe yaani wakoloni pamoja na wamishenari. Wamishenari walitufanya sisi Waafrika kuasi dini yetu na kuiga yao, nao wakoloni wakavamia ardhi yetu yenye rotuba kwa nguvu na ujanja.

### 4.1.2 Taswira

Kulingana na Kahigi na Mulokozi (1979), taswira ni mbinu ya matumizi ya picha katika utungo na katika mawazo ya msomaji wa utungo huo. Aidha, picha ni matumizi ya lugha yanayopambanuliwa na uteuzi mzuri wa maneno, uangalifu na udhahiri wa maelezo yenye kuhusisha na kujumuisha dhana moja ili kuleta taswira na athari maalumu katika mawazo ya msomaji. Wataalamu wengine wanaounga mkono maelezo haya ni kama vile Senkoro (1988: 37), Kuvuna, Mvati na Maliachi (1992: 25) na King’ei na Kemoli (2001: 58). Aidha, King’ei na Kemoli (2001: 58), wanasema kuwa mshairi mara nyingi huunda taswira ili kumpa msomaji picha kamili za kimawazo za yale anayosimulia. Isitoshe, picha hizi huweza kufafanua tukio, hali fulani ya mhusika au kisa fulani.

Hali kadhalika, Senkoro (2011) anaeleza kwamba matumizi mazuri ya taswira hutegemea utunzi wa msanii wa kuweza kuchota mambo yanayomzunguka na jamii yake, pia kutoka katika historia na sehemu nyingine za maisha azijuazo. Aidha, taswira husaidia picha kuganda akilini na kunasisha ujumbe wa msanii kwa wasikilizaji au wasomaji husika. Kutokana na maelezo haya, mshairi mbunifu hutumia taswira ambayo inaonekana waziwazi na huitumia kwa ukamilifu katika kujenga utajiri na uzito wa maudhui ya shairi lake. Matumizi mazuri ya taswira humfanya msomaji wa shairi auelewe ujumbe wa shairi.

Matumizi ya taswira katika diwani teule yana dhima kuu kwa mshairi pamoja na msomaji. Mshairi Kithaka wa Mberia ametumia taswira kimaksudi ili kurahisisha uelewekaji wa kile anachozungumzia. Pia, kuvuta hisia zaidi na kujijengea taswira za ulimwengu mpya. Utafiti wetu unaunga mkono kauli za King'ei na Kemoli (2001: 58) wanaposema kwamba taswira huonyesha mshabaha kati ya ukweli wa maisha na picha inayopatikana. Vilevile, husaidia kupata hisia fulani kutokana na uhalisi wa hali ya kijamii na ya kisiasa, anayoisimulia mshairi.

Kulingana na Senkoro (1988: 41), taswira zinaweza kugawanywa katika makundi matatu: taswira zionekanazo, taswira za mawazo na taswira za hisi. Naye Wamitila (2003: 225), ameainisha taswira katika makundi kadhaa, mathalan, taswira kuu, kimsingi, harufu/mguso, kimaelezo, kiishara, joto, mguso, mwendo, mwonjo, usikivu na za wingine. Taswira hizi zinaweza kutambulika katika shairi moja au mashairi tofauti. Katika utafiti huu, taswira zifuatazo zimeangaziwa:

**a. Taswira zinazoangazia matukio halisi**

Hizi ni taswira ambazo zinadhihirika wazi kwa msomaji kupitia picha inayochorwa akilini mwake kuhusu tukio fulani. Diwani ya *Msimu wa Tisa* ina mifano anuwai ya taswira zinazoangazia matukio halisi. Kwa mfano, katika shairi, 'Usingizini' (uk. 3). Anwani hii inatupa picha ya mtu aliyelala. Aidha, katika kifungu cha pili, mshairi anasema:

> Daima dawa ya thamani inatiririka katika mito
> Inatupita na kumezwa ovyo na bahari na maziwa
> Katika taifa linalonyongwa na mikono ya njaa

Mshairi anatupa picha ya namna wananchi wamefikwa na janga la njaa kutokana na uzembe wao pamoja na tamaa na utepetevu wa viongozi. Tunapata taswira ya udongo wenye rotuba ukisafirishwa kwenye bahari na maziwa na kuacha wananchi hoi wakiwa wamefungwa na minyororo ya njaa.

Katika shairi, 'Mkasa', (uk. 13), katika kifungu cha tano, mshairi anatupa taswira ya mlipuko wa bomu. Anasema:

> Vigae vya vioo, vichane vya mbao na matambara
> Vinatawanyika na kutangaza siku geni nchini
> Hewa imejaa harufu ya mayai yaliyooza
> Ushahidi thabiti wa janga la bomu nchini.

Katika kifungu hiki, tunaona wananchi waliochangamkia kazi zao asubuhi na mapema wakifikwa na janga la mlipuko wa bomu uliotokea katika maeneo ya ubalozi wa Mwewe. Picha ya hali ilivyo inadhihirika katika akili ya msomaji anaposoma.

Katika shairi, 'Darfur', (uk. 26), tunaona picha ya Wasudani wenye ngozi nyeusi katika vijiji vya Darfur. Katika kifungu cha nne, mshairi anasema:

Vijijini, wanawake na wasichana wa rangi ya mpingo
Wanalipuliwa kwa makombora dhalilishi ya ubakaji
Huku jamaa zao wa kiume, bila silaha za kisasa
Wakisakwa na mauti yakibebwa na ngamia
Na kumiminiwa risasi zenye nembo ya serikali

Mshairi anatuchorea taswira ya wenyeji wakishambuliwa na wenzao kwa bunduki, nyumba zao kuchomwa na wanawake na wasichana kubakwa.

Mshairi ameendeleza taswira hii ya mashambulizi na maafa Kusini Sudan katika shairi, 'Mafuta yenye Damu', (uk. 48), kifungu cha 2. Anasema:

Naona majeruhi, dam una maiti
Maiti za wakulima mashambani
Maiti za wachungaji malishoni
Maiti za Watoto shuleni
Maiti za vikongwe vijijini

Mshairi anatupa picha ya maafa yanayotekelezwa kwa wakulima, wachungaji malishoni na watoto shuleni bila kusaza yeyote.

Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, mshairi ametuchorea taswira mbalimbali kupitia ushairi huu. Kwa mfano, katika shairi la mwanzo, 'Rangi ya Anga' shairi la 6, (uk. 8). Mshairi anasema:

Sikiza hiyo sauti
Ulimi ukitoa kauli
Kama upanga mkali
Ukikata mmea mchanga:
    Wewe sasa ni mtu mzima
    Mshale wa mizani ya miaka
    Unaonyesha miaka kumi na minne,
    Mbona usiolewe na Mzee Malimali
    Kusudi mahari ya ng'ombe na mbuzi
    Ituzimie moto wa umaskini
    Kama wingu kuu la masika
    Likizima ukame nyikani?...

Mshairi anazungumzia masaibu yanayokumba jinsia ya kike, si katika ndoa, si katika milki, si katika elimu na ukeketaji. Tunaona taswira ya mzee katika boma akimwambia bintiye kwamba amefikia umri wa kuolewa bila kutilia maanani ya kwamba hiki ni kitoto kichanga cha miaka kumi na minne tu. Katika shairi la 'Wanda', (uk. 30), tunaona jinsi hali ya mazingira ilivyo baada ya wananchi kukata miti, kushiriki kilimo cha lima-hama-lima na kilimo cha mifugo wengi katika vikataa, hatimaye kusababisha mmomonyoko wa udongo.

**b. Taswira za mawazo**

Hizi ni taswira za kuwazika tu na hulifanya fumbo liwe nzito. Humfanya msomaji atafakari zaidi kuhusu kinachozungumziwa na mshairi. Kulingana na Kuvuna, Mvati na Maliachi (1992: 26), taswira za kimawazo huelezwa kwa kutumia hali dhahanifu za kufikirika tu. Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Zimwi la Theluji' linatuchagiza kuwaza zaidi kuhusu 'Zimwi la Theluji'. Anwani hii ina maana gani? Zimwi linaashiria watu walio na ngozi nyeupe waliozuru bara la Afrika na hasa Kenya kwa madhumuni tofauti. Hawa ni Waarabu, Wareno, wamisheni na wakoloni Wazungu. Katika shairi, 'Zimwi la Theluji' (uk. 49-51), zimwi linaashiria Waarabu na Wareno waliozuru Kenya kusudi wasakini na kuendeleza biashara. Katika, shairi lilo hilo, (uk. 51 na 52), zimwi lililotoka upande wa pili, lilikuja na masimulizi ya Baba na Mwana na kudai kwamba Mwana aliwafunza binadamu kula nyama ya mwili wake na kunywa damu yake. Kwa waumini wa dini ya Kikristo, Baba ni Mungu Muumba, Mwana ni Yesu Kristo ambaye alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi za binadamu ili kuwaletea wokovu. Ndiye tu aliandaa Meza ya Bwana; shughuli ambayo inaendelezwa na Wakristo hadi wa leo.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Msimu Mwingine wa Wasaliti' (uk. 12), mshairi anamfanya msomaji awazie kuhusu msimu mwingine wa uongozi baada ya Bunge la Tisa. Ni dhahiri shahiri kwamba viongozi wale wale wasaliti watachaguliwa tena baada ya kulewesha watu na ahadi za uongo. Vilevile, katika shairi, 'Johari Angani' (uk.34), mshairi anatupa taswira ya chombo kinachosafiri angani chenye nembo ya taifa. Msomaji kutoka Kenya atawazia kuwa huenda chombo hiki ni ndege aina ya *Kenya Airways*, kito au johari ya thamani.

Katika shairi, 'Mnara Mwangavu' (uk. 36), mshairi anatupatia nafasi ya kuwazia kuhusu jengo refu linaloangaza kote. Anapotaja kuhusu mapambano ya wenyeji na makaburu na damu kumwagika Soweto, inambidi msomaji awazie kuhusu ukombozi wa Afrika Kusini chini ya uongozi wa Hayati Nelson Mandela. Mshairi anasema:

> …Afrika itasimama uwanjani
> Na kwa sauti imara kama kengele
> Kusema:
> Mnara wetu wa almasi ya utu
> Ni mwangavu kuliko mingine
> Katika fuo za historia

Katika kifungu hiki, ijapokuwa mshairi ametumia sitiari, 'mnara wetu wa almasi', msomaji atakisia kwamba huenda mtajwa ni Hayati Nelson Mandela kutokana na uongozi wake uliozingatia utu badala ya kulipiza kisasi. Anafananishwa na mnara wa almasi ambayo ni madini magumu sana na ya thamani. Kiongozi huyu hakutetereka katika azimio lake la kuweka Afrika Kusini huru kutokana na uongozi dhalimu wa weupe.

Taswira ya mawazo pia inadhihirika katika shairi, 'Ni kweli?' (uk. 55). Mshairi anasema:

…Ni ukweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba baadhi ya wakembe wa kike
Hutiririkwa na machozi na damu
Baada ya wazazi wao halisi wa kiume
Kuwasagasaga kama nyama ya sambusa?...

Mshairi anamwacha msomaji katika hali ya kuwaza kuhusu hali ya maisha na hasa dhuluma dhidi ya mtoto wa kike. Mtoto wa kike anabakwa, anashiriki uzinzi na ukahaba kusudi kukidhi mahitaji ya familia. Shairi hili linampa msomaji nafasi ya kutetea mtoto wa kike.

**c. Taswira za hisi**

Kwa mujibu wa Senkoro (1988: 41), taswira za hisi zina nguvu kubwa ya kuganda akilini na kunasisha ujumbe kwa wasikilizaji au wasomaji wa shairi. Ijapokuwa taswira hizi huingiliana na zile zinazoonekana, hasa hasa hizi hushughulikia hisi za ndani. Hisi huweza kufanya msomaji au msikilizaji awe na wasiwasi, awe na woga, apandwe na hasira, asikie kinyaa, na kadhalika. Maoni haya yanasisitizwa na Kuvuna, Mvati na Maliachi (1992: 25) wanaposema kwamba taswira zinaweza kuibua hisi ambazo humfanya mhusika kuwa na msukumo wa kutenda kitu fulani. Anaweza kuamua kuteta, kupigana au kujiepusha. Vitendo hivi ni matokeo ya msisimko alioupata iwe ni huzuni, hasira, chuki na kadhalika.

Katika utafiti wetu, mshairi Kithaka wa Mberia ametumia taswira za hisi kudhihirisha hisia mbalimbali. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, taswira hisi imetumika katika mashairi mbalimbali, mathalan, katika shairi la ‘Mkasa’ (uk. 14), katika kifungu cha 14. Mshairi anasema:

Baadhi ya waliong’ang’ania wakajifikisha hospitalini
Damu ikiwatiririka kama maji kutoka chemchemi
Wanateleza na kuanguka katika mikono ya mauti
Bado wakisubiri daktari wanaojitahidi kwingine

Katika kifungu hiki, yanayowafika majeruhi wa mlipuko wa bomu katika maeneo ya ubalozi wa Marekani nchini Kenya yanatupa hisia za uchungu. Majeruhi wanatiririkwa na damu kama maji, wengine wanateleza na kuanguka katika mikono ya mauti.

Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 33), hisia za uchungu zinamfika msomaji kutokana na namna mazingira yameharibiwa na binadamu. Mshairi anasema:

> Ole wangu!
> Moyoni
> Napekechwa na uchungu:
> Wakulima
> Wameua miangati,
> Wagemaji
> Wamechinja mikoma
> Wachonga-mizinga
> Wameangamiza mianjate…

Hisia za uchungu zinamfika msomaji anapowaza kuhusu ukataji wa miti, mbinu kongwe za kilimo na ufugaji wa mifugo wengi; jambo ambalo linaathiri mazingira kwa pakubwa.

Hali kadhalika hisia za huzuni zinadhihirishwa katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Katika shairi la ‘Wenda-wazimu Kongo’ (uk. 20), sehemu ya III, kifungu cha 2, mshairi anasema:

> Vijijini, vinywa vya wanaoishi katika jahanamu
> Vinahadithia visa vichafu kama usaha wa kidonda
> Hivi, vimejaza anga harufu yenye mpigo wa nyundo:
> Yule alidhulumiwa kwa zamu na wanaume bila idadi
> Kisha akaingizwa vijiti kwenye njia ya maumbile
> Na kutobolewa matundu mnamowaka moto daima

Hisia za huzuni zinamfika msomaji anapowazia kuhusu ubakaji na dhuluma kwa jinsia ya kike nchini Kongo wakati wa vita au mashambulizi kutoka kwa wanajeshi. Isitoshe, katika shairi, ‘Mafuta yenye Damu’ (uk. 48), hisia za hasira zinamfika mshairi ambazo vilevile hazina budi kuelekezwa kwa msomaji. Mshairi anasema:

…Usiniuzie petroli ya Kusini mwa Sudan
Sitaendesha gari kwa damu ya watu,
Picha za maiti za watoto wachanga
Zinanitumbukiza Hospitali ya Mathare…

Mshairi anafikwa na hasira kunatokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyotokana na mzozo wa umiliki wa mabohari ya mafuta na kusababisha vifo vya wengi. Anakiri kuwa hawezi kuendesha gari kwa petroli ambayo ndicho kiini cha vita na umwagaji wa damu.

Hisi za chuki zinadhihirishwa katika diwani ya *Rangi ya Anga* hasa katika shairi, 'Rangi ya Anga' (uk. 7). Mshairi anasema:

…Mume anamwadhibu mkewe-
Wanawake, ni kama watoto
Usipowarudi hupoteza njia!
...
Mume ana haki thabiti
Anaruhusiwa kumwadhibu mkewe-
Si alilipa mahari!...

Mshairi amefikwa na hisia za chuki kutokana na namna jinsia ya kike inavyodhalilishwa na taasubi ya kiume kuchukua usukani. Hisia za chuki zinajitokeza hata kwa msomaji kutokana na namna mwanamke anapata vipigo kutoka kwa mumewe ambaye anadai ana haki ya kufanya hivyo.

Hisi za furaha pia zinamtawala msomaji anaposoma shairi la 'Siku Angavu' (uk. 95) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Mshairi anasema:

…Baadaye, katika mahoteli na nyumbani
Wahitimu, bado wakivaa umaarufu wao
Wanashirikisha mio zao na za jamaa zao
Katika karamu ya mwisho wa safari ya fahari

Kifungu hiki kinadhihirisha ya kwamba ni siku yenye bashasha kutokana na wasomi kuhitimu na kupata shahada zao; jambo ambalo linawafanya washiriki karamu na jamaa zao. Hisi za woga zinamfika msomaji anaposoma shairi la 'Mkataba Tena' (uk. 28) katika kifungu cha 5 na 6 katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Mshairi anasema:

> …Leo wanawake na wasichana wa nyanda za mazoezi
> Wataishi kwa utulivu bila ukungu mzito wa wasiwasi
> Au jinamizi limerejea kuwafunika kwa wingu la dhiki?
>
> Serikali itawalinda kwa sharia zisizoogopa Bulkinum
> Au wanawake wanatarajiwa kujilinda wenyewe
> Labda, kwa kuvaa sufi za chuma?

Msomaji atabaki akijiuliza maswali chungu nzima. Je, hata baada ya wenyeji wa Sudan kuunda mkataba wa maridhiano, wanawake na wasichana watapata ulinzi imara na wataishi kwa utulivu bila wasiwasi? Je, watakwepaje wabakaji na wahuni? Kutokana na uchanganuzi huu, ni bayana kuwa taswira imetawala katika diwani zote mbili za Kithaka wa Mberia.

### 4.1.3 Sitiari

Wataalamu mbalimbali wana mitazamo mbalimbali kuhusiana na dhana ya sitiari. Kulingana na Myers na Simms (1989: 178), dhana ya sitiari ina asili yake katika lugha ya Kigiriki na ina maana ya kuhamisha au kuvusha hadi upande mwingine. Kwa hivyo, inabainika kwamba kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, sitiari ina maana ya kuhamisha maana/sifa za kimsingi za kitu kimoja hadi kingine kwa kulinganisha vitu hivi viwili. Maana yake ya kimsingi hukiukwa na maana inayorejelewa ni ya kipragmatiki. Kwa mfano, ujana ni moshi. Hii ina maana ya kwamba ujana haudumu milele hupisha uzee. Wataalamu wengine kama vile Kuvuna, Mvati na Maliachi (1992: 27) wanaunga mkono maoni ya wataalamu wa awali kwa kusema kuwa sitiari ni tamathali ya usemi

inayolinganisha vitu viwili ambavyo kwa asili ni tofauti kitabia kwa kufuatisha sifa fulani iliyo katika vyote viwili bila kuitaja sifa yenyewe.

Hali kadhalika, kuna wataalamu wanaoangazia sitiari kwa misingi ya kiuamilifu. Kwa mfano, kulingana na Fiumara (1995: 2), matumizi ya sitiari yamejikita katika misingi ya kiutabaka. Anasema kuwa sitiari imekuwa ikitumika kwa muda mrefu tangu jadi za Warumi na Wayunani. Nyakati hizo ni tabaka fulani tu lililokubaliwa kutumia sitiari. Katika jadi ya Urumi na Uyunani, lugha ya kisitiari ilitengewa watawala, matajiri na waajiri. Watumwa hawakuruhusiwa kuzungumza kwa lugha ya kisitiari kwani ingekuwa sawa na kupigana na kushindana na mabwana wao. Nao watafiti na wataalamu wa hivi majuzi wamefafanua zaidi maana ya sitiari huku wakiunga mkono maoni ya waliowatangulia. Kwa mfano, kulingana na King'ei na Kemoli (2001: 55), sitiari ni matumizi ya lugha yenye kufumba maana ilmuradi kutilia mkazo jambo linaloelezwa kama pambo la lugha. Aidha, vitu viwili hulinganishwa kwa kutumia neno, 'ni'. Kwa mfano, Juma ni simba wetu.

Hali kadhalika, kwa mujibu wa Wamitila (2008: 421), sitiari ni tamathali ya usemi ya ulinganishi usiotumia vilinganishi 'kama', 'mithili', 'ja', 'mfano wa' na kadhalika. Isitoshe, anasisitiza kwamba uelewekaji wa sitiari unaegemea dhana tatu: kilinganishi, kilinganishwa na msingi. Kilinganishi ni kinachotumiwa kama msingi wa kufananisha ilhali kilinganishwa ni kinachofananishwa. Msingi ni sifa ya ulinganishi. Kwa hivyo, kutokana na maelezo haya, inabainika wazi kwamba sitiari haina budi kuwa na sehemu tatu za kimuundo. Kwa mfano, Yeye ni chui. Katika mfano huu, kilinganishi ni 'chui', kilinganishwa ni 'yeye' na msingi wa ulinganishi ni 'sifa ya ukali wa chui'. Zaidi ya

hayo, kulingana na Ndumbu (2014: 19), sitiari ni mojawapo wa semi linganishi tabia. Zaidi ya hayo, ni neno lililozaliwa kutokana na neno ‘sitiri’. Kusitiri maana yake ni kuficha au kufunika, kwa hivyo sitiari maana yake ni namna ya kifuniko au kitu chenye kuficha.

Kutokana na utafiti wetu, sitiari ni tamathali ya usemi inayolinganisha vitu kihali, kitabia au kimazingira kwa kutumia vilinganishi vya moja kwa moja kama vile ‘ni’, ‘kuwa’ au ‘ndi-’. Kwa mfano, yeye ni simba; yeye ndiye simba au yeye alikuwa simba. Katika mfano huu, kilinganishwa (yeye) hubeba sifa ya ushujaa (msingi wa ulinganishaji) ya kilinganishi (simba). Katika ushairi wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*, sitiari ni tamathali ya usemi ambayo ni muhimu sana katika kutilia uzito tabia au hulka mbalimbali za wahusika. Isitoshe, imeonyesha kiwango cha juu cha ubunifu katika utunzi pamoja na kuonyesha ukwasi wa lugha wa mtunzi. Matumizi ya sitiari yanamfanya msomaji avutiwe na ushairi kwa sababu inajenga ujumi wa ushairi wenyewe.

Kulingana na Wamitila (2008: 421), kuna aina nyingi za sitiari katika fasihi ijapokuwa utafiti wetu umerejelea zile aina ambazo zinadhihirika katika diwani mbili teule, mathalan, sitiari sahili, kikaida, shehenezi, thabiti na kitashihisi/kiuhuishi.

**a. Sitiari Sahili**

Sitiari sahili ni sitiari ambayo ni rahisi kueleweka kwa msomaji kutokana na ulinganishi wake ambao ni wa moja kwa moja. Katika diwani teule, sitiari sahili imetumika kurejelea vitu/viumbe wanaofahamika kwa wanajamii. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 52). Mshairi anasema:

…Mwana ambaye
**Ni mkuu wa wavuvi**
Kwenye bahari ambamo
Tonzi na kambare
Na tafi na michumbururu
Na change na chewa
Na mikunga na nguru
Ni wewe nami-
Binadamu!...

Katika kifungu hiki, mshairi ametoa sitiari ya wavuvi na aina mbalimbali za samaki. Shughuli kuu ya wavuvi ni kuvua samaki nao samaki ni kitoweo cha wanajamii fulani. Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu ambaye aliyageuza maji harusini na kuyafanya yawe tembo adimu. Vilevile, ndiye mkuu wa wavuvi aliyejitolea mhanga kuwaokoa wengi kutoka dhambini. Kwa kawaida samaki huvuliwa kutoka majini. Sitiari ya bahari yenye kila aina ya samaki hapa imetumika kuonyesha dunia ambayo ina kila aina ya watu. Kwa hivyo, Yesu Kristo alikuja duniani kama mkombozi wa ulimwengu ambao ni mimi na wewe.

Aidha, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mshairi ametumia hali halisi pamoja na vitu/viumbe halisi kutoa ulinganifu. Kwa mfano, katika shairi la ‘Minyororo ya Njaa’ (uk. 2). Mshairi anasema:

…Anga la nchi si mgeni ni jirani wa miaka na mikaka
Ratiba yake ya awamu za ukarimu na ubahili si siri…

Mshairi ametumia sitiari ya mgeni, jirani, vyombo vya mankuli, makazi, zana za vita na sehemu za mwili kuutoa ujumbe. Mshairi amelinganisha anga na mgeni pamoja na jirani. Mgeni ni mtu ambaye si mwenyeji wa eneo fulani. Anga la nchi ni uwazi ulioko juu ya dunia unaoonekana na kila insia wa eneo hilo. Jirani ni mtu aliye karibu na makazi yako.

Kwa hivyo, mabadiliko ya hali ya anga yanadhihirishwa wazi kwa kila mwenyeji; uwe ni msimu wa mvua au wa kiangazi. Majira haya hayawezi fichika.

Hali kadhalika, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* (uk. 17), mshairi analinganisha ndoto na vigae vya kaure iliyoangukiwa na jabali. Anasema:

> …Waliohimili maisha yao na ya jamaa kwa heshima
> Sasa wanatapatapa katika dimbwi la aibu ya haja
> Ndoto walizofinyanga kwa udongo-kinamo mzuri
> Sasa ni vigae vya kaure iliyoangukiwa na jabali…

Mshairi ametuweka katika hali halisi ya majeruhi walionusurika kifo baada ya mkasa wa bomu katika ubalozi wa mwewe. Tunakisia ya kwamba huu ni mkasa uliotokea nchini Kenya mwezi wa Agosti 1998. Maazimio ya majeruhi pamoja na ndoto zao zilisambaratika kutokana na majeraha waliyopata; sasa ni wahitaji na waliotamauka. Mshairi anafananisha kusambaratika huku na kaure iliyoangukiwa na jabali na kubaki vigae tupu. Kaure ni chombo cha maakuli kinachotengenezwa kutokana na udongo na ambacho ni dhaifu kikilinganishwa na jabali ambalo ni mwamba mkubwa. Sitiari hii inaonyesha athari kubwa ya mkasa wa bomu kwa majeruhi.

Hali kadhalika, katika shairi la 'Macho Mekundu' (uk. 59), mshairi anafananisha vijana wa jinsia ya kike na majani mabichi. Anasema:

> …Wa kike, dhidi ya hiari, dhidi ya heshima
> Dhidi ya malalamiko ya miili isiyokomaa
> Ndio majani mabichi ya kuzima mioto
> Katika damu ya majemedari wa shetani

Majani mabichi huwa ni ya kijani kibichi; bado kunyauka. Vilevile, huwa yanavutia. Vijana wa kike wana maumbile na sura za kuvutia wakilinganishwa na wanawake waliofikia utu uzima. Mshairi ametumia kitenzi, 'ndio' kuonyesha ulinganishi huu wa

kisitiari. Anaonyesha dhuluma dhidi ya watoto wa kike ambao wanatekwa nyara na waasi na kuwatumia kuzima uchu wao wa mapenzi. Vilevile, katika shairi la 'Wingu la Machozi' (uk. 61), mshairi ametumia sitiari kutupa taswira ya majanga yanayowafika waathiriwa wa vita vilivyotekelezwa na kiongozi wa kundi la waasi, Jogoo Foday Senkoh wa Sierra Leone katika harakati za kuondoa serikali mamlakani. Kwa mfano, katika kifungu cha 4, anasema:

…Baadhi ya kuo za macho
Ni mashimo ya gizagiza…

Katika kifungu hiki, mshairi ametumia sitiari hii kitasfida kuficha ukali wa mashambulizi na maovu waliyofanyiwa raia wa Sierra Leone. Badala ya kusema kuwa macho yao yalidopolewa na uwazi kuachwa, anafananisha uwazi huu na mashimo ya giza. Kulingana na TUKI (2004: 514), shimo ni uwazi mkubwa wa duara uliochimbwa kuendea chini. Kwa hivyo, namna shimo linavyozidi kwa kina ndivyo giza linavyoshamiri. Mshairi anampa msomaji taswira ya shimo lililojaa giza ili sitiari hii ieleweke kwa urahisi. Matumizi ya shimo katika muktadha huu yanatupa taswira ya namna kitendo cha kudopoa kilivyotekelezwa kwa ukatili.

**b. Sitiari ya Kikaida**

Sitiari ya kikaida ni sitiari ambayo inafungamana na mila na desturi za jamii. Kila jamii huwa na kaida wanazozithamini na ili kuzirejelea huona fahari katika matumizi ya sitiari. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 2). Mshairi anasema:

Vilele vya milima
Na malimbi ya bahari
Mmwesomweso wa nyota
Na tumba la mbalamwezi,
Bila kupigana mieleka
Kwenye ukumbi wa ugambi
Zinakubaliana kwa pamoja

Kwamba kuwa navyo mkononi
Ni mpini wa upanga
Mkononi mwa mwanamume
Na kiganja cha mwanamke…

Mshairi ametumia vifaa vya kitamaduni kuleta ulinganisho wa kisitiari. Ametumia zana ya kilimo mfano wa upanga kupitisha ujumbe kwa msomaji. Katika kifungu hiki, mshairi amelinganisha umiliki wa ulimwengu pamoja na rasilmali zote na mpini wa upanga mkononi mwa mwanamume. Mpini wa upanga ni sehemu ambayo inatumika kama kishikio wakati wa kukatia chochote. Sehemu ya makali ndiyo ikatayo. Sitiari hii ina maana kwamba kwa muda mrefu, jinsia ya kiume imetawala na kuudhibiti ulimwengu huku jinsia ya kike ikikandamizwa. Mshairi anazidi kusema ya kwamba wakati kiganja cha mwanamke kitaishiwa na stahamala kitashika makali ya upanga na damu kutiririka bila hatia. Ni dhahiri kwamba wanawake wanapambana na wanaume katika kufikia usawa wa kijinsia; jambo ambalo huenda lisizae matunda.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi, 'Macho Mekundu' (uk. 59 na 60), mshairi ametumia zana za vita katika ulinganisho wa kisitiari. Anasema:

…Ole wao; watumwa wa majambazi!
Wao ndio podo za mikoko na miwati
Ndio hupima kina katika ziwa la vita,
Ndio punda na ngamia wa kubebea mizigo
Ndio ngao za kulinda vifua vya afande…

Kutokana na shairi hili, wakati wa vita, zana mbalimbali hutumika ili kujikinga na kuwapa wapiganaji ushindi dhidi ya maadui zao. Mshairi amelinganisha watoto wa kiume na podo na ngao katika uwanja wa vita. Mshairi ametumia neno, 'podo' ambacho ni kifaa cha kubebea mishale. Watoto hawa wa jinsia ya kiume wanalinganishwa na podo kumaanisha wao ndio huwabebea waasi zana za vita. Isitoshe, mshairi ametumia

ulinganishi wa ‘ngao’. Ngao ni zana inayotumika kama kinga wakati wa vita. Watoto hawa wanawekwa katika mstari wa mbele wakati wa vita ili kuwakinga washambulizi kutokana na maadui wao; kitendo ambacho ni cha kikatili. Vilevile, mshairi ametumia ulinganishi wa Wanyama. Wanyama wanaotajwa hapa ni punda na ngamia ambao hutumiwa na jamii nyingi kubebea mizigo mizito bila hiari. Kwa hivyo, watoto hawa wanabebeshwa mizigo mizito na waasi. Sitiari hii inaleta dhana ya ukatili wanaotendewa na waasi.

**c. Sitiari Shehenezi**

Sitiari shehenezi ni sitiari ambayo kilinganishi huwa kina sifa ya ishara na kimefumbata kilinganishwa. Sitiari hii huibua picha ambayo inajengeka katika akili ya msomaji na kumfanya atafakari zaidi kuhusu maana inayochanuzwa. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, katika shairi, ‘Mlima wa Dhahabu’ (uk. 23), mshairi ametumia kilinganishi cha mlima. Anasema:

> …Thamani ya shilingi ilianguka shimoni kwa mgoto
> Gharama za maisha zikapanda hadi vilele vya miti
> Kupata chakula, mavazi, karo, dawa na nauli
> Kukawa ni kupanda kilima cha mwinuko mkali…

Mshairi ametupa picha ya kupanda mlima wenye mwinuko mkali; lazima utokwe na jasho. Ishara hii imeibusha maana ya kudorora kiuchumi, kwa hivyo, kukidhi mahitaji ya kila siku ni jambo ambalo si rahisi; lazima utolee jasho. Katika ushairi uo huo, (uk. 24), mshairi ametumia kilinganishi cha mawimbi na bahari. Anasema:

> Lundo kubwa la waliokosa kazi na riziki
> Liligeuka ardhi ya rutuba kukamea majambazi
> Utekaji nyara wa magari kwenye barabara miji
> Na uvamizi wa magenge ya mauti nyumbani
> Yakawa mawimbi katika bahari ya majonzi

Mshairi amelinganisha kikundi cha watu waliokosa kazi na riziki moja kwa moja, na ardhi yenye rutuba kwa kutumia kitenzi, 'liligeuka'. Ardhi yenye rutuba huifanya mimea inawiri vizuri na kuwa na mazao maridhawa ikilinganishwa na ardhi isiyokuwa na rutuba. Vivyo hivyo, ukosefu wa kazi na riziki ni mazingira bora ya kunawiri kwa ujambazi. Hali kadhalika, mshairi ametumia kitenzi, 'yakawa' kudhihirisha sitiari. Anatupa ishara ya mawimbi ambayo kwa kawaida husababisha msukosuko baharini. Mawimbi haya yanaashiria vurugu au uvamizi nayo bahari inaashiria dunia au ulimwengu. Kwa hivyo, ukosefu wa kazi umesababisha utekaji nyara barabarani na ujambazi nyumbani; mambo ambayo yanaleta ukosefu wa usalama kwa wanajamii pamoja na masikitiko. Katika kifungu kinachofuatia, mshairi ametumia kilinganishi cha ngome. Anasema:

Jitihada za kukinga maisha na kulinda mali
Katikati ya ngurumo za dhiki ya umaskini
Ziligeuza maskani nyerezi katika mitaa mizuri
Zikawa ngome imara zenye milango ya chuma…

Mshairi ametumia kilinganishwa, 'jitihada', kilinganishi 'ngome' na sifa ya ulinzi. Ngome ni mahali pa kujisitiri kutokana na maadui. Ametupatia sura ya makazi mapya ambayo yamezingirwa na kuta na milango ya chuma. Jitihada moja kwa moja haziwezi kuwa ngome imara lakini mshairi ameitumia kama taashira ya maskani ambayo yamezingirwa na kuta na milango ya chuma ili kujikinga na kulinda mali yao kutokana na majambazi.

### d. Sitiari Thabiti

Sitiari thabiti ni sitiari ambayo kwayo sifa dhahania inapewa sifa za kitu thabiti. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 45). Mshairi anasema:

…Ukweli
Hata uwapo mchungu
Ni almasi inayometameta-…

Mshairi ametumia sifa dhahania ya ukweli na kuilinganisha na almasi ambayo ni kito kinachogusika. Almasi ni madini ya thamani sana. Mshairi anasema kuwa madini haya yanametameta. Hii ina maana kwamba ukweli ni wa thamani sana na ni sifa inayofaa kuenziwa na kila mwanajamii. Katika muktadha huu, ukweli ndio utawaokoa wenyeji kutokana na janga la njaa na kiangazi kwa sababu watazinduka baada ya kuona kwamba wao ndio kisababishi cha majanga haya.

**e. Sitiari ya Kitashihisi**

Sitiari ya kitashihisi ni sitiari ambayo kitu hulinganishwa na kupewa sifa ya kitu chenye uhai. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi, 'Mnara Mwangavu' (uk. 37). Mshairi anasema:

…Ewe nyota iliyokataa kuzima!
Ulipokelewa kwa nderemo
Na kuvishwa ushanga adimu…

Mshairi amemfananisha Hayati Rais Nelson Mandela wa Afrika Kusini na nyota iliyokataa kuzima. Nyota imepewa sifa ya binadamu. Rais huyu analinganishwa na nyota; umbile ambalo huangaza gizani. Katika enzi hizo za giza na ubaguzi wa rangi, kiongozi huyu licha ya kudhulumiwa alitetea raia hadi wakapata ukombozi. Alikataa kusitisha mapambano yake dhidi ya ubaguzi na hatimaye akateuliwa kama rais wa nchi hiyo. Aidha, katika shairi, 'Ndimi Zetu', (uk. 87), mshairi anafananisha ndimi na migodi inayostahili heshima. Anasema:

…Ndimi zetu ni migodi inayostahili heshima
Katika methali, misemo na vitendawili
Hadithi, visasili na nyimbo za jadi

Kuna Johari zenye thamani ya fahari
Mchimbuaji mwenye stadi na ujuzi
Ndani vipande vya dhahabu na almasi…

Migodi ni mahali ambapo madini huchimbuliwa kwa ajili ya mauzo ili kupata riziki. Madini haya huwa ya thamani sana. Mshairi ameipatia migodi sifa ya heshima; nazo ndimi zinastahili kuheshimika vilevile kwani mumo humo mna hifadhi ya hekima na maarifa. Ndimi zetu ni hifadhi ya utamaduni wetu.

### 4.1.4 Taashira

Wataalamu mbalimbali wamefasiri taashira kwa njia tofauti. Kundi la kwanza linashikilia kwamba taashira ni alama au mchoro. Kwa mfano, Lewis (1936) anaangazia tofauti iliyopo baina ya taashira na jazanda. Anasema taashira huangazia alama ambayo inazua wazo fulani huku jazanda ikiangazia wazo lililo wazi lakini lenye maana fiche. Naye Plaks (1976: 92-93) anasema ya kwamba taashira ni michoro ya mtu binafsi ambayo ina urejelezi wa nje. Isitoshe, alama hizi ni tuli, hazibadiliki kama ilivyo jazanda ambayo hubadilika kutegemea muktadha. Wataalamu hawa wanaungwa mkono na TUKI (2006: 896) wanaosema kwamba taashira ni mfumo wa alama fulani zitumiwazo kuwakilisha kundi fulani la mawazo; ishara.

Kithaka wa Mberia ametumia taashira kupitia michoro katika jalada. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* (2007) kuna picha ya mwanamume mwenye kitambi ambacho uchi wake unadhihirika wazi, shati lake haliwezi kufungika kutokana na ukubwa wa tumbo lake. Hali hii inadhihirisha dunia iliyojaa uozo mwingi mkiwemo ubinafsi na ufisadi. Aidha, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (2014) kuna picha ya kiatu kinachokanyaga mwanamke kuonyesha namna wanawake wamedhalilishwa katika jamii hasa katika elimu, ndoa na

vyeo. Isitoshe, mna mti uliokauka hadi mizizi kuonyesha namna mazingira yameathirika vibaya.

Kundi la pili lina maoni tofauti kuhusu maana ya taashira. Kulingana na Wamitila (2008: 398), taashira ni mbinu ambapo jina au neno linachukua nafasi ya neno jingine linalohusishwa nalo kwa njia tofauti. Anasema kwamba kuna mbinu kadhaa zinazoweza kuangaliwa kama aina za taashira au metonimu, mathalan, sinekidoki, taniaba na lakabu. Sinekidoki ni mbinu ambapo sehemu ya kitu inatumiwa kusimamia kitu chenyewe au kitu kinachohusishwa na kinachorejelewa. Taniaba ni mbinu ambapo mtu au kitu kinaelezwa kwa kutaja kivumishi au jina linalohusishwa na mtu mwingine kwa sababu jina hilo lina uwezo wa kuchochea sifa fulani maalum miongoni mwa watu. Lakabu ni mbinu ambapo mtu au kitu, mahali au mazingira yanaelezwa kwa jina lisilokuwa halisi, yaani pana matumizi ya jina la msimbo.

Matumizi ya sinekidoki kama aina ya taashira yamejitokeza katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Msimu wa Tisa' (uk. 11), kifungu cha mwisho, mshairi anaposema: 'Na kulishwa mayai, maziwa, asali na nyama ya nundu' kumaanisha maisha bora yenye ustawi na ustaarabu. Mshairi ametuchorea taashira ya viongozi ambao hawajali maslahi ya wananchi ilhali wao wanaishi maisha ya anasa. Aidha, katika ushairi, 'Ni Kweli?' (uk. 55), kifungu cha pili, mshairi anasema:

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba wapo wazazi wanatuma watoto
Kwenda kutega mitego ya virinda hoteli
Kusudi kuleta changu na nguru nyumbani
Kupigana na kikosi kikali cha njaa?

Mshairi ametumia maneno, 'changu na nguru' kumaanisha kitoweo au chakula. Anaonyesha namna watoto wanatumwa na wazazi wao kushiriki ukahaba ili kuleta chakula au kitoweo nyumbani; jambo ambalo linamkera. Aidha, matumizi haya ya sinekidoki yamedhihirika pia katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Zimwi la Theluji' (uk. 51). Mshairi ametumia sinekidoki 'ng'ombe wa kijiji' kumaanisha rasilmali za nchi. Wamishenari walipowasili nchini, kando na kueneza injili, walivutiwa na rasilmali za nchi, nao Wakenya wakawalaki kwa mikono miwili. Aidha, katika shairi la 5 na 6, mshairi anazungumzia 'maziwa'. Anasema:

> …Zimwi la theluji
> …
> Likavamia kiwele
> Na kwa tamaa iliyokithiri
> Kuanza kukamua maziwa
> …
> Karibu na ndege ya mizigo
> Naona mitungi ya maziwa
> Ikingojea kupakiwa chomboni
> Na kubebwa hadi ng'ambo…

Kulingana na kifungu hiki, malighafi au rasilimali za nchi zinafananishwa na maziwa ambayo ni kirutubishi cha wanyama na binadamu. Wamishenari waliwapisha wakoloni wazungu ambao walijizatiti kunyakua rasilmali na malighafi ya nchi na kuyasafirisha hadi ng'ambo ili kuwafaidi wenzao.

Taniaba pia imetumika kwa mapana katika diwani mbili teule. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi, 'Msumbiji' (uk. 71), katika kifungu cha tatu. Mshairi anasema:

> Misafara ya sisimizi kutoka bara
> Inatiririka kuelekea Bahari ya Hindi
> Huku nyuma nderi na kunguru
> Wanasherehekea ndovu na vifaru

Mshairi amerejelea wafanyibiashara wengi wanaoshiriki biashara haramu ya kuuza vipusa vya ndovu na vifaru wakielekea Bahari ya Hindi kwa kuwafananisha na sisimizi; kuonyesha kwamba idadi yao ni kubwa. Aidha, katika shairi lilo hilo (uk. 72), mshairi ametumia mafungu ya maneno, 'zao la teknolojia ya kishetani' kumaanisha dhiki ambayo raia wa Msumbiji waliipitia ilitokana na uvumbuzi wa vilipuzi, bunduki na risasi. Katika ukurasa unaofuatia (uk. 73), mshairi ameonyesha sifa za ujanja wa wakoloni katika kudhibiti uchumi ulimwenguni. Amewafananisha wakoloni na 'Zimwi kuu la dunia'. Ameonyesha ya kwamba japo uchumi unazidi kuimarika katika nchi ya Msumbiji baada ya mkoloni kuondoka, bado mkoloni huyo anadhibiti njia kuu za uzalishaji mali.

Isitoshe, katika shairi, 'Ntharene' (uk. 74), kifungu cha mwisho, mshairi anasema: 'Punde tumbo za malori zitashiba shehena' kumaanisha madereva watapakia mazao ya shambani kwenye malori na kuyasafirisha hadi mjini kuwafaidi wanaoishi mjini pia viwanda. Vilevile, katika shairi, 'Janga Jangwani' (uk. 76), kifungu cha sita, mshairi ameonyesha maafa ya wakimbizi. Anasema:

> Kisu kikali cha kiu na machovu
> Kinashambulia watoto njiani
> Na kufikisha safari yao kikomoni,
> Mijeledi ya shida za ukimbizini
> Inacharaza vikali akili na ndoto
> Na kuacha majeraha machungu

Mshairi ametumia maneno, 'kisu kikali cha kiu na machovu' kumaanisha watoto wanafikwa na makali ya njaa na uchovu huku wakiishia kufariki. Pia ametumia taashira ya 'mijeledi ya shida za ukimbizini inayowacharaza vikali akili na ndoto zao'. Hii ni taashira inayoashiria matatizo wanayoyapitia wakimbizi, matatizo ambayo yanafisha ndoto zao.

Aidha, katika shairi, 'Maadui Wajanja' (uk. 81), mshairi amefananisha viongozi na vibaraka waliosababisha maafa ya wananchi katika nchi za Angola na Msumbiji na 'wakala wa shetani'. Anasema:

> Hawa maadui wa uhai, hili genge la izraili
> …
> Kwa ulimi wa moto, hulamba vifua au migongo
> Au, baada ya kupiga darubini, kushambulia kiunoni
> Na kufuta fahari ya wanaume na kuwaacha bila maana
> Wakati wa kudhulumu, hawa wakala wakali wa shetani…

Mshairi anafananisha vitendo vya genge hili vya kinyama na vitendo vya shetani mwenyewe. Kulingana na KLB (2015: 134), mapigano baina ya vyama viwili, FRELIMO na RENAMO yalisababishia wananchi mateso si haba. Kuna wale waliofariki, walionajisiwa, waliojeruhiwa na waliokimbilia usalama wao katika nchi jirani. Chama cha FRELIMO kilichoongozwa na Samora Machel kilipigia debe mfumo wa ukomunisti huku chama cha RENAMO kilichoongozwa na Andre MatSangaissa kikipinga mfumo huo. Hali hii ilizua mtafaruku baina ya vigogo na wanachama wao na kusababisha vita ambavyo viliwaathiri wananchi kwa ujumla.

Isitoshe, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 5) mshairi amewafananisha wasichana ambao wamekataa kukeketwa na 'waasi', yaani waliokiuka mila na desturi za jamii. Jamii imewatenga kwa sababu wanatia dosari hadhi ya jamii husika. Vilevile, katika shairi lilo hilo (uk. 49-52), mshairi ametumia taniaba, 'Zimwi la Theluji/Jeupe' kuashiria wageni waliozuru nchi ya Kenya kutoka ughaibuni. Kulingana na KLB (2015: 29), Zimwi la kwanza lilikuwa la Waarabu kisha Wamisheni, hatimaye Wazungu walioendeleza ukoloni mkongwe. Haya makundi yote yamefananishwa na 'zimwi' kutokana na nia zao za kinafiki. Waarabu walipoingia pwani walisakini na kunyakua

maeneo yaliyokuwa na rotuba. Baadaye, wamisheni nao waliingia kwa kusudi la kueneza dini yao. Mshairi anasema:

> …Lilikuja zimwi la theluji
> …
> Lilijidai kuwa tarishi
> Wa Muumba wa yote
> Likakunjua hadithi
> Ya Baba na Mwana
> Mwana wa peke
> …
> Mwana ambaye
> Ni mkuu wa wavuvi
> …
> Kwa ukungu na hila
> Zimwi la theluji
> Liliapa kwa mbingu
> Na ardhi na nyota
> Kwamba lilikuwa na dhima
> Ya wakala wa Mungu
> Kuwahamisha wenyeji
> Kutoka kichochoro kichafu…

Wamisheni walijiita, ‘tarishi’ yaani wajumbe wa kueneza ujumbe kuhusu Muumba wa vyote, hadithi ya Baba na Mwana wa pekee. Mshairi amezungumzia Muumba ambaye ni Mungu na Mwanawe ambaye ni Yesu Kristo. Katika kifungu hiki, Yesu Kristo amepewa jina, ‘Mkuu wa wavuvi’, wavuvi ambao ni wafuasi wake. Jina hili linatokana na sifa zake za kubadili mienendo ya wengi na kumuiga yeye. Mshairi amewaita wamisheni ‘mazimwi’ kutokana na kubadili imani za kidini za wenyeji anaposema, ‘lilikuwa na dhimay a wakala wa Mungu kuwahamisha wenyeji kutoka kichochoro kichafu’. Aidha, kundi hili liliwapisha wakoloni ambao walidhamiria kutawala nchi huku wakiwatesa wenyeji na kuvamia rasilmali za nchi. Ijapokuwa wenyeji walipigana na kumwondoa mkoloni bado anaendeleza ukoloni mamboleo.

Hali kadhalika, mshairi ametumia lakabu kuwasilisha ujumbe wake. Kulingana na Wamitila (2008: 400), lakabu ni mbinu ambapo mtu au kitu, mahali au mazingira yanaelezwa kwa jina lisilokuwa halisi, yaani pana matumizi ya jina la msimbo. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi, 'Mkasa' (uk. 13), mshairi anapozungumzia mkasa wa kigaidi uliotekelezwa katika ubalozi wa mwewe ambao tunakisia ni mkasa wa kigaidi nchini Kenya mnamo mwaka wa 1998, amelipa jengo la Ubalozi wa Marekani jina la lakabu, 'Ubalozi wa Mwewe'. Magaidi walichukulia viongozi wa Marekani kuwa maadui zao kutokana na kuwa na uwezo wa kudhibiti uzalishaji mali na uundaji wa silaha za vita ulimwenguni. Zaidi ya hayo, vikosi vya Marekani vilikuwa vimeshambulia maeneo yao kwa hivyo wakaamua kulipiza kisasi kwa kushambulia pia nchi zilizounga mkono Marekani. Aidha, mshairi ametumia lakabu, 'Nipisheni njia' kurejelea ambulensi (uk. 14). Katika shairi, 'Magenge Matatu' (uk. 32), kifungu cha 3, jina, 'Mfalme wa Nzige' limetumika kuashiria rais wa pili katika nchi ya Kenya aliyezungukwa na viongozi walafi, wenye hila, tamaa, uzinzi, ujanja na ufisadi.

### 4.1.5 Tashbihi

Wataalamu mbalimbali wamechanganua dhana ya tashbihi na kuchanuza maana mbalimbali, mathalan, Leech (1969: 74) anasema kwamba tashbihi huwa na maana ya juujuu ikilinganishwa na jazanda ambayo huwa na maana ya ndani. Aidha, tashbihi imedondoshwa kutoka kwa jazanda. Mtaalamu huyu ametoa mfano wa jazanda, 'The ship ploughs the waves' na kutokana na jazanda hii akaunda tashbihi, 'The ship goes through the waves like a plough ploughing the land'. Tafsiri yake ni, 'Meli huchimba mawimbi kama vile plau huchimba shamba'. Zaidi ya hayo, anasema kwamba tashbihi ni

wazi kuliko jazanda kutokana na umahususi wake katika kulinganisha ilhali jazanda ni fumbo.

Aidha, Kuhenga (1977: 3) anafafanua zaidi maana ya tashbihi. Anasema kwamba tashbihi ni mtindo wa kiuneni wa kifani ambao kwao kitu kimoja au zaidi hulinganishwa au kufananishwa na kitu kingine tofauti. Mfanano huu ni wa kiutendaji au kimaumbile kama vile, sura, rangi na jinsi ya kujimudu. Isitoshe, tashbihi ni neno ambalo limezaliwa kutoka kwenye neno, 'shabihi' ambalo lina maana ya kufanana au kulingana na. Kwa mfano, afya mwilini ni kama mafuta katika utambi wa taa. Ni dhahiri kwamba afya humsaidia binadamu kupata riziki jinsi mafuta husaidia utambi kuwaka. Maelezo haya yanatilia mkazo maoni ya Leech (1969: 74) kuhusu uwazi uliopo katika matumizi ya tashbihi.

Kulingana na Msokile (1993: 40), tashbihi ni tamathali ya usemi ambayo huhusisha vitu vitatu ambavyo ni kizungumziwa, kifananishi na kiungo. Kutokana na maelezo haya, lazima tashbihi iwe na viungo hivyo vitatu. Kwa mfano, yeye ni mweusi kama makaa. Katika mfano huu, kizungumziwa ni yeye, kifananishi ni makaa na kiungo ni mweusi (sifa). Maoni haya yanatiliwa mkazo na Wamitila (2003: 222) anayesema kwamba tashbihi ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Aidha, hutambulishwa na viungio: kama, mfano wa, mithili ya, ja, kama vile, sawa na kadhalika. Hali kadhalika, tashbihi katika fasihi inaweza kujitokeza kama tashbihi ya kiutendi pale ambapo inakuzwa na kuendelezwa kwa mapana, kufikia hata mistari ishirini. Matumizi haya hutokea hasa katika tendi. Katika utafiti wetu aina hii ya tashbihi haijatumika, hata hivyo mshairi wa diwani zote mbili ametumia tashbihi kwa wingi.

Vifananishi vilivyotumika katika diwani zote mbili vinashabihiana na mazingira ya mwandishi na wasomaji pia. Kwa hivyo ni rahisi kueleweka kwa hadhira.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, matumizi ya tashbihi yamedhihirika wazi katika mashairi kadhaa. Mwanzo, mshairi ametumia kiunganishi, 'kama' kulinganisha vitu kihali, kitabia na kimazingira. Kwa mfano, katika shairi la 'Minyororo ya Njaa' (uk. 1), kifungu cha 3 na 4, mshairi ametumia tashbihi, 'Mbavu zake zimechomoza kama fito zilizopinda katika ukuta wa udongo uliovamiwa na mvua'. Mshairi anasisitiza makali ya njaa yaliyompata mzee kiasi ya kwamba amekonda na kukondeana sawa na fito. Zaidi ya hayo, katika kifungu cha nne, anasema: 'Kwenye kijiji cha mikakaya, minga na vumbi jamaa na majirani waliovaa huzuni kama veli wanaaga udongo wa fusi la kaburi ya tano'. Hii ina maana ya kwamba njaa imesababisha maafa na kuwaacha wenyeji katika hali ya huzuni; sura zao zimefunikwa na majonzi (veli).

Vilevile, katika shairi la 'Tope la Mizozo' (uk. 6), mshairi anasisitiza ujumbe kwa kutumia tashbihi katika kifungu cha 4. Anasema: 'Punde harufu ya kidonda-ndugu cha ufisadi ilishambulia pua ya taifa kama wingu zito la amonia'. Hii ina maana ya kwamba viongozi ambao hapo awali walipiga vita ufisadi sasa wameingia kwa mkiki na kutekeleza ufisadi huo kwa nguvu zao zote sawa na wingu zito la amonia.

Aidha, katika shairi la 'Msimu wa Tisa' (uk. 9), katika kifungu cha 5, mshairi ametumia tashbihi, '…na kuduwaza watu kwa ujanja wa mlo wa siku moja kabla ya kuhama kama mbayuwayu wakati wa kiangazi'. Tashbihi hii inaashiria ya kwamba baada ya viongozi kuchaguliwa na wananchi na kuwaandalia karamu ya siku moja, walihamia mijini

wasionekane na wananchi tena sawa na vile mbayuwayu hupatikana tu wakati wa mvua kisha kiangazi kiingiapo hutoweka. Mfano huu wa mbayuwayu umetumika pia katika shairi la 'Wenda-wazimu Kongo' (uk. 21), kifungu cha mwisho lakini kuleta dhana tofauti. Mshairi anasema, 'Wanaotenda yanayochoma moyo kwa visu milioni, bado wamo nchini, huru kama mbayuwayu angani'. Tashbihi hii inatumika kulinganisha waliotekeleza mauaji ya kinyama Kongo na mbayuwayu ya kwamba bado wako huru hata baada ya kutekeleza unyama huo.

Katika shairi lilo hilo (uk. 20), mshairi ametumia tashbihi, 'Panda ya miguu ni kinamasi cha damu na usaha ni mtambo wa harufu nzito kama kiwanda cha ngozi' na 'Hiki si kisa nadra kama mbwa mwenye pembe. Hii ni kawaida ya wenda-wazimu Kongo'. Katika tashbihi ya awali, mshairi anafananisha hali ya mwili wa mwathiriwa wa mashambulizi na harufu itokayo katika kiwanda cha ngozi; ni hali ya kutamausha. Katika tashbihi ya pili, mshairi anadokezea kwamba visa vya kinyama nchini humo ni vya kawaida, si tukizi kama mbwa mwenye pembe.

Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, mshairi ametumia kiunganishi, 'kama' kuundia tashbihi. Kwa mfano, katika shairi la 'Wanda' (uk. 2), kifungu cha 1, mshairi anasema: 'Moyoni mwangu hakungekuwa na ilhamu ikiniwasha kwa utukutu kama majani ya mpupu'. Aidha, kifananishi hiki cha 'mpupu' kimetumika kwingineko (uk. 6). Mshairi anasema: 'Wametungia nyimbo sumbufu kama mpupu'. Kinyume na ilivyokuwa katika matumizi ya 'mbayuwayu' katika *Msimu wa Tisa*, mshairi ametumia kifananishi, 'mpupu' kuleta maana sawa ya kutotulia. Katika mfano wa kwanza, mshairi hatulii mpaka azungumzie mtafaruku uliopo wa kijinsia katika jamii. Aidha, ameangazia nyiso

zilizotungwa kusudi kumkashifu mtoto wa kike ambaye hajatahiriwa katika mfano wa pili. Matumizi yaya haya ya vifananishi sawa yanadhihirika katika diwani ii hii (uk. 19 na 26) mshairi anapotumia kifananishi, ‘unga wenye hamira’. Anasema haya:

> …Kuna ya kuficha yasifichuke
> Na yafichwayo yakafichuka-
> Huzuiliwaje siri ambayo kila uchao
> Huumuka kama unga wa ngano
> Uliokolezwa hamira ya thamani?...(uk. 19)
>
> …Rinda la sare ya shule linapobadili sura
> Tumbo linapofura kama unga wenye hamira
> Udadisi unapofichua fasiki aliyevunja miiko…(uk. 26)

Katika matumizi haya ya tashbihi, mshairi anadokezea namna ilivyo vigumu kuficha siri hasa ujauzito uliompata huyu yaya sawa na ilivyo unga wa ngano uliotiwa hamira. Hali kadhalika, katika *Rangi ya Anga*, mshairi ametumia vifananishi tofauti tofauti katika kuundia tashbihi. Kwa mfano, mshairi anasema: ‘Kwa ahadi tamu kama halua, wakala alimrairai mama-mzazi’ (uk. 17). Wakala aliyetumwa kumtafuta mjakazi alimsihi mama-mzazi kwa maneno matamu zaidi ya halua amwachilie huru bintiye akafanye kazi ya uyaya; kazi ambayo hatimaye ilimtia mashakani.

Mshairi pia ametumia kiunganishi, ‘sawa na’ katika matumizi ya tashbihi. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Muuaji Mwenye Furaha’ (uk. 22), kifungu cha 1, mshairi anasema: ‘Alileta mahakamani akiwa na pingu mkononi, ngozi yake, tofauti na zetu, sawa na jaji na mshtaki’. Tashbihi hii inasisitiza tofauti iliyopo baina ya Mwafrika na Mzungu; hawashikani mikono hata kidogo sawa na jinsi ilivyo baina ya jaji na mshtaki.

Mshairi pia ametumia kiunganishi, 'ja' kuleta ulinganifu. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Mlima wa Dhahabu' (uk. 23), kifungu cha 5, mshairi anasema: 'Faida ilipunguka ja maji ya mtungi uliotoboka'. Mshairi amesisitiza namna biashara imeathiriwa vibaya kutokana na kudhibitiwa na nchi za nje sawa na jinsi maji yaliyo kwenye mtungi uliotoboka hayawezi hifadhika.

Kiunganishi, 'mithili ya' pia kimetumika kuleta ulinganifu. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 17). Mshairi anasema:

> …Mwili wake teketeke kwa miaka michache
> Na baridi ya alfajiri isiyocheka na watu
> Zikawa wandani mithili chanda na pete…

Mshairi amelinganisha mwili wa yaya na baridi kwamba asingejitenga na vyote viwili kwani ingebidi atimize majukumu ya mama-mwenye-nyumba. Ilibidi yaya huyu mkembe arauke ili kutekeleza majukumu hayo. Kwa hivyo, katika diwani teule, mshairi ametumia tashbihi kwa wingi ili kusisitiza ujumbe wake pia kumfanya msomaji aweke kumbukumbu ya ujumbe unaopashwa.

### 4.2 Matumizi ya Lugha Kutegemea Muktadha

Lugha ambayo imetumiwa katika diwani teule imesawiri mazingira au miktadha mbalimbali. Kulingana na Mazrui na Syambo (1992: 2), kila utungo wa fasihi una chanzo chake katika maisha ya binadamu. Hazina kubwa ya msanii wa fasihi ni jumla ya maisha yanayopatikana katika mazingira yake. Msanii hupata tajriba na mawazo ya utungo kutokana na mazingira anayokumbana nayo, vilevile huanza kupiga mbizi na kuangalia tulikotoka na kuelewa barabara kilichosababisha hali tuliyonayo na kubashiri yajayo. Aidha, ushairi unaangazia matukio halisi katika jamii. Mazingira haya huathiri lugha

ambayo mshairi atatumia katika utunzi. Haya yanaangaziwa na Wordsworth (1797: 52) anayesema kwamba ushairi unafaa kusawiri hisia na matukio ya binadamu na matumizi ya lugha inayotumiwa katika jamii ndicho chombo muhimu katika kuwasilisha hisia hizo.

Kulingana na Wamitila (2003: 222), lugha hutofautiana kutegemea mazingira na muktadha inakotumiwa lugha hiyo. Aidha, huu ndio msingi wa sajili. Zaidi ya hayo, anasema kwamba sajili ni dhana inayotumiwa kuelezea sifa za kilugha zinazofungamana na kudhibitiwa na muktadha maalum. Uteuzi wa msamiati, sarufi, kiimbo, uakifishi na sauti huathiriwa na matarajio fulani ya kimuktadha. Hali kadhalika, katika kitabu chake, *Kanzi ya Fasihi* (2008: 69), anasema kwamba sajili huelezewa kwa kurejelea sifa kuu za kimuktadha: uwanja (mandhari na lengo la mahusiano), kihusianishi (uhusiano kati ya wahusika) na nyenzo (njia kuu ya mawasiliano). Anaangazia sifa zifuatazo za sajili:

i. Sajili hufasiriwa kwa kuangalia anachokifanya mtumiaji wa lugha na lugha inayohusika katika kipindi fulani maalum.
ii. Sajili huwa na mitindo funge ya msamiati na sarufi inayopatikana katika muktadha fulani.
iii. Sajili hubainishwa kwa kuangalia sifa maalum ambazo ni vitambulishi vya uwanja husika.
iv. Msamiati ulio katika uwanja fulani unaweza kuunda ‘kikoa’ fulani ambacho huweza kuelezwa kwa urahisi.
v. Sajili hufungwa kwa muktadha.

Kutokana na maelezo haya, mshairi Kithaka wa Mberia amefaulu katika matumizi ya sajili kurejelea nyanja mbalimbali. Ameangazia muktadha wa kijiografia, kihistoria, kijamii, kidini, kitamaduni na kisiasa. Mshairi amedokeza sajili mbalimbali, mathalan:

### 4.2.1 Sajili ya Siasa

Kulingana na Heywood (1997), siasa ni taaluma ya utetezi wa hoja za umma, uongozi au ugawaji mamlaka na rasilmali. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* (2007), mshairi ameegemea sana katika sajili ya siasa kwa sababu mashairi mengi yanaakisi utawala na changamoto zilizopo.

Ushairi katika diwani ya *Msimu wa Tisa* umejikita katika mazingira ya kihistoria na kijiografia ya bara la Afrika. Mshairi Kithaka wa Mberia aliandika wakati ambapo bara la Afrika lilikuwa likipitia changamoto anuwai. Anwani alizotumia zinatokana na hali halisi katika nchi ya Kenya na nchi zinginezo barani Afrika. Waafrika walijizatiti kupigania uhuru wao na kumwondoa mkoloni ambaye alikuwa anawakandamiza kila kuchao. Mawazo haya ameyaendeleza katika diwani ya *Rangi ya Anga* (2014), anapoangazia shairi la 'Zimwi la Theluji' (uk. 48). Anaangazia ujio wa wageni ambao ni Waarabu, Wazungu wamisheni na wakoloni ambao kupitia kuwahadaa wenyeji wa Kenya, hatimaye wakajitwalia maeneo yenye rotuba, rasilmali na malighafi. Wakati wenyeji walizinduka walianza vita ambavyo vilisababisha maafa na wakoloni wakarudi makwao. Ijapokuwa walirudi, bado wanatawala njia kuu za uzalishaji mali ulimwenguni; tuko chini ya himaya yao.

Ushairi huu unatilia mkazo maoni na uchunguzi wa Fatton (1990) anayesema kwamba uongozi wa kiuchumi na kijamii katika mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni ulikuwa wa kudhalilisha na kukandamiza. Wakoloni walimiliki mashamba na kuunda sheria zilizowafaa huku wakiwakandamiza watawaliwa. Ukombozi wa mataifa mengi ya Afrika ulitarajiwa kuleta nafuu kwa wananchi lakini ikawa ni balaa si beluwa. Viongozi waliochukua usukani waliendeleza kasumba ya kikoloni huku nao ukoloni mamboleo ukishika kasi. Kithaka wa Mberia anaonyesha namna viongozi wamekuwa mbioni kujilimbikia mali kupitia ufisadi, unyanyasaji na unyonyaji; jambo ambalo linazidi kuwakera watawaliwa na wanyonge. Vita vya kikabila, mizozo ya kisiasa, ugaidi, njaa, ukame na maafa ni wimbo wa kila siku katika maisha ya wanyonge na watawaliwa. Nchi zilizoathirika zaidi tangu mwaka wa 1963 ni kama vile Kenya, Sudan, Kongo, Msumbiji na Afrika Kusini.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mtunzi ameangazia misimu ya utawala katika bara la Afrika hasa tangu nchi ya Kenya kujipatia uhuru mwaka wa 1963. Misimu hii ya utawala imetawaliwa na njaa, mizozo ya kisiasa, ufisadi, ugaidi, vita vya kikabila, maafa, unyonyaji, ukimbizi na masuala mengineyo. Kwa mfano, ameangazia vita vya kikabila nchini Kongo, mzozo wa rasilmali nchini Sudan, misimu mitatu ya uongozi nchini Kenya tangu 1963, ubaguzi wa rangi katika nchi ya Afrika Kusini, mizozo ya kisiasa nchini Msumbiji na mengineyo.

Mazingira ya kijamii na kitamaduni yamechangia pakubwa katika kuendeleza jamii/uongozi. Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la ‘Rangi ya Anga’ (uk. 1), mshairi anatuchorea taswira ya namna tofauti za kijinsia zinavyowaathiri wanajamii.

Kwa mfano, wanawake wanadhalilishwa kielimu, katika ndoa na katika urithi wa mali. Mambo haya na mengineyo yanazua mgogoro katika jamii na wanawake kuamua kutetea usawa wa kijinsia. Mshairi amezingatia sifa zifuatazo za matumizi ya lugha kubainisha sajili ya siasa:

i. Matumizi ya msamiati teule katika utunzi. Mshairi ametumia msamiati unaorejelea uongozi. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Tope la Mizozo' (uk. 6), mshairi ametumia msamiati kama vile, serikali iliyobeba vibuyu vya ahadi za asali, kumaanisha viongozi ambao waliwahadaa wananchi kwa ahadi za uongo ili wawapigie kura lakini baada ya kupigiwa hawajatimiza ahadi hizo. Aidha, anasema ya kwamba miguu ya taifa imetawaliwa na tope nzito la mizozo, kumaanisha wananchi wametawaliwa na viongozi walio mbioni kujilundikia mali kwa njia za ufisadi bila kuwajali wananchi. Vilevile, katika shairi la 'Msimu wa Tisa' (uk. 9), kuna msamiati kama vile, 'wimbo wa uzalendo'. Mshairi anashangaa ni nani atakayeimba wimbo wa uzalendo katika huu uongozi laanifu. Aidha, anaangazia namna mawaziri wanasusia vikao vya bunge huku wakijishughulisha na anasa kama vile kucheza gofu.

   Lugha hii ya kisiasa vilevile inataja nchi mbalimbali ambazo zilikumbwa na mizozo. Kwa mfano, nchi ya Kongo (uk. 19), Sudan ya Kusini (uk. 29, 48, 49), Angola na Msumbiji (uk. 81) na nyinginezo. Vilevile, ametaja miji mbalimbali kama vile Darfur (uk. 26), Soweto, Pretoria (uk. 37). Hali kadhalika, ametaja bara la Afrika mara kadhaa; dhihirisho kwamba anaangazia uongozi katika bara hili. Kwa mfano, shairi 'Muungano wa Afrika' (uk. 91) na 'Nyota angavu ya Afrika' (uk. 39) katika shairi, 'Mnara Mwangavu (uk. 36).

Katika siasa za kijinsia, mshairi ametumia msamiati unaoashiria jinsia ya kiume na kike. Isitoshe, ameangazia msamiati unaosawiri dhuluma kwa jinsia ya kike ambayo inatokana na taasubi ya kiume kutawala katika jamii, kwa hivyo kuzua mtafaruku. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Rangi ya Anga', mshairi anaangazia masuala mbalimbali yanayozua mgogoro baina ya wanawake na wanaume. Kwa mfano, haki ya kumiliki ardhi ni ya wanaume (uk. 3), mwanamke kubezwa katika usemi, kutwezwa anapotenda, kudharauliwa sokoni, kudhalilishwa nyumbani na kusutwa kwa kuleta duniani watoto wa kike pekee (uk. 6), wanawake wanaokataa kukeketwa ni kinyume na utamaduni (uk. 6), mke kuadhibiwa eti alilipiwa mahari (uk. 7), mwanamke atimiapo miaka kumi na minne ni wa kuozwa (uk. 8) na masuala mengineyo.

Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Ni Kweli' (uk. 55), uozo wa kimaadili unadhihirika pale ambapo anayeumia ni mtoto wa kike. Mshairi anachachawishwa na suala la jinsia ya kike kudhulumiwa kila kuchao na wanaume. Swali analotumia, 'Ni kweli?' linamtia mshawasha msomaji kutetea haki za wanawake katika jamii. Mtoto wa kike anatega mitego ya virinda hotelini kusudi kuleta changu na nguru nyumbani. Baadhi ya wakembe wa kike wanatiririkwa na machozi baada ya wazazi wao halisi wa kiume kuwabaka. Isitoshe, wanachukua nyadhifa za wazazi wao wa kike kutimizia wazazi wao wa kiume haja zao za kimwili. Haya yote ni kutokana na taasubi ya kiume kutawala katika jamii.

Katika shairi, 'Macho Mekundu' (uk. 59), mshairi anamulika dhiki wanayopitia watoto; jambo ambalo linamghadhabisha zaidi kwa sababu haki za watoto

zimekiukwa. Kwa mfano, wanashiriki dawa za kulevya, wanatekwa nyara na kuishi msituni kula matunda mwitu na warudipo vijijini wanawanyang'anya watu vyakula, kuwaua na kuwabaka ndugu zao. Isitoshe, wao ndio huwekwa mbele na wanamgambo wakati wa vita huku wa kike wakizima uchu wao. Kwa ujumla ametumia msamiati teule kuelezea dhuluma kwa watoto.

ii. Mshairi ametumia lugha ya lakabu katika utunzi wa mashairi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 100), lakabu ni jina la bandia analotumia mwandishi fulani. Katika diwani teule, kusudi kuu la mshairi kutumia majina ya lakabu katika ushairi unaohusu siasa ni kuficha siri fulani asije akashutumiwa na wanajamii au walengwa. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mshairi ametumia majina kadhaa ya lakabu, mathalan, katika shairi la 'Mkasa' (uk. 13), kifungu cha sita, anatumia, 'Ubalozi wa Mwewe' kumaanisha ubalozi ulio adui wa magaidi. Ubalozi huu ni wa Marekani unaopiga vita ugaidi ulimwenguni. Katika ukurasa unaofuatia (uk. 11), ametumia lakabu, ving'ora vya 'Nipisheni Njia! Hii ni dharura' kumaanisha ambulensi. Katika shairi la 'Magenge Matatu' (uk. 32), mshairi ametumia lakabu, 'Mfalme wa Nzige', kumaanisha kiongozi wa nchi ambaye utawala wake ulijaa ufisadi, hila, tamaa na uzingizi, kwa hivyo alihitaji kutolewa mamlakani.

iii. Matumizi ya lugha ya kijazanda katika kusawiri maudhui na wahusika. Kama tulivyoelezea awali, jazanda ni lugha ambayo ina maana fiche. Mara nyingi washairi hulenga viongozi walio mamlakani wanapoandika ushairi wao. Mshairi ametumia anwani za kijazanda katika mashairi mengi yanayogusia siasa. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la Usingizini' (uk. 5), mshairi anaangazia usingizi

wa kisiasa; kutozinduka kwa wanajamii na kutambua rasilmali na uwezo walio nao wa kujiendeleza kiteknolojia na kilimo. Katika shairi la ‘Tope la Mizozo’ (uk. 6), mshairi anaonyesha kwamba serikali inajumlishwa na viongozi ambao wako mbioni kujilundikia mali kupitia ufisadi na kila mmoja anang’ang’ania upande wake, kwa hivyo kusababisha migogoro. Katika shairi la ‘Magenge Matatu’ (uk. 32), mshairi anaangazia misimu mitatu ya uongozi nchini Kenya chini ya marais watatu tangu mwaka wa 1963. Genge hili ni kundi la viongozi wasiofaa kutokana na matendo yao maovu. Hali kadhalika, matumizi mengi ya jazanda yameangaziwa katika sifa ya tatu ya matumizi ya mtindo.

iv. Matumizi ya vifananisho yamedhihirishwa katika miktadha ya siasa. Lugha ya siasa husheheni matumizi mengi ya tashbihi na sitiari katika kuelezea hulka za wahusika. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Ni Kweli?’ (uk. 55), mshairi anatumia tashbihi anaposema:

> …Hutiririkwa na machozi na damu
> Baada ya wazazi alo halisi wa kiume
> Kuwasagasaga kama nyama ya sambusa…

Mshairi ametumia tashbihi, ‘kuwasagasaga kama nyama ya sambusa’ ili kukashifu tabia potovu za wazazi wa kiume kuwabaka watoto wao wa kike. Aidha, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 10), mshairi anaonyesha ukali alio nao mzazi wa kiume kwa mtoto wa kiume. Anasema:’usicheke kiholela kama wewe ni mwanmke’ na ‘ushindwaye na madogo kama mavazi yako ni kamisi na rinda’. Baba anamkaripia mwanawe wa kiume kwa kuwa na tabia za mwanamke ilhali anafaa kuwa dume.

Mshairi pia ametumia sitiari kuangazia sifa chanya za viongozi. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Mnara Mwangavu’ (uk. 39), anafananisha kiongozi Nelson Mandela na ‘Mnara wa Almasi ya utu’; ni Johari la kujivunia katika bara la Afrika.

v. Lugha ya kejeli imetumiwa hasa pale ambapo viongozi/wanajamii wamekiuka maadili. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Msimu Mwingine wa Wasaliti’ (uk. 12), mshairi anawakejeli viongozi kwa kuwaita ‘vitimbakwiri’ yaani viongozi wenye ubinafsi. Anasema:

> Vitimbakwira watarudi karibuni kutoka karamu haramu
> Utaziona barakoa za tabasamu kwenye nyuso zao
> Watakuja kutugawia peremende zenye sumu ya akili…

Katika shairi, ‘Waharifu Huru’ (uk. 30), mshairi anakejeli viongozi waliosababisha vita vya kikabila nchini Kenya baada ya kutoridhishwa na matokeo ya urais.

> Badala ya wenye damu viganjani kutupwa korokoroni
> Wanaendesha mashagingi yenye bendera za mamlaka
> Wanalipwa mishahara minono wakiitwa “viongozi wa taifa”!

Kulingana na kifungu hiki, viongozi hawa bado wako huru wakizidi kupokea mishahara minono huku waathiriwa wakikoseshwa haki mahakamani.

vi. Lugha ya kusifu viongozi wenye utu katika jamii imetumiwa. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Mnara Mwangavu’ (uk. 36), mshairi anamsifu kiongozi wa Afrika Kusini, Nelson Mandela, ambaye alijizatiti kutetea uhuru wa Waafrika nchini kutokana na ubaguzi wa rangi. Anamtaja kama mwenye moyo pendezi kama taa, yeye ni sawa na nyota iliyokataa kuzima, aliyeongoza bila sumu ya ubaguzi na aliyesuka utaifa kama wavu adimu.

### 4.2.2 Sajili ya Dini

Sajili hii ya maabadini imesheheni lugha ya dini kwa pakubwa. Katika diwani ya Rangi ya Anga, sajili ya dini imetumika katika shairi la 'Zimwi la Theluji' (uk. 52) wakati mshairi anaangazia wamisheni waliokuja kueneza injili ya Ukristo nchini Kenya. Lugha hii ina sifa zifuatazo:

i. Msamiati wa maabadini umetumiwa. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 52), msamiati kama vile: Muumba wa yote (Mungu), Baba na Mwana (Mungu baba na mwanawe Yesu Kristo) na Mkuu wa wavuvi (mkuu wa wafuasi wake) umetumika.

ii. Mshairi pia ametumia lugha shawishi inayonasa hisia za mrejelewa. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 52), wamisheni walipokuja walikuwa na simulizi zenye vituko vya ajabu vilivyolemaza akili za wenyeji; visa vilivyohusu kutembea juu ya maji na kufufua wafu; kugeuza maji arusini na kuyafanya tembo adimu.

iii. Lugha ya kijazanda imedhihirishwa katika sajili ya dini. Kwa mfano, Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 52), mshairi anasema kwamba Mwana wa Pekee aliwafunza binadamu kula nyama ya mwili wake na kunywa damu yake. Hii inamaanisha kushiriki Meza ya Bwana ambapo 'kula mwili wake' ni kushiriki naye katika mateso aliyopata msalabani na damu iliyomwagika ili ituoshe sisi Wakristo tupate kutakasika.

iv. Mshairi ametumia lugha ya taniaba katika sajili hii kwa kusudi la kufananisha. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 52), mshairi anasema: 'Yesu Kristo ni mkuu wa wavuvi'. Vilevile, ametajwa kama 'Mwana wa Pekee wa Mungu'.

v. Lugha ya sitiari imetumiwa kufananisha walimwengu na aina mbalimbali za samaki. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk.52). Anasema:

> …Mwana ambaye
> Ni mkuu wa wavuvi
> Kwenye bahari ambamo
> Tonzi na kambare
> Na tafi na michumbururu
> Na change na chewa
> Na mikunga nan guru
> Ni wewe nami-
> Binadamu!..

Katika kifungu hiki, mshairi ametumia mifano ya aina mbalimbali ya samaki kama vile: kambare, change, tonzi na wengineo na kuwafananisha na binadamu.

### 4.2.3 Sajili ya Zaraa

Mshairi ametumia lugha inayohusiana na shughuli za kilimo ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wake. Sajili hii imesheheni sifa zifuatazo:

i. Msamiati teule umetumiwa kuangazia aina mbalimbali za kilimo kama vile kilimo cha mimea na kilimo cha mifugo. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Ntharene’ (uk. 74), mshairi ametaja mazao ya mimea kama vile mapapai, tamata, ndizi, parachichi, viazi vikuu na viazi vitamu. Vilevile, matunda mengi zaidi yametajwa katika shairi la ‘Ukarimu wa Ekweta’ (uk.78). Matunda yaliyonawiri vizuri yametajwa. Kwa mfano, chungwa, embe, tufa, pera na plamu. Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la ‘Wanda’ (uk. 31), mshairi ametaja mashamba yaliyonawiri mimea mbalimbali kama vile, mawele, kunde, wimbi, mtama, mahindi na mbaazi. Hali kadhalika mshairi ametaja kilimo cha mifugo kama vile ng’ombe (uk. 32).

ii. Majina ya mandhari maalum yametumiwa. Kwa mfano, mshairi ametaja mandhari yaliyoathiriwa na mbinu za kilimo zisizofaa kama vile kufuga mifugo wengi kupita kiasi katika kikataa, kilimo cha lima-hama-lima, kulima karibu na mito na kushambulia misitu kwa panga huku mazingira yakiharibiwa. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Wanda' (uk. 40), Mto Thanantu umeathirika pakubwa, maskani yaliyokuwa ya ndege, samaki na vyura sasa yamekuwa ganjo. Maeneo mengine ni kama vile Kereka, Gitugu, Kamwathu, Kaguma, Kamanyaki, Gaciongo, Gakauni, Kamaindi, Mutino, Nkarini, Ntoroni, Kamajagi na Ntumira (uk. 41-42).

iii. Viarifa vya kusifu na kukejeli vimetumiwa. Ili mimea inawiri inahitaji virutubishi na pembejeo. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Ukarimu wa Ekweta' (uk. 78). Mshairi anasema:

> Asanteni jua, mvua, udongo na hewa
> Ushirikiano wenu na mkono wa mkulima
> Umeifanya meza ya kiamshwa-kinywa
> Kuwa mwandani wa kutamanika
> Katika urafiki wa kuaminika…

Katika kifungu hiki, mshairi amesifu jua, mvua, udongo, hewa na mkulima. Vilevile, amekashifu vitendo vya kilimo ambavyo havifai. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Wanda' (uk. 30), mshairi amekashifu kilimo cha lima-hama-lima ambacho kimepotosha panga kwa kushambulia mimea kwenye kingo za mito, miinuko ya vilima na chemchemi adimu. Aidha, amesema kilimo kikongwe kimehujumu ardhi, kugofua rotuba na kupambua mazingira.

iv. Mshairi ametumia tashhisi kudhihirisha hisia nzito kuhusu suala fulani. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Ukarimu wa Ekweta' (uk. 78). Mshairi anasema:

> Kesho, liamkapo jua, nanasi litachukua zamu
> Likishirikiana na embe, tufa, pera na plamu,
> Kwa nyoyo kunjufu, yanikaribishe mezani…

Katika kifungu hiki, mshairi amesifia jua na mazao ya shambani kwamba ameweza kupata mlo. Aidha, matumizi ya tashhisi yamedhihirishwa katika diwani ya *Rangi ya Anga*, (uk. 41) ambapo Mto Thanantu umepewa sifa ya rafiki. Mshairi anasema:' Ewe Thanantu! Sahibu wa utotoni…Ewe Rafiki niliyeamini…'. Mshairi ameghadhabishwa na mazingira ya Mto Thanantu ambayo yameharibiwa na binadamu kutokana na kilimo kisichofaa.

v. Vifananishi vimetumiwa kulinganisha hali moja na nyingine. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 33). Mshairi anasema:

> Kutoka anga la kiangazi
> Dhuluma
> Zinanguruma kwa nguvu
> Na kubabaisha mabonde
> Na mawanda na vilima
> Mithili mto ulioghafirika
> Na kuasi kingo kwa hasira…

Katika kifungu hiki, mshairi ametumia tashbihi kufananisha makali ya kiangazi na hasira za mto ulioghafirika.

vi. Katika kuangazia maudhui ya kilimo, mshairi ametumia uradidi kwa kusudi la kusisitiza ujumbe. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 33). Mshairi anasema:

> Ole wangu!
> Moyoni
> Napekechwa na uchungu:

Wakulima
Wameua miangati,
Wagemaji
Wamechinja mikoma,
Wasonga-mizinga
Wameangamiza mianjate…

Mshairi ameatuliwa moyo na uharibifu wa misitu huku mimea ya kiasili ikizikwa katika kaburi la sahau. Ametumia takriri silabi (wa na me) kusisitiza ujumbe huu.

vii. Mshairi ametumia lugha inayodhihirisha hisia alizonazo. Katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 34), anasema yafuatayo:

Tazama jinsi kondoo
Kuku
Kurumbizi
Pimbi
Mikowe
Mbuzi
Mibono
Na sisimizi
Wanavyotapatapa
Katika dimbwi la joto-
Bwawa la huzuni!

Tazama jinsi sura ya udongo
Ilivyo na alama ya jakamoyo
Kwa kukaangwa kwenye tanuri
Ya jua lenye inda!...

Katika vifungu hivi, mshairi ameonyesha kughadhabishwa na kilimo kisichofaa ambacho kina athari hasi kwa mimea, mifugo, ndege na hata udongo.

viii. Maswali balagha yametumiwa kumchochea msomaji atafakari zaidi kuhusu athari hasi za mazingira. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga* (uk. 37). Mshairi anasema:

…Mvua, ewe mvua, mpendwa
Rafiki wa viumbe na mimea
Ungepata hasara ya kimo gani
Ungekaa kwa miezi mingine miwili
Ukaendelea kuhudumia hizi wanda
Kwa dawa yako isiyokadirika thamani?...

Katika kifungu hiki, mvua inayonyesha haitoshi kuistawisha mimea. Mshairi anatamani iwapo ingenyesha kwa muda zaidi basi ingekuwa ya manufaa zaidi lakini sivyo. Kwa hivyo, kutokana na uchanganuzi huu, sajili ni muhimu sana kwa mshairi katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Hadhira nayo hupata nafasi ya kujikita katika muktadha wa ushairi na kuuelewa vyema zaidi.

## 4.3 Hitimisho

Sura hii imehakiki sifa za kimtindo za kitamathali na zinazoegemea muktadha katika diwani teule za *Rangi ya Anga* na *Msimu wa Tisa*. Sifa hizi hujenga tafakuri ya msomaji na kumfanya aelewe ujumbe wa shairi kwa utondoti. Vilevile, humwelekeza msomaji kufasiri ujumbe ipasavyo. Ni dhahiri kwamba mashairi teule hayawezi kukamilika bila matumizi ya sifa za kitamathali, hasa, jazanda, taswira, sitiari, taashira na tashbihi. Aidha, matumizi ya lugha kutegemea muktadha ambapo sajili mbalimbali zimechanganuliwa. Ni bayana kwamba miundo ya lugha na lugha ya kitamathali huonyesha jinsi lugha inavyoathiri maana kwa njia fulani. Sura ya sita na ya mwisho inaangazia matokeo ya utafiti, matatizo tuliyokumbana nayo katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data, vilevile mapendekezo ya nyanja za kufanyia utafiti.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, hitimisho na muhtasari wa masuala muhimu katika utafiti huu yameshughulikiwa. Aidha, matokeo ya utafiti yametokana na maswali na malengo ya utafiti. Hali kadhalika, sura hii imetoa changamoto ambazo mtafiti alikumbana nazo katika kufanya utafiti na uchanganuzi wa data. Isitoshe, imetoa mapendekezo ambayo yatawachochea watafiti wengine kushughulikia pengo lililopo katika ushairi huru wa Kiswahili. Mapendekezo haya yakitiliwa maanani yatazidi kuimarisha ushairi hhuru wa Kiswahili na kuupa umaarufu zaidi.

### 5.1 Muhtasari

Uchanganuzi wa data umeegemea katika maswali na malengo ya utafiti. Utafiti huu kwa ujumla ulilenga kutathmini dhima ya vipengee vya muundo na mtindo katika diwani teule. Mathalan,

1. Kuhakiki sifa mbalimbali za muundo katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga.*
2. Kuchunguza dhima ya sifa za kigrafolojia katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.
3. Kuchambua sifa za kitamathali na zinazotegemea muktadha katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

Katika kutathmini dhima ya muundo na mtindo, mashairi kutoka diwani za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga* yamechanganuliwa huku yakiwakilisha tungo zingine za ushairi

huru katika diwani teule na ushairi huru kwa ujumla katika kipindi cha sasa. Tasnifu hii imegawanywa katika sura sita. Sura ya kwanza imeangazia ufafanuzi wa istilahi, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada. Aidha, misingi ya nadharia, upeo na mipaka na yaliyoandikwa kuhusu mada yameshughulikiwa pia. Zaidi ya hayo, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data ni maeneo ambayo yameshughulikiwa pia. Sura hii imetupa mwangaza wa suala la utafiti ambalo ni Muundo na Mtindo katika Diwani za *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*.

Kutokana na utafiti wetu, sifa za kimuundo na kimtindo katika diwani teule zimeshughulikiwa kwa undani na kwa namna dhahiri ili kumwelekeza msomaji wa ushairi na watunzi ibuka. Hali kadhalika, utafiti huu umeshughulikia dhima za kila mojawapo ya sifa za kimuundo na kimtindo katika diwani teule huku mifano mwafaka ikitolewa.

Katika sura ya pili, sifa za kimuundo zimechanganuliwa. Mathalan,

i. Matumizi ya idhini nyingi za kishairi.
ii. Matumizi ya lugha ya kimuziki
iii. Muundo wa ushairi unaathiri upokezi wa ujumbe.
iv. Muundo wa ushairi huathiriwa na vipengele mbalimbali.
v. Utumiaji  michoro kuwasilisha ujumbe maalum.
vi. Matumizi ya mistari yenye urefu tofauti.

Vipengele hivi vya kimuundo katika diwani teule ni muhimu katika kuufasiri ujumbe wa mshairi.

Sura ya nne na ya tano zimeshughulikia dhima ya vipengee vya mtindo. Katika sura ya nne, vipengee vya kigrafolojia vimechanganuliwa. Mathalan, ukiukaji wa njia za kawaida za uakifishaji, matumizi ya takriri na marudio, matumizi ya lugha ya kawaida yenye uwezo wa kuibua hisia, mguso na taathira pamoja na matumizi ya toni katika kuwasilisha ujumbe. Katika sura ya tano, sifa za kitamathali na matumizi ya lugha kutegemea muktadha ndivyo vipengee ambavyo vimechanganuliwa kwa undani. Diwani teule zisingekamilika bila vipengele hivi vya kimtindo. Isitoshe, vinaonyesha ubunifu na ukwasi wa lugha wa mtunzi. Uchanganuzi wa data umeongozwa na nadharia mbili: nadharia ya uhakiki ya umuundo na nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Nadharia ya uhakiki ya umuundo imefafanuliwa na Culler (1975: 126), aliyesisitiza kwamba ushairi ni ishara zinazojisimamia bila kudhibitiwa na mtunzi na ufasiri wa maana unatokana na namna vipengee vya kimuundo huchagizana kimaana. Pia, nadharia ya uhakiki wa kimtindo iliyoasisiwa na Coombes (1953) imetumika ili kuchanganua mtindo, ambao unaegemea katika matumizi ya lugha.

Mihimili mikuu ya nadharia zote mbili imetumika katika uchanganuzi wa data. Katika kuchanganua sifa za kimuundo, mihimili mitatu imetumika. Mathalan, viwango vya kimofolojia na kisintaksia ni msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matumizi ya lugha yenyewe. Mhimili huu umetumiwa kuhakiki sifa za kimuundo kama vile matumizi ya idhini nyingi za kishairi, matumizi ya lugha ya kimuziki na urefu wa sentensi. Vilevile, mhimili huu umetumiwa katika kuhakiki sifa za kimtindo zinazotegemea muktadha. Aidha, mhimili wa matumizi ya maumbo ya picha na ya kipekee ili kuonyesha umilisi wa mtunzi katika kuelezea hisia zake umetumiwa kuhakiki matumizi ya michoro. Isitoshe, mhimili mwingine uliotumika ni kwamba vipashio mbalimbali vya muundo huingiliana

na kujengana. Mhimili huu umetumika kuchanganua matumizi ya lugha ya kimuziki, athari ya vipengele mbalimbali kama vile dhamira na wahusika katika ushairi pamoja na idhini za ushairi. Katika kuchanganua sifa za kimtindo, mihimili mbalimbali ilitumika. Kwa mfano, matini ya kifasihi huweza kuwa na sifa za kimaandishi zinazochimuzwa na kutiliwa mkazo katika ukiushi. Mhimili huu ulitumika kuhakiki sifa za kigrafolojia. Aidha, miundo ya lugha na lugha ya kitamathali huonyesha jinsi lugha inavyoathiri maana kwa njia fulani. Mhimili huu ulitumika kuchanganua sifa za kitamathali na zinazotegemea muktadha katika diwani teule.

Mashairi teule katika diwani mbili za Kithaka wa Mberia: *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014), yametumika kama data ya kimsingi katika upambanuzi wa vipengee teule katika mashairi teule. Zaidi ya hayo, data ya nyanjani iliyohusisha mahojiano na mtunzi teule imechangia pakubwa katika kutia uketo matokeo ya utafiti. Hasa, katika kuelewa kiini cha utunzi wake pamoja na matumizi mbalimbali ya vipengee vya kimuundo na kimtindo.

**5.2 Matokeo ya Utafiti**

Uhakiki wa vitabu teule: *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*, umeonyesha kwamba vipengele vya kimuundo na kimtindo katika mashairi teule ni vipengele vya kimsingi katika utunzi na usomaji. Maswali na madhumuni ya utafiti yametumiwa kama msingi wa kuchanganua data husika. Utafiti huu ulilenga kutathmini sifa za kimuundo katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Uhakiki umethibitisha kwamba mashairi teule yana sifa zifuatazo za kimuundo:

1. Mashairi teule yana idhini nyingi za utunzi wala sio lugha ya kinathari kama wasemavyo wataalamu wa kimapokeo. Kwa mfano, yamepangwa katika mafungu ya maneno kuyatofautisha na riwaya au hadithi. Aidha, yanatumia mistari mishata, mipangilio mbalimbali ya sauti, maneno na mistari kimaksudi pamoja na matumizi ya lugha ya mkato na yenye mnato. Sifa hizi ni muhimu katika kujenga wizani ya ushairi. Nadharia teule zimedokeza kwamba viwango vya kimofolojia na sintaksia ni msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matumizi ya lugha yenyewe. Jinsi mawazo yanavyotiririka katika akili ya mtunzi ndivyo anavyoyaweka katika matini. Mtiririko huu unajenga aina fulani ya wizani ambayo msomaji ataitambua kupitia mpangilio wa sauti, maneno, mafungu ya maneno na mistari.
2. Mashairi teule yametumia lugha ya kimuziki inayowaathiri wasomaji. Mahadhi yake yanafanana au kukaribiana na nyimbo za Kibantu. Kwa hivyo yanaweza kuimbika.
3. Mpangilio wa mafungu ya maneno, mistari na sauti katika mashairi teule husawiri fikra za mtunzi zinazodhihirika kupitia utunzi. Mpangilio huu humwathiri msomaji kwa pakubwa.
4. Muundo wa mashairi teule hubadilika kutegemea dhamira, maudhui, matumizi ya lugha, wakati, wahusika na upekee wa mtunzi katika kuwasilisha kazi yake. Kwa hivyo, muundo wake si tengemano. Masuala haya yanaathiri utunzi na mtiririko wa mawazo wa mshairi Kithaka wa Mberia. Kwa mfano, anapobainisha wahusika katika ushairi anatumia uruwazaji. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la ‘Kitini’ (uk. 18) anapobainisha usemi wa waziri na wananchi. Wakati anapoangazia maudhui, kwa mfano, maudhui ya kijinsia, anabadili usimulizi na

kutumia usemi halisi kuashiria jinsia ya msemaji. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la 'Rangi ya Anga'.

5. Mashairi teule yametumia michoro ya kimaksudi kuwasilisha ujumbe maalum. Ni njia mojawapo ya kuibusha ujumi na ubunifu wa mshairi. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, shairi la 'Muungano wa Afrika' (uk. 90), ambapo mshairi anawashajiisha Waafrika kuishi kwa umoja. Aidha, michoro aliyoitumia mshairi inampa msomaji nafasi ya kutafakari zaidi kuhusu anachokizungumzia.
6. Mashairi teule yamezingatia matumizi ya mistari yenye urefu tofauti kutegemea mtiririko wa mawazo katika akili ya mtunzi. Ni bayana kwamba jinsi jamii inavyokua ndivyo ushairi unavyozidi kupanuka kimuundo.

Isitoshe, utafiti huu ulilenga kuchunguza malengo mawili ya kimtindo. Mathalan, ulilenga kuchunguza sifa za kigrafolojia katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Uhakiki umeonyesha kwamba vipengele vya kigrafolojia anavyotumia mtunzi vina dhima kuu katika ujenzi wa mashairi teule. Hususan, matumizi ya viakifishi kama vile herufi kubwa, koma, nukta pacha na viakifishi vinginevyo, yanakiuka njia za kawaida za kuakifisha. Kusudi kuu ni kudhibiti usomaji wa mashairi teule pamoja na kujenga wizani. Aidha, kuna matumizi ya marudio na takriri ili kusisitiza ujumbe. Isitoshe, kuna matumizi ya lugha ya kawaida yenye uwezo wa kuibua hisia, mguso na taathira kwa msomaji pamoja na matumizi ya toni kuwasilisha ujumbe. Jambo hili linaupa ushairi uhalisia.

Hali kadhalika, utafiti huu ulilenga kuchambua sifa za kitamathali na zinazotegemea muktadha katika ushairi huru wa *Msimu wa Tisa* na *Rangi ya Anga*. Kuna matumizi

mengi ya vipengele vya kitamathali kuliko vya kiarudhi katika uwasilishaji wa dhamira. Vipengele hivi ni kama vile jazanda, sitiari, taashira, taswira na tashbihi. Mshairi ametumia tamathali hizi kuwasilisha masuala nyeti katika jamii kama vile siasa, migogoro ya kijinsia na uharibifu wa mazingira. Aidha, mtunzi ametumia tamathali hizi ili kukuza uwezo wa msomaji wa kufasiri ujumbe ipasavyo, kujenga umakinifu na kuchochea hisia zake ili kutekeleza wajibu wake katika jamii. Vipengele hivi pia vimetumika kusisitiza ujumbe. Kwa mfano, mshairi ametumia jazanda ya 'Magenge Matatu' katika diwani ya *Msimu wa Tisa* kudhihirisha viongozi wadhalimu chini ya viongozi watatu waliowahi kutawala nchini Kenya.

Vilevile, lugha inayotumiwa katika mashairi teule inaegemea sajili mbalimbali kama vile siasa, mazingira ya kilimo na dini katika jamii. Watunzi wengi huathiriwa na mazingira walimokulia, kwa hivyo kupanua ufahamu wa msomaji wa kihistoria, kijiografia na kisosholojia. Kulingana na Mazrui na Syambo (1992: 2), kila utungo wa fasihi una chanzo chake katika maisha ya binadamu. Hazina kubwa ya msanii wa fasihi ni jumla ya maisha yanayopatikana katika mazingira yake. Kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kwamba, msanii hupata tajriba na mawazo ya utungo kutokana na mazingira anayokumbana nayo. Vilevile, huanza kupiga mbizi na kuangalia tulikotoka na kuelewa barabara kilichosababisha hali tuliyonayo na kubashiri yajayo. Mtunzi Kithaka wa Mberia ni mzaliwa wa Kenya kutoka kaunti ndogo ya Tharaka na amekulia katika mazingira ya Kenya barani Afrika; mazingira ambayo yamemtia mshawasha wa kuandika kazi zake za fasihi akilenga jamii husika. Kutokana na uchanganuzi wa data katika diwani teule, mshairi amechochewa na mazingira yake kwa pakubwa. Ushairi huu unaangazia matukio halisi katika jamii kama vile dhuluma kwa jinsia ya kike, uharibifu

wa mazingira na ukoloni mkongwe na mamboleo katika nchi za Afrika na hasa Kenya. Anatilia mkazo maoni ya Wordsworth (1797: 52) kwamba ushairi husawiri hisia na matukio yanayomzunguka binadamu. Mazingira haya ya kihistoria, kijiografia na kijamii yamewasilishwa kwa matumizi ya lugha. Aidha, maisha ni safari. Mtunzi wa diwani teule anawasilisha kazi yake kwa kutumia motifu ya safari; safari ambayo ni ya kujisaka ili tuzinduke na tujielewe sisi ni kina nani na tunaishi vipi. Mtunzi anaangazia mazingira yake na kwa sababu anayaelewa ni rahisi kuyazungumzia bila utata wowote. Kwa mfano, anapozungumzia maeneo ambayo alikulia kama vile, 'Ntharene', 'Mwea', 'Ukarimu wa Ekweta' na mashairi mengineyo. Kwa hivyo, uhakiki huu umedhihirisha kwamba jinsi jamii inavyobadilika ndivyo utunzi wa mashairi unavyoathirika pia.

## 5.3 Changamoto

Katika utafiti huu, kuna baadhi ya changamoto ambazo tulikumbana nazo. Mwanzo, katika usomi tulitambua vipengele vingi zaidi kuliko vile tulivyokusudia awali; jambo ambalo lilizidisha muda wa uchanganuzi wa data.

Pili, data nyingine ya asili ilikuwa katika lugha ya Kiingereza na ilibidi kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Ilikuwa changamoto kutafsiri maana ya istilahi mbalimbali ambazo zina ukinzani wa maana na ambazo wataalamu wengi hawajabainisha wazi.

Tatu, ukosefu wa usanifishaji wa istilahi mbalimbali za Kiswahili. Kuna tamathali za usemi ambazo bado hazijasanifishwa kwa hivyo kuingiliana na kuleta utata katika ufafanuzi wa maana. Kwa mfano, jazanda na istiara.

## 5.4 Mafanikio

Licha ya changamoto tulizokumbana nazo, kutokana na utafiti wa kina, istilahi tata zimefasiriwa vilivyo kimuktadha na kuondoa utata uliokuwepo hapo awali. Aidha, ni bayana kwamba mashairi teule yana sifa za kishairi wala si kazi ambayo imeandikwa kwa lugha nathari. Sifa hizi zinayapatia mashairi teule upekee na kudhihirisha ubunifu wa mtunzi katika kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji.

Isitoshe, mtunzi ametumia lugha ya kitamathali na ya kawaida katika utunzi wake. Lugha hii ina ina uwezo wa kuibusha hisia ambazo zinamwathiri msomaji. Hali kadhalika, uwasilishaji wa mashairi teule katika utunzi unadhihirisha kiwango cha juu cha ubunifu. Hii ni njia mojawapo ya kukuza sanaa ya Kiswahili kwa kuibusha mitindo mipya ya utunzi kuliko kuegemea katika ile mitindo iliyozoeleka ya vina na mizani. Ni matumaini yetu kuwa washairi chipukizi watazingatia sifa za kimuundo na za kimtindo tulizofafanua kutunga mashairi ya kisasa.

## 5.5 Mapendekezo

Kutokana na utafiti huu, imedhihirika kwamba sifa za muundo na mtindo ni vipengee muhimu katika utunzi, usomaji na ufasiri wa ujumbe katika mashairi teule. Katika uchanganuzi wa sifa za kimuundo, sifa mbalimbali zimefafanuliwa kwa undani kwa kurejelea diwani teule za Kithaka wa Mberia. Utafiti zaidi unaweza kufanywa kuangazia watunzi wengine ibuka ili kupata sifa zaidi. Uchanganuzi wa kimtindo umeangazia vipengee vichache, mathalan, jazanda, taswira, taashira, tashbihi, sitiari, sajili, toni, hisia, mguso na taathira. Kuna vipengele vingi ambavyo vinahitaji kufanyiwa utafiti. Utafiti zaidi unaweza kutekelezwa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Matumizi ya wizani katika kudhibiti ushairi wa Kiswahili.
ii. Mchango wa vipengele vya isimu katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili.
iii. Ulinganifu uliopo kati ya ushairi wa watunzi wa Kenya na wa Tanzania.
iv. Matumizi ya sajili katika ushairi wa Kiswahili.

## MAREJELEO


Abedi, A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Ali, J. (2015). *Matumizi ya Kinaya katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia*, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Bruff, A. (2015). *Mr. Bruff's Guide to GCSE English Literature*. Independently Published.

Chapman, R. (1982). *The Language of English Literature*. London: Edward Arnold.

Chatman, S. (1971). *Literary Style*: *A Symposium*. Oxford: Oxford University Press.

Chiraghdin, S. (1977). *Malenga wa Mrima: Tungo za Mwinyihatibu Mohamed*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Cluysenaar, A. (1976). *Introduction to Literary Stylistics*. London: Batsford.

Coombes, H. (1963). *Literature and Criticism.* Newyork: Chatto and Windows.

Crystal, D. & D. Davy (1969). *Investigating English Style.* London: Longman Group Limited.

Culler, J. (1975). *Structuralist Poetics. Structuralism, Linguistics & the Study of Literature*. London: Routledge.

Fatton, R. (1990). "Liberal Demecracy in Africa". *Political Science Quarterly* 105 (3): 455-473.

Fiumara, C. G. (1995). *The Metaphoric Process: Connections Between Language and Life*. London: Routledge.

Freeman, M. H. (2007). "Poetic Iconicity. Cognition in Language": Volume in Honour of Professor Elzbieta Tabakowska, Wladyslaw Chlopicki, Andrzej Pawelec and Agnieszka Pokojska, eds., pp. 472-501, *Annual Review of Cognitive Linguistics*, Krako'w: Tertium.

Gicuku, M. (2011*). Usawiri wa Maudhui ya Ndoa katika Ushairi wa Euphrace Kezilahabi na Kithaka wa Mberia*, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Gromov, M. (2006). "The Question of Kiswahili Style Again? The Poetry of Kithaka wa Mberia", katika *KISWAHILI Juzuu 69*. Dar es Salaam: TUKI.

Heidegger, M. (1971). *Poetry, Language and Thought.* Translations & Introduction by Albert Hofstadter. Newyork: Harper & Row.

Heywood, A. (1997). *Politics*. London: Springer Nature Limited.

Hoopes, J. (Ed.). (1991). *Pierce on Signs: Writings on Semiotic by Charles Sanders Pierce*. Chapel Hill London: The University of North Carolina Press.

Indede, F. (2008). *Mabadiliko katika Umbo la Ushairi na Athari zake katika Ushairi wa Kiswahili: SWAHILI FORUM 15*:73-94.

Juma, N. (2015). *Ulinganishaji wa Uwasilishaji wa Mashairi ya Euphrace Kezilahabi na Kithaka wa Mberia*, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kahigi, K. na M. Mulokozi (1976). *Malenga wa Bara*. Nairobi: East Africa Literature Bureau.

Kahigi, K. na M. Mulokozi (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.

Kezilahabi, E. (1988). *Karibu Ndani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (2008). *Dhifa*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Kibaru, C. (2016). *Taashira ya Mazingira katika Ushairi wa Kiswahili: Mfano wa Diwani ya Sauti ya Dhiki na Msimu wa Tisa,* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

King'ei, K. na A. Kemoli (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Santex Publishers.

King'ei, K. na C. Kisovi (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

KLB (2015). *History and Government, Form Three Students Book*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kuhenga, C. (1977). *Tamathali za Semi*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Kuvuna, S. M. na wenzake (1992). *Nuru ya Ushairi: Mwongozo na Uchambuzi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London & New York: Longman.

Leech, G. & M. Short (1981). *Style in Fiction*: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose 2nd Edition. Harlow: Longman Group Ltd. *; Essays and Reviews on 19th & 20th Century Literature*. London: Routledge & Kegan Paul.

Lodge, D. (1988). *Modern Criticism & Theory*. London: Longman.

Lewis, C. S. (1936). *The Allegory of Love*. London: Oxford University Press.

Lutomia, D. (2017). *Mwanga wa Ushairi kwa Shule za Upili.* Kakamega: Double Shasa Limited.

Maitaria, J. (2012). *Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Dhima ya Methali*, Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Masinde, E. (1992). *Mashairi Huru- Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Massamba, D. P. B. (1983). "Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili" katika *Makala ya Semina za Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*: *Fasihi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Kur. 54-95.

Mayoka, J. (1984). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mazrui, Alamin. (1988). *Chembe Cha Moyo*. Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Mazrui, A. na B. K. Syambo (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mberia, K. (1997). *Mchezo wa Karata*. Nairobi: Maimba Publications Ltd.

Mberia, K. (2001). *Bara Jingine*. Nairobi: Maimba Publications Ltd.

Mberia, K. (2005). *Redio na Mwezi*. Nairobi: Maimba Publications Ltd.

Mberia, K. (2007). *Msimu wa Tisa.* Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mberia, K. (2014). *Rangi ya Anga.* Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mberia, K. (2018). *Doa.* Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mdee, J. S. na wenzake (2018). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Mohamed, S. (1980). *Sikate Tamaa*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Momanyi, C. (1998). *Usawiri wa Mwanamke Mwislamu katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.

Mulokozi, M. na K. Kahigi (1979). Kunga za Ushairi. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M. (1989). *Mgawanyo wa Tanzu na Vipera vya Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI

Mulokozi, M. na T. Sengo (1995). *History of Kiswahili Poetry*. Dares Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Mnyampala, M. (1970). *Diwani ya Mnyampala*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Kifasihi*. Dar es Salaam: East African Education Publishers.

Mwai, W. (1988). *New Trends in Ushairi*, Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwania, J. (2006). *Usambamba katika Ushairi Huru*, Tasnifu ya shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Myres, J. and M. Simms (1989). *The Longman Dictionary of Poetic Terms*. London and New York: Longman Ltd.

Ndumbu, J. (2014). *Matumizi ya Takriri NA Sitiari katika Utenzi wa Rasi'lghuli*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ngara, E. (1982). *Stylistic Criticism and The African Novel*. London: Heinemann.

Njogu, K. (1993). *Dialogic Poetry: Contestation and Social Challenge in East African Poetic* Centres, Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Yale. (haijachapishwa).

Njogu, K. na R. Chimera (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njuguna, H. (2015). *Ukiushi katika Ushairi wa Amri Abedi na Kithaka wa Mberia*, Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ntarangwi, M. (2003). *Gender, Performance & Identity*. NewYork: Africa World Press.

Onyancha, W. (2016). *Changamoto za Mikondo Mipya ya Utunzi wa Mashairi ya Kiswahili*, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Perry, B. (2004). *A Study of Poetry*. LLC: Kessinger Publishing.

Pierce, C. & V. Welby (1977). *Semiotic and Significs*. Canada: Indiana University Press.

Plaks, A. H. (1976). *Archetype and Allegory in The Dream of The Red Chamber*. Princeton and Guidford: Princeton University Press.

Pricket, S. (1975). *Wordsworth, W. & Coleridge, S. The Lyrical Ballads*. London: Edward Arnold.

Saussure, F. (1966). *Course in General Linguistics*. Newyork: Mc Graw-Hill.

Scholes, R. (1974). *Structuralism in Literature: An Introduction*. New Haven & London: Yale University Press.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi na Nadharia ya Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Senkoro, F. E. M. K. (2006). *English- Swahili Dictionary: Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Swahili Literature-History and Criticism*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.

Simpson, P. (2004). *Stylistics*. London & NewYork: Routledge.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R. M. na K. Njogu (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (1999). "A Rhetorical Study of Kiswahili Classical Poetry. An Investigation into The Nature and Role of Repetition", katika *Research in African Literatures*. Indian University Press. Vol. 30 Pg. 58-73.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi. Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wamitila, K. W. (2012). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press.

Wekesa, A. (2008). *Matumizi ya Taswira katika Ushairi Huru wa Kiswahili*. Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wordsworth, W. (1797). *Lyrical Ballads*. London: Methuen & Company Ltd.

Zubkova- Bertoncini, E. (2008). "Some Remarks on Kithaka wa Mberia's Poetry", Makala yaliyowasilishwa katika kongamano la 21st Century Swahili-Kolloquium, Chuo Kikuu cha Bayreuth. 02-04 May.

## VIAMBATISHO

## ORODHA YA VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO 1: MASHAIRI

### MASHAIRI YA KITHAKA WA MBERIA:

***MSIMU WA TISA***

### Minyororo ya Njaa (uk. 1)

Tumerudi kwenye dimbwi la huzuni
Kana kwamba Kamba isiyoonekana
Inatuvuta kila baada ya  miaka mitano
Kuturejesha kwenye bonde la machozi

Kurasa za magazeti na viwambo vya runinga
Vinaonyesha tena picha zinazoshtua hisia:
Watoto waliomumunywa na kinywa cha njaa
Wakabakia na macho yanayodondoka dhiki
Na vipande vya mianzi mikavu ya miguu

Mzee anayekemewa na tumbo inayolalamika
Amekalia gogo huku ukungu wa kukata tamaa
Umezidisha idadi ya miaka usoni mwake
Mbavu zake zimechomoza kama fito zilizopinda
Katika ukuta wa udongo uliovamiwa na mvua

Kwenye Kijiji cha mikakaya, minga na vumbi
Jamaa na majirani waliovaa huzuni kama veli
Wanaaga udongo wa fusi la kaburi ya tano
Wametoa kwaheri zenye moto wa uchungu
Kwa mtoto aliyeshikwa mkono na njaa
Akaambiwa: Njoo nikupeleke kuzimu!

Kwenye Kijiji ng’ambo yam to usiokauka
Mama asiyethubutu kukata tamaa liwe liwalo
Anachemsha matunda-mwitu machungu
Kushawishi kokwa jeuri zilainike chunguni
Kuokoa Watoto wenye miguu ya vunjajungu

Jijini, wimbo ni uleule wa kughasi hisia
Wanasiasa wanalaumu anga kwa janga
Hawaoni kwamba njaa isiyohama nchini
Ni tunda chungu la siasa ya pesa-nane
Siasa bila ramani, bila dira, bila kurunzi

Asemaye kwamba ukame ni kudura ya Mungu
Anenaye njaa ni kazi ni kazi ya uovu wa anga bahili
Ahurumiwe; ameazima ubongo wa bongo!

Anga la nchi si mgeni ni jirani wa miaka na mikaka
Ratiba yake ya  awamu za ukarimu na ubahili si siri
Udongo tunaolima hauna mafumbo yasiyofumbulika:
Unapokabwa koo na kiu hausikii mwito wa wakulima!

Linalotabirika wazi kama kuchomoza jua asubuhi
Litaitwaje ajali ila na mwongo anayehitaji dawa
Au binadamu mwenye ubongo wa kongoni!

### Usingizini (uk.3)

Ardhi yenye siha na uchangamfu wa rutuba
Imelala usingizi katika kitanda cha maumbile
Tukinong'onezana: "Anga linaonea nchi!"
Tambarare zenye uwezo wa kuhimili mamilioni
Zimeachiwa nguchiro, panya, mchwa na nyenze
Katika taifa linalotapatapa katika dimbwi la njaa

Daima dawa ya thamani inatiririka katika mito
Inatpita na kumezwa ovyo na bahari na maziwa
Katika taifa linalonyongwa na mikono ya njaa

Majira yanapofungua mlango mku angani
Na dawa kuteremka kutoka maghubari ya neema
Tunasimama tukitabasamu huku akili zimefunga
Na kuacha tiba ipotee katika mito, bahari na maziwa
Na kuacha taifa likisinzia hadi lishtuliwe njaa

Ni lini reli na barabara za lami na changarawe
Zitaingia katika vijiji vya mikakaya na vikwata
Ili ukame unapoanza vita dhidi ya wafugaji
Masoko ya nyama na ngozi yawe kikimbilio
Kabla ya mifugo kuwa karamu kwa nderi?

Kwa nini wenye nyoyo za kusaka riziki kwa juhudi
Hawana stima ya kuzungumza na chuma na mbao
Katika viwanda chini ya mitini na miembe
Kuunda miavuli ya kujikinga kutokana na njaa?

Wanaonyongwa nyoyo na Mafuta ya utajiri
Wamebana mikononi maelfu ya ekari za rutuba
Huku wajukuu wa waliopokonywa uriyhi kwa mijeledi
Wakiwa hawana vikata vya kukuza vihimili vya maisha!

Kwa nini tunajifanya nyumbu wa Maasai-Mara
Ambao bila kuchukua hatua, miaka na mikaka

Hupigwa difirau na hasira nyekundu ya Mto Mara
Na kuwa karamu murua kwa mamba na nderi
Bila nyumbu asemaye: " Hayatakuwa tena!"

Ni lini tutaimarisha urafiki na teknolojia ya kilimo
Tufue tupa kama mataifa yanayokula bila aibu
Tukate hii minyororo dhalilishi ya masiba wa njaa
Ambayo imetufunga kwenye chuma ya huzuni?

Ni nani anayejua siku adhimu au mwezi azizi
Ambamo wanaokoroma kwenye makochi ya uongozi
Wataamka kutoka usingizi wa siasa bila ramani
Wafikiche macho kwa viganja vya uona-mbali
Waongoze taifa kutoka hili bonde la aibu?

**Tope la Mizozo (uk. 6)**

Serikali iliyoingia ikibeba vibuyu vya ahadi za asali
Ikivaa gwada pendezi lenye rangi za upinde-wa-mvua
Ni kama binadamu aliyekula kiapo kisichovunjika:
"Naapa, kamwe sitafuata barabara ya lami na usalama
Daima nitapita kwenye njia ya tope zito la mizozo
Ewe Mungu usiniondoe kutoka dimbwi la huzuni!"

Kabla ya mwangwi wa shangwe zetu kuyeyuka
Tulioshngilia katika bustani pendezi ya matumaini
Walianza kugongana kama vyuma katika kapu
Likivurutwa na watoto katika mchezo usiokoma

Katika ukungu wa werevu bila maarifa
Wenye tamaa kubwa ya kuwapiku wengine
Walitumia ujanja kwenye sinia ya mamlaka
Wakajitwalia minofu na kuwachia wenzao makano
Gundi ya mkataba uliounga pamoja makundi
Ikayeyushwa na moto wa hamaki ya haki

Punde harufu ya kidonda-ndugu cha ufisadi
Ilishambulia pua ya taifa kama wingu zito la amonia
Na kuanzisha mieleka ya miguno, jasho na vumbi
Baina ya waliokuwa wenza katika vita dhidi ya uoza

Wendao kwa magari yakipeperusha bendera za jaha
Wameburura sheria za nchi kwenye mtaro mchafu:
Wakitumia ujanja kupigia debe mkataba wa umma
Wamehonga kwa mbuga za Wanyama na viti vya ardhi

Wakitumia genge la wahuni wenye dharau kwa wenyeji
Mamluki wenye lugha inayonuka kama samaki waliooza
Wale tuliopatia wadhifa wa kutulinda pamoja na mali zetu
Wamevamia haki zetu kwa kichaa cha usiku wa manane

Wahuni wa kigeni wamekaribishwa nchini kwa siri
Na kupewa vyeo vikuu na funguo za milango ya chuma
Wameishi starehe wakijinaki kwa maneno yenye uvumba
Wakitishia polisi kwa mbwa wakali katika kasri zao
Kijeuri, wakichomoa bastola dhidi ya wahudumu wa umma
Wafadhili wao wenye mashagingi yanayopeperusha bendera
Wakiwatetea kwa lugha thabiti dhidi ya raia na taifa

Misukumano inavuma kama bahari yenye hasira
Ukitafuta mwamuzi humwoni akijaribu kuzima moto
Haneni neno la kukwamua muungano topeni
Miguu ya taifa inataaliwa na tope zito la mizozo

## Werevu (uk. 8)

Angalipuuza mashauri ya wajanja waliomzunguka
Na kuthamini maana ya maneno ya wimbo wa taifa,
Angalizingatia kanuni za mkataba wa majemedari
Silaha iliyokomboa taifa kutoka minyororo ya huzuni,
Angalifahamu uaminifu ni akiba inayozaa matunda
Na kukubali usemi: "Werevu mwingi huondoa maarifa",
Angaligawa mapato kwa ratili iliyopangwa awali
Na kwa kuheshimu kiu cha kambi yake nay a wenza,
Mti wa uelewano ungezidi kuzaa matunda matamu
Leo, kwa furaha, tungalikuwa tukiyala yakiwa mabivu

Badala ya kuongozwa na ndoto ya taifa angavu
Mgavi aizingatia sauti laini za genge la walafi
Akawapakulia thuluthi mbili za sinia la ngawira
Na kuwapunja simba waliopigana kwa meno na kucha

Si ajabu, walioliwa bang una kuteswa na moto wa majuto
Walijiandaa na kusubiri kwenye medani ya mkataba mkuu
Punde viganja vilikazwa katika kamba ya "Vuta Tuvutane!"
Vidole vya miguu vikajikita katika udongo mzito wa kinamo
Weru wakaangushwa na kubururwa kwenye tope la aibu

Gari la siasa likaacha barabara ya lami
Na kujitosa kwenye ujia wenye udongo chepechepe
Mwendo wa kasi tuliotarajia utufikishe kwenye ufanisi
Ukawa safari ya kusukumwa na kuvuta matopeni
Kusudi mgavi asukumiwe gari lipite kinamo lovulovu

Kwa kuogopa kutereza na kukwama kwenye mitaro
Amelainisha makabila kwa mabenzi yenye bendera
Na kuongeza idadi ya  wanaokamua nchi kwa fujo
Kinyume na ahadi iliyong'aa jana kama nyota

**Msimu wa Tisa (uk. 9)**

Leo, ukumbi wa ulumbi umejaa vumbi jeuri
Kimbunga cha ubinafsi, uzembe na kiburi
Kinavuma kama bahari inayoteta na tufani

Ni nani atakayeimba wimbo wa uzalendo
Katika huu ukumbi wa msimu laanifu wa tisa
Ambamo nyoyo za waliotumwa kujenga taifa
Zinadunda kwa mpigo wa ubinafsi uliokithiri-
Ukumbi ambamo wingu la nzige wa jangwa
Linakula karamu haramu kweye mti wa jamhuri

Punde walipokula kiapo cha uaminifu kwa nchi
Bila kujali vinywa vinavyopiga miayo ya njaa
Walivamia ghala la taifa kwa tamaa iliyovuma

Waliovishwa makoja katika baraza la walaji wapya
Walipeperusha bendera kwenye mabenzi ya bei duwazi
Kinyume na ahadi zenye ubani katika majukwaa ya jana
Ambamo tuliahidiwa majira ya nidhamu iliyonga'aa

Zilifuata ziara za kubenua vifua na kuteuka vijijini
Walijinadi kwa akina yahe waliovaa matambara
Walitifua vumbi kwa mabenzi na mapajero mapya
Na kuduwaza watu kwa ujanja wa mlo wa siku moja
Kabla ya kuhama kama mbayuwayu wakati wa kiangazi

Baada ya kupingwa kutunyang'anya mwishoni mwa msimu
Wameshika rungu nzito ya kupiga dafirau bajeti ya taifa,
Kwa ubinafsi usiojali walio kwenye minyororo ya ukame
Wamejitwalia marupurupu laanifu eti ya kulipia usafiri
Kama kwamba dawamu wanasafiri hadi ukingo wa bara

Jukumu waliloomba kwa kupiga magoti na kutoa ahadi
Tukawapa tukidhania watatusafirisha kutoka bonde la huzuni
Wanalitimiza kwa kujikokota kama konokono au yungiyungi
Wamegeuza ukumbi wa taifa nembo ya uzembe na aibu

Vikao vya majadiliano vinavunjwa kwa kukosa idadi murwa
Wanaoitwa kwa jina lenye marashi na kulipwa kwa dhahabu
Hawaji ukumbini wakafika thelathini kutimiza kanuni
Wakija huja wamevaa machovu kama magwada ya chuma
Mambo huwapita usingizini wakidondokwa na udenda

Viongozi wa kamati za kupiga miswada daruni
Wanayumba hawana nguvu za kubeba jukumu adhimu
Hawakupata nyadhifa baada ya kupimwa kwenye ratili
Uchaguzi ulikuwa kazi shaghala-baghala ya waliosinzia

Muda wa swali adimu kwenye ratiba uwadiapo
Muulizaji hayumo miongoni mwa wachache ukumbini
Ameketi hoteli akipumbaza vizuu wake kwa vinywaji
Akipanga njama ya kunyakua taji la mkuu wa kabila

Swali la pili limeulizwa limechangamsha akili kwa ubora
Bali kiu cha kusikiza jawabu hakitakatika hadi juma lijalo
Waziri hayumo anacheza gofu na majambazi wa kigeni
Badala ya naibu wake kuwapo kujaza pengo la wizara
Yumo kitandani amelemazwa na manofu ya nyama ya jana

Karaha ya upungufu kwenye ukumbi wa *waheshimiwa*!
Inapoendelea kughasi hisia siku zisizofika mwisho
Wachache wanaopiga miayo kwa ulemavu wa machovu
Wanakata kauli  ya kuzunguza ufunguo wa sefu ya taifa
Mabilioni yanatolewa kwa matumizi bila kumulikwa kwa kurunzi

Vitabu vya historia vitakapomlika  msimu wa tisa
Vitatesa pua kwa harufu kali kama uzushi wa kicheche-
Mnuko wa wasaliti waliovishwa magwada ya heshima
Na kulishwa mayai, maziwa, asali na nyama ya nundu
Kwa miaka mitano ya usaliti unaonguruma kama radi

Msimu Mwingine wa Wasaliti (uk. 12)
Vitimbakwira watarudi karibuni kutoka karamu haramu
Utaziona barakoa za tabasamu kwenye nyuso zao
Watakuja kutugawia peremende zenye sumu ya akili
Watalewesha watu kwa pombe kutoka vibuyu vya maneno
Wataahidi kesho yenye mapipa ya maziwa na mitungi ya asali
Nasi, tukiongozwa na ramani ya tumbo na dira ya ubinafsi
Tutapanga milolongo katikam mvua na matope ya Disemba
Kukaribisha, labda, msimu mwingine wa wasaliti

**Mkasa (uk. 13)**

Kama kawaida,ndege wanaimba kwa uchangamfu
Asubuhi  inachanua ,mali inapamba ang ana ardhi
Wanakijiji wnamiminika kutafuta riziki halali
Pilikapilika zinahinikizwa ndani na nje ya mijengo
Mdundo wa maisha unaendelea kwa kasi ya dawamu

Kwa makeke ,gari  la manjano likibeba janga
Linazuiliwa na kizuizi cha mlingoti wa chuma
Linanyimwa uhuru wa kuingia chini ya jengo
Na kufikia majengo ya ubalozi wa nchi tajika

Abiria aliyepagawa na pepo za chuki ya miongo
Anapiga shoti kama mwenye kichaa kilichokolea
Baada ya kugundua ameacha bunduki garini
Awashtua walinzi kwa mipasuko ya gruneti

Garini ,mkono wa dereva unabonyeza kiteguzi
Mlipuko wa kwanza unaashiria  mwanzo wa mkasa
Wa pili unajaza anga vumbi,moshi na takataka

Vigae vya vyoo, vichane vya mbao na matambara
Vinatawanyika na kutangaza siku geni nchini
Hewa imejaa harufu ya mayai yaliyooza
Ushahidi thabiti wa janga la bomu jijini

Jengo karibu  na ubalozi wa mwewe
Linashindwa kuhimili hasira kali ya baruti
Linakata tamaa na kugeuka fusi la takataka

Barabarani, akili za madereva na wenda-miguu
Ghafla zimekumbwa na tufani isiyo kifani
Baadhi, bila kujua waendako,wakitetea uhai
Wnatimua mbio zinazochatika juhudi
Mbele,wnakutana ana kwa ana na moshi na moto
Wengine, baada ya kugundua magari hayafui dafu
Wanaacha mitokaa barabarani na kujitetea kwa miguu

Barabarani ,karibu  na ubalozi ,basi lenye abiria
Linapigwa na wimbi kutoka kiini cha mlipuko
Linatafunwa na moto na kubakia ghalili jeusi
Baadhi ya waliokuwa abria hivi punde
Sasa ni vipande vya miili kandokando mwa mijengo

Mikoba,vibeti,viatu na damu mbichi kila mahali
Ndio sura mpya ya jiji lilioamka katika mani
Likaishia kuwa mwathiriwa bila hatia
Katika vita baina  ya hilali na mwewe

Taa za rangirangi za magari ya kubeba mahututi
Zinamwesmwesa katika kasi ya kutetea uhai
Ving’ora vy ``Nipisheni njia!Hii ni dharura!”
Vinachanachana anga katika juhudi adhimu

Machela  zikibeba majeruhi bila fahamu
Zinakimbizana na kupitana kwa kasi hospitalini
Kujaribu  kuzuia mauti zikizama kama kibatari cha uhai

Kwa siku kadha zilizofunikwa na ukungu wa huzuni
Madaktari,wnafunzi,wauguzi na wananchi
Wanajikakamua majeruhi wasiteremke kaburini

Baadhi ya walionng’ang’ana wakajifikisha hospitalini
Damu ikiwatiririka kama maji kutoka chemichemi
Wanateleza na kuanguka katika mikono y amauti
Bado wakisubiri daktarin wanaijitahidi kwingine
Katika vitanda vinavyomtia mtazamaji ganzi
Dondoko katika mipira inayoungana na chupa

Zinapitia kwenye sindano zilizozama mikononi
Kupambana na ukame katika mishipa ya damu
Bendeji zenye mabaka yalioloa wekundu
Zimefunika makuo kwenye nyuso zilizopandwa
Na kubana miguuna mikono iliyovunjika

Sakafuni,maiti zilizofunikwa kwa mablanketi
Zimepangwa kwa safu kwa heshima ya huzuni
Zikikumbusha kwamba Maisha ni kabatari
Kinawaka uwanjani anga likuwa tulivu
Bali kuzimwa na upepo mwovu si kazi

Katika jengo la kuhifadhia waliohama dunia
Jamaa wenye matumaini yanayoyumbayumba
Wamesongamana katika joto kali la wasiwasi
Wakitafuta vipenzi kwa macho yenye ukungu

Wenye nyoyo zisizomudu kumbo la uhalisia
Wanapokabiliana ana kwa ana ukweli na ukweli katili
Ambao umewatenga milele na jamaa wapendwa
Wanaanguka mwanguko wa mwisho maishani

Kwenye mabamba ndani ya tumbo za majokofu
Maiti zinasubiri kutambuliwa na kusafirishwa vijijini
Au kupewa kwaheri katika makaburi ya umma jijini

Sakafuni,mifuko mieusi ya plasitiki
Inatenga ulimwengu wa nje na maiti zilizomo ndani
Kuzuia macho na nyoyo kukutana na mateso
Katika galili refu lililokuwa jengo la fahari
Picha za harakati zilizokidhia wafanyikazi haja
Zimehifadhiwa katika sanamu za maiti baridi:
Vidole nadhifu kwenye herufi za kompyuta
Kiganja kikishikilia kalamu juu ya karatasi
Mikono kwenye simu juu ya meza

Chini ya jengo lililoporomoka la chama cha ushirika
Chini yam awe, vigae vya vioo na takataka
Maiti arobaini za wasichana vipenzi vya taifa
Wananchi waliokuwa wakipanda mbegu za riziki
Ni ushaidi wa kina kirefu cha janga bila kifani

Kwenye ua wa ubalozi wa bender ana nyota ya milia
Kwa kiburi, bunduki za wanamaji kutoka mbali
Zinaelekeza mitutu kwa waokoaji wenyeji
Ikitishia, kijeuri, kutema moto w amauti
Waokoaji wakithubutu kuingiza vifaa ndani

Kwenye eneo la milipuko iliyotingisha nchi
Kwa siku kadhaa zilizoloa machozi na majonzi
Bila kujali usingizi, machovu, kiu na njaa

Taifa likiunganishwa na saruji ya uzalendo
Kwa ushirikiano na mikono ya kutoka mbali
Linapambana na ukaidi wa mawe, chum ana vioo
Kuokoa wanaoning'inia kwenye lango la kaburi

Kila mwathiriwa anapofikwa kabla ya uhai kuzima
Hisia za waokoaji zinaungana katika fataki ya furaha,
Kila majeruhi anapovuta pumzi kwa mara ya mwisho
Na kuutoroka mkono wan usura unaochakura karibu
Nyuso nan yoyo zinapiga mbizi kwenye majonzi

Baada ya siku tano za juhudi zilizometameta
Ambamo dini, kabila, taifa na rangi ziliyeyuka
Kukabakia jumuiya moja ya binadamu wema
Moto wa matumaini dhidi y amauti ulizimika
Na kuacha kumbukumbu za ujasiri mwangavu

Miaka kadha baada ya Agosti ya mito ya damu
Majeraha kwenye nyuso, shingo na mikono
Yameponywa na wataalam yamebakia makovu
Bali katika fahamu za waliotembelewa na jahanamu
Bado damu inatiririka kutoka majeraha yasiyopona
Hasa vijiti vinapotumbukizwa kwenye kumbukumbu
Maisha ya waliotumbukia jahanamu na kurudi
Yamebaki na nyufa kama kuta baada ya mtetemeko
Kwenye uwanja bila saruji, kkokoto wala mchanga
Wa kujikarabati yakini kiuchumi na kijamii

Waliohimili maisha yao na ya jamaa kwa heshima
Sasa wanatapatapa katika dimbwi la aibu ya haja
Ndoto walizofinyanga kwa udongo-kinamo mzuri
Sasa ni vigae vya kaure iliyoangukiwa na jabali

Katika familia zilizopokonywa mkono wa riziki
Mwangaza wa maisha ya jana umemezwa na ukungu
Watoto waliokuwa wakisafiria barabara ya lami
Sasa wamekwama kwenye mchanga didimizi wa ulitima
Wale walioota ndoto angavu za kupaa katika anga la ufanisi
Hawaoni mbali yanachekelewa na wingu zito la uyatima

Urafiki wetu na wenye maadui wasioogopa kufa bora waue
Umetugeuza nyasi ya kijani katika uwanja wa vita vya fahali

## Kitini (uk. 18)

Tulipoguna kwa maumivu makali kwenye misuli
Juhudi za kizalendo zilizopamba moto yakini
Tulipotokwa kwa michirizi ya jasho tukisaka utu
Tulipopambana na dhiki ya giza ya miongo miwili
Waziri aliridhika, alitushauri kwa ulimi wa kinaya

Juhudi zenu zenye nia ya kung'oa chama
Ni sawa na ubwege wa kutaka kukata mtini
Kwa wembe ulionyolea ten ana tena!

Alipotanabahi kwa chombo chake kilikuwa taabani
Ukweli wa siasa mbaya ya kutumia na kutupa jaani
Ulipommulika machoni kwa mwangaza wa ufahamu
Alijibambua ngozi kuukuu kama nyoka mjanja
Akaingia uwanjani kwa mwili uliometameta
Akipiga pembe adimu ya mkombozi wa umma

Baada ya umma uliochoshwa na kiu cha haki
Kumiminika shambani wakiimba kwa umoja
Na kung'oa mikalatusi iliyonyima umma maji
Waliotukejeli kwa tashbihi za mtini na mwembe
Sasa, wameketi kwenye kiti cha bembea cha taifa
Wakila matunda ya mti uliopandwa na waliosahaulika

### Wenda wazimu Kongo (uk. 19)

I

Shambulio la genge la wahuni wa jeshi la taifa
Mbio za kufa na kupona hadi mafichoni kichakani
Maombi ya kutetemeshwa na baridi ya wasiwasi
Mawazo milioni katika akili inayofahamu Mikasa

Kichakani, mafichoni, bahati nasibu inampuuza:
Bila kujali kite na nduru kama kimya cha usiku
Bila kujali uja-uzito wake wa miezi tisa
Genge la wahuni wenye nembo ya usalama
Kwa zamu ya chuki na dhuluma bila kifani
Linashambulia, sio kwa ngumi au makofi
Bali kwa gruneti mwilini na mabomu akilini

Kwenye sehemu zinazowaka makaa ya uchungu
Inafuata dhiki kali ya vijiti na mitutu ya bunduki
Matundu yanayotiririka damu kwa fujo
Yanaunganisha njia jirani za mwili

Mtetemeko wa dhuluma katika mji wa uzazi
Kujinyonga mwili kutokana na uchungu
Kunazima uhai wa kiumbe ndani ya kiumbe

II

Sasa, baada ya miezi ya kumbukumbu za dhiki
Tumboni, kimbunga cha uchungu kisichokoma
Kinavuma kwa ghadhabu isiyo mfanowe
Na visu elfu vyenye bapa ndefu na kali
Vinamkatakata ndabi kwa fujo bila kikomo
Kwenye nyayo zenye milia ya unyevunyevu

Mwashomwasho wa kemikali kutoka kibofu
Unamwadhibu mdhulumiwa kwa pilipili hoho

Janga lililomkumba lilivunja kufuli za mwili
Panda ya miguu ni kinamasi cha damu na usaha
Ni mtambo wa harufu nzito kama kiwanda cha Ngozi
Pua za jamaa zake na wenza vilishindwa kustahimili
Ametengwa kama mwenye ndwele ya kuambukiza
Upweke unamzungusha kwenye kizingia cha aibu

III

Hiki ni kisa nadra kama mbwa mwenye pembe
Hii ni kawaida ya wenda-wazimu Kongo

Vijijini, vinywa vya wanaoishi katika jahanamu
Vinahadithia visa vichafu kama usaha wa kidonda
Hivi, vimejaza anga harufu yenye mpigo wa nyundo:
Yule alidhulumiwa kwa zamu na wanaume bila idadi
Kisha akaingizwa vijiti kwenye njia ya maumbile
Na kutobolewa matundu mnamowaka moto daima

Sasa siri ndogo na kubwa za mwili
Zinakutana ndani kwa ndani na kupigana mieleka

Lile ni kaburi la aliyeangushwa uani na wanajeshi:
Baada ya masaa milioni ya mwako wa dhiki gizani
Roho ilikata tamaa na kufunga safari ya kuzimu

Huyu ni ndugu wa kiume wa marehemi
Kwa miezi sita ameishi katika pipa la pilipili:
Baada ya dadake kufariki katika bwawa la aksidi

Wimbi la wendawazimu wa majambazi lilimkumba
Akaambiwa "Dadako amekwenda na kutuacha na kiu
Chukua mzigo, mbebee, hadi mwisho wa safari!"

IV

Wanaotenda yanayochoma moyo kwa visu milioni
Bado wamo nchini, huru kama mbayuwayu angani
Mbali na vizimba vya mashtaka ya jinai dhidi ya binadamu
Mbali na vifungo vya kuwakwangua wenda-wazimu
Mafunzo kwa wenye akili zilizooza na kukosa sura

## Mlima wa Dhahabu (uk. 23)

Ahadi za makasha ya fedha kutoka ng'ambo
Hazina nzuri ya kuhifadhi kupe mamlakani
Zinawasha moto katika akili ya vitimbakwira
Wakaondoa kanuni za chum ana sigenge
Zinazolinda lango la mbele la Benki Kuu

Mjanja alibeba makasha ya hazina ya umma
Bila ahadi zake zilizopakwa asali ndani nan je
Kuleta dola, euro, franga, yen na kroner
Kuziba pengo hatari katika Benki Kuu

Thamani ya shilingi ilianguka shimoni kwa mgoto
Gharama za Maisha zikapanda hadi vilele vya miti
Kupata chakula, mavazi, karo, dawa na nauli
Kukawa ni kupanda kilima cha mwinuko mkali

Bei za petrol, diseli, Mafuta ya ta ana gesi
Zilipanda angani na kuungana na mawingu
Katika nyumba zilizozoea tabasamu adimu
Mioto ya hasira baina ya wake na waume
Ikawa na kuunguza uelewano na amani

Nguvu za kuzalisha mali zilipeperushwa na upepo
Ndoto za fahari zikaporomoka kama kuta zilizotota
Katika viwanda na biashara za huduma
Faida ilipunguka ja maji ya mtungi uliotoboka
Punde, kufuli zikavamia milango ya makampuni
Biashara zikaanguka na kuchanganyika na vumbi
Kama majani kiangazi kinapoingia kwa kishindo

Moto katili wa ukosefu wa karo na sare
Uliunguza maisha ya kesho ya Watoto
Haja ya kukidhi mahitaji ya maisha
Ikawavuta baadhi kutoka mienendo safi
Ikawatupa katika mitaro ya tabia chafu

Tulishindwa kujipamba kutoka maduka
Kuvaa mitumba kukawa mtindo kuu wa taifa
Nchi ikageuka kapu la kutupa mavazi makuukuu
Tukawa warithi wa jasho la nchi nyingine

Lundo kubwa la waliokosa kazi na riziki
Liligeuka ardhi ya rutuba kukamea majambazi
Utekaji nyara  wa magari kwenye barabara miji
Na uvamizi wa magenge y amauti nyumbani
Yakawa mawimbi katika bahari ya majonzi

Jitihada za kukinga maisha na kulinda mali
Katikati ya ngurumo za dhiki ya umaskini
Ziligeuza maskani nyerezi katika mitaa mizuri
Zikawa ngome imara zenye milango ya chuma

Katika vituo vya afya na hospitali za umma
Ulitima uliyeyusha chupa na pakiti za dawa
Na kuacha rafu zikipiga miayo kwa miezi na miaka
Waliokuja kujitetea dhidi ya mwito wa kaburi
Walirejea nyumbani katika majeneza yam bao rahisi

Kimbunga cha malalamiko na migomo ya wafanyakazi
Kilitifua wingu la vumbi katika biashara na huduma
Na kujaza anga ukungu mwekundu kama machweo
Uchumi ukawa kwenye ukingo wa giza la usiku

Umaa ukiteseka katika pipa la aksidi ya umaskini
Majambazi waliojifanya wanabiashra wa bidhaa za nje
Na wenzao waliendesha magari yenye bendera
Waliishi kama Sultani wa Bunei au Billy na Melinda
Bilioni walizozoazoa kutoka mlima wa dhahabu
Zikilipia anasa iliyozungukwa na tufani ya ulitima

Tunaambiwa siku ya kunywa mabakuli ya nyongo
Imewadia kwa waliotufikisha kwenye bonde la giza
Lakini utawala unaotapatapa katika tope la mizozo
Utathubutu kutumbukiza simba marara vizimbani
Au utawaacha waendelee kutubeua wakiteuka?

Bilioni haramu katika mabenki ng'ambo ya bahari
Zitarejeshwa kwa walioziunda kwa jasho adimu
Au utawala wenye sura inayochanganya leo na jana
Utangojea tusinzie na kudidimia katika usingizi
Baada ya kuua uwezo wa akili na neva zetu
Kwa kutudunga sindano ya tume ya rais?

## Darfur (uk. 26)

Kutemewa mate kwa kuwa na ngozi nyeusi
Na kuwekewa vikwazo wasifikie sinia ya taifa,
Kunyimwa kauli kuhusu usukani wan chi
Na kupagazwa uzito wa maonevu na dhuluma
Kuliwasha nyoyo moto uliowaka bila kuzima
Wa kudai haki, heshima  na shibe

Waliofungiwa njia kwa magogo na mawe
Waliodhalilishwa kwa sera na kanuni za chuki
Waliamua uchungu uliokithiri ni shida isiyovumilika
Wakapaza sauti kudai utu na hadhi iliyokamilika

Majirani wenye viremba na bunduki mikononi
Walichemkwa na nyongo ya kiburi na chuki
Wakageuka jinamizi linalonguruma jangwani
Likisambaza mauti kwa miguu na kwa ngamia

Nyumba zilizowasitiri wazazi na wanao
Zinashambuliwa kwa moto na Janjaweed
Na kubakia magofu yanayotawaliwa na kimya
Mimea iliyopamba mashamba kwa fahari
Imenyongwa na kwekwe baada ya kuhama jembe
Akiba iliyowekwa maghalani kama ngao dhidi ya njaa
Imetafunwa na mwako sasa ni jivu na masizi

Vijijini, wanawake na wasichana wa rangi ya mpingo
Wanalipuliwa kwa makombora dhalilishi ya ubakaji
Huku jamaa zao wa kiume, bila silaha za kisasa
Wakisakwa n amauti yakibebwa na ngamia
Na kumiminiwa risasi zenye nembo ya serikali
Kwa nini waliojitwika jukumu la polisi wa dunia
Wamesimama kimya wakiangalia upande wa pili
Maisha ya watu milioni mbili yakiungua katika mwako?

Wanaochinjwa na kubakwa vijijini Darfur
Wasingekuwa na ngozi nyeusi kama mpingo
Wenye misuli ya kutishatisha wakazi wa ulimwengu
Wangefumba macho kwa muda waliyoyafumba
Au wamgepiga shoti kukomesha tufani ya maonevu
Kama walivyofanya kibunga kilipovuma katika Balkani?

### Mkataba Tena (uk. 28)

Kalamu zimesimama kwenye karatasi
Kuupa uhai mkataba mpya wa machozi:
Majeshi kutoka milki ya ng'ambo ya bahari
Yamepata kibali kutoka kwa manahodha wan chi
Kuchafua ardhi kwa baruti, risasi na mabomu
Na kukanyagia matopeni haki za wananchi

Jana, vifaa vya mauti vilivyobakia malishoni
Vililipua miguu na ndoto azizi za wafugaji
Na kuwaangusha waliojichumia kwa heshima
Katika mtaro mchafu wa aibu ya kutojiweza

Jana, waliokuja hawakuwa askari wa mazoezi
Walikuwa magenge ya wahuni na wabakaji-
Kwa vitisho vya jambia na mitutu ya bunduki
Au kwa kutenga wanawake kwa vyambo wavuvi
Walitwangwatwangwa mbugani au malishoni
Na kuwaacha na mashavu yaliyoloa machozi
Na akilini chenye vidonda vichungu visivyopona

Leo, kalamu zimeinama kwenye karatasi tena
Kama kwamba vitendo vya magenge ya jana
Vilikuwa harakati za kuimarisha saruji ya urafiki

Leo, wanawake na wasichana wa nyanda za mazoezi
Wataishi kwa utulivu bila ukungu mzito wa wasiwasi
Au jinamizi limerejea kuwafunika kwa wingu la dhiki?

Serikali itawalinda kwa sheria zisizoogopa Bulkinum
Au wanawake wanatarajiwa kujilinda wenyewe
Labda, kwa kuvaa sufi za chuma?

## Waharifu Huru (uk. 30)

Bila kutarajiwa, onyo za mashambulizi dhidi ya "wageni"
Zilipaa na kuchafua anga kama harufu ya amonia
Vilifuata vijinga vikilipuzwa na pumzi hatari za wanasiasa,
Taya za miako zilitafuna mbao, fenicha, nguo nav yeti
Maghala ya vyakula na matumaini ya kesho yenye shibe
Yalifutiliwa mbali na upepo wa wendawazimu wa kupangwa;
Kutoka mikononi mwa fukara walioleweshwa kwa chuki
Mishale ilipiga mbizi katika miili ya wakazi wa makabila mengine
Panga za ghadhabu zilishuka baina ya vichwa na viwiliwili
Vituo vya biashara vilivyonawirisha kwa maisha na heshima
Vilichomwa na kubakia magofu yenye mwangwi wa huzuni;
Mashamba yaliyohimili familia kwa mimea tele na mifugo
Yalivamiwa na kwekwe jeuri na kuminywa afya ya jana
Wajane na mayatima walibaki katika dukuduku la kukata tama;
Chemchemi za karo ya Watoto zilikauka na kubakia na makuo tasa

Vijana wa kike walifuata njia ya mchanga didimizi wa ukahaba
Wa kiume walikwama kwenye bonde la madawa ya kulevya
Na kisha kutumbukia katika dimbwi la wizi na unyang'anyi;
Bali katika wingu la unafiki wa "amani, upendo na umoja:
Badala ya wahandisi wa jakamoyo kutetemeka mahakamani
Badala ya wenye damu viganjani kutupwa korokoroni
Wanaendesha mashagingi yenye bendera za mamlaka
Wanalipwa mishahara minono wakiitwa "viongozi wa taifa"!

## Tume za Rais (uk. 31)

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tumnunulie kila mwanatume Hummer
Ichunguze kama njaa inaweza kuua
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Ihariri taarifa ya tume ya rais

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tumjengee kila mwanatume kasri
Ichunguze jina la rais wa Jamhuri
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Imtangazie Rais jina la Rais

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tuitengee nusu ya akiba ya Banki Kuu
Ichunguze kama rais ni rais bila tume za rais
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Imshauri rais kuhusu rais na tume za rais

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tuilipe kwa mkopo kutoka vitanzi vya Breton Woods
Baada ya miaka mitano ya kumandari na kunywa mvinyo

Wamshauri rais namna ya kuficha taarifa za tume za rais
Katika sefu za vyumba vya ndani vya mijengo ya rais

### Magenge Matatu (uk. 32)

Genge la kwanza la mazimwi
Lilituahidi nchi bila minyororo ya kutojua, maradhi na umaskini
Tukanenguka nenguka viwanjani kwa shangwe na vigelegele;
Mwongo na nusu wa upepo wa ulafi na ukungu wa ufisadi
Ukazima mwenge wa utaifa na kuangusha uzalendo mtaroni
Harufu ya ukabila ikachafua nchi kama uzushi wa kicheche

Genge la pili la mazimwi
Lilituahidi majira maangavu ya Amani, upendo na umoja
Tukajijeruhi koo kwa kuimba "Juu! Juu! Juu sana!"
Baada ya miongo miwili viwavi na nzige wakitafuna nchi
Jamhuri ilishuka katika jahanamu ya moto wa AK47
Zao la umaskini unaovuma kama bahari kwenye miamba

Genge la tatu, nusu-mazimwi
Lilituahidi katiba mpya na dawa kali dhidi ya ufisadi
Tukaamini wimbo "Yote yawezekana bila Mfalme wa Nzige"
Baada ya miaka minne ya hila, tamaa na uzingizi ulingoni
Ahadi iliyomwesamwesa kama nyota ya taifa jipya
Imemezwa na wingu la ujanja na harufu ya ufisadi

### Johari Angani (uk. 34)

Majira yaliyoyapa macho kisogo
Na kuyoyomea katika ukungu wa wakati
Nilipotembelewa na ndoto ya kusafiri
Ili kuvuka maziwa, milima na bahari
Niliruka kwa vyombo vya ng'ambo
Nikiviona kuwa havishindiki angani
Kwa mizani ya usalama na huduma,
Kumbe mabawa yenye nembo ya taifa
Ni Johari iliyomeremeta kwa fahari

Leo nimo ndani ya mabawa tofauti
Yenye rangi pendezi za nyumbani:
Kila mboni zinapomandari
Panatumbuiza macho kama lulu,
Matangazo ya kanuni adimu
Yanatiririka kwa sauti laini,
Mwendo wa kasi kwenye lami
Mbinu ya kujiandaa kuaga ardhi
Na Ushahidi wa mikono mahiri,
Nao mwinuko wa kujiunga na anga
Umejaa rangi pendezi za ujuzi

Juu, juu ya zulia la mawingu
Kinyume na karaha za siasa
Tofauti na aibu kali ya wabunge,
Juhudi na heshima za wahudumu
Zinang'aa kama almasi za kuteua-
Wanahudumu kwa uzoefu mwangavu-
Ujuzi katika kuzima njaa ya abiria
Unashangiliwa na tete za ndimi
Na kusifiwa na mio na tumbo,
Navyo vinywaji vikali au laini
Haviji kupitia bilula bahili
Vinatiririka bila kinyongo

Leo, kila abiria na kiwambo chake
Akitaka filamu au ramani ya safari
Mwamuzi si mhudumu mteuzi
Ni moyo wa msafiri kupenda

Anayesikia sauti ya maumbile
Na kuinuka kwenda kuitika mwito
Anakaribishwa na faragha nadhifu
Pua na macho hupenda mandhari

Baada ya kuaga bonde la Heroe
Kuruka juu ya milima ya Nuba
Na kuvuka uchi wa Sahara,
Baada ya kupita magofu ya Carthigie
Na kutazama Buluu ya Mediteraneani
Baada ya kupita nchi ya Da Vinci
Na kutafakari Niaccolo Machiavelli,
Baada ya nyoyo za wapenda maumbile
Kuimba pamoja na theluji ya Alps,
Baada ya mifereji na vinu vya upepo
Kukaribisha katika nchi ya Van Gogue,
Sasa ni wakati wa "Kwa heri, Anga!"

Mshuko wa mwororo bila mishtuko
Na kubana mwendo kwenye lami
Ni kazi bila chembe za dosari
Ni mifano ya kuigwa na marubani

Mabawa yanapotua uwanjani
Na abiria watulivu kushuka,
Nyoyo zao zinabakia angani
Zikipiga makofi kwa kuridhika.

### Mnara Mwangavu (uk. 36)

Badala ya koja la mwaridi
Heko kwa wakili mahakamani,

Badala ya akaunti ya fahari
Katika benki ya watajika,
Badala yar aha ya mvinyo
Na mabusu yenye marashi,
Baada ya kuitwa na jukumu
Uliitikia mwiti mwangavu
Wa kujiunga na ndoto ya utu,
Ulifuata miali ya thamani
Ya mwangaza wa heshima,
Uliimba wimbo wa usawa
Katika ukungu wa ubaguzi

Baada ya wavu wa makaburu
Kukunasa katika mapambano,
Baada ya mahakama ya Rivonia
Kuandaa ujanja wa kisheria,
Mshale wa dira ya maisha
Ulilenga upande mpya:
Misuli ya mikono ya wakili
Ingepigana vita na majabali,
Na macho yako ya msomi
Yangepambana na vumbi
Katika dhiki ya korokoroni

Ndani ya ngome katili kisiwani
Moyo wako pendezi kama taa
Ulikataa katakata kukata tama
Kusagwasagwa na jiwe la mateso,
Kwa Mafuta adimu ya matumaini
Ulikinga akili na mwili dhidi yak utu
Unyevunyevu wa baridi ya upweke
Ukashindwa kutafuna chuma ngumu
Iliyozunguka ndoto yako ya ushindi

Damu change ya Soweto
Ilipowaka moto wa uzalendo
Na mwako kumulika anga
Na wenye vifua vyenye nyoyo
Kujiunga na vita dhidi ya giza
Lango la jela kuu Pretoria
Lilikupa uhuru usiozoeleka
Wa kujiunga na miali ya jua

Ulirudi kutoka tanuri la dhuluma
Ndoto yako ya maisha yenye utu
Maisha yaliyojengeka vyema
Kwa chum ana mawe ya haki
Ikiwa bado imara moyoni,
Ewe nyota iliyokataa kuzima!
Ulipokelewa kwa nderemo
Na kuvishwa ushanga adimu

Wa shanga za matumaini,
Ulipewa usukani mikononi
Kuendesha mashua ya taifa
Katika bahari mawimbi hatari
Na mikondo ya chini kwa chini

Tofauti na wasaliti wajanja
Katika ikulu kuu za Afrika
Ulikataa kumimina kwenye umio
Makopo ya kileo hatari cha mamlaka
Badala yake dawa ya kutuliza akili
Ukaongoza bila sumu ya ubaguzi
Wala nyongo ya kulipiza kisasi,
Ulikataa kutupa bazuka za kisirani
Dhidi waliokukaanga katika tanuri,
Ulicheza mahadhi matamu
Kwenye marimba ya uadilifu,
Ulialika rangi zilizozozana
Kuja pamoja kwa ukunjufu
Kuunda nchi inayopendeza
Kama upinde- mvua asubuhi

Kwa dawa ya matamshi na vitendo
Ilizuia virusi vya *ebola* vya kisiasa
Kuvamia mwili wa taifa change

Katiak bara la giza la ikulu
Kwa miaka mitano miangavu
Kwa viganja bila hatia ya ujanja
Ulisuka utaifa kama wavu adimu
Ukachangamsha nyoyo za marafiki
Na kufunga vinywa vya maadui
Vilivyosubiri ndimi tayari
Kushusha hadharani:
        Mwafrika hawezi!

Baada ya kufikisha mashua ya taifa
Kwenye bandari ya miaka mitano
Kinyume na majambazi wa ikulu
Badala ya kuwa shujaa wa ujanja
Na kugandama kwenye usukani
Uliinuka kitini kwa unyenyekevu
Kutoa nafasi kwa nahodha mpya

Hongera, nyota angavu ya Afrika
Wengine watakapotaja Rosevelt
Au kujigamba na Chrchill
Afrika itasimama uwanjani
Na kwa sauti imara kama kengele
Kusema:
        Mnara wetu wa almasi ya utu

Ni mwangavu kuliko mwingine
Katika fuo za historia

### Mafuta yenye Damu (uk. 48)

Wasio na macho ya kuona ukunguni
Wanaona Mafuta safi ya bei nafuu
Wanaona bidhaa nzuri ya Khartoum

Naona majeruhi, dam una maiti
Maiti za wakulima mashambani
Maiti za wachungaji malishoni
Maiti za Watoto shuleni
Maiti za vikongwe vijijini

Naona titimko la wakazi wa Kusini
Wakimiminika Kenya na Ethiopia
Wakikwepa dhamira imara za risasi
Wakitoroka mauti kutoka Antonov
Huku vifaa vya kuchimba Mafuta
Vikivamia maganjo yanayonuka damu

Usiniuzie petrol ya Kusini mwa Sudan
Sitaendesha gari kwa damu ya watu,
Picha za maiti za Watoto wachanga
Zitanitumbukiz ahospitali ya Mathare

### Ni Kweli? (uk. 55)

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba tunapokuwa nna Watoto
Daima tumulike jamaa zetu wa kiume
Kwa kurunzi kali ya uangalifu?

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba wapo wazazi wanatuma Watoto
Kwenda kutega mitego ya virinda hoteli
Kusudi kuleta change nan guru nyumbani
Kupigana na kikosi kikali cha njaa?

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba baadhi ya wakembe wa kike
Hutiririkwa na machozi na damu
Baada ya wazazi wao halisi wa kiume
Kuwasagasaga kama nyama ya sambusa?

Ni kweli upepo wa nchini unavyosema:
Kwamba leo katika baadhi ya nyumba
Wake wanapokuwa katika shughuli za nje

Nyadhifa zao kuu za usiku wa manane
Hutekelezwa kikamilifu na mabinti?

## Mdundo wa Dhiki (uk. 56)

Njoo! Pamoja tusikize mdundo wa dhiki
Unaovuma bila kuamsha wanaolala fofofo
Wakiota ndoto za nyongeza ya mishahara
Kuendeleza vitambi vyao vya ujenzi wa taifa:
Vumbi jeuri la migodi na machimbo
Likichochewa na ndoto za utajiri
Linavamia mapafu laini na dhaifu
Na kulowea ndani bila nia ya kuhama
Baridi yenye hasira nzito kama ukungu
Rafiki wa mashamba ya majani-chai
Inapiga mbizi hadi uboho na wengu
Inatesa wakembe kama amiba katika ini,
Kemikali za kupigana na maadui watukutu
Wenye kisirani na maua na kahawa
Zimejenga makazi katika dam una figo
Taratibu zinapanga mazishi ya baadaye,
Mate makali ya kinywa cha bahari
Wakazi wa fuo za kuzoa chumvi na utajiri
Yanabambuabambua ngozi change bila kinga
Na kuacha mikono na miguu ikinung'unika,
Sakafu za nyumba za waungwana mijini
Zikishirikiana na malundo machafu ya nguo
Zinaadhibu mifupa ya nyonga na migongo
Asubuhi ya Maisha tayari ina gizagiza la jioni,
Tanzu zenye ahadi danganyifu kama mazigazi
Katika hizi nyanda za sifa za mairungi
Ni nyavu zinazoshika ndoto njianai ya shule
Na kuzitupa katika pipa la kutupa takataka

## Mkimbizi (uk. 57)

Masikio ya kumbukumbu bado yanasikia
Yanasikia miluzi na hasira za risasi hewani
Zikisaka roho za watu bila hatia wala silaha,
Yanasikia vilio vya Watoto wachanga
Vikiraruararua anga kama nyembendogo,
Yanasikia miguno ya mifupo ya vikongwe
Katika juhudi za mwendo wa kobe usiku

Mboni za kumbukumbu bado zinaona
Zinaona waja-wazito wakijizatiti mbioni
Wakijisukuma na kusukuma wanaosubiriwa,
Zinaona miili inayobubujikwa na damu
Ikijikokota kutafuta kivuli cha usalama,

Zinaona viwiliwili vya jamaa na marafiki
Vikiliwa na mafunza kandokando mwa njia!

Nilikuwa na bahati kama mtende
Mbio za usiku wa kelele gizani
Zilinitema kutoka kinywa cha mauti
Kama mbarika kutoka ganda la mboni
Sasa, katika mandhari, mikono mitupu
Jina langu limefunikwa na ukungu
Nimebakia na bandiko: mkimbizi

Maswali yenye mwangwi wa wasiwasi
Yaniandama yakinigongagonga
Yakinitesa kama mbung'o wajeuri
Likisumbua mtamba wa ng'ombe malishoni:
Wazazi walivuka mpaka wa uhai n amauti
Au walimezwa na chatu wa maangamizi
Ndugu, marafiki na majirani wapendwa
Waliokolewa na blanketi jeusi la giza
Au wauaji waliwazima roho kwa panga?

Moyo unatamani sauti tamu za jamaa zangu
Una kiu ya kugusa tena kuta za jengo la sala
Ungependa kunusa harufu ya udongo wa sokoni
Una hamu ya kuona tena vinyago vya utotoni

Ukungu was haka umfunika njia ya maisha
Naona hatua moja ya pili ni siri haidhihiriki
Baridi kali ya upweke imejenga kiota moyoni
Imezalia humo makinda hawaachi kelele za kejeli
Sina mzungu ansukwasukwa na kizunguzungu
Ninahangaika nimo kwenye mlango wa bahari
Ambamo maji ya ndoto angavu za jana
Yanazozana na mkondo wa uhalisi katili.

### Macho Mekundu (uk. 59)

Hawatumbuizi na visa vya sungura
Wala kusikiza hadithi za kobe,
Hawachezi kibe na wenza nyumbani
Wala kukimbiza vimulimuli uani,
Macho yao, tofauti ya Watoto wengine
Hayachangilii rangi za upinde-wa-mvua
Wala kuvutiwa na wadudu warembo,
La! Yamezoea wekundu wa damu
Yana dhiki, ni mekundu kama hoho
Ni mateka, wamefungwa minyororo
Yamekamatwa na dawa za kulevya

Moyo wangu una uchungu mkali
Unateswa na miiba yah ii picha
Unalizwa na majonzi ya Watoto,
Ole wao! Kama Wanyama wa porini
Watoto wanaishi katika mbuga katili,
Kama nyani, kima na tumbili
Wanajihimili kwa kula matunda-mwitu
Mpaka watakaporejea vijijini walikozaliwa
Kunyang'anya wakazi chakula
Wakiwakata koo wazazi na majirani
Na kuwabaka ndugu na binamu wa kike
Thibitisho la ujasiri na utiifu imara
Kwa majemedari waliowateka nyara
Na kuwafanya mtambo w amauti

Ole wao; watumwa wa majambazi!
Wao ndio pondo za mikoko na miwati
Ndio hupima kina katika ziwa la vita,
Ndio punda na ngamia wa kubebea mizigo
Ndio ngao za kulinda vifua vya afande
Ndio wapishi na wakanguraji vyombo
Ndio wanyang'anyi wakazi ng'ombe na mbuzi
Mchuzi wa kuhimili wakala wa mauti mbugani,
Wa kike, dhidi ya hiari, dhidi ya heshima
Dhidi ya malalamiko ya miili isiyokomaa
Ndio majani mabichi ya kuzima moto
Katika damu ya majemedari wa shetani

**Msumbiji (uk. 71)**

Kutoka upeo wa nili ya bahari
Matanga ya vyombo kutoka mbali
Yanatangaza majilio yasoeleweka,
Wageni ambao hawakualikwa
Hawakutarajiwa, hawatakikani
Wanashuka kutoka tumbo la meli
Shingoni wakivalia ukrosto bandia
Alama ya taasubi, kiburi na dharau
Vasco da Gama na genge lake
Wameingia na ndege mbaya

Wingu zito la tamaa linatanda
Na tufani ya uporaji rasilmali
Inamiliki vilima na mabonde

Misafara ya sisimizi kutoka bara
Inatiririka kuelekea Bahari ya Hindi
Huku nyuma,nderi na kunguru
Wanasherehekea ndovu na vifaru

Katika mashamba ya dharau na bezo
Mijeledi motomoto migongoni mieusi
Inaamrisha kazi za sulubu na dhiki

Maisha ya kutemewa mate ya dharau
Miongo ya miiba mikali nyoyoni
Majira ya vibunga vichwani
Uamuzi wenye mashiko:
Dawa ya moto ni moto!

Upepo imara wa uzalendo
Unavuma na kuamsha waliolala
Simba wa uhuru na hadhi
Wananguruma na kutetemesha nchi
Kimuli cha moto usiozimika
Kinatupa ndimi mijini na vijijini
Bendera dhiki miongoni mwa uma
Inararuliwa vipande vidogovidogo
Vigelelgele vitamu na fataki pendezi
Zinapamba nyanda ardhi na anga
Matumaini ya jua jipya angavu
Yanachanua kama maua kitaluni

Badala ya rangi za urembo wa shani
Petali za maua ya amani na ujenzi
Zikiimbia macho nyimbo tamu,
Majira mapya ya ndimi za moto
Yanazuka yanazuka kutawala Maisha

Ngoma ya machozi na mauti:
Mbele uwanjani, RENAMO
Nyuma , chini kwa chini, CIA
Vijijini, macheo yanapowadia
Ndlakama anawasha moto mkali
Asubuhi ,ghadhabu ya FRELIMO
Inachemka kama Mafuta sufuriani
Na kusababisha vidonda vichungu

Dhiki inayofichwa udongoni
zao la techknolojia ya kishetani
Inazaa viwete milioni bila hatia –
Watoto bila miguu, bila mikono
Mashamba yakiguswa kwa jembe
Ardhi inalipuka na kutafuna uhai
Kwenye magofu ya miji ya jana
Buibui wanajenga mitego ya chakula
Vijijini,wanapend kupima mikasa
Wanashindwa kuhesabu maiti
Na wajane,mayatima na viwete
Mipakani,watu wakigura makwao
Waniga nyumbu wa Maasai Mara

Wakivuka Mara kuelekea Serengeti

Vijukuu wa Millan na Vorster
Wantungua Machel kutoka angani
Kuzima nyota nyingine ya Afrika

Mahdhi ya wimbo wa amani
Yanaanza kutumbuiza masikio
Milio ya bunduki na bazuka
Inakoma kutesa akili nan nyoyo
Umati wenye wasiwasi na hofu
Wanakabili mto wa uchaguzi
Na kuvuka bila kuanguka majini
Jua la demokrasia na kuvumiliana
Linachomoza kumulika msumbiji

Sasa magurudumu ya uchumi
Yanaenda kwa kasi ya fahari
Ingawa barabara ina mashimo
Yanayochimbwa kwa ujanja
Na trekta za zimwi kuu la dunia

**Ntharene (uk. 74)**

Ndoto angavu ya kujimudu maishani
Na juhudi za misukli imara ya wakulima
Zimeungwa mkono bilakuulizwa mawsali
Na udongp mwekundu na mawingu karimu
Na miali imara ya jua la Ekweta

Ntharene , nembo ya ukarimu wa mashamba:
Kandokando mwa barabara ya mizingozingo
Wnakijiji wenye urafiki shakiki na udongo
Wamepanga wanga,mapapai,tamata na ndizi
Na parachichi,viazi vikuu na viazi vitamu

Wanaorejeaa jijini kutoka masharikimwa mlima
Wafikapo kituoni,hupinda sukani kushoto
Na kushuka magarini wakipapasa mifuko,
Wanalakiwa na suati bembelezi za wanawake
Zinazovuta mteja kwa nguvu huku na kule
Katika kinyanganyiro cha kuchuma riziki

Leo ni sikuy maalum katika ramani ya juma
Malori kutoka mbali , tayari yamefika sokoni
Hili limepakia nusu na lile  thuluthi mbili
Wabebejio bado wanaingia na mazao mibichi
Mabegani wamesheheni mikungu ya fahari
Ikilindwa na majoho ya majani ya migomba
Ili ulimi wa jua usiilambelambe na kuitia dosari

Punde tumbo za malori zitashiba shehena
Yang'oe nanga katika safari yam ji mkuu
Kulisha wanaolima katika ofisi na viwanda
Kuudimisha urafiki baina mashamba na miji

**Janga Jangwani (uk. 75)**

Moyo wangu usiopenda sura ya damu
Unabubujikawa na machozi mekundu
Uonapo hii janga la moto jangwani

Bunduki zenye kiburi na kejeli
Zinaimba wimbo unaokirihi masikio,
Waliokuwa wenza wa kufa kufaana
Katika ngoma ya kumtimua adui sugu
Wanakaangana wenyewe kwa wenyewe
Katika Mafuta ya wenda-wazimu

Uhai wa askari wasiotaka vita
Unazimwa kutoka angani,
Maiti zinapakaa kichakani
Kama wadudu waliopigwa dawa,
Katika miji ya mipakani
Rafu zilizojaa bidhaa za biashara
Zimeporwa na kuachwa uchi,
Kabla mwako wenye hasira
Kutafuna rangi na mbao
Na kuguguna mawe na mabati

Zilizokuwa nyumba na malazi
Sasani magofu ya masizi na jivu,
Iliyokuwa akiba ya nafaka maghalani
Inatafunwa polepole na moto,
Mashamba ya kuhimili Maisha
Hayajalimwa yankaliwa na magugu

Enyi zalazambesaa na tesseney
Miji katika mikono ya mauti,
Maiti katika mikono y amauti,
Maiti za askari waliokonda kwa njaa
Na mizogo ya  Wanyama na magari
Imetapkaa ardhini yenye huzuni
Kama majani yaliyokuputika,
Malori na mabasi ya wakimbizi
Yanatifua vumbi barabarani,
Misafara ya wanaotoroka kifo
Inakwenda kwa msukumano

Kisu kikali cha kiu na machovu
Kinashambulia Watoto njiani
Na kufikisha safari yao kikomoni,
Mijeledi ya shida za ukimbizini
Inacharaza vikali akili na ndoto
Na kuacha majeraha machungu

Walioishi kwenye tumba la mapenzi
Wakitegemeana katika afya na ndwele
Wametengana na wandani wa thamani
Na kuacha nyoyo zikindondoka upwe

Ambao jana, walikula na kunywa
Na kulala bila kidumbwedumbwe
Sasa wametekwa nyara na wahaka,
Abadani hawajiwezi wanaomba nusura
Kutoka mashika ya huduma za huruma

Kila jua lingiapo angani na kuondoka
Kila maskini baina ya fukara wawili
Kama kizuu au punguani asiyejitambua
Hutupa hazina adimu katika moto wa vita
Akinunua ZU 23 kutoka jalala
Na mizinga iliyootea kutu Mashariki
Na vifa vya mawasiliano ya maafa
Kusudi kushinda rafiki wa jana
Na kuhifadhi ukanda wa jangwa

Huku nguo zao zimeloa jasho na damu
Waliovaa kiburi kama joho la chuma
Wanakubali kuketi na kutumia ndimi
Baada ya majira ya mito ya machozi
Jamaa wakililia wapenzi laki kaburini
Baada ya vidonda vya nyoyo na akili
Vinavyotesa wakazi katika kambi
Wakimbizi wanakoishi wakitazma vigae
Baada ya ndot kuangukia sakafu ya vita

**Ukarimu wa Ekweta (uk. 78)**

Asanteni jua,mvua,udongo na hewa
Ushirikiano wen una mkono wa mkulima
Umeifanya meza ya kiamsha-kinywa
Kuwa mwandani wa kutamanika
Katika urafiki wa kuaminika

Leo, muda mfupi baada ya macheo
Katika maili ya machweo ya Novemba
Kwa pamoja,parachichi,chungwa na papai
Yakishirikiana na karakara na ndizi
Zilinitumbuiza kinywa kwa uhodari
Na kuimarisha ngome ya maisha yangu

Kesho, liamkapo jua, nanasi litachukua zamu
Likishirikiana na embe,tufa,pera na plamu,
Kwa nyoyo kunjufu , yanaikaribishe mezani
Pamoja na wakazi wengine wa kiota changu
Tukae kwenye viti vya kiamsha-kinywa
Tufurahie ukarimu wa anga la Ekweta

**Maadui Wajanja (uk. 81)**
Hwa maadui wa uhai,hili genge la izraeli
Kwa ujanja mkali,kwa ujuzi mwingi
Hujijificha vumbini,huchutama mitaroni
Huegemea vigingi,huiga makopo ya kawaida,
Bila kuonya,huvamia mkulima na mpita-njia
Hushambullia Watoto michezoni au malishoni
Kufumba na kufumbua ,hutupa maiti kaburini
Wasipofuaulu kuzima maisha, wakishindwa kuua
Hwa wakala wa mauti, kwa hasira ya moto
Hulipua mikono,kusaga miguu na kutafuna visigino
Kwa ulimi wa moto hulamba vifua na migongo
Au,baada ya kupiga daruni,kushambulia kiunoni
Na kufuta fahari ya wanaume na kuwaacha bila maana
Wakati wa kudhulumu,hawa wakala wakali wa shetani
Hufumba macho, kuangalia upande au kuangalia angani
Iloi wasione iwapo aingiaje kwenye mtego wa mauti
Ni mwenye mkongojo mkonononi au ubwabwa shingoni
Hushidilia pamba masikioni au kuyaziba kwa udongo
Ili asisikie kama atakayepigwa,atakayesagwasagwa
Ana maarifa juu ya faseti,bazuka,au AK 47
Au ni mwnakujiji asiyetofautisha bastola na kipuri za gari
Sasa, Angola na Msumbiji, kaburi za wasiokuwa na hatia
Zinakumbusha wananchi wapenzi waliondoka bila kuaga
Mashamba ya rutuba yasiolimika,malisho yasiyolishika
Yanachekelea bara lianloishi katika kizingizia za njaa
Na picha za viwete wanasimama kandokando mwa Maisha
Ziankumbukwa mshairi mieleka ya CIA,KGB na Havana
Na kuleta mwangwi wa ``wapiganapo fahali,ziumizo ni nyasi”

**Kasisi (uk. 82)**
Ulishuhudia mito ya damu
Ikitiririka katika Bonde la Ufa,
Uliona mvua ya machozi
Ikilowesha kambi za wakimbizi,
Ulitazama ndoto za makabwela
Zikunguzwa na kubakia jivu,
Ulikuwa na bakuli lililojaa habari
Kuhusu manahodha wa njama,
Ulielezwa kisa cha mwanasiasa
Aliyembaka binadamu yake ofisini
Ulijua dhiki ya wasichana wachanga
Waliozimwa heshima ya uanamwari

Ulikuwa na hamu ya thamani
Kusimama wima mahakamani
Na kwa silaha madhubuti ya ulimi
Kuwa jemedari hodari uwanjani
Katika vita vya kutetea utu
Dhidi ya genge la wahuni

Leo tumekukuta chini ya mnga
Mwili uliotengwa na walio hai
Kwa radi ya risasi kichwani

Wanasema ulijitungua mwenyewe
Bali sisi wageni katika nchi
Tunakumbuka ya juzi na jana;
Si muhali walikushona midomo
Ili kimya chako kiwe ngao kwao.

**Asubuhi Hasiri (uk. 85)**

Macho yao ya miaka michache
Yamekamatwa na unyevunyevu,
Kwenye pua isiyojua manukato
Kumegandama makopo machafu,
Mvuke hatari wa gundi ya viatu
Unateka nyara mapafu na akili

Huku wamefanana na matambara
Hawa waliotupwa kwenye jalala,
Wanaomba kwa ishara ya mikono
Na kwa sauti inayodondoka ukiwa,
Wadogo wanamwandama mpitaji
Sawa na ‘ndamata’ au ‘nconge’ nguoni

Kwenye mapipa ya masalio ya vyakula
Wanateta na kutukanana na chungu,
Karibu na malundo na vitupwa vya jiji
Wakasirisha kunguru na kongoti,
Karibu na mijengo ya biashara za nyama
Wanashindana na mbwa, panya na nzi,
Wakiwania mabaki ya nyama-choma
Na mabaki ya ugali, viazi na bofulo…

Baada ya gundi kukolea kwenye ubongo
Inakoambia akili “kufa na kupona ni sawa”,
Wanatembea kwa mwendo legelege
Kana kwamba viwiliwili vimeazima miguu,
Lugha kutoka vinywa visivyojali

Inajikokota kama naji yam to uliochoka

Baadhi wamevuka mpaka wa wema
Wanatembea wakiwa wameficha dhamira hatari
Wapatapo nafasi waitafutayo kama Johari
Wanyakua saa za mikono, mikufu na mikoba
Kwa wepesi kama kipanga mawindoni

Jua linapoondoka na usiku kuvamia jiji
Watoto wanaolea kwenye wingu bandia
Wanapigana mieleka mikali na baridi isiyojali
Na kupambana na vikosi vya mbu watukutu

Akili namwili zinamomonyoka
Zinaacha magofu ya kuhuzunisha
Tayari safari ya kutembea na kifo
Imeanza kwa mwendo imara

Macho ya wanasiasa hayawaoni ukweli
Yamegandama kwenye vipande vya kuku
Katika sinia haramu wanayoizunguka,
Akili za wananchi hazidadisi kisanga
Zimekwama kwenye miiba ya vitandamboo
Katika kichaka cha kutafuta stara ya maisha

Ofisi ya Makavu wa Rais wa Jamhuri
Ilifunua meza kitambaa kwa ujasiri
Na kutuonyesha mradi uliometameta
Wa kukarabati maisha yaliyopinda
Na kuingia kutu na sumu kali mjini

Punde, siasa yay owe la katadole
Ilifunika mpango kwa vumbi tifutifu
Kuzoa Watoto na kuwahamishia vituoni
Sasa ni hadithi; si harakati zenye uhai.

Tusingekuwa na macho ya bundi au popo
Tungeona wabakaji na majambazi sugu
Tungeona Sankor na miwani yake ya giza
Tungeona mbegu ya machozi mekundu
Ambayo tumepanda kwa uchangamfu
Kwa siasa ya waropokwaji wa kulipwa
Na mfumo wa uchumi wa “kila mtu kivyake”

**Ndimi zetu (uk. 87)**

Ndimi zetu,nafsi ya utu wetu
Nembo za utamaduni wetu
Makavasi ya tajriba ya karne tele
Maktaba za habari za kila taaluma
Hifadhi za maarifa na falsafa

Hongera mababu zetu,walimu
Maarifa ya kilimo na ufugaji
Matibabu ya binadamu na mifugo
Dawa za kutibu mizozo na vita
Ramani za maadili na mbeko
Mmezihifadhi katika maghala

Ndimi zetu ni migodi inayostahili heshima
Katika methali, misemo na vitendawili
Hadithi, visasili na nyimbo za jadi
Kuna johari zenye thamani ya fahari
Mchimbuaji mwenye stadi na ujuzi
Ndani vipande vya dhahabu na almasi

## Muungano wa Afrika (uk. 90)

"Tumezaa,
tukate kiunga mwana kwa makini
Tumlee,
tumtunze kwa mikono mikunjufu
Tumlishe,
tumpe chakula chenye lishe bora
Tumgange,
tumtibu akumbwapo na ndwele
Tumlinde,
tumkinge maadui wasimnyonge
Tumjenge,
tumwimarishe kano na misuli
Atuafu,
atufungua minyororo na unyonge
Atuinua,
atukweza hadi kilima cha shibe?"

## MASHAIRI YA *RANGI YA ANGA*

## RANGI YA ANGA

**I**

Baina ya wawili maishani
Uzito wa safari
Ungelingana kama shilingi kwa ya pili,
Utulivu kwenye kumbi za nyoyo
Ungekuwa wa mizani sawa,
Singejipa wadhifa wa mgambo
Singejipa pembe ya swala pala
Kuwakutanisha wanakijiji;
Moyoni mwangu
Hakungekuwa na ilihamu
Ikiniwashawasha kwa utukutu
Kama majani ya mpupu;
Mwashomwaso usiokuwa
Haungekuwa ukirusha mawimbi
Yakibeba mvumo wa sauti
Ukisema kwa uradidi;
Himahima shika pembe
Piga mbiu ya mgambo!

**2**

Vilele vya milima
Na Malindi ya bahari,
Mmwesomweso wa nyota
Na tumba la mbalamwezi,
Bila kupigana mieleka
Kwenye ukumbi wa ugambi
Zinakubaliana kwa pamoja
Kwamba kuwa navyo mkononi
Ni mpini wa upanga mkali
Mkononi mwa mwanmume,
Na kiganja cha mwanamke
Kinapoishiwa na stahamala
Na kujiinua mapambanoni
Hushika makali ya bapa
Ikatiririka damu bila hatia
Na ndoto ya kufikia usawa
Katika vuta nikuvute ya jinsia
Kuingia baridi

Kaida zenye kutu ya karne
Zimemkumbatisha nani
Haki ya kumiliki ardhi
Ambamo mikahawa na kawa
Na migomba na miparachichi
Inadarizi mandhari azizi

Kama zulia jamala
La kijani cha thamani?

Kwa mujibu wa ibara za kimila
Ni nani mmiliki wa hili bonde
Ambamo tete za mawele
Na za mtama na za wimbi
Zinametameta asubuhi
Kama tembe za dawa -kinga
Ngao imara ya wakazi
Wasijeruhiwe na michomo
Ya visu vya msimu wa njaa?

Kwa kanuni za mababu
Ni nani atakayerithi shamba
Ambamo mnukio adhimu
Wa maembe na matomoko
Na machungwa na malimau
Umepamba chembe za hewa
Kama moshi-manukato
Wa ubani au ambari?

Kwa kaida za kitamaduni
Tunatarajia nani, kwa furaha
Atwae tambarare zenye rutuba
Ambamo viazi-vikuu vya thamani
Na mihogo na viazi-vitamu adimu
Na karoti pendezi na wanga change
Na vitunguu duara na karanga jamala
Zimejificha ndani ya udongo
Kama zana za wazalendo
Zikisubiri zamu iwadie
Zitetee uhai na uhuru?

Kwenye kumbukumbu za wakazi
Ni nani, kwa tabasamu angavu
Atakayerithi bila vikwazo
Haya mawimbi ya minazi
Yanayoimba wimbo mtamu
Yakipokezana na muziki asilia
Wa ala pendezi za bahari?

Katika fahamu za walio mbali na bahari
Ni nani, kwa nyoyo changamfu
Atakayepokea mbarika wenye afya
Walio na Ngozi laini ya kuvutia,
Beberu wenye ndevu na ndeo
Wakitembea vichwa juu malishoni
Kondoo ndume wenye mazulia mwilini
Wakininginiza Mafuta kwenye mikia
Na kuyaweka kwenye maghala ya mikia,

Fahali wenye kengele shingoni
Wanaoongoza ng’ombe wenza malishoni?

Ni nani, nadadisi kusudi kujua
Atayerithi hii mizinga mviringo
Inayovuma nyuki lufufu
Kwa weledi bila kimbelembele
Wakizungumza na mbelewele
Kutoka vilele vyeupe vya minga
Na vikwata, miyombo na mijunju
Kuundia asali inayotajika kwa ubora?

Ni nani, iwapo unazielewa mila
Ambaye katika kupokezana viunzi
Kwenye mbio za marika na vizazi
Atapokea hili shamba la mairungi-
Kichaka chenye vitawi chapa-pesa
Vinavyotafunwa karibu na mbali
Na kufunga wanaume mabarazani
Huku kwa baridi ya upweke
Wake wakifurukuta vitandani
Mpaka nyimbo angavu za zuriwanda
Zinaanza kukaribisha mwanga wa jua?

**5**

Kwa macho dadisi
Tumeona mikwaruzo na kovu
Katika mikono na shingo
Na mashavu na vipaji
Kama kwamba chui aliyeudhika
Amepigana vita vya kulipiza kisasi
Dhidi ya binadamu kizimbani
Tulipomulika kwa uchunguzi
Jawabu likatugonga masikioni
Kama kikawe cha manati:
  Mume amemwadhibu mkewe-
  Wanawake, ni kama watoto
  Usipowarudi, hupoteza njia!
Nyuso zetu zilipoingia kunyanzi
Kwa kutoridhika nyoyo
Sauti ‘ilifafanua’
  Mume ana haki thabiti
  Anaruhusiwa kumwadhibu mkewe
  Si alilipa mahari!

Kwa masikio yenye huruma
Tumesikia mlio wa makofi
Viganja vikitua mashavuni;
Tumesikia ngumi ngumu
Zikilia juu ya goko na mitulinga
Na kutoa sauti nzitonzito

Kama kwato za ng'ombe
Zikikanyaga mawe njiani

Hujaona uvimbe mweusi
Ukichekelea kwa dhihaka
Juu ya uso au shingo,
Au matone ya damu
Yakidondoka puani
Au kutoka kinywani,
Au meno yaliyokuwa imara
Yaliylegezwa mizizi
Na kutoroka kutoka taya,
Au macho yaliyoigiza nyota
Yakavamiwa na genge la makofi
Yakawa fumbo la dhiki ya ndoa?

**6**

Sikiza hiyo sauti
Ulimi ukitoa kauli
Kama upanga mkali
Ukikata mmea mchanga:
　　Wewe sasa ni mtu mzima
　　Mshale wa mizani ya miaka
　　Unaonyesha miaka kumi na minne,
　　Mbona usiolewe na Mzee Malimali
　　Kusudi mahari ya ng'ombe na mbuzi
　　Ituzimie moto wa umaskini
　　Kama wingu kuu la masika
　　Likizima ukame nyikani?

Kwa masikio matatu
Mawili kichwani
Na la tatu akilini,
Katika cafeteria
Katika chou kikuu
Nilisikia profesa
Vyeti nyumbani
Fedha mifukoni
Kipara utosini
Ndevu kidevuni
Tabasamu midomoni
Na *T-bone* viganjani
Akijigamba kwa wenza-
　　Nilipoposa, nikachumbia
　　Niliyemchumbia, nikamuoa
　　Hakuzidi kumi na tatu
　　Kwenye mizani ya miaka!

Wasemaji tuseme nini
Au tutulie yakini
Kama maji ya mtungi-

Aliyetunga mimba
Na kuibeba kwa miezi tisa
Na kwa uchungu na miguno
Kuleta mkazi ulimwenguni
Na kwa moyo mkunjufu
Kulea kwa mapenzi ya mama
Apandapo kwenye akili ya mwanawe
Sio mmea wenye majani ya tiba
Bali wenye matunda ya sumu
Kwa kubeza akisema:
    U mwanmume gani
    Ushindwaye na madogo
    Kama mwanamke?

Watazamaji tuseme nini
Au tutumbue macho
Kama komba mtini
Profesa wa kike
Mwenye shahada ya uzamili
Ateteapo viini vya matende
Akibeua:
Hiyo
    Si taasubi
        Ni destruri na mila!

Hizo
    si nyanyaso
        Ni kanuni za jadi!

Hizo
    Si dhuluma
        Ni kaida za utamaduni!

**7**

Sikiza sauti ya mzazi
Ambayo inakuja juu
Kama wimbi la sumu
Ikimimina kemikali kali
Katika akili asubuhi:
    Usicheke kiholela
    Kama wewe ni mwanamke!
    Nyamaza! Futa machozi!
    Ushindwaye na madogo
    Kama mavazi yako
    Ni kamisi na rinda!

**10**

Walikuwa wachanga
Katika kivuli cha shule
Hisia za ujana zilipovutana
Mithili ya sumaku na chuma;

Nyoyo zikalainika
Miili ikaitika mwito mkali-
Moto wa maumbile uliwaka
Na kisha kuzimika
Mithili mwako mbugani
Utupao ndimi angani
Na kisha kukata roho
Baada ya wingu la mvua
Kupasuka katika mbingu

Mmoja wa wawili washiriki
Aliendelea na mwendo shuleni
Akakusanya vyeti vya maana
Na kupata jina adimu nchini,
Leo, asubuhi, anakula mayai
Na asali na siagi ya thamani,
Anavalia mavazi ya kuteua
Na kulalia godoro la gharama,
Anatumia fenicha ya mvuli
Na kukalia matakia ya veliveti,
Anakanyaga mazulia laini
Na kunawa kwa sabuni ya marashi,
Anakulia sahani zenye nakshi
Na kunywia kauri za kutajika,
Anaogea katika bafu ya moto
Na kujikagua kwa vioo ukutani,
Anaendesha gari ghali
Na kutumia ofisi inayotuliza hisia,
Lakini, kichefuchefu maalumu
Kilishambulia wa pili
Asubuhi zikavurugika bila kikomo
Akajipata katika ulimwengu mpya,
Ndipo Halmashauri ya Shule
Ilipotaja kanuni za wizara
Na kaida za kuendesha shule,
Ilinukuu miongozo miteule
Na masharti ya kuzingatiwa,
Baada ya kulaumu na kubeza
Iliangusha shoka lenye makali
Likakata safari ya mja-mzito

Banati alipotimuliwa, alitimuka
Alipotimuka, aliteguka
Alipoteguka
a
k
a
a
n
g
u

k
a
!

Leo, mjijini
Akibeba njaa kama saratani ya tumbo,
Na kuvaa umaskini kama joho la miba
Pamoja na wenza, anazurura jijini
Akitegea na kuchungua magari yapitayo
Na kulenga shabaha yanayochochea ndoto
Kusudi, kwa uganga wake wa faraghani
Ahimili maisha ya huzuni ya mama
Na kunusuru uhai unaotetereka
Wa mtoto asiyejua baba

**12**
Kwa ahadi tamu kama halua
Wakala alimrairai mama-mzazi
Akamnyakua binti kutoka shamba
Akambwaga kwenye vimetemete jijini
Kutunza Watoto wa watu mtaani
Kupigana mieleka na kazi za jikoni
Na kuipa nyumba sifa kwa unadhifu

Katika nyumba ya mawe na vigae
Orodha ya maagizo na matarajio
Matakwa ya mama-mwenye-nyumba
Yalimtenga kijana na usingizi wa macheo
Mwili wake teketeke kwa miaka michache
Na baridi ya alfajiri isiyocheka na watu
Zikawa wandani mithili chanda na pete

Amri yenye meno kama ya msumeno
Mama mwajiri akitangaza majukumu
Ikakerezakereza masikio machanga
Huku macho dadisi dadisi ya baba-mtoto
Yakimkaguakagua mjakazi umbo la mwili
Yakimmulika tangu kichwani hadi nyayoni
Ndoto isiyoogopa miiko ya jamii
Ikimfukuta kama moto wa shonde kavu

Zilianza chichiri za chini kwa chini
Leo hanchifu Kesho chokoleti au keki
Mtondogoo mafuta ya kufurahisha ngozi
Na kisha mavazi yasiyotajwa hadharani

Punde miiko inayowawekea mipaka wazima
Kamba inayowafunga waliojifunga kwa pete
Ilichomwa na harara za hamu ya baba-watoto
Ikawa mnyama hatari bila kizuizi

Asubuhi ya kuraukia kazi ya mshahara
Mlango wa nyumba ulipomwaga mama
Baba aliyetangulia kuondoka nyumbani
Hugeuza gari na kuliekeza lilikotoka
Hadi nyumbani kwenye sumaku ya mwili
Na kwa mawaridi mekundu ya maneno
Kuanza kutunga koja nyerezi
Akizungumzia sio lishe ya watoto
Sio unadhifu wa nyumba au nguo
Bali akimshawishi mhudumu mchanga
Waunde chombo cha kuchanganyia hisia
Kiwainue kutoka sakafu ya utulivu chapwa
Hadi anga la tufani za bashasha

Hayawi! Hayawi! Yakawa ya kuwa
Yakawa ndiyo ngoma isiyokoma
Ikawa ndiyo siri vifuani mwa wawili
Mama-watoto asiyejua malimwengu
Akaendelea kutabasamu katika giza totoro

Kuna ya kuficha yasifichuke
Na faichwayo yakafichuka-
Huzuiliwaje siri ambayo kila uchao
Huumuka kama unga wa ngano
Uliokolezwa hamira ya thamani?

Baada ya rinda la mhudumu mchanga
Kukataa katakata kuwa mshiriki siri
Uhai wa miezi mitano ya mchachato
Ulijitangaza kwa lugha fasaha

Mama-matoto alipoona fumbo la rinda
Hakupata harufu ya donda la ndoa
Alisalia kwenye gizagiza la kutojua
Akammwagia mhudumu matusi
Akimchongea ujanja na kiherehere
Akimsingizia kuleta malofa nyumbani

Kwa joto la kelele Nyingi
Kama kwamba kimburu mkaidi
Anafukuzwa asile kuku uani
Mhudumu na virago vyake mgongoni
Alitimuliwa kutoka nyumba ya watu

Baada ya miezi minne ya machozi
Kiumbe kipya kilifungua mlango
Kikajibwaga kwenye mwanga wa dunia
Mama mkembe na mtoto wa siri
Wakaanza safari ngumu bila ramani
Punde si punde wakaingia kichakani
Wakawa mateka wa michongoma

**WANDA**

**1**

Joto
Linapeperusha bendera
Linatawala kwa maringo
Na kiburi,
Linanyanyasa tosi
Na macho,
Harara hii inachokoza kwapa
Na kukereketa migongo

Tazama!
Tazama mayowe kimya
Yakiwayawaya angani
Na kwa ukaidi wa alasiri
Kutisha majani na maua
Na kubabaisha mijusi na nyuki.

Jua!
Ewe jua!
Jua la adhuhuri,
Mbona kwa ghadhabu
Unaadhibu chembe za udongo
Kwa halijoto kama ya tanuri?

Jua!
Ewe jua!
Jua la wanda za mikwaju
Mimea na samaki
Ndege na wadudu
Na Wanyama na mito
Walikutenda ovu gani
Kukuchochea ulipishe kisasi
Kwa ghadhabu pujufu?

**2**

Ewe makazi wa wanda
Wewe
Adui wa maumbile,
Wewe
Hasidi wa wewe mwenyewe,
Wewe
Ambaye umetia kitanzi
Kwenye shingo ya mazingira
Shingo yako mwenyewe
Shingo za wajukuu na vitukuu

Ambapo kwa karne
Kwa nyundo imara
Maumbile yalishawishi miamba

Na taratibu kubembeleza mawe
Na kwa sepetu adhimu
Kuchanganya viungo
Kuundia udongo wa thamani
Ikamea miti na nyasi,
Wewe
Kwa miaka isiyotosha gao
Bali inayofurika dharau
Umetabanga ardhi-
Ukuta azizi baina yetu
Na makombora y amauti

Leo
Yaliyokuwa makazi mema
Yaelekea kuwa kaburi kuu
La kuzika mikunguru
Nungu
Panzi
Nyigu
Ng’ombe
Mitilili
Kwale
Mikoma
Swara
Miswaki
Na binadamu!

Kilimo cha lima-hama-lima
Utendaji usioheshimu matuta
Au kutia maanani mche wa mti
Ila unapoahidi matunda
Hicho kilimo cha jadi
Kimepotosha panga
Kushambuliwa mimea
Kwenye kingo za mito
Miinuko ya vilima
Na chemchemi adimu

Kilimo kikongwe
Bidii za kijungujiko
Kimehujumu ardhi
Na kugofua rutuba,
Kimeishi kwa inda
Na kupambua mazingira,
Kimealika mabaka bahili
Na kuyapa makazi,
Kimakaribisha mawe
Kutoka vizimba vyao
Katika lindi la ardhi,
Na kupokea mivo
Kwa moyo mkunjufu

Hizi kovu kirihi
Ambazo kwa kinaya
Zinaangalia mpita njia
Jana zilikuwa mashamba
Kulistawi:
Mawele
Kunde
Wimbi
Mtama
Mahindi
Na mbaazi
Bali leo
Hutu mhisani wa jana
Amesahauika na wakulima
Kama kitambara bila thamani
Kwenye lundo jalalani

Majira ya mvua
Na kijani kibichi
Kikosi cha taya za ng'ombe
Hushambulia nyasi change
Na kuhujumu miche adimu,
Hutafuna mashina na majani
Na kuwa kizuizi cha chuma
Dhidi ya ngome ya kijani

Wakati wa kiangazi
Na mazigazi
Ndimi kakamavu za mifugo
Huzoazoa madakata ardhini
Na kunyima miti lishe,
Hudhoofisha ngao ya ardhi
Na kuinyima uimara
Wa kuhimili mashambulizi
Ya matone buka ya mvua
Na mtiririko wa fujo
Wa maji mekundu

Tazama jinsi kwato za ng'ombe
Zilivyoleta kisanga,
Tazama zilivyojeruhi ardhi
Na kuiacha katika maumivu

**3**

Vikwata
Mitini
Tumbili
Kwembe
Na kanga
Wanashuhudia vimbunga
Vikija kwa mizunguko peperu

Vikivingirisha maghubari angani
Kama pia-kuu nyekundu
Na kupepeta masakasaka
Kwa pepeto za fujo

Tazama ambavyo
Kwa mori
Tufani
Inaruka mabonde makavu
Kabla ya mikono yake myepesi
Kuishika mitambaapanya
Na kuvurumisha chini mapaa
Na kuacha kuta za udongo
Zikisimama na huzuni
Kama wanakijiji wafiwa
Siku ya kaburi na machozi

Ole wang!
Moyoni
Napekechwa na uchungu:
Wakulima
Wameua miangati,
Wagemaji
Wamechinja mikoma,
Wasonga-mizinga
Wameangamiza mianjate;
Vizazi vya mijunju
Migunga
Mibarao
Na mitanda-mboo
Vimetumbukizwa kaburini;
Ngao ya maumbile
Imeingia dosari
Sasa dhoruba yenye kiburi
Imepata fursa mwafaka
Kuhasiri ardhi kwa hasira

**4**

Kutoka anga la kiangazi
Dhuluma
Zinanguruma kwa nguvu
Na kubabaisha mabonde
Na mawanda na vilima
Mithili mto ulioghafirika
Na kuasi kingo kwa hasira

Tazama jinsi kondoo
Kuku
Kurumbizi
Pimbi
Mikowe

Mbuzi
Mibono
Na sisimizi
Wanavyotapatapa
Katika dimbwi la joto-
Bwawa la huzuni!

Tazama jinsi sura ya udongo
Ilivyo na alama ya jakamoyo
Kwa kukaangwa kwenye tanuri
Ya jua lenye inda!

**5**

Leo mawingu yametanda
Na kupanga turubai ya alasiri
Kwa utomvu mwekundu-
Yametimu majira mapya
Majira ya ukarimu na shibe
Na hujuma na hasara

Ambamo mkazi wa jana
Alikuwa mchanga mweupe
Kimya ukitazama mpita-njia
Au miamba myeusi tititi,
Au ya kijivu au zambarau
Ikitulia bila wasiwasi,
Sasa maji ya hisia mekundu
Yanatiririka kwa fujo-
Mto uliokuwa ukilia kwa kiu
Umekunywa maji umekinai
Sasa, badala ya kuwa na kikuku
Unashindana na mito isiyokauka
Kuona ni nani mwenda kasi Zaidi

Kwenye mito bila sifa
Ambamo jana alasiri
Maji ya kijani
Yalijikokota kwa uzembe
Yakinung'unikia kwa ukongwe,
Mgeni mwekundu
Sasa ananguruma kwa ari
Akivurumisha magogo,
Mawe
Mizizi
Mizoga
Shonde
Manyoya
Vigae vya mayai
Na magamba ya nyoka

**12**

Pengine,
Jua likichomoza
Tiba adhimu ya maji
Itazifikia hizi nyanda
Ndipo kwa sauti ya mantiki
Muulizaji
Aulize waulizwa
    Huku kuhamahama
    Ili kuanzisha upya kone
    Kunaleta shida gani
    Kuliko shamba aushi
    La kabeji
    Sukuma-wiki
    Tamata
    Mbiringanya
    Pilipili-mboga
    Mpunga
    Mtama
    Mahindi
    Karoti
    Kunde
    Mbaazi
    Wanga
    Uto
    Pamba
    Machungwa
    Maembe
    Na mapera?

Hii milolongo ya taya
Na pembe na nundu
Inafaidi vipi nyumbani
Zaidi ya viwele vichache
Vya ng'ombe wateule?

## ZIMWI LA THELUJI

**4**

Lilifika zimwi la theluji
Kutoka upande wa pili
Wa mvumo wa mawimbi,
Janga kutoka ng'ambo
Ya bakuli kuu la chumvi

Lilipowasili asubuhi
Lilimkuta ng'ombe wa Kijiji
Akiningisha kiwele
Akichungwa malishoni

Lilikuja zimwi la theluji
Likibeba simulizi
Mkururo wa vituko vya ajabu
Viroja vilivyolemaza akili
Hadithi ya visa vya kihurafa
Katika kitabu maalum
Lilijidai kuwa tarishi
Wa Muumba wa yote
Likakunjua hadithi
Ya Baba na Mwana
Mwana wa pekee
Ambaye
Kabla ya kuuawa
(Alijua angeuawa
-Alijua yote)
Aliwafunza binadamu
Kula nyama ya mwili wake
Na kunywa damu yake
Kama ushirika imara
Na binadamu-Mungu
Mwana ambaye
Kutembea juu ya maji
Na kufufua wafu
Na kigeuza maji harusini
Kuyafanya tembo adimu
Ilikuwa suala jepesi;
Mwana ambaye
Ni mkuu wa wavuvi
Kwenye bahari ambamo
Tonzi na kambare
Na tafi na michumbururu
Na change na chewa
Na mikunga na nguru
Ni wewe nami-
Binadamu!

Kwa ukungu wa hila
Zimwi la theluji
Liliapa kwa mbingu
Na ardhi na nyota
Kwamba lilikuwa na dhima
Ya wakala wa Mungu
Kuwahamisha wenyeji
Kutoka kichochoro kichafu
Ambamo giza la dhambi
Lilinguruma kama radi,
Kichochoro ambamo
Moma na mamba
Wanatambaa kwa fahari
Na swila na bafe
Huota jua bila wahaka;

Lilidai lilisukumwa na fahamu
Kuja kuwaita wenye roho za giza
Watoke kwenye janga
Waingie kwenye bustani
Ambamo mkindu na misapo
Na miale na misanaki,
Huburudisha macho,
Bustani ya vijito pendezi
Vito ambamo
Maziwa na asali
Hutiririka kwa ukunjufu
Pasipo msimu bahili,
Bustani ambamo
Nyimbo tamu za nyonza
Na muziki laini
Wa upepo mwanana
Ukipiga majani pambaja
Hutumbuiza masikio
Na akili na damu,
Na nakshi za mawaridi
Na virukia na afu
Na vilua na haibiskasi
Hufurahisha macho,
Chini ya mininginio
Ya machungwa na matomoko
Na mapaipai na maembe
Na matomoko na mafenesi

**5**

Kama maji ya Mto Nili
Sekunde na dakika
Zilitiririka bila kikomo,
Katika mto wa wakati
Zikapita siku na miezi,
Katika upeo wa macho
Miaka ikayoyoma
Huku kwa ghiliba
Zimwi la theluji
Likimnyatia ng'ombe

Lilimfikia malishoni
Na kwa ujuzi wa hila
Kumtia kitanzi pembeni
Kitanzi madhubuti
Sio cha kamba ya mgoza
Sio cha katani au mkonge
Sio cha mbuyu au mfungate
Bali cha chuma cha pua

Lilimfunga utanzuni
Kwenye mti ambao

Umejikita ng’ambo
Lakini tanzu zake
Zimesambaa hadi mbali
Ambako kuzikata
Hadi hakika kukatika
Wakati mwingine
Huhitaji wakazi kukakamka
Na kumwaga jasho
Hata damu

Zimwi la theluji
Lilipokaza fundo
Kwa mikono imara
Lilichukua mitungi
Likavamia kiwele
Na kwa tamaa iliyokithiri
Kuanza kukamua maziwa
Na akiwa amechangamka
Kuyapikia katika vyombo
Na kwa tabasamu motomoto
Kuyasafirisha hadi ng’ambo

## KIAMBATISHO 2: WIMBO

### Musa Sukuma (Equator Sound Band)

Musa nimevumilia sana
Kupigwapigwa kama mimi punda
Na sura yangu imeharibika
Taabu…taabu…taabu

Kweli Musa uliponioa
Sura yangu_____
Haikuwa na alama
Hata moja
Nilikuwa na afya nzuri
Nilinona kama ngoima
Ya Kirige

Musa kweli tafadhali ndugu
Tafuta bibi atakayeweza
Kuvumilia hizo tabia zako
Ukinywa pombe
Waninywea yeye
O kinywa munyeke
Wamnywea yeye
Taabu tabu…taabu…taabu

## KIAMBATISHO 3: HOJAJI

**HOJAJI KWA MTUNZI WA DIWANI ZA *MSIMU WA TISA* NA *RANGI YA ANGA*: KITHAKA WA MBERIA**

Tafadhali jibu maswali yote kulingana na maagizo yafuatayo:

i. Yatoe majibu yote kwa kuzingatia utaratibu wa maswali.

ii. Maswali haya ni mwongozo wa mahojiano.

MASWALI

1. Kwa nini ukayapa mashairi yako anwani, 'Msimu wa Tisa' na 'Rangi ya Anga'?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

2.
    a. Ushairi wako unakaribianaje/unafananaje na ushairi wa kimapokeo kimuundo?

    ______________________________________________
    ______________________________________________
    ______________________________________________

    b. Ushairi wako unatofautianaje na ushairi wa kimapokeo kimuundo?

    ______________________________________________
    ______________________________________________
    ______________________________________________
    ______________________________________________

    c. Mashairi huwa na miundo mbalimbali kutegemea watunzi. Je, upekee wa kimuundo unadhihirikaje katika ushairi wako?

    ______________________________________________
    ______________________________________________
    ______________________________________________
    ______________________________________________
    ______________________________________________

3. Katika utunzi, ni vipengele gani vya kimtindo ambavyo unapenda kutumia?

   a. Vitaje.

      ______________________________________________
      ______________________________________________
      ______________________________________________

   b. Toa sababu za uteuzi wa vipengele hivyo katika swali la 3.a.

      ______________________________________________
      ______________________________________________
      ______________________________________________
      ______________________________________________

4. Una maoni gani kuhusu mchango wa ushairi huru katika maendeleo ya taaluma ya ushairi?

   ______________________________________________
   ______________________________________________
   ______________________________________________
   ______________________________________________
   ______________________________________________

## KIAMBATISHO 4: ORODHA YA WAHOJIWA

**Kithaka wa Mberia**

Ni mtaalamu wa Lugha na Isimu, mtunzi wa vitabu na mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi nchini Kenya.